Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Tisa - Tarehe 29 Juni, 2010**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge katika mkutano huu wa ishirini unaoendelea, Bunge lilipitisha Muswada mmoja wa sheria ya Serikali uitwao *The Finance Bill,* 2010. Mara baada ya kupitishwa na Bunge na baadaye kupitia katika hatua zake zote za Uchapishaji, Muswada huo ulipelekwa kwa Mheshimiwa Rais wetu ili upate kibali chake kwa mujibu wa Katiba.

Kwa taarifa hii nawafahamisha kwamba Mheshimiwa Rais ameshatoa kibali chake na sasa Muswada huo ni sheria ya nchi na inaitwa *The Finance Act, 2010* Na. 15 ya mwaka 2010. Nadhani hii ni faraja kubwa kwa wenzetu wanaokusanya kodi na ushuru na mapato ya Serikali kwamba kesho kutwa unapoanza mwezi mpya au mwaka mpya wa fedha wanayo sheria nyuma yao, Ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hatua ya haraka kuweza kutekeleza hilo.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**MHE. MASOLWA C. MASOLWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):**

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Cosmas Masolwa, nadhani hii ni mara yako ya kwanza kusimama hapo. Kwa hiyo, nakupongeza sana. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Kabwe Zitto, hukuwapo kwa muda wa kama siku kumi na nne hivi. (*Makofi /Kicheko*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa Jimboni.(*Kicheko*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO, MSEMAJI MKUU WA KAMATI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MIUNDOMBINU**:

Taarifa ya Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**:

Randama za Makadiro ya Matumizi ya Wizara ya Sayansi, Teknolojia, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge swali la kwanza nilaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Luhahula wa Bukombe. Hayupo, kwa niaba yake Mheshimiwa Masunga.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Dah, jamani vilemba hivi, ndio sio rahisi wanabadili kila siku hawa. Mheshimiwa Joyce Masunga. *(Kicheko)*

Na. 131

### Kuwajengea Uwezo Wenyeviti Wa Kitongoji na Serikali za Vijiji

**MHE. JOYCE M. MASUNGA (K.n.y. MHE. EMMANUEL LUHAHULA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuwajengea uwezo viongozi wa Serikali katika ngazi zote ni jambo zuri katika kuleta utawala bora:-

(a) Je, nani anawajibika kutoa elimu na semina kwa wenyeviti wa vitongoji na Serikali za vijiji katika maeneo husika?

(b) Je, katika Wilaya ya Bukombe semina za wenyeviti wa vitongoji na vijiji zimefanyika tarehe ngapi tangu waingie madarakani mwaka 2004?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wewe pia karibu Bungeni nadhani pia ulikuwa Jimboni.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kuchukua nafasi hii kusema kwamba alinituma Kigoma kule kwa ajili ya sherehe hizi za Serikali za Mitaa.

Napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwapongeza wananchi wa Kigoma pamoja Uongozi kwa kazi nzuri sana inayofanyika katika Mkoa wa Kigoma na ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa kikwelikweli. Wana umeme, wana barabara nzuri na kipekee tunawapongeza kwamba wametufundisha kwamba tuwe tunasherekea sherehe hizi kwa kufanya kazi, tumefyatua matofali na barabara. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Mkoa wa Kigoma.

Baada ya salamu hizo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wajibu wa kutoa elimu, semina na mafunzo kwa Wenyeviti wa Vitongoji na Serikali za Vijiji ni Halmashauri yenyewe kwa kuzingatia mahitaji mahususi katika eneo lake.

Fedha zinazotumika ni vyanzo vya Halmashauri (Mapato ya ndani na ruzuku inayotolewa kwa ajili ya kujenga uwezo). Aidha, Viongozi hao wanapatiwa mafunzo kuhusu utawala bora, uwakilishi wa wananchi katika vikao vyenye kufanya maamuzi pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe semina kwa Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji zilifanyika kuanzia tarehe 4/6/2007 hadi tarehe

21/6/2007. Kufuatia semina hiyo, jumla ya Wenyeviti wa Vitongoji 488 na wajumbe 608 wa Halmashauri za Serikali za Vijiji walihudhuria na kushiriki kikamilifu katika semina hiyo. Mada zilizotolewa ni kama zifuatazo:-

(i) Misingi ya Utawala Bora.

(ii) Wajibu na majukumu ya Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji.

(iii) Utaratibu katika kuendesha vikao na mikutano kwenye ngazi za Vitongoji,Vijiji na Kata.

(iv) Aina ya vikao, mikutano inayopaswa kufanyika kwenye maeneo yao.

(v) Upangaji wa mipango shirikishi jamii.

(vi) Usimamizi wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mafunzo yaliyotajwa yaligharamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kupitia fedha za kujenga uwezo *(CBG)* zilizotelewa na Serikali katika mwaka wa fedha 2006/2007 ambapo jumla ya shilingi 7,800,000 zilitumika katika kuendesha mafunzo hayo.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ardhi ndio rasilimali ya wananchi Vijijini na kuna sheria namba 5 ya mwaka 1999 ndio inayowaweka sawa wananchi hao ili waweze kutumia vizuri rasilima hiyo, lakini elimu ya sheria hiyo katika Vijiji vyetu na Viongozi wake haipo kabisa. Je, Mheshimiwa Waziri, Wizara ya TAMISEMI ina mikakati gani ya maksudi kuwapa semina ya kutosha Viongozi wetu wa Serikali za Vijiji ili waielewe vizuri sheria hii, ili kupunguza matatizo na kutenda haki kwa wananchi walioko Vijijini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rished, Mbunge wa Pangani kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Rished kwamba ardhi ni rasimali muhimu sana katika Kijiji na kama ambavyo tumekuwa tunajibu hapa ndani, ardhi ya kijiji ukutaka kuitumia ni lazima upate ridhaa ya Kijiji chenyewe na mkutano mkuu lazima ukubali kwamba ardhi ile itumike.

Sasa ni kweli kama anavyosema maeneo mengine sheria hii haijafahamika vizuri na kueleweka vizuri na kuna haja ya kuendelea kutoa elimu, tunatoa mafunzo ya aina mbalimbali na katika reform program ile kwanza nah ii ya pili pia hayo yamekuwa yanazingatiwa na kama tulivyojibu hapa semina mbalimbali zimekuwa zikitolewa kwa

ajili ya Wenyeviti wetu wa Vijiji pamoja na Wenyeviti wa Vitongiji pamoja na watendaji wetu katika Vijiji.

Kwa hiyo, nakubaliana naye kabisa kwamba elimu hii tutaendelea kutoa kufuatana na mahitaji, lakini *the bottom line is* Halmashauri ya Wilaya ya Pangani ai Halmashauri nyingine yeyote kuna tatizo na kuona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo na pale tutakapotakiwa kufanya hivyo kama Serikali, hatutaacha kwenda kwa ajili ya kutoa elimu hiyo.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika ngazi ya Taifa, Mkoa wa Wilaya, Serikali imeandaa wataalamu maalum kwa ajili ya usimamizi wa fedha na kwa kuwa sasa hivi takribani asilimia 25 ya bajeti nzima inapelekwa Wilayani kwa lengo la kwenda Vijijini kutekeleza miradi na huku hakuna wataalamu walioandaliwa, je Wizara sasa iko tayari kutoa mwongozo rasmi kwamba hawa Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji pale uchaguzi unapofanyika lazima wafanye semina kadhaa za kuwawezesha kusimamia hizi fedha, mabilioni ambayo yanapelekwa Vijijini ili hela hizi zisipotee bila kupata matunda?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza mimi nikiri kabisa kwamba ili tatizo ambalo yeye kila wakati tunaposema hapa ni Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounts Committee* kwa hiyo, yuko *conversant* na eneo hilo. Nikiri kwamba katika eneo hili lote analozungumzia kwenye *procurement* tuna matatizo, katika maeneo ya fehda nako tuna matatizo na hili tunaliona na tumekuwa tunashirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, tumekuwa tunashirikiana pia katika Ofisi ya Rais, Utumishi ili kuona kwamba hilo eneo tunawapata watu wengi ambao watatusaidia kwa ajili ya kufanya kazi hii anayozungumza Dkt. Willbrod Slaa na nikiri kabisa kwamba wanapokuwa wamechaguliwa Wenyeviti wetu wapya, mwingine anaweza kwenda pale amechaguliwa ndio, lakini majukumu yanayomuhusu kama Mwenyekiti wa Kijiji hayajui.

Kwa hiyo, cha kwanza kabisa tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba wanapata, lakini la pili ni kuhusu watendaji wetu wa Vijiji, kwa sasa hivi tumesema kwamba mtendaji wowote wa Vijiji lazima katika programu hii ya miaka mitatu ahakikishe kwamba amesoma walau mpaka kidato cha nne, amefaulu, hakufauli we don’t care lakini at least afike form four. Hii yote ni katika kujenga huwo uwezo na kuhakikisha kwamba tunakuwa na watu ambao ni competent ili Serikali zinazoenda katika eneo lile zisije zikapotea. Tunakubaliana na wewe kwamba tutafanya kazi ya kutoa elimu katika eneo hilo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa mara nyingi Serikali inapojibu maswali hasa yanyowahusu Wenyeviti wa Vitongoji ambao mimi najua wanafanya kazi kubwa sana za kiserikali kwa

sababu ni wawakilishi wa Serikali kwa ngazi ya Vitongoji na Vijiji, inapeleka mzigo kwenye Halmashauri za Wilaya, ambazo Halmashauri za Wilaya hizo hazina mapato ya kutosha kama ilivyo Serikali kuu. Je, haoni Waziri anapojibu hivyo haoni kama anakwepa jukumu la Serikali lenyewe la msingi la kuendesha nchi Utawla Bora?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mbunge wa Nzega kama ifuatavyo na rafiki yangu pia, nilisahau kusema hivyo:-

Mheshimiwa Spika, hela zinazoenda katika Halmashauri na zile zinazoenda kule kwako Urambo huwa tunazipitisha hapa, bajeti ni mpango wa Serikali unaoonyesha jinsi hela zitakavyopatikana na hela zitakavyotumika.

Ukishamaliza hapo, ukishapitisha hapa, huwezi kupitisha senti tano nyingine nje ya Bajeti itakayopitishwa hapa. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba juzi tumeelezwa hapa, hela zinakwenda katika Halmashauri katika Bajeti hii tumepitisha hapa trilioni 2.7 na hela zinazokwenda katika Halmashauri zetu hizi ni asilimia 23 ya bajeti, kwisha, zikishapita hapa ni basi.

Sasa kwa hiyo, Mheshimiwa Selelii na sisi tumeshaipitisha na Bajeti yenyewe kama anataka tuongeze hela ziende kwenye Halmashuri, itabidi sasa tuombe *Supplementary Budget* hapa. Lakini nataka nikiri kwamba ni kweli kabisa anachosema kwamba majukumu ambayo yamepelekwa katika Halmashauri ni kubwa, sasa hivi *Secondary Schools* zote zimepelekwa kule. Hapa tunazungumza habari ya hospitali, ziko kule zote.

Kwa hiyo, unaona kabisa kinachozungumzwa hapa ni kwamba tumpe hela zaidi Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aweze kutekeleza majukumu yake *comfortably* na wanasema kwamba hela zinakwenda kule *functions* ziliko ndicho anachosema Mheshimiwa Selelii.

Kwa hiyo, sisi tunakubaliana na hoja yake lakini sasa tunafanyaje kwa sababu tumefungwa mikono. Hapa kuna *ceiling* wanasema usiende nje ya 10%. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba Mheshimiwa *Member of Parliament* anasema jambo la maana lakini mwisho ni kwamba lazima ninyi hapa mseme kama mnataka mtuongezee nyingine hapa, tuko tayari tutachukua halafu tutapeleka kule Nzega.(*Makofi na kicheko*)

Na. 132

**Sifa za Katibu Muhtasi**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR (K.n.y. MHE. MWANNE I. MCHEMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika ajira ya mtumishi wa kada ya Katibu Muhtasi (*Personal Secretary)* inamlazimu awe na cheti cha *Shorthand*/ Hatimkato ndipo aweze kuajiriwa au kupandishwa cheo, na kwa hivi sasa huduma hizo hazitumiki kutokana na Sayansi na utandawazi inamtaka mtumishi kujua *computer stage one* na *stage two* au zaidi:-

Je, Serikali iko tayari kufanya marekebisho kwa ulazima huo ambao ni wa muda mrefu ili kwenda na wakati?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)( K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sifa za msingi ili mtu aweze kuajiriwa katika kazi za Katibu Muhtasi ni kuwa na elimu ya kidato cha nne pamoja na cheti cha uhazili cha kufaulu mtihani wa hatua ya tatu. Aidha, anatakiwa kufaulu somo la hati mkato ya Kiingereza na Kiswahili maneno 80 kwa dakika moja, na pia awe amepata mafunzo ya kompyuta katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kila taaluma ina umahili wake na ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata Makatibu Muhtasi walio mahiri katika fani hii, sifa ya hatimkato ni kigezo muhimu kinachomjenga Katibu Muhtasi kuwa na uwezo wa kuandaa taarifa kwa muda mfupi na kwa wakati, hivyo kompyuta haiwezi kuwa mbadala katika ujuzi huu wa hatimkato.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri kwa jibu lake zuri lakini nilikuwa nataka atufahamishe jambo moja tu kompyuta hivi sasa tunaenda mpaka katika kiwango cha Kimataifa, hizi hatimkato bado tuna nia ya kuwasomesha vijana wetu wakafikia katika hatua ta *degree* ya somo hili la hatimkato. Na la pili hivi hawa Makati Muhtasi mara nyingi katika ofisi zetu huwa tunaona kuna wanawake na wanaume; Mheshimiwa Waziri anaona ni lipi bora kuwa na Katibu Muhtasi mwanamke au mwanaume?

**SPIKA:** Hili la pili sio swali ambalo linahusiana na swali la msingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri jibu kuhusu hatimkato.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, hatimkato ni muhimu sana kwa Makatibu Muhtasi na kama wengi ambao tumewahi kuwa viongozi ni mashahidi kwamba kuna baadhi ya

wakati unamwita katibu muhtasi, unamwelezea kwa kifupi tu nini unachotaka aandike na yeye anachukua kwa haraka sana anaenda kukutaharishia lile dokezo, nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Hafidh Ali kwamba hatimkato ni muhimu na itaendele kuwa ni muhimu. Lakini sina uhakika kama inatolewa hadi katika hatua ya *degree*. *(Makofi)*

Na.133

**Watumishi Kutolipwa Fedha zao za Uhamisho**

**MHE. IDD M. AZZAN (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni kawaida ya Serikali kuwahamisha watumishi wake kutoka kituo kimoja kwenda kingine na kwa kuwa zoezi hilo hufanyika hata kwa watumishi wa ngazi ya atrafa, Kata na vijiji; na kwa kuwa, yapo malalamiko katika ngazi hizo kuwa hawajalipwa fedha zao za uhamisho:-

(a) Je, ni watumishi wangapi ambao hawajalipwa fedha zao za uhamisho hadi sasa?

(b) Je, ni sababu gani zinazosababisha wasilipwe fedha zao kwa wakati husika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, madai yote ya watumishi ikiwa ni pamoja na madai ya uhamisho yamefanyiwa uhakiki kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkoa na Halmashauri zinazohusika. Uhakiki huu ulifanyika kati ya tarehe 19 Aprili, 2010 na atrehe 8 Mei, 2010.

Mheshimiwa Spika, taarifa kamili ya idadi ya watumishi ambao hawajalipwa itatolewa mara baada ya Ofisi ya mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukamilisha kuunganisha taarifa ya Halmashauri zote.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayosababisha watumishi waliohamishwa kutolipwa fedha ni kutokana na waajiriwa mbalimbali kuwahamisha watumishi bila kuwa

na fedha ni kutokana na waajiri mbalimbali kuwahamisha watumishi bila kuwa na fedha za kugharamia uhamisho huo katika Bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, Serikali imechukua hatua kama ifuatavyo:-

1. Kutoa maelezo mahususi kwa mamlaka za ajira kutohamisha watumishi bila kwanza kutenga fedha za kugharamia uhamisho huo.

2. Katika mkutano uliofanyika mjini Morogoro tarehe 22-23 Januari, 2010, Serikali imekubaliana na wawakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi kufanya uhakiki wa madai hayo na yale yatakayoonekana kuwa sahihi yatalipwa kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za fedha.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili la uhamisho na kucheleweshwa kwa fedha za uhamisho linasababisha vile vile kwa watumishi wanapofika sehemu ile wanayohamia pia kuchelewa kwa mishahara yao kitu ambacho Halmashauri nyingine hutumia hekima kuwalipa posho kwa kutumia Ofisi zao. Lakini Halmashauri nyingine inashindikana kufanya hivyo.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwasaidia watumishi hawa ambao malipo ya uhamisho yanachelewa na hata mishahara yao inachelewa hata kama wamepeleka *Data Sheet* mapema ili iwe kama mwongozo kwa watumishi wote kwamba wanapohama wasaidiwe kupewa pesa kwa kutumia OC ili waweze kuishi na familia zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, nataka niseme tu kwamba Mheshimiwa Mwanri sasa hivi ameelezea kwamba unapohamisha mtumishi na ukawa huna fedha katika bajeti na wakati huo huo bajeti imeshapitishwa yule mtumishi *definately* utamhangaisha kwa sababu utamlipa kupitia kifungu gani, unapomlipia kwa kutumia OC maana yake *Other Charges*, unafanya kosa. Hii inakuwa ni kumsaidia lakini unafanya kosa. Mwongozo ambao tumekwishautoa Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Hazina kwamba tusihamishe watumishi mpaka uwe na kasma yake kwa maana fedha zake za mshahara huko anakokwenda na fedha zake za uhamisho hapo anapotoka. Huu ndiyo mwongozo sahihi utakaotupelekea sote kuwa na *discipline*. Vinginevyo tutakuwa hatuna *discipline* na matumizi ni *discipline* na Bunge hili linapitisha matumizi kwa maana kwamba wenzetu wanaosimamia wawe na *discipline.*

Namwomba Mheshimiwa Mbunge tusisitize hilo katika Halmashauri zetu vinginevyo tutakuwa tunafanya makosa na vinginevyo tutakuwa tunawaonea hawa ambao tunaowahamisha bila kuwa na fedha za uhamisho na bila kuwa na mshahara wake.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, niongezee majibu mazuri sana ambayo ametoa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi. Kile kikao cha Morogoro kilichofanyika Morogoro, Mwenyekiti wake alikuwa mimi.

Nilikuwepo pale na wakati tulipokutana pale na viongozi wafanyakazi, tulikubaliana mambo yafuatayo kwamba ni kweli kabisa ukiangalia wafanyakazi wengine wote nje ya walimu walionekana kwamba wana mapunjo, walionekana wengine wamekwenda likizo hawakulipwa, wengine wamehamishwa hawakulipwa. Tukakubaliana kwamba tuta-*compile* na tuhakikishe kwamba tunapata madeni halisi ambayo wafanyakazi wale wanadai. Baada ya pale tukasema kwamba yatapelekwa kwa CAG. CAG aseme kwamba ninaridhika kwamba sasa haya ni madai halali. Ndivyo ilivyofanyika.

Baada ya hapo Mheshimiwa Mbunge anazungumza habari ya mfanyakazi kwamba atakuwa amekwenda katika eneo lake na akapewa hela kule. Utaratibu ule umekwisha. Tumekubaliana kutoka sasa kwamba hela zitakwenda pale za Magu na mwalimu akienda kule au mfanyakazi azikute kule. *Data Sheet* zitakuwa zinapelekwa *retrospectively*. Yaani zitakwenda kinyume nyume ndiyo zinapelekwa kule. Sasa itatokeaje hiyo.

Mheshimiwa Spika, kama ikitokea hiyo inayosemwa hapa maana yake ni kwamba mwalimu au mfanyakazi alipangwa kwenda Newala, akaacha kwenda Newala akaenda Siha akienda Siha kule hatakuta mshahara wake. Ndiyo unapata hiyo *phenomena* anayoizungumza hapa. *(Makofi)*

Na. 134

**Fidia kwa wafanyakazi wanaoathirika kutokana na Mazingira mabaya ya kazi**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wafanyakazi wa viwandani, machimboni, mashamba makubwa na sehemu nyingine za sekta binafsi hupata athari kubwa sana zinazotokana na mazingira mabaya ya sehemu za kazi kama vile kupata ajali katika viungo vyao vya mwili, kuchubuka ngozi kutokana na kemikali, kupofuka macho na kadhalika wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kikazi.

Je, fidia gani wanalipwa wafanyakazi hao pindi wanapopata athari hizo wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kikazi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wanaopata ajali au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi hulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa wafanyakazi Sura 263 iliyotungwa mwaka 1948 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1982. Sheria hii imeweka wazi utaratibu wa kisheria unaopaswa kufuatwa wakati wa kushughulikia madai ya fidia.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria hiyo, wafanyakazi wanaopata ajali au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi hulipwa fidia zifuatazo:-

1. Fedha tasilimu kulingana na kiwango cha maumivu ambacho hukadiriwa na daktari.

2. Viungo bandia kwa anayepoteza kiungo kama mkono au mguu.

3. Kulipiwa gharama za matibabu hadi atakapothibitika kuwa amepona.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa Sheria hii imepitwa na wakati na viwango vya fidia vinavyolipwa ni kidogo sana na haviendani na hali halisi ya sasa. Kwa kutambua hilo Serikali imekwisha kutunga Sheria mpya ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008 na maandalizi ya kuanza kutumika kwa Sheria hii yapo katika hatua za mwisho. Chini ya Sheria hii viwango vipya vya fidia vitakavyolipwa kwa Wafanyakazi watakaoumia au kuugua magonjwa yatokanayo na kazi vitaboreshwa.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKARI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa fidia kwa waathirika hao hazitoshi kutokana na madhara makubwa wanayoyapata. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ni vema kuwawekea bima badala ya fidia?

La pili, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anatambua kwamba wafanyakazi wetu wa mahotelini hasa katika majiji makubwa hasa katika Jiji la Dar es Salaam huwa wanaathirika sana na wananyanyaswa sana na waajiri wao kwa kutokuwawekea mikataba ya kazi. Unaweza ukafanya kazi siku ya pili ukafukuzwa. Ukaja tena siku ya tatu ukafukuzwa. Ni matatizo. Wafanyakazi wengi wa mahotelini hasa katika Jiji la Dar es Salaam wanapata matatizo kama hayo, kama yeye anayajua hayo anayachukulia hatua gani hawa waajiri hasa wa mahoteli? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, pendekezo lake la kwamba tutumie bima badala ya fidia.

Mimi niseme kwamba tutumie vyote viwili na nasema hivyo kwa sababu fidia ina sheria yake na bima ina sheria yake. Kuwa na fidia maeneo ya kazi au kupata magonjwa yatokanayo na kazi ni sheria ambayo ni nzuri na inalenga moja kwa moja kumhudumia mfanyakazi pale anapopata ajali kazini au akiugua magonjwa yanayotokana na kazi.

Lakini hii haimzuii mfanyakazi au mwajiri wake kuchukua bima aina mbalimbali kama bima ya maisha ili vile vile aweze kulindwa kwa upande huo. Kwa hiyo ningeshauri tu kwamba pamoja na hii Sheria ya Fidia bado wafanyakazi wetu tuwachukulie bima ili waweze kupata mafao zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu wafanyakazi wa mahotelini hasa Dar es Salaam. Mimi ningeshauri tu kwamba hawa wafanyakazi watumie taratibu za kawaida. Kwanza kwa kutumia chama chao cha CHODAU cha wafanyakazi, ili malalamiko yao sasa yafike kwetu kwa utaratibu ambao unakubalika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi.

Mimi nina hakika CHODAU wakitoa malalamiko yao na sisi tutayaangalia na kwa sababu tuna taratibu zetu basi tutachukua hatua zinazostahili ili wafanyakazi hawa wa hotelini waweze kupata haki zao kutoka kwa waajiri.

**MHE. MOHAMMED S. SINANI:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mwaka jana nakumbuka nilipokuwa nachangia moja ya hoja zilizoletwa hapa Bungeni nilizungumzia juu ya athari wanazozipata wafanyakazi wa kiwanda cha korosho cha OLAM.

Nakuomba Wizara kama si mwenyewe Waziri au wataalam wake waende wakawatembelee wananchi wale wapatao 4,000 na wengi wakiwa akina mama. Akawaone na kuwasikiliza na kujaribu kuwasaidia. Je, Mheshimiwa Waziri ile ahadi itatekelezwa haraka iwezakanavyo kama si wewe mwenyewe basi ujumbe mzito wa Wizara yako? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, nimesikia kilio chake na nikitoka hapa nitawaagiza wenzetu wa OSHA waende mara moja wafanye kazi hiyo ya kukagua kiwanda hicho.

Na. 135

**Hali ya nafasi za ajira nchini**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kuongeza ajira nchini ni eneo mojawapo la utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM):-

(a) Je, ni maeneo gani ambayo yameongezeka ajira kiasilimia?

(b) Je, nafasi za nafasi za Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, Udiwani, Ubunge, na Urais ni miongoni mwa ajira hizo zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi?

(c) Je, ni ajira gani zenye mvuto zaidi kwa Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli Ilani ya Uchaguzi ya CCM ilidhamiria kuongeza ajira zisizopungua 1,000,000 kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2006 hadi 2010. Nafurahi kusema kuwa mpaka sasa ajira zilizoripotiwa ni 1,313,561. Takwimu hizo ni taarifa rasmi hadi kufikia Desemba 2008 kwa sekta binafsi na hadi kufikia Aprili mwaka 2010 kwa sekta ya umma, sekta binafsi inaongoza kwa kutoa ajira 1,185,387 sawa na asilimia 90.2 na Serikali imetoa ajira mpya 128,174 (9.8%).

Mheshimiwa Spika, uchanganuzi zaidi unaonesha baadhi ya sekta muhimu ambazo zimezalisha ajira mpya ni pamoja na:-

(1) Ujenzi: 118,378 (ambapo wanawake 9,688, wanaume 108,690) sawa na asilimia 9.31 ya ajira zote.

(2) Elimu: 37,740 (ambapo wanawake 13,458, wanaume 24,282) sawa na asilimia 2.97 ya ajira zote.

(3) Afya: 36,776 (wanawake 25,949, wanaume ni 10,827) sawa na asilimia 2.89 ya ajira zote.

(4) Usafirishaji na mawasiliano: ajira 15,536 (wanawake 997, na wanaume 14,539) sawa na asilimia 1.22 ya ajira zote.

(5) Huduma za fedha: 7,787 (wanawake 3,908, na wanaume 3,879) sawa na asilimia 0.61 ya ajira zote kwa upande wa huduma za fedha.

(6) Sekta nyingine rasmi kama vile hoteli, viwanda, madini, na kadhalika, zimetoa ajira 20,165 sawa na asilimia 1.6 ya ajira zote.

(7) Sekta isiyo rasmi: imetoa ajira 1,039,420 sawa na asilimia 81.7 ya ajira zote.

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, zaidi ya asilimia 81 ya ajira zote zimetokana na sekta isiyo rasmi ambapo wananchi wamejihusisha zaidi kwenye shughuli kama vile biashara ndogo ndogo na utoaji wa huduma.

Aidha, mchanganuo wa takwimu za ajira mpya kuhusu kilimo, uvuvi na ufugaji kiasilimia zinatarajiwa kutolewa mara baada ya zoezi la uchambuzi wa Sensa ya Kilimo iliyofanyika mwaka 2009 kukamilika. Sensa hii imehusisha kilimo cha mazao, ufugaji na uvuvi.

(b) Mheshimiwa Spika, nafasi za Ubunge na Urais si miongoni mwa ajira mpya zilizoripotiwa kwa kuwa nafasi hizo zilikuwepo kabla ya zoezi la utambuzi kuanza. Aidha, nafasi za Mwenyekiti wa Kitongoji, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na Udiwani ni nafasi ambazo wahusika hawalipwi mishahara bali hulipwa posho za vikao husika, kwa maana hiyo hazikuhesabiwa kama ajira mpya.

(c) Mheshimiwa Spika, ingawa ajira kwenye sekta isiyo rasmi imeongezeka kuliko sekta rasmi, kwa uchambuzi wa kisayansi haimaanishi moja kwa moja kwamba ajira hizo zina mvuto zaidi bali kiuhalisi kuna fani mbalimbali zenye mvuto katika soko la ajira. Mvuto huu huendana na mabadiliko ya mahitaji katika soko na ujira unaolipwa.

Serikali inategemea kulifanyia utafiti suala hilo ili tuweze kubaini ni ajira gani zenye mvuto zaidi kwa Watanzania. Aidha, kuongezeka ajira kwenye sekta isiyo rasmi kunachangiwa na sababu za urahisi wa kuanzisha shughuli ndogo ndogo ambazo zinahitaji mtaji mdogo, urahisi wa upatikanaji wa malighafi, miradi kumilikiwa na kaya, mahitaji ya teknolojia, mahitaji ya taaluma na ushindani katika sekta rasmi.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri wake na Serikali kwa ujumla kwa mchanganuo mzuri kabisa huu ambao umesaidia kuonyesha ni nini kimefanyika katika eneo hili. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua, je Serikali imetoa mwongozo wowote wa kuelekeza vijana ili wachague masomo kwenye vyuo ambayo yana uwezekano kabisa ya kujipatia ajira badala ya kutegemea ajira ambazo hazina uhakika?

Je, wananchi ambao wanahusisha Ubunge na uzee na ujana haoni kwamba wanavunja Katiba, Ibara ya 67 kwa sababu sifa za Mbunge zimeelezwa wazi wazi kwenye Katiba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya Serikali napokea pongezi zake kwa uchambuzi ambao tumeufanya na mimi nieleze tu kwamba kwa kweli Chama cha Mapinduzi kimetekeleza Ilani katika eneo hili. *(Makofi)*

Lakini kuhusu maswali yake kwamba mwongozo kama Serikali imetoa ni aina gani ya fani zinafaa kwa wanafunzi ili wasichukue fani ambazo hazina mvuto wa ajira. Mimi nadhani hili ni la kuangaliwa na wanafunzi wenyewe.

Lakini nieleze tu kwamba kwa kweli fani ambazo zinaonekana kuwa na ajira ambazo ni za uhakika ni fani ambazo wanafunzi wengi mara nyingi huziogopa kwa sababu fani hizi zinaendana na mambo ya hesabu na Sayansi na unakuta kwamba kule kidogo wanafunzi wengi wanaogopa na wanakwenda kwenye masomo mengine ambayo kwa ajira unakuta kuna matatizo kidogo.

Lakini mimi nadhani katika juhudi zetu za kukazania masomo haya ya sayansi na hesabu basi tutaendelea kupata wanafunzi wengi katika fani hizi ambazo zina uhakika wa ajira.

Lakini ni vema kila mwanafunzi na kila mzazi aelekeze mtoto wake eneo ambalo anajua linaweza kuwa na ajira ingawaje uwezo vilevile unategemea nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu baadhi ya wananchi kuhusisha uzee na vijana, sasa kwa upande wa sisi kama watu tunaoangalia ajira, kwanza ajira yetu sisi hufikia miaka 60. Sasa hii ya wazee na vijana, mimi nakiri kwamba kwenye suala la Ubunge, kusema kwamba kuna wazee na vijana ni suala ambalo wanakosea. Na mimi ninakubaliana na wewe kwamba wanavunja Katiba, lakini halihusiani moja kwa moja na ajira ambayo tunaizungumzia hapa. Kwa hiyo, mimi ninamshauri Mheshimiwa Shelukindo, asiwasikilize hao wanaosema, ilimradi wananchi wake bado wanampenda, nina uhakika kwamba wataendelea kumchagua pamoja na uzee.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya

Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye ametoa takwimu inayoonesha 81% ya ajira zilizo nyingi zilizopatikana ni ajira binafsi. Sijui anayo habari kuwa hawa vijana wengi wanaofanya kazi zao binafsi badala ya kusaidiwa, huwa wanabughudhiwa sana hasa sehemu za mijini kama vile Dodoma na Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Spika, swali langu ningependa kumwuliza tu, katika hizi ajira hata hii ya kuokota chupa barabarani inahesabiwa kuwa imo katika ajira? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, napenda kujibu, sasa sijui nijibu swali moja Mheshimiwa Spika? Ni lipi kati ya hayo?

Mheshimiwa Spika, hili la kusumbuliwa niseme kwamba, pamoja na Serikali kutaka vijana wajiajiri na wasaidiwe kuweza kupata ajira, sheria lazima zifuatwe. Kitu cha msingi ambacho kinatakiwa kifanywe kama Serikali, ni kuwawezesha vijana hawa wapate maeneo rasmi ya kufanyia biashara na sio kufanya biashara hovyo hovyo na katika kufanya hivyo wavunje sheria. Hili wanatakiwa wao walizingatie, lakini ninakubaliana kwamba Serikali ina jukumu la kuwaelekeza ni namna gani na mahali gani waweze kufanya biashara. Na hilo tunalifanya hasa Dar-es-Salaam, ambako na mimi ni Mbunge kule; tunajitahidi sana kufanya hilo lakini kama tunavyojua vijana wetu kuna wakati wanavunja sheria na inabidi tuelekezane. Mheshimiwa Spika, sasa hili lingine la wanaookota makopo au chupa barabarani; hao hawamo kwenye ajira ninayozungumzia. *(Makofi)*

Na. 136

**Kuendeleza Usafiri wa Reli Toka Mombasa – Moshi**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa watalii wengi huanzia utalii Kenya na hasa Mombasa na baadaye kuja Tanzania; na kwa kuwa wengi wa watalii hao hupenda kuja kuuona na kuupanda mlima Kilimanjaro lakini hukatishwa tama na mzunguko wa kupitia Nairobi na Namanga:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuendeleza usafiri wa reli kutoka Mombasa kuja Moshi ili kuvutia watalii wengi kuja Moshi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba watalii wengi huanzia utalii nchini Kenya na hususan Nairobi na Mombasa; japokuwa wapo baadhi ya watalii wanaotokea Nairobi kupitia Namanga, Arusha hadi Moshi. Lakini pia watalii wanaotokea Mombasa kwa ajili, ya kupanda mlima Kilimanjaro, hawana sababu ya kupitia njia ya Namanga – Arusha – Moshi kwa vile kuna barabara inayotoka Mombasa kupitia Voi hadi Holili na Tarakea.

Kwa hiyo, hoja ya kuendeleza usafiri wa reli kutoka Mombasa kuja Moshi ili kuvutia watalii kwa sasa haina uzito.

Mheshimiwa Spika, huduma ya usafiri wa reli kutoka Mombasa hadi Moshi ulikuwepo huko nyuma na ulisitishwa baada ya kuonekana kuwa kibiashara haukuwa na tija na hasa kutokana na kuwepo usafiri mbadala wa barabara baada ya kuimarishwa miuondombinu ya barabara nchini. Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ya kwamba mara itakapoonekana kuwa huduma hiyo ina tija, Serikali kupitia Kampuni ya Reli ikishirikiana na Serikali ya Kenya itaangalia uwezekano wa kuirejesha. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, ninayo maswali mawili madogo tu ya nyongeza, ambayo ningependa nipate majibu. Usafiri wa reli unamilikiwa na Serikali, usafiri wa barabara kwa kiwango kikubwa unaendeshwa na wafanyabiashara wakubwa wakubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu, Serikali haioni ni wakati muafaka wakawekeza kwenye reli badala ya kuzidisha uwekezaji katika barabara kwa sababu reli ni mali ya umma?

Mheshimiwa Spika, pili ni ukweli usiopingika kwamba barabara zinauwa kuliko reli na majanga ni mengi sana. Badala ya Serikali kulinda Reli zetu ili tulinde maisha ya Watanzania, tunawapeleka kwenye barabara ambapo wanakufa, hiyo ni sawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mzee wangu Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo, na kusema kweli ninaomba niyajibu kwa pamoja:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba huduma ya usafiri wa reli kwa sasa hivi kwa kiwango kikubwa inasimamiwa na Serikali na huu usafiri wa barabara kwa kiwango kikubwa unaendeshwa na watu binafsi, lakini hasa baada ya kuimarishwa kwa miundombinu ya barabara ambayo inafanywa na Serikali. Kwa hiyo, niseme tu kwamba vyote viwili barabara na reli, hata kama huduma ya barabara inafanywa na watu binafsi lakini vyote viwili barabara na reli vinaimarishwa na kujengwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme kwamba tunaliona na tunaona umuhimu wa ujenzi wa reli, pia hata katika usafirishaji wa mizigo. Ndio maana sasa hivi kupitia

Jumuiya ya Afrika Mashariki, tuna mpango kabambe, yaani *East African Railway Master Plan,* ambao tunauandaa kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba tunaunganisha maeneo yetu mengi ya reli ili tuweze kusafirisha mizigo yetu kwa urahisi. Hiyo itaweza kuepusha vilevile na haya mengine ambayo ameyasema Mheshimiwa Mbunge, ya kuepusha ajali za barabarani, kama wananchi watavutika kusafiri kwa usafiri wa reli. Lakini vyote hivyo vinahitaji fedha. Kwa hiyo, baada ya mpango huu kuandaliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, fedha zitaendelea kutafutwa ili kuimarisha usafiri wa reli nchini.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa swali la nyongeza. Mimi ninaona swali hili limejibiwa bila utafiti ndio maana halina takwimu. Kwa kuwa, reli ya Kenya inafika mpaka Voi, tatizo ni kipande hiki cha Voi mpaka Taveta. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, swali ni Je, Serikali haiwezi kuona kwamba watalii ni wengi na ndio maana Kenya wamejenga kituo kizuri na cha kisasa cha Forodha pale Holili na sasa wana mpango wa kujenga uwanja mkubwa wa kimataifa wa ndege?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninataka tu niseme ya kwamba sikubalianinaye kabisa kwamba swali hili lilijibiwa bila utafiti wowote; tumefanya utafiti kwa sababu, huduma hii ya usafiri wa reli ambayo nimeizungumza katika jibu la msingi ilikuwepo huko nyuma na ilikuwa inatumika wakati ambapo barabara zetu zilikuwa bado hazijaimarika. Lakini baada ya kuimarika kwa barabara, huduma hii ya reli ikakosa wasafiri na mizigo mingi sasa hivi inakwenda kwa barabara. Sasa kama Mheshimiwa Mbunge, angependa tumpe takwimu hizo lakini ashiria ya wazi tu ni kwamba mizigo mingi ambayo kwa sasa hivi ilikuwa inatakiwa isafirishwe na reli inasafirishwa kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Spika, na mimi nilipojibu swali la msingi hapa, sikusema kwamba watalii hawapitii katika eneo hili la Mombasa, nimesema baadhi yao wanapitia kule. Lakini swali la msingi lilikuwa linasema watalii wengi, nilichokanusha mimi nikasema kwamba, sio watalii wengi wanaopitia huko; baadhi yao wanapitia huko, lakini kama nilivyokuwa nimejibu katika jibu la msingi hapa, tunaendelea kuiimarisha miundombinu ya barabara na reli kama nilivyosema. Kama itaonekana kwamba kuna haja, tutaendelea kuifufua na kuendelea kuitumia.

**MHE. DR. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nikiuliza juu ya hayo hayo mambo ya reli; reli yakutoka Dodoma kwenda Singida, Manyoni – Singida, ambayo imejengwa na Watanzania wenyewe kwa mali ya Watanzania bila msaada wa mtu yeyote. Je, Serikali haioni umuhimu wa reli hii kwa heshima yetu sisi wenyewe, kwamba ni sisi tulioijenga hivi juzi juzi kuona kwamba haifungwi na badala yake inafanya kazi ili kuweza

kuwasaidia wananchi wa mkoa wa Singida na mikoa ya jirani kama vile Shinyanga, na kadhalik? *(Makofi).*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mzee wangu Mheshimiwa John Samweli Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikubaliane na yeye moja kwa moja kwamba reli hii imejengwa kwa nguvu za wananchi wenyewe. Jambo ambalo kusema kweli ninataka vile vile nitambue juhudi zake wakati akiwa Serikalini akiwa ni Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na hatimaye Waziri Mkuu. Amesimamia mambo haya vizuri sana na kusema kweli tungependa tumpongeze. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa kwamba reli hii isifungwe, mimi ninakubaliana na yeye kwamba kuna kipindi tu ambapo reli hii ilisuasua kama wote tunavyofahamu, Menejimenti tuliyokuwa tunaendesha shirika la reli kwa pamoja, kulikuwa na udhaifu ambao sasa hivi Serikali imeshaondokananao kwa kuvunja mkataba na wabia wenzetu wale wa India. Lakini ninataka nimhakikishie tu kwamba kwa juhudi za Serikali na mipango mingine tutakayoifanya, tutahakikisha kwamba huduma za reli hii ya Manyoni – Singida, haifungwi. *(Makofi).*

Na. 137

**Ombi la Kukuza Pembe za Ndovu (Meno ya Tembo)**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Katika Mkutano wa *CITES* uliofanyika Doha mwaka huu 2010 Tanzania iliomba kuuza sehemu yake ya meno ya nduvo yaliyojaa kwenye ghala la Ivory Room, Dar es Salaam lakini ombi hilo halikukubaliwa:-

Je, Serikali inawaambia nini Watanzania juu ya hatma ya meno hayo ya ndovu?

**SPIKA:** Ningewashauri, maswali matatu yanayofuata yana utangulizi mrefu, kwa sababu wanaouliza huwa wanapewa siku moja kabla haya majibu. Nadhani kama tungeacha utangulizi tukaenda kwenye jibu, itaokoa muda kidogo. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kwa maelezo mafupi ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa kudhibiti biashara ya kimataifa ya wanyama na mimea iliyo hatarini kutoweka *(convention on Internation Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora – CITES)* ulisainiwa *Washington Marchi, 1973*, na ukaanza kutekelezwa rasmi mwaka 1975 na Tanzania ikawa imeuridhia mwaka 1979 na ikaanza kuutekeleza rasmi mnamo mwaka 1980 na hadi sasa mkataba huu una wanachama 175.

Mheshimiwa Spika, kutokana hali ya ujangili kuongezeka na biashara haramu ya meno ya tembo kuongezeka sana, mwaka 1988 Tanzania ilisimamaisha biashara ya meno ya tembo. Na katika kusisitiza msimamo huo, ilipandisha hadhi ya tembo wa Tanzania kutoka daraja la pili kuwa daraja la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa idadi kubwa ya tembo nchini, kutoka 55,000 mwaka 1989 hadi kufikia 110,000 mwaka 2009, na hivyo kuongezeka kwa gharama ya kutunza meno ya tembo pamoja na athari nyingine, Tanzania iliamua kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya *CITES* Muswada wa kuuza meno ya tembo ili ujadiliwe na kukubaliwa kama ingewezekana katika mkutano wa nchi wanachama uliofanyika Dohar, Qatar mwezi Machi, 2010. Utaratibu huu ni wa kawaida na tayari kulikuwa na nchi ambazo zimekuwa zikifanya hivyo kwa mujibu wa Mkataba wa *CITES.*

Mheshimiwa Spika, sababu na malengo ya Tanzania kufanya hivyo ilikuwa ni kuruhusiwa kuuza zaidi wastani wa tani 89,000 za meno ya tembo ambayo yalikuwa yamehifadhiwa maghalani na ilikusudiwa kupatikana wastani wa shilingi bilioni 20 kama mauzo hayo yangefanyika. Faida nyingine pia ilikuwa ni kuondoa athari za utunzaji ikiwemo uwezekano wa moto na ajali nyingine, zikiwemo gharama za kutunza ambazo zinafikia shilingi milioni 50 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri zilizofanyika, ombi hilo halikuweza kupitishwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kubwa mbili kama ifuatavyo:-

(i) Propaganda dhidi ya Tanzania ambazo ziliendeshwa na mashirika mbalimbali ya kimataifa yasiyo ya kiserikali zikiwemo baadhi ya nchi za jirani zilizotoa hisia potofu. Na nyakati nyingine kulitokea ushawishi wa kuamini kuwa fedha ambazo zingepatikana zingetumika katika Uchaguzi Mkuu wa 2010 na si katika kuendeleza kama ambavyo ilikuwa imekusudiwa.

(ii) Kulingana na utaratibu wa mkataba wa *CITES*, mara nchi inapowasilisha Muswada wake, wataalam wa *CITES (Panel of Experts)* hutembelea nchi husika kufanya ukaguzi wa mambo mbalimbali kabla ya mkutano husika. Hivyo, taarifa ya wataalamu waliotembelea Tanzania ilibaini baadhi ya mapungufu, ambayo yalichangia kufanya Muswada usipitishwe.

Kwa mfano, licha ya kuwa na kumbukumbu zote kwenye kanzidata ya kompyuta, lakini nyaraka zote zilizotumika kutoa meno ya tembo kutoka mikoa kuja kwenye ghala kuu Dar es Salaam, hata kama ni za mwaka 1980, zilitakiwa ziweze kuoneshwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu, kwamba mapungufu na ushauri uliotolewa kwenye mkutano wa Doha, unafanyiwa kazi ili Tanzania iweze kuwasilisha upya Muswada mwingine kwenye mkutano ujao wa *CITES*.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kutoa pole nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Ujumbe mzima wa Tanzania ulikwenda kule Doha kwenye majadiliano haya, kwa propaganda chafu dhidi ya Tanzania ambazo zilifanyika katika Mkutano ule, zikiongozwa na majirani zetu, na mimi kama Mbunge ninaweza kutaja tu, Kenya ikiungana mkono na Rwanda, ambao wote tuko katika Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Sasa, kwa kuwa Bunge hili linalaani vikali kitendo hiki cha tabia zisizokuwa za kidiplomasia na ujirani mwema. Je, Serikali inachukua hatua gani, angalao za kuonyesha kwamba Watanzania tumekasirishwa sana, za kununa tu kidogo dhihi ya Kenya na Rwanda? *(Makofi).*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, unaweza ukanuna kidogo? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndugai, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hali iyojitokeza, haikumfurahisha kila mmoja na tayari mawasiliano yameshafanyika katika ngazi ya kidiplomasia, kuonesha jinsi ambavyo Tanzania haikufurahishwa na jambo hilo. Lakini tu kubwa zaidi ni kwamba wenzetu wa nchi jirani wameshashirikishwa sana sasa kuelezwa msimamo na makusudio yaliyokuwepo na hatutegemei kama itatokea tena mifarakano ya aina hiyo kwenye nia ijayo ya kuwasilisha Muswada wetu.

Na. 138

**Mapato Yanayotokana na Sekta Ya Utalii**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA K. n. y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Je, Serikali inafahamu kuwa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani kuna vivutio vya kuwezesha nchi kuendeleza utalii lakini havitumiki kwa ukamilifu kuisaidia nchi kujipatia mapato kutokana na utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALI ASILI NA UTALIII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Mzindakaya, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya utalii katika kukuza pato la Taifa.

Aidha, kama alivyobainisha ni kweli kuwa nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii ambavyo kama vitaendelezwa vinawezaku panua wigo na kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Sekta ya Utalii nchini unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999. Sera imeelekeza bayana mikakati ya kukuza na kuendeleza mazao ya utalii ikiwa ni pamoja na kuendeleza mazoa yaliyopo na kukuza mazao mapya kwa lengo la kuongeza muda wa mtalii kuwepo nchini na hivyo kuongeza mapato yanatokana na sekta hii. Aidha, upo mpango wa kuendeleza utalii (*Tourisms Master Plan*) ambapo kuanzia mwaka 2000 umetilia mkazo kuendeleza ukanda wa Utalii wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mikakati iliyoandaliwa katika kuendeleza na kuboresha utalii hapa nchini, mnamo mwaka 2002 Wizara kwa ufadhili wa Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)* ilifanya utafiti wa kuendeleza utalii hapa nchini hususan katika ukanda wa Kusini ambapo rasilimali za utalii zilizopo na changamoto katika kuendeleza utalii zilibainishwa.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Sekretariati za mikoa imekuwa ikianisha vivutio vya utalii na m aeneo ya uendelezaji wa utalii katika mikoa mbalimbali hapa nchini ikiwemo mikoa ya Mbeya, Iringa, Mwanza, Mara, Kagera, Singida, Mtwara, Lindi, Ruvuma na Rukwa. Taarifa zinaoonesha hali ya vivutio hivyo na shughuli zinazofaa kufanyika katika maeneo hayo zimeandaliwa na kutumwa kwenye uongozi wa mikoa husika ili zitumike katika kupanga mpango ya uendelezaji utalii katika maeneo hayo.

**MHE. ENG. STELA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kulifanyika jitihada za kuendeleza vivutio vya maeneo yaliyohusika kama Kusini na kwa kuwa *CD* yake ambayo inaonyesha au inauza utalii wa Tanzania yaani *marketing* imekataa kabisa maeneo ya Kusini hususan Mkoa wa Ruvuma ambayo hakuna kivutio hata kimoja kinachoonekana mle. Je, Wizara ina mpango gani wa kufanya haraka marekebisho ili vivutio vya mikoa hiyo viweze kuonekana?

Kwa kuwa utalii hauhusishi mbuga za wanyama tu na maumbile ya kijiografia bali pia ni pamoja na utamaduni wetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa pia na *CD* vivutio vya tamaduni zetu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NAUTALII:** Mheshimiwa Spika, kuna *CD* nyingi ambazo zimeandaliwa na kusambazwa kwenye maeneo mbalimbali zinazoonyesha vivutio mbali mbali.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba *CD* ambayo ameiona inaweza ikawa ni mojawapo ya *CD* ambayo ilikuwa na makusudio ya kutangaza utalii wa maeneo fulani. Nchi yetu ni kubwa na vivutio ni vingi sana na hauwezi ukaviweka vivutio vyote katika *CD* moja kwa hiyo kumekuwepo *CD* mbalimbali zipo *CD* za Serengeti, *CD* za mikoa ya Kusini, lakini katika mpango mzima wa Wizara ni kutangaza vivutio vyote kupitia machapisho na *CD* mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la swali la kwanza la nyongeza ni kwamba kuna *CD* zinazoonyesha vivutio vingine zaidi ya mbuga za wanyama. Zipo *CD* zinaonyesha fukwe, vivutio vya mambo ya kale kama mji mkongwe wa Zanzibar pamoja na maeneo maeneo mengi kwa mfano Mbuga ya Selu, na Kilwa Kisiwani pamoja na vivutio vingine. Kwa hiyo, *CD* mbalimbali zinaonyesha vivutio mbalimbali. Kwa hiyo, si kwamba tumelenga wanyamapori tu au mbuga peke yake lakini pia zipo zinazokusudia kutangaza vivutio vingine.

**SPIKA**: Muda hauruhusu Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Na. 139

**Kuandaa sera na sheria kwa ajili ya *Bio-Technology***

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH (K.n.y. MHE. CHARLES N. KEENJA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, utaalam wa kisasa wa uzalishaji wa viumbe *bio-technology* unamanufaa makubwa katika kuongeza uzalishaji, ukinzani magonjwa, ubora wa mazao na kadhalika.

(a) Lini Serikali itaandaa sera, sheria na kanuni za kusimamia uingizaji wa teknolojia nchini?

(b) Kwa kuwa kuna hofu kwamba teknolojia hiyo inaweza kuwa na madhara. Je, ni madhara gani hayo na kuna ushahidi gani unaothibitisha kutokea kwa madhara hayo?

(c) Je, ni lini teknolojia hiyo itaingizwa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Charles Ndelianaruwa Keeja (Ubungo) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Bio-teknolojia ni teknolojia inayotumia viumbe hai katika uzalishaji wa mazao au bidhaa katika fani mbalimbali kama vile bidhaa za kilimo, mifugo, Afya (ikiwemo uzalishaji wa madawa), uhandisi na nyingine nyingi kutokana na mahitaji ya wanadamu. Matumizi ya baiteknolojia ni ya siku nyingi katika historia ya binadamu. Kwa mfano, baioteknolojia imetumiwa kwa miaka mingi katika kutengeneza mvinyo, pombe, mikate na vyakula mbalimbali vitokanavyo na maziwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Ndelianaruwa Keenja, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali imeona umuhimu wa usimamizi wa matumizi ya baioteknolojia nchini. Hivyo, sera ya taifa ya baioteknolojia imekamilika mwaka 2009 ilipopitishwa na Baraza la Mawaziri na tayari imechapishwa.

Sera hii imezingatia dira ya taifa ya mwaka 2025 inayolenga kuwa na uchumi imara na kuinua hali ya maisha ya Watanzania wa kuhakikisha kwamba nchi yetu inahimiza matumizi ya teknolojia mbalimbali ikiwemo ya baiteknolojia na kuzingatia usalama endelevu wa chakula, afya na mazingira. Sera hii inatoa mwongozo mahsusi wa jinsi ya kupanua matumizi ya baiteknolojia nchini na kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na teknolojia hiyo.

Aidha, mkakati wa utekelezaji wa sera hii umekwishaandaliwa. Sheria na kanuni (*Biosafety Regulations*) za kusimamia utekelezaji wa sera hii zimeanza kuandaliwa na zinategemewa kukamilika katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha wa 2010/2011.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda niungane na Mheshimiwa Keenja kukubali kuwa ni kweli kuna hofu kwamba teknolojia ya kupandikiza vinasaba inaweza kuleta madhara iwapo itatumiwa vibaya. Madhara yanayoweza kutokea ni pamoja na:-

(i) Uwezekano wa kupoteza aina za asili za mazao;

(ii) Nchi kuwa tegemezi kwenye makampuni yanayozalisha mbegu ambayo yana haki miliki duniani;

(iii)Kuongezeka kwa usugu wa wadudu waharibifu na magugu kwa madawa na; na

(iv)Kupungua kwa bioanwai. Madhara haya yamethibitishwa na tafiti mbalimbali zilizofanyika duniani. Aidha, mpaka sasa hakuna ushahidi wa kitaalamu unaoonyesha

kuwepo kwa madhara ya kiafya kwa watumiaji wa mazao yaliyozalishwa kwa njia ya bioteknolojia.

(c) Mheshimiwa Spika, matumizi ya baioteknolojia nchini, bado yako katika kiwango cha chini japo tumekuwa tukitumia teknolojia hii katika kutengeneza mvinyo, pombe, mikate na vyakula vya mazao yanayotokana na maziwa kwa kiwango kikubwa. Tayari kwa upande wa utafiti na uzalishaji wa mimea kwa njia ya chupa (*Tissue Culture*) tumekwishaanza kunufaika. Kwa mfano katika uzalishaji wa migomba, kahawa, chai, mibuni, miti na mimea mingine mingi.

Aidha, hakuna matumizi ya mazao yatokanayo na kupandikiza vinasaba (*genetic*) katika kuboresha mimea, wanyama na vimelea. Hivyo sera hii imetungwa ili kuhakikisha matumizi ya teknolojia hii yanaendelezwa katika mtitiriko unaoweza kuliletea taifa faida huku uangalifu ukizingatiwa ili kuepuka madhara. Juhudi zinaendelea kufanywa ili kuwafundisha wataalam wetu wa ndani juu ya kutumia teknolojia hii ili hapo baadaye nchi yetu iweze kunufaika zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. kwa kuwa Serikali iko mbio katika kufanya utafiti zaidi katika masuala kama haya na nafahamu kwamba hata sasa hivi tumepiga hatua nzuri tu katika kutengeneza mtindi mzuri tu hapa nchini.

Hivi sasa kuna mbegu za mahindi ambazo zinatengenezwa ambazo zinajulikana kama *genetically modified seeds* ambazo zinapigwa vita duniani na mategemeo yangu ni kwamba Serikali ya Tanzania itafuata mkondo huo huo wa kupiga vita. Je, Serikali inasemaje katika sual hili kwa upande wetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika dunia inayoendelea na Tanzania nayo imo kwa hivyo hatutopiga vita suala hili isipokuwa tutaenda sambamba kuona ile teknolojia ambayo haina madhara kwetu na ina tija kwa wananchi wetu ili iweze kutumika. Hivi ninavyozungumza Mheshimiwa tafiti nyingi tu zinafanyika hapa na ni kweli kuna mbegu ile ya mahindi ambayo inazalishwa na iliwahi kuleta tija kubwa Zambia walitaka ile mbegu mara ya kwanza walipopelekewa wakakataa lakini njaa ilipokuwa kubwa sana wakakubali lakini ndiyo hiyo hiyo ya *GMO*.

Kwa hiyo, ni kwamba pale ambapo tunaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo, baada ya utafiti ku-*prove* tunaweza tukafanya lakini hili hatulazimishwi lakini wana sayansi lazima tuwape nafasi zao na wao wafanye tafiti kwa manufaa ya nchi yetu kwa ajili ya uzalishaji, kama India wanazalisha *cotton* na ni muda mrefu sasa wanafanya toka mwaka 1975, shughuli hizi zinafanyika hatuwezi kusema na sisi Tanzania tubaki nyuma katika sekta ya sayansi na teknolojia.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mbali na uzalishaji wa viumbe hivyo katika bioteknolojia kwa kuwa tumebahatika Tanzania viko viumbe hai au viumbe ambavyo vinatumika katika *farmer statuary company* duniani, na viumbe hivyo au vimelea hivyo vinaibiwa katika bahari zetu za *tropic* hasa katika kisiwa cha Misali ambako kuna watalii wanaotoka Kenya na wengine wa hapa hapa wanaokuja Tanzania ambao wanatumia teknolojia ya *diving* kuiba vimelea hivyo. Je Tanzania mna mpango gani wa vimelea vinavyopatikana hapa Tanzania katika bahari zetu za *tropic* ambapo hatujavitumia na utajiri mkubwa kuliko Almasi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, niseme tu kama kuna kitu kama hicho kinafanyika tuwaombe wahusika ambao wapo wenye kazi zao waanze kufanya shughuli zao.

Sisi kwenye sekta yetu ya sayansi tutasimamia suala la tafiti mbalimbali zinafanyika nchi na ambazo zinaweza zikaleta tija kwa nchi yetu, niseme tu nadhani sekta hii mambo ya *bio-technology* inagusa sekta nyingine zaidi kwa mfano, kilimo, *environment,* mazingira, afya sisi ni kama ni *coordinator* wa kuona masuala haya yanafanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

Na. 140

**Kujinasua katika Bajeti Tegemezi**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Tanzania inategemea wahisani katika Bajeti yake ya maendeleo kwa asilimia kubwa:-

Je, Serikali imejipanga vipi ili kujinasua katika hali hiyo ya kutegemea wahisani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMARI YUSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamisi Juma, Mbunge wa Jimbo la Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wahisani wamekuwa wakichangia Bajeti ya Serikali. Pamoja na misaada ya kibajeti na mikopo yenye masharti nafuu tunayoipata, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kujenga mazingira ya kujitegemea, ikiwa ni pamoja na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, hatua ambazo Serikali inazichukua, kwa umoja wake zitasaidia kwa kiwango kikubwa kuinua uchumi wa nchi yetu, kuongeza mapato ya Serikali na hatimaye kupunguza utegemezi. Hatua hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuhakikisha kuwa kila anayestahili kulipa kodi analipa kwa mujibu wa sheria.

(ii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa makusanyo kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato.
(iii) Kuendelea kupunguza misamaha ya kodi kwa lengo la kuongeza mapato.

(iv) Kuliimarisha dirisha la Kilimo chini ya Benki ya Rasilimali na hatimaye kuwa na Benki ya Kilimo ili mikopo yenye masharti nafuu ipatikane na hatimaye kukuza uwekezaji na kuongeza uzalishaji.

(v) Kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na umeme, ambayo kwa sehemu kubwa ni chachu ya ukuaji wa uchumi wetu.

(vi) Kusimamia uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda pamoja na maeneo maalum ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo ya nje *(EPZ).*

(vii) Kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuendelea kupunguza utegemezi kutoka kwa wahisani hatua kwa hatua. Hata hivyo, suala la uwekaji wa mazingira mazuri ya usimamizi wa uchumi ukiambatana na ujenzi wa miundombinu ni njia muhimu ambayo itatuongezea mapato ya Serikali. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushirikiana kwani jukumu hili ni la Watanzania wote. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niulize maswali mawili ya nyongeza, pamoja na Wafadhili hawa kutusadia lakini kuna baadhi yao huwa wanachelewesha fedha hizo ambazo huwa wameahidi katika Bajeti. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na changamoto hii?

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika maelezo yake amesema hapa kwamba ili kuongeza Bajeti ya Serikali watahakikisha kuwa kila mtu anayestahili awe analipa kodi na kwa kuwa katika nchi hii kuna watu wengi ambao huwa wanastahili kulipa kodi lakini hawalipi kodi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kutueleza au unaweza kulieleza Bunge hili kuwa Serikali itatumia mbinu gani ili kuhakikisha watu wanaostahili kulipa kodi wanalipa kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMARI YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali tayari imeshakaa na wafadhili na

inaendelea kukaa na wafadhili kulizungumzia suala hili ili kujua hili tatizo la kuchelewa misaada yao.

Tumeshakubaliana na tumeandaa ratiba kwa kila mfadhili misaada hiyo itoke katika awamu gani na kwa kiwango gani. Suala hili ninaamini kwamba wafadhili wataheshimu makubaliano yetu na sisi kwa upande wetu vilevile tutaheshimu makubaliano tuliyofikia baina yetu na wao.

Mheshimiwa Spika, swali la pili mbinu ambayo Serikali inazichukua ili kuhakikisha kwamba kila anayepaswa kulipa kodi analipa kodi, mbinu ni nyingi lakini nataka nizitaje chache tu.

(i) Ule utaratibu wa wafanyabiashara ambao wamekuwa *VAT register* kusema kwamba ukitaka na *receipt* basi bei yake ni hii ukitaka bila *receipt* bei yake ni hii utaondoka hivi karibuni kwa sababu kila mfanyabiashara ambaye yuko *VAT registered* atapewa mashine ya *electronic* itaonyesha item aliyouza na bei aliyouza kwa maana hiyo kutakuwa hakuna kukwepa kulipa kodi ya *VAT*.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine, wewe ni shahidi na Bunge lako Tukufu ni shahidi tayari Serikali imeshaidhinisha fedha sio kidogo kwa ajili ya vitambulisho ili kila raia wa Tanzania atakuwa na kitambulisho chake na tutaweza ku-*identify* nani anayepaswa kulipa kodi na kwa kiwango gani na wote watakuwa katika *book* la ku-*register* kwa ajili ya kulipa kodi. Mipango mingine mingi Mheshimiwa Mbunge namwomba tukae tuzungumze ili niweze kumsaidia sitapenda kupoteza muda.

**SPIKA:** Ahsante sana na nakupongeza kwa jinsi unavyojibu kwa ufanisi mkubwa maswali ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwishapita matangazo, tutaanza na wageni. Sasa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Miundombinu ni watendaji wakuu wa Wizara wakiongozwa na Mheshimiwa Mhandisi Omar Chambo Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ya Miundombinu, karibu sana ahsante sana. *(Makofi)*

Pamoja naye wapo Viongozi wazito kama ifuatavyo wa Wizara hiyo na Taasisi; yupo Bwana Ephraim Mgawe, Mkurugenzi Mkuu wa Mahakama ya Bandari, Bwana Prosper Tesha, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Bwana Israel Sekirasa, Mkurugenzi Mkuu wa SUMATRA, Bwana John Haule, Meneja Mfuko wa Barabara, Bwana Makumba Kimweri, Mtendaji Mkuu wa TBA Wakala wa Majengo ya Serikali, Mhandisi Ephraim Mrema, Mtendaji Mkuu wa TANROADS; pole sana na vigongo unavyofanyiwa lakini inapendeza kumwomba Mungu tu mambo mengine ya dunia haya ni magumu sana. Tunaye pia Dr. Agnes Kijazi, Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Taasisi ya Hali ya Hewa; hayo ni makofi zaidi ya Wabunge jinsia ya Wanawake huwa wanafurahi sana wakiona wenzao waliofanikiwa na bado hatujamaliza yuko Mhandisi

Margret Munyagi, Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga; karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Mhandisi Lekuyani Manase, Kaimu Mtendaji Mkuu wa TEMESA, pia Captain Kennan Mhaiki, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ndege za Serikali. *(Makofi)*

Wapo wengi tu Wakurugenzi pamoja na Wakurugenzi Wasaidizi wa Idara mbalimbali za Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu, ambao wamekuja kufuatilia mjadala wa Hotuba ya Bajeti. Aidha, Mheshimiwa Waziri Kawambwa ana wageni wake binafsi ambao ni Wanakamati wa Kombe la Kawambwa. Hili litakuwa ni la mchezo wa soka nadhani, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Hashim Akida Diwani wa Kata ya Dunda. Karibuni sana na mnafanya vyema kuja kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri.

Wageni wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Chiku Maulid Kavula, Diwani wa Viti Maalum Chama cha Wananchi (CUF) Wilaya ya Urambo; Ndugu Winfrid Kangole, Mumewe Mheshimiwa Chiku na mtoto wao anaitwa Ramadhan Kangole. Naona hapa katika familia hii Mama ndiye ana maamuzi, kwa sababu Baba anaitwa Winfrid lakini mtoto wake anaitwa Ramadhani kwa hiyo mambo ni mazuri tu. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wa Mheshimiwa Azzan Zungu ni wanafunzi 30 kutoka Shule ya Sekondari ya Jangwani Ilala, wakiongozwa na Mwalimu Geraldina Mwanisenga. Tunawatakia mafanikio katika masomo, fanyeni bidii Tanzania inawahitaji sana muwe wanataaluma wazuri na wenye maadili. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Ramadhani Maneno, ambao ni Walimu 38 kutoka Shule za Msingi Lugoba na Lunga, wakiongozwa na Mwalimu Maximillian Mabele. Hii ni dalili nzuri kwamba, Mheshimiwa Ramadhani ana Jeshi la Walimu nyuma yake, kwa hiyo, inapunguza *pressure* kidogo. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Savelina Mwijage ni Mheshimiwa Felishen Bigambo, ambaye ni Diwani Kata ya Bukoba Mjini wa Chama cha CUF. Karibu sana Mheshimiwa Diwani, umesafiri kutoka mbali sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Zabein M. Mhita, ambao ni wanafunzi 50 na Walimu 6 kutoka Shule ya Msingi Kondoa inaitwa Modeli; naomba wasimame. Umuhimu wa shule hii ni kwamba, miaka kadhaa iliyopita Mheshimiwa Zabein M. Mhita akiwa bado binti mbichi kabisa, alikuwa anasoma hapo. Hongera sana na kwa hiyo hata ninyi wanafunzi mnaweza kufika mbali zaidi mnaopita katika Shule hii ya Modeli. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mohamed Sinani wa Lindi, ana mwanaye anaitwa Amin Sinani, ambaye ni Mhandisi anafanya kazi au anasoma Uingereza, karibu sana lakini ukimaliza urudi kwetu hapa ufanye kazi siyo kubaki hukohuko tena. Hatupendi vijana mnaozamia nje ya nchi na hali sisi tunawahitaji. (*Makofi*)

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Damas Nakei, ambao ni Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kutoka katika Jimbo lake la Babati Vijijini, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Issa Kassim Issa ambao ni wanaye Yahya Issa Kassim na Zuwena Issa Kassim. (*Makofi*)

Kuna Viongozi saba kutoka mtandao wa Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali unaojulikana kama *Forum SYD* kutoka Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Ndugu Athanas Evarist, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia wapo wanafunzi 30 kutoka Shule ya Sekondari ya Jamhuri hapa Dodoma, nadhani hawakupata nafasi labda wako Ukumbi wa *Basement.*

Kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati na ambao pia ni wageni wangu ni Ndugu Naomi Kapambala, Katibu wa CCM wa Mkoa wa Singida; huyu ni mmoja wa Makatibu hodari sana katika mfumo mzima wa Chama cha Mapinduzi. Sisemi hivyo kwa sababu anatoka Mkoa wa Tabora lakini ni ukweli. Bi Sikujua Semwenda, Katibu wa CCM Wilaya ya Iramba. Kwa propaganda huyu Sikujua ni hatari tupu! Pia yupo Bi. Mary Maziku, Katibu wa CCM Wilaya ya Singida Mjini, kwa kweli Timu ya Singida basi tu! Yupo pia Ndugu Cosmas Kasangani, Katibu wa CCM Singida Vijijini, alipokuwa Umoja wa Vijana alikuwa Urambo na tulimnoa vizuri sana ndiyo maana anapanda vyeo tu. (*Makofi*)

Yupo pia Ndugu Mathias Shidagisha, Katibu wa CCM Wilaya ya Manyoni. Pia yupo Bi. Esther Mwinuka, Katibu wa UWT Mkoa wa Singida na Msaidizi wao Bwana Bakari Khamis. Karibuni sana, nadhani tutapata fursa baadaye ya kuonana ili tuweze kuzungumza kidogo mambo ya Singida. (*Makofi*)

Wapo pia Viongozi wa Taasisi ya *Tanga Islamic Centre* ambao ni Ustaadh Abdallah Chambuso na Ndugu Ahmed Ayubu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Basi hao ndiyo wageni wetu wa leo, lakini kuna tangazo la kazi; Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini mkutane katika Ukumbi Namba 231, saa saba mchana leo. Huo ndiyo mwisho wa Matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 – Wizara ya Miundombinu

**SPIKA:** Sasa namwita Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha sisi kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge unaojadili Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu mkubwa na kudumisha umoja, amani na utulivu tangu amekabidhiwa madaraka ya kuliongoza Taifa letu. Kwa umahiri mkubwa, ameendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 na kuendelea kutekeleza yale ambayo ameahidi kwa Wananchi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, amjalie afya njema, hekima na busara ili aendelee kuliongoza Taifa letu kwa amani na utulivu. Aidha, napenda pia kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kwa hekima katika utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa kuendelea kuongoza vyema shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa hekima, umahiri na busara unazotumia katika kuliongoza Bunge hili Tukufu ambalo limefanya maamuzi mazito katika kipindi hiki cha miaka mitano. Maamuzi hayo yamethibitisha uwezo wa Bunge katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini. Mimi naamini kuwa, Wananchi wa Urambo Mashariki wameona umahiri na juhudi zako na bila ya shaka watakutendea yaliyo mema. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ila tu hiyo itawezekana kama Barabara ya Tabora kwenda Urambo itajengwa. (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kuchukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa msiba mkubwa uliolikumba Taifa letu kwa kuondokewa na Waziri Mkuu Mstaafu na Muasisi wa TANU na CCM, Marehemu Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa. Pole hizo pia ziifikie familia ya marehemu, ndugu, jamaa na Watanzania wote. Aidha, napenda kutoa pole nyingi kwako wewe binafsi, Bunge lako Tukufu, Kamati ya Bunge ya Miundombinu, familia ya marehemu na Wananchi wa Jimbo la Ruangwa, kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Sigifrid Seleman Ng'itu. Tutamkumbuka Marehemu Mbunge kwa michango aliyoitoa katika vikao mbalimbali ndani na nje ya Bunge kwa lengo la kuleta maendeleo ya nchi yetu. Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi, *Amen*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene wa CCM na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu wa CUF, walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uteuzi wao ni ushahidi wa imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwao. Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wa Jimbo la Bagamoyo kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kuendelea kushirikiana nami katika kipindi chote cha utumishi wangu katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Nitaendelea kuienzi fursa adhimu waliyonipa kuwa mwakilishi wao. Kwa sababu hiyo, naomba kuwatamkia rasmi Wananchi wangu wa Jimbo langu la Bagamoyo kuwa nina nia ya kusimama tena katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi wa Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo. Kipindi kikifika, nitaomba waniunge mkono na kunipa nafasi nyingine ya kushirikiana nao katika juhudi za kuliletea maendeleo Jimbo letu la Bagamoyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hali ya utendaji ilivyokuwa kwenye Sekta ya Miundombinu katika maeneo ya uchukuzi, ujenzi na hali ya hewa kwa kipindi cha 2009/10, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Jimbo la Singida Kusini, kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Sekta hii. Ushauri na maelekezo mazuri ya Kamati yaliiwezesha Wizara kusahihisha dosari mbalimbali katika mipango na utendaji, kwa lengo la kuongeza ubora wa huduma zitolewazo na sekta. Ushauri wa Kamati utaendelea kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika kuwapongeza na kuwashukuru Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mashariki na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa jumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba za Mawaziri waliotangulia. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge hao, yamesaidia kuboresha mipango ya serikali katika Sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, tunapoingia katika kipindi cha mwaka 2010/2011, ni vyema tukatafakari utekelezaji wa maendeleo ya Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa CCM ya Mwaka 2005 na Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali ili tuweze kupima kiwango cha utekelezaji wa Ilani na maendeleo tuliyopata pamoja na changamoto tulizokabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua nafasi hii, kufanya mapitio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, majukumu ya kisera na kiutendaji na ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali. Aidha, nitaelezea utekelezaji wa Mpango wa Wizara kwa mwaka 2009/10 na malengo na makadirio ya bajeti kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 ilielekeza Wizara ya Miundombinu kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 44: Barabara - Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Barabara. Serikali imekuwa ikiongeza kiasi cha tozo ya mafuta ambapo hadi mwaka 2007/08 ilifikia shilingi 200 kwa lita. Katika kipindi cha mwaka 2009/10, Mfuko wa Barabara ulikusanya jumla ya Shilingi bilioni 284.1 ikilinganishwa na Shilingi bilioni

73.082 zilizokusanywa mwaka 2005/06. Ongezeko hili la fedha limeboresha hali ya barabara kutoka wastani wa asilimia 78 mwaka 2005 hadi asilimia 95 mwaka 2009.

Hatua nyingine ni kuunda kikosi kazi ili kubaini mianya ya uvujaji wa mapato na kufunga kifaa cha kusoma na kujua kiasi cha mafuta yanayoingizwa nchini kupitia Bandari za Tanga na Dar es Salaam. Taarifa zake zilipelekwa moja kwa moja kwenye Bodi ya Mfuko wa Barabara ili kudhibiti mapato ya mafuta. Aidha, Wizara inaendelea na mchakato wa kuainisha vinazo vingine vya mapato.

Kukamilisha ukarabati wa barabara zote ambao unaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwishaanza katika Barabara Kuu. Barabara hizo ni Dodoma – Manyoni; Manyoni – Singida; Singida – Shelui; Shelui – Igunga; Igunga – Nzega – Ilula; Muhutwe – Kagoma; Nangurukuru – Mbwemkulu – Mingoyo; Mkuranga – Kibiti; Pugu – Kisarawe; Chalinze – Morogoro – Melela; Tunduma – Songwe; Kiabakari – Butiama; Dodoma – Morogoro; Kagoma – Biharamulo – Lusahunga; Tabora – Kaliua – Malagarasi – Uvinza – Kigoma; Usagara – Chato – Biharamulo na Ndundu – Somanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha jumla ya miradi 12 kati ya miradi 17 iliyopangwa kutekelezwa kwa kiwango cha lami. Hii ni sawa na asilimia 71 ya lengo. Miradi 12 ya barabara zilizokamilika kujengwa kwa kiwango cha lami katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Nne zina Km. 1,034.6. Miradi iliyokamilika ni kama ifuatavyo: Singida – Shelui (km 110), Shelui – Igunga – Nzega (km108), Nzega – Ilula (km 138), Muhutwe – Kagoma (km 24), Nangurukuru – Mbwemkuru – Mingoyo (km 190), Mkuranga – Kibiti (km 121), Pugu – Kisarawe (km 3.6), Chalinze – Morogoro – Melela (km 129), Tunduma – Songwe (km 71), Kyabakari – Butiama (km 11.4), Dodoma – Morogoro (256), Dodoma - Manyoni (km 127), Buzirayombo - Kyamyorwa (km 120) na Buzirayombo – Geita (km 100).

Mheshimiwa Spika, miradi 5 iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo: Ujenzi wa sehemu ya Manyoni - Isuna (Km 54) unaendelea ambapo jumla ya kilomita 34 za barabara ya lami zimekamilika; Kuhusu mradi wa Kagoma-Lusahunga (Km 154) mkataba mpya ulitiwa saini mwezi Juni, 2009 na mpaka sasa kilometa 15 zimejengwa kwa kiwango cha lami; Mradi wa Tabora – Kaliua – Malagarasi – Uvinza – Kigoma (km 422):-

(i) Sehemu ya Tabora-Urambo-Kaliua (km 126): zabuni za kazi za ujenzi zimetangazwa mwezi Aprili, 2010 kwa sehemu ya kutoka Tabora hadi Ndono (km 42) na Ndono hadi Urambo (km 48);

(ii) Sehemu ya Kaliua-Malagarasi-Ilunde (km 156): Juhudi za kutafuta fedha za kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami zinaendelea;

(iii) Daraja la Malagarasi na Barabara zake (km 48): Taratibu za kumpata Mkandarasi wa Ujenzi wa Daraja zinaendelea chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea

Kusini. Fedha zilizopo zinatosheleza ujenzi wa daraja tu na sasa serikali inaendelea na mazungumzo ya kupata fedha zaidi ili barabara za viungio nazo zijengwe;

(iv) Sehemu ya Ilunde-Uvinza-Kidahwe (km 104): Mkataba wa mkopo kutoka ABU DHABI kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa km 77 umesainiwa Oktoba, 2009. Uchambuzi wa zabuni ili kupata mkandarasi uko kwenye hatua za mwisho na inatarajiwa kazi za ujenzi zitaanza katika mwaka wa fedha 2010/2011.

(v) Sehemu ya Kidahwe – Kigoma (km 36): Mkandarasi amekamilisha kujenga jumla ya km 35 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ni:-

(i) Usagara - Chato - Biharamulo (km 220)*:* ambapo sehemu ya Usagara - Sengerema - Geita (km 92), ujenzi unaendelea na kiasi cha kilometa 78 zimekamilika, sehemu ya barabara kutoka Geita – Bwanga (km70) zimejengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami. Sehemu ya Bwanga - Biharamulo (km 69), Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, na

(ii) Ndundu – Somanga (Km 60): Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami unaendelea. Hivi sasa ujenzi wa makalvati na tuta umefikia asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu kuendelea kuimarisha barabara nchini zitakazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami; Makao Makuu ya Mikoa yote pia kwa barabara za lami na kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya zote kwa barabara zinazopitika wakati wote kwa ajili ya ustawi wa uchumi wa nchi yetu na jamii kwa ujumla. Hadi sasa nchi jirani zilizokwishaunganishwa na nchi yetu kwa barabara za lami ni 7 kati ya 8 ambazo ni Zambia na DRC eneo la Tunduma, Malawi eneo la Kasumulo, Uganda eneo la Mutukula, Kenya eneo la Sirari na Namanga, Burundi eneo la Kobero na Rwanda eneo la Rusumo. Jitihada za kuunganisha nchi yetu na Msumbiji kwa barabara ya lami kupitia Daraja la Umoja zinaendelea.

Pamoja na nchi yetu kuunganishwa kwa barabara za lami na nchi jirani, kuna miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa inayolenga kuboresha usafirishaji kwa njia ya barabara kati ya nchi yetu na nchi jirani. Miradi hiyo ni pamoja na barabara zifuatazo: Arusha – Namanga (km105), ujenzi unaendelea kwa kiwango cha lami, Tanga – Horohoro (km 65), Mkataba wa ujenzi ulitiwa saini Disemba, 2009 na tayari kazi zimeanza, Mwandiga – Manyovu (km 60), ujenzi umeanza Disemba, 2008 na kiasi cha kilometa 20 zimekamilika na Masasi – Mangaka – Mtambaswala (km 119) itakayounganisha nchi yetu na Msumbiji upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Sehemu ya Masasi – Mangaka (km 54) inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami kwa msaada kutoka Serikali ya Japan na kiasi cha kilometa 32 zimekamilika. Aidha, usanifu wa Mangaka – Mtambaswala (km 65) umekamilika. Serikali ya Tanzania na Msumbiji zinaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa sehemu ya Mtambaswala – Mueda (Msumbiji) kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi za jirani zimeunganishwa na barabara za lami, Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi waishio kandokando ya barabara hizo kutumia fursa hiyo ili kuibua rasilimali zilizopo kwa kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili Sekta ya Miundombinu iendelee kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa nchi, Serikali imeunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote nchini kwa barabara za lami isipokuwa mikoa minne tu ambayo ni Rukwa, Kigoma, Tabora na Manyara. Mipango ya kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa hii ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa: Maandalizi ya kuanza ujenzi wa Barabara ya Tunduma – Sumbawanga itakayounganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Rukwa na Mbeya kwa msaada wa fedha toka Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la Changamoto ya Milenia *(Millenuim Challenge Corperation - MCC)* yanaendelea. Kazi zinatarajiwa kuanza Julai, 2010. Kwa sehemu ya Laela – Sumbawanga, sehemu kati ya Tunduma hadi Laela, mchakato wa kuwapata makandarasi upo hatua za mwisho.

Mkoa wa Kigoma: Ujenzi wa Barabara ya Kigoma - Tabora utakaounganisha Makao Makuu ya Mikoa ya Tabora na Kigoma upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama nilivyoeleza katika aya ya 12 ya hotuba yangu.

Mkoa wa Tabora: Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Itigi - Manyoni itakayounganisha Mikoa ya Tabora na Singida upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mchakato wa kupata makandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara kati ya Tabora – Nyahua na Manyoni - Itigi - Nyahua upo hatua za mwisho.

Mkoa wa Manyara: Ujenzi wa Barabara ya Singida - Babati - Minjingu kwa kiwango cha lami itakayounganisha Mikoa ya Manyara, Arusha na Singida unaendelea. Hivyo, Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara (Babati), yatakuwa yameunganishwa na Mikoa ya Singida na Arusha.

Barabara zote zinazounganisha Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa hivi sasa zinapitika majira yote ya mwaka isipokuwa Wilaya za Makete na Ludewa ambazo bado zinapitika kwa tabu wakati wa masika. Juhudi zinaendelea kufanywa ili kuhakikisha kwamba, barabara za wilaya hizi zinaboreshwa ili ziweze kupitika majira yote ya mwaka. Wizara imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa tano kwenye Barabara ya Njombe – Makete kwa kuanzia Makete. Aidha, maeneo korofi yote kwenye barabara hii yanaendelea kuimarishwa kwa kiwango cha changarawe.

Kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo: Tunduma – Sumbawanga; Marangu – Tarakea – Rongai; Minjingu – Babati – Singida; Rujewa – Madibira – Mafinga; Mbeya – Chunya – Makongorosi; Msimba – Ikokoto – Mafinga; Arusha – Namanga; Tanga – Horohoro na ukarabati wa Barabara ya Kilwa (Dar es Salaam), Barabara ya Mandela (Dar es Salaam) na Barabara ya Sam Nujoma (Dar es Salaam).

Mheshimiwa Spika, miradi mipya ya barabara iliyoainishwa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami ni kumi na mmoja. Kazi ya ujenzi imeanza katika miradi yote isipokuwa mmoja tu. Kati ya miradi hiyo ambayo ujenzi wake umeanza katika kipindi cha mwaka 2005 - 2010, miradi miwili imekamilika ambayo ni Barabara za Sam Nujoma na Barabara ya Kilwa katika Jiji la Dar es Salaam. Ujenzi wa barabara kwa miradi hii mipya imezalisha barabara za lami zenye urefu wa jumla ya km 161.1. Miradi iliyobaki ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi kwa kiwango cha lami. Miradi hiyo ni pamoja na Tunduma – Sumbawanga; Marangu – Tarakea – Rongai; Minjingu – Babati – Singida; Rujewa – Madibira – Mafinga; Mbeya – Chunya – Makongorosi; Msimba – Ikokoto – Mafinga; Arusha – Namanga; Tanga – Horohoro na ukarabati wa Barabara ya Mandela (Dar es Salaam).

Mheshimiwa Spika, Marangu – Tarakea – Rongai (km 98):-

(i) Tarakea – Rongai – Kamwanga (km 32) - Kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami imekamilika;

(ii) Rombo Mkuu - Tarakea (km 32) - Jumla ya km 25 za barabara zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami;

(iii) Marangu - Rombo Mkuu - Mwika - Kilacha (34 km), kazi ilianza Juni, 2008 baada ya kusitishwa kwa mkataba wa mkandarasi wa kwanza kutokana na kushindwa kutimiza majukumu yake ya kimkataba. Hivi sasa ujenzi wa barabara hii umekamilika kwa asilimia 70; Nelson Mandela (km 15.6), utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 60; Arusha – Namanga (km 105) ujenzi kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 25; Mbeya – Chunya – Makongolosi (km112) Mkataba wa ujenzi wa barabara hii sehemu ya Mbeya – Lwanjilo (km 36) kwa kiwango cha lami umesitishwa tangu Mei, 2009 kutokana na utendaji usioridhisha wa Mkandarasi. Kazi zilizotekelezwa kabla ya kusitishwa mkataba ni kusafisha eneo la barabara asilimia 50 na ujenzi wa tuta la barabara asilimia 33. Mkandarasi mwingine atatafutwa baada ya kesi iliyoko mahakamani kukamilika.

Msimba – Ikokoto – Mafinga (km 124), jumla ya km 45 zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami. Kazi ya ujenzi inaendelea na inatarajiwa kukamilika Septemba, 2010; Tunduma – Sumbawanga (km 224.5), Mhandisi Msimamizi wa barabara hii amepatikana Septemba, 2009. Barabara hii imegawanywa katika sehemu tatu, sehemu hizo ni Tunduma – Ikana (km 63), Ikana – Laela (km 64) na Laela – Sumbawanga (km 98). Barabara hii inajengwa kwa fedha za MCC na tayari mkandarasi kwa sehemu ya Laela – Sumbawanga amepatikana na anajiandaa kuanza kazi. Tanga – Horohoro (km 65), Mkataba wa ujenzi ulitiwa saini Disemba, 2009 na ujenzi rasmi ulianza Aprili 2010. Minjingu – Babati – Singida (km 224), Mkataba wa kuanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ulisainiwa Januari, 2009. Kazi za ujenzi zinaendelea vizuri. Rujewa – Madibira – Mafinga (km 151), kazi ya usanifu na uandaaji wa michoro ya madaraja pamoja na kuandaa vitabu vya zabuni imekamilika; hatua inayofuata sasa ni ya kupata mkandarasi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

Kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu barabara zifuatazo kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami: Maganzo – Maswa – Bariadi – Mkula – Lamadi; Babati – Dodoma – Iringa; Sumbawanga – Kigoma – Nyakanazi; Musoma – Fort Ikoma; Korogwe – Handeni – Kilosa – Mikumi; Nzega – Tabora – Sikonge – Chunya; Mtwara – Masasi – Songea – Mbamba Bay; Manyoni – Itigi – Tabora; Ipole – Mpanda – Kigoma na Bagamoyo – Saadani.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyoainishwa kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu ni kumi. Miradi yote iliyoainishwa imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu isipokuwa miradi miwili tu ambayo kazi ya upembuzi na usanifu inaendelea. Kati ya miradi hiyo, ujenzi umeanza katika miradi mitatu. Maelezo ya kina ya miradi hiyo ya barabara ni kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Maganzo – Maswa – Bariadi – Mkula – Lamadi (km 171): Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Bariadi – Lamadi katika barabara hii ulisainiwa Septemba, 2009. Mkandarasi yupo katika kipindi cha matayarisho ya kuanza kazi.

(ii) Barabara ya Babati – Dodoma – Iringa (km 530), sehemu ya Babati – Dodoma (km 265): Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Mkataba wa ujenzi wa barabara hii sehemu ya Dodoma - Mayamaya (km 43.65) umesainiwa Mei 2010 na hivi sasa mkandarasi amekusanya vifaa vya kazi tayari kuanza kazi. Sehemu ya Babato – Bongea (km 19.2) pamoja na Daraja la Kolo mikataba ya ujenzi pia imesainiwa. Aidha, sehemu iliyobaki (km 188.5) Serikali ya Japan imeonesha nia ya kusaidia ujenzi kwa kiwango cha lami. Dodoma – Iringa (km 265): Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Mkopo wa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo (JICA) kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiii ulisainiwa Oktoba, 2009. Kazi za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zitaanza katika mwaka wa fedha 2010/2011.

(iii) Barabara ya Sumbawanga – Kigoma – Nyakanazi (km 800): Kazi ya kufanya usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara sehemu ya Mpanda – Kigoma – Nyakanazi (km 562) imekamilika. Aidha, Mkataba wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami sehemu ya Sumbawanga – Kanazi (km 75) na Kanazi - Chizi – Kibaoni (km 76.6) umesainiwa Juni, 2009. Kazi za ujenzi kwa sehemu ya barabara zimeanza.

(iv) Barabara ya Musoma – Fort Ikoma Gate (km 140): Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika Mei, 2006. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

(v) Barabara ya Korogwe – Handeni – Kilosa – Mikumi (km 363): Usanifu wa kina na matayarisho ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii umekamilika. Aidha, mikataba ya ujenzi kwa ajili wa barabara hii sehemu ya Korogwe – Handeni (km 65), Handeni – Mkata (km 54), Dumila – Rudewa (km.45) na Magole –

Turiani (km 49) ilisainiwa Juni, 2009. Makandarasi wameanza kazi za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

(vi) Barabara ya Nzega – Tabora – Sikonge – Rungwa - Chunya (km 679): Usanifu wa kina na matayarisho ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi yalikamilika Januari, 2010. Aidha, sehemu ya Nzega - Tabora (km 116) mchakato wa kumpata mkandarasi upo hatua za mwisho na hivyo kazi za ujenzi rasmi zinatarajiwa kuanza Agosti 2010.

(vii) Barabara ya Mtwara – Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 826): Masasi – Mangaka (km 54), ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Masasi – Matumbushi – Nangalamo (km 32.5) umekamilika. Kazi zimeanza katika sehemu iliyobaki ya kilometa 22 kutoka Nangalamo hadi Mangaka. Mangaka – Tunduru - Namtumbo (km 331), Serikali kwa kutumia fedha za ndani itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Mangaka – Tunduru (km 146) kuanzia mwaka wa fedha 2010/11. Kuhusu sehemu ya Tunduru – Namtumbo (km 194), usanifu wa kina umekamilika na maandalizi ya kupata mkandarasi wa kujenga sehemu hii ya barabara yameanza kwa fedha za mkopo wa ADB na mkopo toka Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la JICA. Namtumbo - Songea – Mbamba Bay (km 235), usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za Zabuni umekamilika. Mhandisi Msimamizi wa barabara hii amepatikana Septemba, 2009. Mkataba kwa ajili ya ujenzi kwa sehemu ya Namtumbo – Songea (km 67) umesainiwa mwezi Mei 2010 na Peramiho – Mbinga (km 78) mkataba wa ujenzi unatarajiwa kusainiwa mwezi Julai 2010. Ujenzi unatumia fedha za MCC.

(viii) Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 264): Mchakato wa kupata makandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa sehemu ya Tabora – Nyahua (km 80) na Manyoni – Itigi – Chaya (km 85) upo katika hatua za mwisho.

(ix)Barabara ya Ipole – Tabora - Mpanda (km 338): Mkataba wa kufanya usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni za barabara hii sehemu ya Mpanda - Ipole - Tabora (km 359) umesainiwa Juni, 2009. Mkataba huu ni wa miezi 20 na hivyo kazi itakamilika mwezi Aprili, 2011.

(x) Barabara ya Bagamoyo – Saadani - Tanga (km 118): Kazi ya usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni ya barabara hii yanaendelea.

Kuhimiza maandalizi na ujenzi wa Daraja la Kigamboni chini ya Uongozi wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kuunganisha Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia maandalizi ya ujenzi wa daraja la Kigamboni ambalo utekelezaji wake upo chini ya Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Mtaalam Mshauri aliyeajiriwa na NSSF kuandaa nyaraka za zabuni na kumpata Mbia mwenza kutoka sekta binafsi atakamilisha nyaraka za zabuni hizo mwezi Agosti,

2010. Nyaraka hizo zitasambazwa kwa wabia sita waliopatikana ili waoneshe uwezo wao kifedha na hatimaye ateuliwe mbia mmoja atashirikiana na NSSF kugharamia ujenzi wa daraja la Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, Kivuko kipya cha Kigongo - Busisi kinachoitwa M.V. Misungwi chenye uwezo wa kubeba tani 250 kimepatikana na kinafanya kazi tangu Mei 2008.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa daraja jipya la Mpiji ambalo litawezesha njia mbadala ya Dar es Salaam – Tanga umekamilika.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa Nyaraka za Zabuni kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kilombero zimekamilika Desemba, 2009. Ujenzi wa daraja hili utaanza katika mwaka 2010/11. Kuhusu daraja la Mto Mwatisi, ujenzi wa Daraja umeanza Agosti, 2009 na umefikia kiwango cha asilimia 25 na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, usanifu na ujenzi wa daraja la Mto Ruvu umekamilika Septemba, 2008 na kufunguliwa rasmi na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kushirikisha Sekta binafsi. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kukamilisha Sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kupitishwa kwa sheria inayohusiana na masuala haya. Aidha, Serikali itatumia mwongozo na kanuni hizi kuhakikisha kuwa Sekta Binafsi inashirikishwa kikamilifu katika ujenzi na matengenezo ya Miundombinu ya Uchukuzi kwa mfumo wa Jenga, Endesha na Kabidhi (BOT).

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Umoja lenye urefu wa meta 720 ambao unajumuisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa km 5 pande zote za daraja, ulikamilika na kufunguliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Mheshimiwa Armando Emilio Guebuza katika Kijiji cha Mtambaswala, Mtwara. Ufunguzi huu ulifanyika tarehe 12 Mei, 2010. Daraja hili linategemewa kuongeza fursa za kibiashara kati ya nchi hizi mbili pamoja na kukuza ukanda wa maendeleo wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa programu ya Taifa ya Usafiri Vijijini. Suala la uboreshaji wa huduma za usafiri vijijini ni muhimu kwa kutambua kwamba, asilimia 80 ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini ambapo sehemu kubwa ya shughuli za kilimo hufanyika. Kutokana na gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya barabara, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeendelea kuhimiza matumizi ya teknolojia stahili ya nguvu kazi ambayo inatumia gharama nafuu. Aidha, Wizara kupitia Chuo cha Matumizi Stahili ya Nguvu Kazi imeendelea kutoa mafunzo kwa Makandasi wa Nguvu kazi pamoja na Wahandisi kutoka Halmashauri mbalimbali na Sekta Binafsi. Mafunzo hayo yametolewa pia kwa wanawake wanaofanya kazi kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi na

wanaotarajia kuanzisha kampuni za ukandarasi kwa kutumia teknolojia Stahili ya Nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 45: Usafiri na Uchukuzi. Serikali imeendelea kuboresha huduma za Usafiri na Uchukuzi kwa kushirikisha Sekta Binafsi na kuboresha miundombinu ya uchukuzi. Maboresho haya yanaenda sambamba na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 ambayo ilielekeza sekta hii kuchukua hatua zifuatazo:-

Kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa lengo la kulipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa bidhaa na abiria wa ndani na wa nchi jirani. Pia, Shirika litaendelezwa kama mhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa Kati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utendaji usioridhisha wa Menejimenti ya TRL, mwezi Machi, 2010 Serikali ilifanya uamuzi wa kusitisha mkataba wa uendeshaji wa TRL kwa kununua hisa asilimia 51 za RITES. Hatua zinazoendelea ni Serikali kufanya mazungumzo na RITES ili kuweza kuzinunua hisa hizo. Baada ya kukamilisha ununuzi wa hisa za RITES, Serikali itaendesha shughuli zote za reli ya kati mpaka hapo atakapopatikana Mbia mwingine.

Serikali inaendelea kufanya matengenezo na ukarabati wa njia ya reli baada ya kuharibiwa na mvua nyingi zilizonyesha mwezi Disemba, 2009 na Januari, 2010 na hasa maeneo ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuliimarisha Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA) ili liweze kuhimili kwa uwezo mkubwa zaidi majukumu ya kuboresha huduma kwa bidhaa na abiria na kusaidia shughuli za uendelezaji wa mpango wa eneo la Ukanda wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Zambia kwa pamoja zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuimarisha TAZARA. Disemba, 2009, Mawaziri wenye dhamana ya Reli ya TAZARA kutoka Tanzania na Zambia walifanya ziara ya kikazi nchini China kwa lengo la kuwasilisha maombi ya msaada wa fedha na ufundi kwa ajili ya kuendesha shughuli za TAZARA. Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilikubali maombi hayo kimsingi na kutoa mapendekezo ambayo yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo, Itifaki ya 14 ya mkopo nafuu wa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 39.3 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilisainiwa tarehe 19 Disemba, 2009. Mkopo huu ni kwa ajili ya kuimarisha TAZARA kwa kuiongezea uwezo wa injini, mabehewa, nyenzo mbalimbali za uendeshaji na mafunzo kwa wafanyakazi. Katika makubaliano hayo, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China pia imefuta nusu ya deni la ujenzi wa Reli ya TAZARA na imeahidi kutuma wataalam kuja kutathmini matatizo na mahitaji ya TAZARA kwa nia ya kuboresha huduma za shirika. Serikali za Tanzania na Zambia kwa upande wao zinaendelea kuandaa mikakati inayofaa

kuchukuliwa ili kuimarisha utendaji wa TAZARA. Kuimarika kwa Reli ya TAZARA kutachochea maendeleo ya miradi iliyoko katika ukanda wa maendeleo ya kiuchumi wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya za Arusha – Musoma, Isaka – Kigali na eneo la Ukanda wa Mtwara, ambayo itaunganisha Bandari ya Mtwara, Songea, Mbamba Bay, Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa reli hizi katika kukuza uchumi wa nchi yetu, Serikali imeweka miradi hii katika vipaumbele vya miradi ya maendeleo. Aidha, reli hizi ni kati ya miradi iliyo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Mpango Kabambe wa Reli *(East African Railway Master Plan)*, wenye lengo la kuboresha huduma za uchukuzi za Afrika Mashariki.

Katika ujenzi wa reli ya Arusha – Musoma, Serikali za Tanzania na Uganda zinaandaa mkakati wa pamoja kutekeleza ujenzi wa reli hii ili isaidie kusafirisha mizigo ya Uganda na Ukanda wa Kaskazini kupitia Bandari ya Tanga. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa reli mpya kati ya Musoma na Arusha, ujenzi wa reli mpya kati ya Kange na Bandari mpya ya Mwambani (Tanga), ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani, uboreshaji wa reli kati ya Tanga na Arusha na upanuzi wa Bandari ya Musoma.

Kuhusu Reli ya Isaka – Kigali, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa reli ya Isaka – Kigali/Keza – Gitega – Musongati ilikamilika Septemba 2009. Kazi inayoendelea ni kufanya maandalizi ya usanifu wa kina wa reli hii. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imekubali kutoa fedha jumla ya *"units of accounts"* milioni 1.66, sawa na Shilingi za Kitanzania bilioni 3.9 kwa ajili ya kufanya usanifu huo. Kamati ya Wataalam inaendelea na mchakato wa kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya usanifu wa mradi huu.

Ujenzi wa reli itakayounganisha Bandari ya Mtwara, Songea, Mbamba Bay, Mchuchuma na Liganga ni sehemu ya Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara. Juhudi za kuwatafuta wawekezaji katika maeneo ya Mchuchuma na Liganga pamoja na ujenzi wa reli hii muhimu zimeanza chini ya uratibu wa Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC).*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha Bandari za Kigoma na Kasanga ili ziweze kuhudumia vyema wakazi wa maeneo yanayozunguka Ziwa Tanganyika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa gati mbili katika Bandari ya Kasanga ili kuwezesha meli mbili kutia nanga kwa wakati mmoja na ukarabati wa barabara za kuingia bandarini. Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2010. Katika bandari ya Kigoma, kazi ya kuondoa mchanga na kuongeza kina cha maji *(dredging)* imekamilika. Kazi ya kujenga cherezo *(docking yard)* inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kuvutia uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na uchukuzi wa reli, barabara, maji na anga katika Kanda za Maendeleo ili kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani na kuwafanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na

huduma zitakazozalishwa. Aidha, uwekezaji katika kanda hizi utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kuendeleza wajibu wake wa kuzihudumia nchi jirani zisizo na bandari.

Mheshimiwa Spika, katika kutumia nafasi ya Tanzania Kijiografia, Serikali imechukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuwavutia wawekezaji katika Sekta ya Miundombinu kwa lengo la kukuza uchumi wetu. Wizara inaendelea kutekeleza Mpango wa miaka kumi ya Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi nchini, Mpango Kabambe wa Bandari *(Port Master Plan)* na Mpango Kabambe wa Kukuza Usafiri wa Anga *(Civil Aviation Master Plan).* Mipango hii imebainisha miradi mbalimbali ya kipaumbele inayolenga kuendeleza na kupanua huduma za uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia Wakala za Uwezeshaji wa Biashara na Uchukuzi katika Ukanda wa Kati *(Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency – TTFA)* na Ukanda wa TANZAM *(Dar es Salaam Corridor)* inaweka mazingira mazuri ya biashara katika Sekta ya Uchukuzi na kuratibu huduma za usafirishaji. Aidha, Sekretariati ya Kudumu ya TTFA imeshaanza kazi kwa msaada wa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Sekretariati ya TANZAM *(Dar es Salaam Corridor)* kwa ufadhili wa fedha kutoka Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID)* na fedha kutoka mashirika ya umma na binafsi kutoka nchi wanachama wa TANZAM. Hatua hii itawezesha kuongeza ufanisi wa shughuli za kibiashara kupitia nchini mwetu kwenda nchi jirani na hivyo, kuvutia wafanyabiashara wengi zaidi kutumia miundombinu yetu ya uchukuzi ikiwemo Bandari ya Dar es Salaam kupitishia mizigo yao.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuutengenezea mazingira mazuri ya kibiashara Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Dar es Salaam yatakayoweza kuundeleza kuwa kiungo *(hub)* cha usafiri wa anga kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mkakati wa kuandaa mazingira mazuri ya kibiashara ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere ili kiwe kiungo *(hub)* cha usafiri wa anga kitaifa, kikanda na kimataifa. Kazi zifuatazo zinaendelea kufanyika hivi sasa; kukamilisha utekelezaji wa awamu ya pili ya ukarabati na ujenzi wa barabara za viungio na maegesho, barabara ya kuruka na kutua ndege, kuweka taa za kuongozea ndege *(Apron Ground Lights-AGL),* ukarabati wa maegesho ya ndege ya *Terminal I,* maegesho ya ndege za mizigo (*cargo apron*) pamoja na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa jengo jipya la watu mashuhuri *(VIP Lounge)* eneo la *Terminal II* imekamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja na usanifu wa ujenzi wa jengo jipya la abiria *(Terminal III),* usanifu wa ujenzi wa jengo jipya la mapokezi ya ugeni wa kitaifa *(State Reception Building),* kukamilisha uhamishaji wa wananchi waliojenga ndani ya eneo la kiwanja ili kupisha upanuzi ambapo mpaka sasa wakazi 1,221 wa Kipawa wamehamishwa. Vile vile taratibu za kupata eneo la Kigilagila zimeanza zitakazowezesha ulipaji wa fidia wakazi wa eneo hili na kuwahamisha. Kazi nyingine ni kuweka mitambo ya kisasa ya ukaguzi wa abiria *(check in system)* na mitandao ya habari na mawasiliano. Aidha, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa mtandao wa habari na mawasiliano *(ICT Network)* imekamilika.

Mheshimiwa Spika, kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe na kuimarisha viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa awamu ya tatu na ya mwisho ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe unaendelea vizuri. Ujenzi wa kiwanja hiki unategemewa kukamilika mwezi Machi 2011. Kazi zinazofanyika ni pamoja na kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege na barabara za viungo *(Taxi ways).* Aidha, jengo la abiria na ununuzi wa vifaa vya ukaguzi *(x-ray machines)* ni sehemu ya mradi huu.

Kuhusu viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora, Serikali itakarabati viwanja hivyo katika mwaka wa fedha wa 2010/11 kwa kujenga barabara za kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha lami na hivyo kuviwezesha kutumika majira yote ya mwaka. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, Serikali kwa kushirikana na Benki ya Dunia, imekamilisha kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja hiki. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mabasi ya Usafiri wa haraka katika jiji la Dar es Salaam umeendelea kutekelezwa kwa awamu. Ili kuanza ujenzi wa miundombinu ya Mradi huu, tayari Mtaalam Mshauri atakayesimamia ujenzi wa miundombinu hiyo ameajiriwa na kuanza kazi. Mchakato wa kuwapata makandarasi wa ujenzi umeanza Oktoba, 2009 na inatarajiwa kuwa kazi za ujenzi wa miundombinu zitaanza mwaka 2011. Aidha, rasimu ya zabuni ya kampuni mbili kwa ajili ya kutoa huduma za uendeshaji, ukusanyaji nauli na menejimenti ya fedha kwa awamu ya kwanza ya DART zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, suala la kuimarisha huduma za hali ya hewa nchini kwa kutumia vyombo vya kisasa ni muhimu kwa usalama na maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla.

Hivi sasa Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu ipo katika mchakato wa kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa. Sera hii ndiyo itakayokuwa mwongozo katika uimarishaji, uboreshaji na utoaji wa huduma ya hali ya hewa nchini. Katika kipindi cha 2009/2010, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za hali ya hewa na utoaji wa huduma za hali ya hewa ambazo ni pamoja na utabiri wa kila siku wa hali ya hewa, utabiri wa hali ya hewa wa msimu na tahadhari ya hali mbaya ya hewa hususan majanga ya asili kama ukame, mafuriko na vimbunga.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliweza kuongeza vituo vikuu vya utabiri wa hali ya hewa *(Synoptic Stations)* kutoka 26 (2008/09) hadi 28 (2009/10), vikijumuisha vituo vya Kilwa Masoko na Mpanda, kuongeza vituo vya hali ya hewa na kilimo kutoka 11 hadi 13 vikijumuisha vituo vya Matangatuani (Pemba) na Mbozi Mkoani Mbeya na kuongeza vituo vya mvua kutoka 600 hadi 1400. Serikali pia kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea na ununuzi wa mitambo na vifaa mbalimbali vya hali ya hewa ikiwemo mitambo ya utabiri *(Synergie System)* na *(Hydrogen Plant)* na mifumo ya utabiri ya *Weather Research Forecasting- WRF* na *High Resolution Model- HRM.*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na Serikali kununua *radar* ya hali ya hewa. Kazi inayoendelea ni ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu katika eneo litakalotumika kama Kituo cha Radar cha Hali ya Hewa nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam. Taratibu za ununuzi wa *radar* hiyo zimekamilika na inatarajiwa kuwasili nchini Julai, 2010 na kuanza kufanya kazi Agosti, 2010 baada ya kufungwa. Matumizi ya *radar* za hali ya hewa katika utoaji wa huduma ni muhimu kwani huongeza usahihi wa taarifa za hali ya hewa.

Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa imeongeza miundombinu ya mawasiliano na uchambuzi wa taarifa za hali ya hewa katika Kituo Kikuu cha Taifa cha Utabiri wa Hali ya Hewa ili kuhakikisha kwamba taarifa na tahadhari za matukio ya hali ya hewa mbaya yanapokelewa na kusambazwa kwa taasisi zinazohusika na wananchi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali imeendelea kulisaidia Shirika la Ndege la Tanzania ili lichukue nafasi yake ipasavyo ya kuwa Shirika la Ndege la Taifa *(National Flag Carrier)* kwa lengo la kuliwezesha Taifa kufaidika zaidi na mapato yatokanayo na Utalii katika kujenga uchumi wa Taifa letu kwa kutoa fedha ili kuwezesha kulipia gharama mbalimbali ikiwemo mishahara na mafuta. Ili kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa Kampuni, Novemba 2009, Serikali ilitoa shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya mafao ya wafanyakazi 155 waliopunguzwa kazi. Aidha, Serikali imeendelea kuisaidia Kampuni kwa kulipa madeni mbalimbali ya Kampuni. Kwa sasa Serikali inafanya mazungumzo na wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuwekeza ndani ya Kampuni. Lengo ni kuliunda upya Shirika la Ndege la Taifa kwa kushirikisha Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, imeendelea na nia yake ya kutambua, kuthamini na kujali mahitaji mbalimbali ya watu wenye ulemavu. Wizara imekwishaelekeza kuwa, majengo yote ya Serikali yanayobuniwa yazingatie mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. Utekelezaji wa agizo hili unaendelea kusimamiwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Aidha, Wizara iko katika mchakato wa kuandaa rasimu ya Sheria ya Kudhibiti na Kusimamia Majengo nchini ambayo itahimiza juu ya ujenzi wa majengo kwa kuzingatia usalama wa watumiaji na mahitaji ya watu wenye ulemavu. Hatua nyingine zinazochukuliwa ili kuboresha mazingira kwa ajili ya walemavu ni kuendelea kujenga mwamko kwa umma wa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemamavu katika majengo ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina nia ya kuboresha mazingira ya kuishi kwa watumishi wake kwa kuwapatia nyumba bora. Wizara kupitia Wakala wa Majengo ya Serikali imeendelea kujenga nyumba za kuwauzia watumishi wa Umma. Katika kipindi cha 2005 hadi 2010, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu imejenga jumla ya nyumba 527 kwa ajili ya kuwauzia Watumishi wa Umma na nyumba 185 kwa ajili ya kuishi Viongozi mbalimbali wa Kitaifa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kuwauzia Watumishi wa Umma na matumizi ya Viongozi wa Kitaifa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kulingana na malengo na mikakati tuliyojiwekea, utendaji wa Sekta ya Miundombinu katika maeneo ya uchukuzi, ujenzi na hali ya hewa umeendelea kuimarika. Mafanikio hayo yanatokana na uboreshaji wa miundombinu na huduma zinazotolewa na Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Utendaji wa sekta umeendelea kuzingatia Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA, Mkakati wa Kushirikiana na Wahisani (JAST), Malengo ya Milenia (MDGs), Sera za Kisekta, Mikataba tuliyoridhia, makubaliano na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yanayohusu sekta zetu pamoja na utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Jumla ya miradi ya barabara 26 yenye urefu wa km 2,237 ilitekelezwa, miradi ya ujenzi wa barabara 28 yenye jumla ya urefu wa km 2,208 inaendelea kutekelezwa, miradi 7 yenye urefu wa jumla ya km 1,562 inaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na matayarisho ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi. Miradi iliyokamilika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ni 11 yenye urefu wa jumla ya km 2,745.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla barabara nchini zimeendelea kufanyiwa matengenezo katika viwango vya lami na changarawe ili ziweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka.

Kuhusu ujenzi na ukarabati wa Barabara Kuu na za Mikoa, jumla ya km 218 za Barabara Kuu zilifanyiwa ukarabati katika kiwango cha lami na km 156 kujengwa katika kiwango cha lami. Aidha, jumla ya km 42 za barabara za Mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na km 591 zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe. Kuhusu ujenzi wa madaraja, Serikali ilikamilisha ujenzi wa madaraja 51 ikiwa ni pamoja na Daraja la Umoja linalounganisha nchi ya Tanzania na Msumbiji.

Kuhusu matengenezo ya madaraja, jumla ya madaraja 4,365 yalifanyiwa matengenezo ya kuzuia uharibifu *(Preventive Maintenance)* na madaraja 231 yalifanyiwa matengenezo makubwa katika Barabara Kuu. Katika barabara za Mikoa, jumla ya madaraja 4,020 yalifanyiwa matengenezo ya kuzuia uharibifu na madaraja 429 yalifanyiwa matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kutimiza azma yake, iliunda Kikosi Kazi cha kuandaa Mkakati wa makusudi wa kuendeleza Makandarasi Wazalendo. Rasimu ya Mkakati huo imekamilika Februari, 2010. Wizara inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya Mkakati huo. Lengo la Mkakati ni kukuza uwezo wa makandarasi wazalendo kwa kuwapa kazi kubwa ambazo kwa sasa wanapewa makandarasi wa kigeni. Makandarasi hao watasaidiwa kupata mitambo, wataalamu na amana za fedha na watafanya kazi chini ya uangalizi wa karibu wa wataalamu Washauri. Matarajio ya Serikali katika mradi huo wa miaka mitano ni kuwa na makandarasi wazalendo wanaoweza kushindana na makandarasi wa kigeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, ubora wa baadhi ya barabara nchini umekuwa hafifu kutokana na changamoto zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa Makandarasi. Ili kukabiliana na upungufu huo, Wizara kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi, Baraza la Ujenzi la Taifa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi, imeendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Makandarasi wa Kizalendo ili wasimamie na kutekeleza vizuri mikataba ya ujenzi na matengenezo ya barabara. Aidha, Wizara imekuwa ikihakikisha kuwa makandarasi wanakabidhi barabara baada ya ujenzi au ukarabati kukamilika na kwa kuzingatia viwango vilivyokubalika.

Mheshimiwa Spika, huduma za usafiri wa anga zimeendelea kutolewa kwa kiwango cha kuridhisha ingawa kulikuwa na changamoto zilizoikumba sekta hii. Changamoto hizo ni pamoja na mtikisiko wa uchumi duniani, kupanda kwa bei ya mafuta. Kampuni za ndege za ATCL na PrecisionAir ni wadau wakuu wa usafirishaji kwa njia ya anga ndani ya nchi, zikiunganisha miji mikubwa nchini na nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Pamoja na Kampuni hizi mbili, kuna Kampuni ndogo za ndani zinazotoa huduma ya usafiri wa anga kibiashara na kijamii kama vile Community Air Line, Zan Air na Coastal Travel ambazo hutoa huduma hasa kwa Sekta ya Utalii. Aidha, mashirika ya nje yamekuwa yakitoa huduma za usafiri kati ya nchi yetu na nchi mbalimbali. Huduma hiyo ya usafiri wa anga imekuwa ikitolewa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuingia mikataba mipya na kuipitia upya mikataba ya usafiri wa anga kati ya Tanzania na baadhi ya nchi. Lengo la mikataba hii ni kutoa fursa kwa kampuni za ndege nchini kutoa huduma za usafiri wa anga katika nchi hizo na kampuni za nchi hizo kutoa huduma nchini mwetu. Katika mwaka 2009/2010, mikataba mipya iliyotiwa saini ni kati ya Tanzania na Uturuki, Jordan na Bahrain. Mikataba iliyopitiwa upya kwa lengo la kuiimarisha ni ile ya Tanzani na Kenya, Afrika Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), iliendelea kusimamia na kudhibiti usalama wa usafiri wa anga nchini. Katika mwaka 2009/10, hakuna ajali iliyotokea inayohusu upotevu wa maisha ya binadamu. Mwezi Machi, 2010, ndege ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) aina ya Boeing 737-200 ilipata ajali ilipokuwa inatua kwenye kiwanja cha ndege cha Mwanza na kusababisha uharibifu mkubwa wa ndege. Aidha, kumekuwepo na matukio madogo ya kibinadamu yanayotokana na uhafifu wa miundombinu katika viwanja vilivyo kwenye mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, huduma za uchukuzi kwa njia ya Reli zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA). Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa miundombinu ya njia ya reli, vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo na ya abiria na usalama wa usafiri wa njia ya reli vinaboreshwa. Serikali ya Tanzania na Zambia zimefanikiwa kupata msaada wa fedha na ufundi kwa ajili ya kuboresha miundombinu na uendeshaji wa Reli ya TAZARA. Serikali za Tanzania na Zambia zinaendelea kutafuta mwekezaji au mwendeshaji binafsi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za TAZARA.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa TRL, katika kipindi cha 2009/2010 haukuwa wa kuridhisha kutokana na utendaji hafifu wa Menejimenti ya TRL, uchakavu na ubovu wa miundombinu ya njia ya reli pamoja na mabehewa ya mizigo na abiria. Utendaji wake uliendelea kuathiriwa zaidi na uharibifu wa njia ya reli uliotokana na mvua nyingi zilizonyesha kati ya Disemba, 2009 na Januari, 2010. Mvua hizi ziliathiri miundombinu ya reli na barabara. Katika harakati za kurudisha miundombinu katika hali yake ya kawaida, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 15.6 kwa ajili ya ukarabati wa reli. Ukarabati wa miundombinu umefikia hatua ya kuridhisha na kazi iliyobaki ni uimarishaji wa maeneo yaliyokarabatiwa hususan tuta na kingo za mto Mkondoa. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wataalam wa Wizara ya Miundombinu, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, RAHCO, TRL na Uongozi wa Mikoa ya Morogoro na Dodoma kwa kufanikisha ukarabati wa eneo lililoathirika na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri majini, Serikali iliendelea kutoa huduma za uchukuzi katika maeneo ya pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu. Lengo ni kuhakikisha kwamba, huduma zinazotolewa na bandari zetu zinakidhi matakwa siyo tu ya nchi yetu, bali pia ya nchi jirani. Njia hii ya uchukuzi inasaidia kukuza huduma za biashara katika nchi yetu na nchi za Rwanda, Burundi, DR Congo, Uganda, Zambia na Malawi. Kwa ujumla utendaji wa sekta hii ulikuwa wa kuridhisha kutokana na ukuaji kasi wa uchumi wetu na wa nchi jirani.

Ufanisi wa utoaji huduma katika Bandari ya Dar es Salaam uliongezeka kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya bandari, mfumo wa upokeaji na utoaji mizigo bandarini pamoja na kuongezeka kwa eneo la kuhifadhi makasha ndani na nje ya bandari baada ya kujengwa *ICDs* za makampuni na watu binafsi, kupunguza muda wa makasha kukaa bandarini na kupungua msongamano wa meli na mlundikano wa makasha katika bandari ya Dar es Salaam. Mafanikio mengine yanatokana na utendaji mzuri katika utoaji wa huduma wa bandari za Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa pamoja na bandari za Tanga na Mtwara.

Changamoto katika sekta hii ni uchakavu wa miundombinu ya bandari na kupungua kwa huduma za reli ambazo zimechangia kuchelewa kwa utoaji wa mizigo bandarini, hasa inayosafirishwa kwa njia ya reli na barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za hali ya hewa, Serikali kupitia Wakala wa Hali ya Hewa imeendelea kutoa huduma hizo pamoja na tahadhari dhidi ya hali mbaya ya hewa katika kiwango cha kuridhisha. Taarifa za hali ya hewa zimekuwa zikitolewa katika baadhi ya vyombo vya habari na magazeti kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kujua hali halisi na kutumia taarifa hizo kupanga mipango yao ya kilimo, ujenzi, usafiri na shughuli mbalimbali. Pamoja na huduma nzuri zilizotolewa, sekta hii ilikabiliwa na changamoto za ufinyu wa bajeti na ongezeko la watumiaji wa huduma za hali ya hewa linalotokana na kukua kwa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Pia wamejitokeza watoaji huduma za hali ya hewa ambao hawafuati taaluma, miongozo na viwango vinavyotakiwa. Serikali iko kwenye mchakato wa kutengeneza Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa itakayosimamia na kudhibiti sekta ndogo ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa majengo nchini imeendelea kujenga nyumba za Serikali kwa lengo la kuwauzia watumishi wake. Hata hiyo kumekuwa na changamoto kadhaa zinazotokana na zoezi zima la kuboresha makazi ya watumishi wa serikali.

Moja ya changomoto hizi ni uuzwaji wa nyumba katika maeneo ambayo nyumba hizo hazikutakiwa kuuzwa. Wizara imeendelea kusimamia mchakato wa kulimaliza tatizo hili kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Sekta kwa mwaka 2009/2010 na Malengo ya mwaka 2010/2011: Maelezo yaliyotangulia yanaonesha hali ya utendaji wa jumla wa Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na hali ya hewa kwa kipindi cha 2009/2010. Wizara ya Miundombinu kwa upande wake, imeendelea na jukumu lake la kusimamia Sera, kuendeleza miundombinu na utoaji huduma katika Sekta za Uchukuzi, Ujenzi na hali ya hewa.

Katika mwaka 2010/11, vipaumbele vimetolewa kwa kuzingatia miradi inayoendelea; miradi ambayo Serikali imeingia mikataba ya ujenzi; utekelezaji wa Sera za Kitaifa na Kimataifa, ahadi za Viongozi Wakuu wa nchi, ahadi za Serikali Bungeni na miradi inayofadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kueleza kwa kina kuhusu utendaji wa sekta katika kipindi cha mwaka 2009/10 na malengo kwa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, ubunifu na utekelezaji wa Sera za Sekta. Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera za Kisekta. Sera hizo ni Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003), Sera ya Taifa ya Ujenzi (2003) na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009). Aidha, Wizara imeendelea kukamilisha Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa pamoja na kuifanyia mapitio Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003) na Sera ya Ujenzi (2003). Sera hizi zinatumika kama miongozo ya kusimamia maendeleo ya sekta pamoja na kutoa taratibu za uwekezaji katika kufikia malengo ya muda wa kati na muda mrefu. Malengo hayo ni pamoja na kuweka lami kwenye Barabara Kuu zote ifikapo mwaka 2018, kuhakikisha kuwa barabara za Mikoa zinakuwa angalau katika kiwango cha changarawe au lami nyepesi na zinazopitika wakati wote ifikapo mwaka 2015. Malengo mengine ni kuhakikisha kuwa bandari zetu kuu zinahudumia mizigo tani milioni kumi ifikapo mwaka 2015.

Kuhusu usafiri wa anga, malengo ya muda wa kati yanayotekelezwa ni pamoja na kuishirikisha Sekta Binafsi ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi; na kukifanya kiwanja cha ndege cha Mwalimu Julius Nyerere kuwa kiungo *(hub)* cha usafiri wa anga katika Kanda. Kwa upande wa sekta ya reli, mkakati wa muda mfupi unaotekelezwa ni kuongeza uwezo wa reli kwa kuondoa reli yenye uzito mdogo (ratili 56.12 kwa yadi) na kuweka yenye uzito mkubwa (ratili 80 au zaidi kwa yadi).

Serikali ina mkakati wa muda mrefu wa kuiboresha reli ya kati kwa kuibadili njia yake toka kwenye muundo wa sasa wenye njia nyembamba na wenye uwezo mdogo *(metre gauge)* na kuifanya iwe pana *(standard gauge)* na yenye uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma zitolewazo na Kitengo cha Makasha katika Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza ushindani, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* kwa upande mmoja na Kampuni ya Hutchison Port Holdings Limited na Tanzania International Container Terminal Services (TICTS) kwa upande mwingine, walitiliana saini nyongeza ya Mkataba (Addendum No. 3) katika Mkataba wa Ukodishaji wa Kitengo cha kontena katika Bandari ya Dar es Salaam. Nyongeza ya Mkataba huo ilihusu kuondoa kipengele kinachoipa TICTS ukiritimba wa kuhudumia meli zinazobeba Makasha. Kufuatia uamuzi huo, sasa Wawekezaji na Waendeshaji mbalimbali wanaruhusiwa kuhudumia meli zinazobeba makasha katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utendaji usioridhisha wa Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Februari, 2010, Serikali iliamua kununua hisa zote za RITES kiasi cha asilimia 51 ndani ya TRL. Ili kufikia azma hiyo, Serikali ilitoa ridhaa ya kujadiliana na RITES ili kununua hisa hizo. Kwa mantiki hiyo, mkataba kati ya Serikali na RITES utafutwa na hivyo Serikali itamiliki Kampuni ya TRL kwa asilimia mia moja mpaka hapo atakapopatikana mwekezaji au mwendeshaji mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa TAZARA, Disemba, 2009, Mawaziri wenye dhamana ya Reli ya TAZARA walifanya ziara nchini China kwa madhumuni ya kusaini Itifaki ya 14 ya Ushirikiano wa Kiufundi na Kiuchumi kuisaidia TAZARA. Aidha, Mawaziri walijadili mapendekezo ya Serikali za Tanzania na Zambia ya kushirikisha sekta binafsi kutoka China kuendesha shughuli za TAZARA. Katika ziara hiyo, Serikali ya China ilikubali kutoa mkopo wenye masharti nafuu wa jumla ya RMBY milioni 270, sawa na USD milioni 39.3 kwa ajili ya kununua injini mpya za treni, mabehewa mapya ya mizigo, kufufua mabehewa ya mizigo na kukarabati injini za treni. Itifaki hii imeanza kutekelezwa Januari, 2010 na itakamilika baada ya miaka mitatu.

Kwa upande wa ushirikishwaji wa Sekta Binafsi kutoka China kuendesha shughuli za TAZARA, Serikali ya China itatuma vikundi viwili, kimoja cha wataalam wa kiufundi *(Technical Team)* na cha pili cha Wataalam wa Menejimenti *(Operational and Management Team)* kutoka Wizara ya Reli ya China kufanya tathmini ya hali halisi ya miundombinu ya reli na menejimenti ili kutoa uamuzi wa jinsi ya kurekebisha uendeshaji wa reli. Timu zote mbili zitaungana na wataalam kutoka Zambia na Tanzania kufanya kazi hiyo kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuiwezesha UDA kuwa na mtaji wa kujiendesha yenyewe. Wawekezaji mbalimbali wamekuwa wakijitokeza ili kuendesha UDA. Hata hivyo, wawekezaji hao wamekuwa hawakidhi viwango vinavyotakiwa na hivyo kushindwa kukabidhiwa uendeshaji wa Shirika.

Serikali ilimwajiri Mtaalam Mwelekezi wa kuandaa nyaraka muhimu kama vile thamani ya mali na kutafuta thamani ya hisa ili kukamilisha zoezi la uuzaji wa hisa za serikali katika Shirika la UDA.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA), Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuiwezesha UDA kuwa na mtaji wa kujiendesha yenyewe, hii ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mapendekezo Serikalini ya kufuta madeni ya muda mrefu ya UDA yenye thamani ya shilingi milioni 612.189 kwa lengo la kuboresha mezania ya Shirika ili iweze kupata fedha kutoka taasisi mbalimbali za kifedha. Aidha, kutokana na mapendekezo ya Bodi ya UDA kuhusu hatma ya shirika, Serikali iko katika majadiliano na mwekezaji ambaye amejitokeza kununua hisa za Serikali za aslimia 49. Kupatikana kwa mwekezaji kutawezesha UDA kuongeza uwezo wake wa kutoa huduma za usafiri Jijini Dar es Salaam na kushiriki katika mradi wa mabasi yaendayo kasi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imechukua hatua mbalimbali ili kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege (ATCL). Hatua hizo ni pamoja na Serikali kufanya uthamini wa kina wa mali za Kampuni ili kujua thamani yake, Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kulipa madeni ya ATCL na kufanya mazungumzo na Kampuni ya *China SONANGOL International Limited (CSIL)*, ambayo ilionesha nia ya kununua asilimia 49 ya hisa za Serikali katika shirika jipya la Ndege la Taifa badala ya kuwekeza kwenye ATCL ya sasa. Mazungumzo kati ya pande mbili hizi hayajakamilika. Aidha, kwa kuwa majadiliano na *CSIL* yamechukua muda mrefu, Serikali inajipanga kuanza mchakato wa kumpata mwekezaji au mbia mwingine.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali pamoja na kanuni zake ili kuimairisha usimamizi na utendaji na hivyo kuleta ufanisi katika sekta. Bunge lako Tukufu katika Mkutano wake wa 18 lilipitisha Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi 2010 *(The Architects and Quantity Surveyors Registration Act, 2010)* kwa lengo la kusimamia na kuratibu mienendo na ubora wa shughuli na taaluma za wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi nchini. Aidha, kanuni 12 chini ya sheria mbalimbali zimewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kama ifuatavyo: *The Engineers Registration Regulations 2009; The Engineers bylaws 2009; The Procurement and Supplies Professionals and Technicians Code of Ethic and Conduct 2009; SUMATRA Tariff Regulations 2009; SUMATRA (Inquiry Procedures) Rules 2009; SUMATRA (Procedures for Settling Claims for Late Delivery of Cargo) Rules 2009; The Transport Licensing (Motorcycle and Tricycles) Regulations 2009; TCAA (Rates and Charges) Rules 2009; The Roads Use Regulations 2009; The Civil Aviation (Procedures for Complaint Handling) Rules 2009; The Road Reclassification Order, 2009;* na *The Road Sector (Environmental Protection) Regulations 2009.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara imepanga kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Miswada mitatu. Miswada hiyo ni kama ifuatavyo: Muswada wa Sheria ya Majengo ambayo imelenga kudhibiti ujenzi wa majengo ili kuzuia ujenzi holela na hivyo kupunguza ama kuondoa kabisa madhara yatokanayo na nyumba zilizojengwa bila kuzingatia ubora; Muswada wa Sheria ya Utafutaji na Uokoaji wenye dhumuni la kuweka utaratibu wa kuratibu masuala ya utafutaji na uokoaji wakati wa ajali na dharura; na Muswada wa Sheria ya Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, Programu ya miaka 10 ya Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi *(Transport Sector Investment Programme – TSIP*), imeendelea kutekelezwa kikamilifu kupitia Bajeti ya Serikali pamoja na fedha za nje. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya miaka mitano ya Programu hii imeendelea kufuata mpango wa kuoanisha miradi iliyopewa kipaumbele na mpango wa muda wa kati wa Matumizi ya Serikali *(Mid Term Expenditure Review Framework - MTEF).* Katika mwaka 2009/10, Wizara ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Programu hii kwa lengo la kufahamu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wake. Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha kwamba, hadi kufikia Juni 2009 karibu asilimia 40 ya Miradi ya TSIP ndiyo iliyokuwa tayari imetekelezwa. Matokeo haya yanaonesha changamoto tuliyonayo katika utekelezaji wa Programu hii hasa ufinyu wa Bajeti ya Serikali pamoja na mchango mdogo wa sekta binafsi katika kuchangia utekelezaji wa Programu hii. Lengo la Serikali katika Programu hii ni kuona kwamba, Sekta Binafsi inapewa fursa ya kutosha kushiriki katika utekelezaji wa *TSIP* hususan miradi inayoweza kutekelezwa kupitia mpango wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Miundombinu imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali. Ili kuziibua na kuzijadili changamoto hizo, Wizara imekuwa ikiandaa Kongamano la Sekta za Miundombinu *(Joint Infrastructure Roundtable).* Katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara iliandaa Kongamano la Pili la Sekta za Miundombinu mwezi Oktoba, 2009 ambalo lilijumuisha sekta zinazojihusisha na miundombinu. Sekta hizo ni Uchukuzi, Ujenzi, Nishati, Maji na Mawasiliano.

Masuala yaliyojadiliwa katika Kongamano hilo ni pamoja na mpango wa kuifanya Tanzania kuwa kiungo cha usafirishaji *(Logistic Hub)* kati yake na nchi jirani za Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda, DRC, Zambia, Msumbiji na Malawi na jinsi ya kuboresha usafiri wa Jiji la Dar es Salaam kupitia mpango kabambe wa mabasi yaendayo kasi wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utaratibu wake wa kila mwaka wa kupima utendaji wa Sekta ya Miundombinu kupitia Kongamano la Pamoja kati ya Serikali na Wahisani *(Joint Infrastructure Sector Review – JISR).* Mwezi Oktoba 2009, Wizara iliandaa Kongamano la Tatu lililopima utekelezaji wa shughuli za sekta kwa kipindi cha mwaka 2009/10. Masuala yaliyojadiliwa kwa kina katika Kongamano hilo ni pamoja na umuhimu wa kutekeleza kwa ufanisi Sera mpya ya Usalama Barabarani iliyopitishwa na Serikali mwezi Januari 2010 pamoja na kupitia upya Sera ya Uchukuzi kwa lengo la kutoa mwelekeo mpya wa Sekta ya Uchukuzi kulingana na wakati uliopo. Moja ya Mikakati ya Serikali katika utekelezaji wa Sera ya Usalama Barabarani ni kuunda Wakala wa Usalama Barabarani utakaokuwa na jukumu la kusimamia usalama barabarani kwa lengo la kupunguza vifo vinavyoongezeka kupitia ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyojitokeza kwa Serikali katika Kongamano hilo ni lile la kutafuta mbinu mpya za kutekeleza Programu ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Uchukuzi *(TSIP)* hasa mpango wa kushirikisha sekta binafsi katika miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnerships - PPPs).* Masuala yaliyoonekana kuwa na nafasi ya kutekelezwa kupitia mpango huo ni pamoja na upanuzi

wa miundombinu ya reli, bandari, viwanja vya ndege na barabara kwa miradi iliyofanyiwa tathmini ya kuonekana kuleta faida kwa mwekezaji. Aidha, suala la ongezeko la gharama za ujenzi lilionekana kukwamisha mipango ya Serikali na Wahisani katika kufanikisha malengo ya kuimarisha na kupanua miundombinu ya uchukuzi na ile ya ujenzi hapa nchini. Wizara itaendelea kutumia Kongamano hili ili kupima utendaji wa sekta za ujenzi, uchukuzi na hali ya hewa kwa lengo la kutathmini ukuaji wa sekta hasa katika kutekeleza mkakati wa Serikali wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara mikoani na vijijini, pamoja na uendelezaji wa miundombinu, zimeendelea kusimamiwa na Wizara ya Miundombinu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na Sekta Binafsi. Kwa ujumla huduma za uchukuzi na idadi ya watoa huduma katika maeneo ya barabara za mikoa umeendelea kuimarika hasa baada ya miundombinu ya uchukuzi kuboreshwa. Hata hivyo huduma za usafiri vijijini zimeendelea kuwa za wastani kutokana na uhafifu wa miundombinu. Uhaba wa miundombinu bora ya uchukuzi unakwamisha maendeleo katika maeneo hayo na hivyo kuwa kero na kusababisha kikwazo katika upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii.

Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuhakikisha kuwa Sera ya Uchukuzi, Sera za Ujenzi pamoja na mikakati iliyojiwekea inatekelezwa ipasavyo ili kuboresha miundombinu hiyo.

Katika mwaka 2009/10, Wizara kwa kiasi kikubwa, iliendelea kuishirikisha sekta binafsi kutoa huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara ili kuhakikisha kuwa wananchi wa vijijini na mijini wanapata huduma bora za usafiri. Aidha, shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zimeendelea kutegemea usafiri kwa njia ya barabara kutokana na matatizo yanayoikabili sekta ya reli.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Usafiri kwa Njia ya Barabara. Sekta binafsi imeendelea kutoa huduma ya usafiri katika miji yetu, na katika hali ya ushindani ambao umesaidia kuinua kiwango cha ubora wa huduma na kurahisisha upatikanaji wake. Aidha, SUMATRA imeboresha utaratibu wa utoaji leseni kwa kusogeza huduma karibu zaidi kwa wateja na hivyo kuwapunguzia muda wa kusafiri kwenda katika ofisi za Mamlaka katika makao makuu ya Mikoa. Katika mwaka 2009/10, jumla ya leseni 13,047 na ratiba 1,739 za mabasi ya abiria zilitolewa ikilinganishwa na leseni 11,194 na ratiba 1,600 zilizotolewa katika mwaka 2008/09. Ongezeko hili linadhihirisha kuhamasika kwa wasafirishaji kutumia Sheria na Kanuni za uchukuzi na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari katika miji mikubwa nchini utapungua kwa kuimarisha usafiri wa Umma. Kuimarika kwa usafiri wa umma na hasa kutumia mabasi makubwa kutavutia watu wenye magari madogo ya binafsi kutumia usafiri wa umma, hatimaye kupunguza msongamano.

Ili kupunguza msongamano wa magari kwa kuanzia na Jiji la Dar es Salaam, Wizara kwa kushirikiana na SUMATRA ilianza juhudi za kupunguza magari madogo ya abiria (vipanya) kwa kusimamisha utoaji wa leseni ya kuingia katikati ya Jiji. Hatua hii

imesaidia kuingiza mabasi makubwa katika usafiri wa umma Jijini Dar es Salaam, hatimaye kuboresha huduma. Takwimu zinaonyesha kuwa tangu utaratibu huu uanze, mabasi madogo yamekuwa yakipungua. Katika mwaka 2006 kulikuwa na mabasi madogo (Vipanya) 3,382 na mabasi makubwa 1,273 ikilinganishwa na mwaka 2009/2010 ambapo kuna mabasi madogo (Vipanya) 2,086 na mabasi makubwa 3,488.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu umezingatiwa katika utekelezaji wa mradi wa mabasi yaendayo kasi jijini Dar es Salaam (BRT). Kazi ya ulipaji fidia ya majengo na rasilimali zitakazoathiriwa na upanuzi wa miundombinu ya mradi wa mabasi ya usafiri wa haraka katika Manispaa za Ilala na Kinondoni imekamilika isipokuwa kwenye maeneo machache yaliyokuwa na malipo ya fidia ya nyongeza kutokana na malalamiko yaliyowasilishwa. Ulipaji fidia kwa eneo la Gerezani Kota unasubiri amri ya mahakama.

Serikali imeanzisha Mradi wa kuboresha na kuongeza mtandao wa barabara za Jiji ili kupunguza msongamano wa magari. Kwa kuanzia barabara zilizo katika mradi huu maalum ni; Jet Corner – Vituka Devis Corner (km 12.0), Ubungo Bus Terminal – Maziwa – Kigogo Round About (Km 6.4), Kigogo Round about – Jangwani - Twiga (km 2.7), Mbezi (Morogoro Rd.) – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km14), Old Bagamoyo - TPDC (Garden) road (km 9.1), Tangi Bovu hadi Goba (km 9.0), Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni (km 2.6), Kimara – Kilungule – External (Mandela Road (km 9) na ukarabati wa mtaro mkubwa wa maji kuanzia Barabara ya Nyerere hadi barabara ya Uhuru. Kazi za ujenzi zimeanza katika barabara 3 nazo ni Jet Corner – Vituka Devis Corner (km 12.0), Ubungo Bus Terminal – Maziwa – Kigogo Round About (Km 6.4), Kigogo Round About - Jangwani - Twiga (km 2.7).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa idadi ya magari ya kusafirisha abiria mijini imeongezeka, bado idadi hiyo haikidhi mahitaji ya miji yetu ambayo inapanuka siku hadi siku. Kwa kuwa magari hayatoshi, hivyo yanachukua abiria wengi kuliko uwezo wake na kusababisha ajali. Katika mwaka 2010/11, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uchukuzi na Sera ya Usalama Barabarani kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuongeza idadi ya wawekezaji katika sekta ndogo ya usafiri na kuzuia ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, Usalama Katika Miundombinu ya Uchukuzi. sote tumeshuhudia mara kadhaa taifa letu likikumbwa na simanzi zinazosababishwa na majanga mbalimbali yanayotokea kwenye miundombinu yetu na kuleta hasara kubwa. Baadhi ya majanga ambayo taifa letu haliwezi kuyasahau ni lile la kuzama kwa meli ya MV Bukoba iliyotokea mwaka 1996 ambapo watu wengi walipoteza maisha na mali zao, ajali ya Treni Reli ya kati iliyotokea mwaka 2002 ambapo watu wengi walifariki na mali nyingi kupotea, kuporomoka kwa baadhi ya majengo kwenye miji mbalimbali nchini na ajali za barabarani zinazotokea mara kwa mara. Aidha, kwa kipindi kirefu sasa tumeshuhudia matumizi yasiyo stahiki ya miundombinu yetu yanayosababisha uharibifu na uchafuzi wa mazingira hususan kwenye mtandao wa barabara, reli, usafiri majini na usafiri wa anga.

Uharibifu wa miundombinu na uchafuzi wa mazingira licha ya kuwa ni mojawapo ya vyanzo vya ajali lakini pia huzorotesha ustawi wa jamii na kukua kwa uchumi wa taifa letu. Ili kukabiliana na chagamoto hizi, katika mwaka 2009/10 Wizara iliunda rasmi Idara ya Usalama na Mazingira mahususi kutatua matatizo ya uchafuzi wa mazingira na ajali katika sekta ya miundombinu ikiwa ni pamoja na kusimamia sera, sheria na kanuni husika za kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nieleze kwa kifupi ukubwa wa tatizo la ajali, uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa rasilimali katika sekta ya uchukuzi, usafirishaji na ujenzi.

Kwa upande wa ajali za barabarani, ajali zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali na wadau mbalimbali kutoka Jumuiya za Kitaifa, Kimataifa na Sekta binafsi. Ajali hizi zimeleta athari kubwa za kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Kwa mfano, mwaka 2007 watu 2,224 walipoteza maisha na watu 16,308 walijeruhiwa katika ajali 17,753 zilizotokea. Mwaka 2008 watu 2,429 walipoteza maisha na 17,861 walijeruhiwa katika ajali 20,615 zilizotokea, Mwaka 2009 watu 3,223 walipoteza maisha na watu 19,263 walijeruhiwa katika ajali 30,836 zilizotokea. Kwa wastani taifa hupoteza takriban asilimia tatu ya pato *(GDP)* lake kila mwaka kutokana na ajali za barabarani na takriban asilimia mbili kutokana na uharibifu wa miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajali za barabarani hapa nchini linaongezeka kwa kasi kutokana na sababu kuu zifuatazo: Uendeshaji mbaya, mwendo kasi, elimu duni na ufahamu mdogo wa sheria za usalama barabarani kwa watumiaji hususan madereva, waendeshaji na wapandaji pikipiki, baskeli na watembea kwa miguu; ubovu wa vyombo vya usafiri unaotokana na matengenezo hafifu na vipuli duni yakiwemo matairi yasiyokidhi viwango; dosari katika usanifu ujenzi na matengenezo ya miundombinu yasiyozingatia vigezo vya usalama; upungufu katika sheria zilizopo na usimamizi wake; ushirikiano hafifu wa wadau wa masuala ya usalama barabarani; kuwepo kwa mafunzo duni ya udereva na utoaji leseni kiholela; uharibifu wa barabara kutokana na magari kuzidisha uzito; na ulevi, uchovu *(fatigue)* na matumizi ya simu kwa madereva wakati wa kuendesha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10 Wizara ilifanya mambo yafuatayo katika kukabiliana na changamoto zilizopo:-

(i) Kuwahamasisha watumiaji mbalimbali wa barabara kuanzisha vyama/vikundi kama chama cha madereva wa malori, mabasi, wapanda pikipiki, wapanda baiskeli, chama cha shule za udereva na kadhalika. Lengo ni kurahisisha utoaji elimu na mafunzo. Vilevile wizara iliendelea Kuendesha warsha za kuelimisha vikundi hivi 1,250 vya watumiaji wa miundombinu ya usafiri katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

(ii) Kusimamia utekelezaji wa sera ya usalama barabarani kwa kuandaa mikakati *(road safety strategy),* kuanza mchakato wa kuunda wakala, kutunga sheria mpya ijulikanayo kama *Road Traffic and Safety Act.*

(iii) Kuandaa, kuchapisha na kusambaza mitaala ya mafunzo ya shule za udereva, kanuni za barabara *(Highway code),* miongozo ya udereva wanafunzi, miongozo ya alama za barabarani *(a guide to traffic sign).*

(iv) Kutoa elimu kwa umma kutumia redio, magazeti na runinga.

(v) Kuandaa mafunzo ya ukaguzi wa usalama barabarani *(Road Safety Audit)* na kufanya ukaguzi kwa baadhi ya barabara ili kubaini kasoro zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha masuala ya usalama barabarani na kulinda miundombinu ya barabara zetu, katika mwaka wa fedha 2010/2011 wizara yangu itaendelea kusimamia kikamilifu uzingatiaji na utekelezaji wa sera ya usalama barabarani, kukamilisha sheria mpya ya usalama barabarani na kwa kupitia wakala wa barabara *(TANROADS),* wizara itaimarisha utendaji kwenye vituo vya mizani ili kudhibiti uharibifu wa barabara. Wizara itaandaa mpango kabambe wa ujenzi wa vituo vya mapumziko kwa madereva na wasafiri kwenye mtandao wa barabara zetu na kufanya maandalizi ya kujenga vituo cha kutahini madereva.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa reli; katika mwaka 2007 watu 43 walipoteza maisha na watu 23 walijeruhiwa katika ajali 111 zilizotokea. Mwaka 2008 watu 25 walikufa na watu 21 walijeruhiwa katika ajali 177 zilizotokea. Mwaka 2009 watu 32 walipoteza maisha na watu 20 walijeruhiwa katika ajali 158 zilizotokea. Ili kuboresha usalama wa usafiri wa reli, Wizara itaimarisha ukaguzi wa miundombinu ya Reli ya Kati na Reli ya TAZARA na ukaguzi na usimamizi wa mazingira ya reli zetu. Vilevile wizara inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa, mawasiliano katika sekta hii ya usafirishaji yanaimarika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za usafiri wa majini, ajali zilizotokea mwaka 2007 zilihusisha watu 18 walipoteza maisha katika ajali 11 zilizotokea. Mwaka 2008 watu 71 walipoteza maisha katika ajali 12 zilizotokea na mwaka 2009 watu 35 walipoteza maisha katika ajali 13 zilizotokea. Ili kuboresha usalama wa usafiri na usafirishaji majini, wizara inaendelea na mipango ya kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa taasisi husika zilizo chini yake na utekelezaji wa sheria ya usafiri majini ya mwaka 2003 na nyingine zinazohusiana na kupunguza matukio ya ajali yanayojitokeza mara kwa mara hususan kwenye bandari zisizo rasmi. Wizara pia itaendelea na maandalizi ya kanuni ya kuzuia uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za uchukuzi majini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007, zilijitokeza ajali za ndege 14 na mtu mmoja alipoteza maisha na watu watatu kujeruhiwa. Mwaka 2008, ajali 15 zilitokea ambapo watu 12 walipoteza maisha na watu 5 kujeruhiwa. Katika mwaka wa 2009, ajali za ndege 15 zilitokea lakini hakuna mtu aliyepoteza maisha wala aliyejeruhiwa.

Kwa upande wa ajali za ndege, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri wa Anga, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Wadau wengine na kufanya ukaguzi wa viwanja vyetu ili vilingane na viwango vya kimataifa. Aidha, Wizara itaendelea kuongeza uwezo wa utendaji kazi kwa kutoa mafunzo kwa wote wanaohusika kwenye sekta hii ndogo ya usalama na mazingira.

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa vyanzo vikuu vya ajali za barabarani, reli, maji na zile za anga zinatokana na upungufu ya kibinadamu *(human error)*, uchakavu na ubovu wa vyombo vya usafiri na dosari katika usanifu na ujenzi wa miundombinu yenyewe. Kwa upande wa ajali za barabarani; upungufu wa kibinadamu huchangia takriban asilimia 76, Ubovu na uchakavu wa magari unachangia takribani *asilimia 16* ya ajali zote za barabarani zinazotokea nchini na ubovu wa miundombinu huchangia takribani asilimia 8. Kwa upande wa reli upungufu wa kibinadamu huchangia asilimia 21, reli yenyewe huchangia asilimia 29 na *rolling stolk* huchangia asilimia 50. Wakati usafiri wa anga upungufu wa kibinadamu huchangia asilimia 73, ubovu wa viwanja huchangia asilimia 16, hitilafu za ndege huchangia asilimia 5 na utabibu wa hali ya hewa na mengineyo huchangia asilimia 6. Kwa upande wa usafiri wa majini, tatizo kubwa ni uchafuzi wa mazingira, ubovu wa vyombo na ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni za usafiri majini. Kwa ujumla, usafiri wa kutumia barabara huchagia zaidi ya asilimia 80 ya ajali zote zinazotokea kwenye Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/10, Wizara ilipanga kujenga Barabara Kuu zenye urefu wa km 261.3 kwa kiwango cha lami na ukarabati wa km 111.8 kwa kiwango cha lami. Hadi kufika mwezi Machi 2010, jumla ya km 373 zilijengwa kwa kiwango cha lami na kukarabati km 60.3 kwa kiwango cha changarawe.

Jumla ya km 9,552.7 za barabara kuu na madaraja 1,026 yalipangwa kufanyiwa matengenezo mbalimbali. Kati ya kilomita hizo km 5,147.4 ni za barabara za lami na km 4,505.3 za barabara za changarawe. Hadi kufikia Machi, 2010 jumla ya km 8,216.5 zimefanyiwa matengenezo na madaraja 966 yametengenezwa. Kati ya barabara zilizofanyiwa matengenezo, km 3,737.3 ni za kiwango cha lami na km 4,479.2 ni za kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Mikoa; Wizara ilipanga kujenga jumla ya km 60.3 za barabara kwa kiwango cha lami, ukarabati wa km 1,006 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja 13. Hadi kufikia Machi, 2010 jumla ya km 41.17 za lami zimejengwa, km 515.59 za changarawe zimefanyiwa ukarabati na madaraja 8 yamejengwa.

Kuhusu matengenezo ya barabara za mikoa pamoja na madaraja; Wizara ilipanga kutengeneza jumla ya km 19,210 za barabara na madaraja 1,207. Kati ya hizo, km 18,434 ni za udongo/changarawe na km 776.1 ni za lami. Hadi kufikia Machi, 2010 jumla ya km12, 202.8 za barabara za udongo/changarawe na km 481.7 za barabara za lami zimefanyiwa matengenezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, Wizara imekabiliana na changamoto mbalimbali za kiutendaji. Changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa miundombinu ya

usafiri hususan barabara na reli uliosababishwa na mvua zilizonyesha kati ya Disemba, 2009 na Januari, 2010 na hivyo kusababisha ongezeko la mahitaji ya fedha za matengenezo.

Changamoto nyingine ni ufinyu wa bajeti ambao ulisababisha kushindwa kulipa Makandarasi kwa wakati pamoja na kuchelewa kufanya malipo ya awali kwa miradi mipya iliyosainiwa Juni 2009, hivyo kusababisha kuchelewa kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kupitia TANROADS, itaendelea kuzifanyia matengenezo Barabara Kuu, Barabara za Mikoa na Madaraja. Lengo ni kuzifanyia matengenezo mbalimbali barabara Kuu zenye urefu wa kilomita 10,345.5. Aidha, jumla ya madaraja 1,221 yatafanyiwa matengenezo makubwa na ya kuzuia uharibifu. Kuhusu barabara za Mikoa, jumla ya km 20,153 zitafanyiwa matengenezo mbalimbali na madaraja 1,211 yamepangwa kufanyiwa matengenezo makubwa na ya kuzuia uharibifu.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika mwaka 2010/11, inajumuisha ukarabati wa jumla ya km 268.5 na kujenga km 634.2 kwa kiwango cha lami katika barabara Kuu. Madaraja kumi (10) yatakayoanza kujengwa ni Nanganga, Nangoo, Sibiti, Maligisu, Kilombero, Kavuu, Kagera, Ruhekei, Mbutu na Malagalasi.

Kwa upande wa barabara za Mikoa, miradi ya maendeleo itakayotekelezwa itahusu ukarabati kwa kiwango cha changarawe jumla ya km 1,350.9 na kujengwa kwa kiwango cha lami jumla ya km 98.55 na kujenga Madaraja 17.

Kati ya km 1,350.9 zitakazokarabatiwa kwa kiwango cha changarawe, km 1,023.1 zitatumia Mfuko wa Maendeleo na km 327.8 zitatumia Mfuko wa Barabara. Aidha, kati ya km 98.55 zitakazojengwa kwa kiwango cha lami, km 68.55 zitagharamiwa na Mfuko wa Maendeleo na km 30.0 Mfuko wa Barabara. Kiambatanisho Na. 2.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha wanawake kushiriki kwa wingi katika kazi za ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi nchini. Katika mwaka 2009/10, Wizara iliendesha mafunzo kwa wanawake Mjini Tanga kuhusu namna ya kusimamia kazi za ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia ya Nguvu Kazi. Washiriki katika mafunzo hayo walikuwa wanawake makandarasi kutoka mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha na Kagera. Lengo ni kuwawezesha wanawake kuanzisha na kuendeleza Kampuni za ukandarasi na kushiriki kazi za matengenezo na ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi. Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa mpango huu na kuendelea kuhamasisha wanawake kushiriki katika kazi za ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi ili kujiongezea kipato na hivyo kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Wizara ina mpango wa kutekeleza kazi mbalimbali zikiwa ni pamoja na kuendesha mafunzo ya Ukandarasi kwa Kampuni za wanawake 15, kuandaa miongozo ya ushiriki wa wanawake katika kazi za ujenzi wa miundombinu, kuhamasisha na kufuatilia maendeleo ya miradi inayotekelezwa na Kampuni zinazoendeshwa na wanawake.

Mheshimiwa Spika, Usafiri na Uchukuzi Majini; Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imeendelea kutoa huduma ya uchukuzi wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu ya Tanganyika, Victoria na Nyasa. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, jumla ya tani 123,279 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 137,938 zilizosafirishwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 11. Aidha, abiria 474,252 walisafirishwa katika mwaka 2009/10 ikilinganishwa na abiria 487,201 waliosafirishwa mwaka 2008/2009 ikiwa ni pungufu kwa asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, *MSCL* inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na meli nyingi kuwa chakavu na hivyo kuchukua sehemu kubwa ya mapato yapatikanayo kwa matengenezo ya mara kwa mara na kusababisha ongezeko la matumizi ya mafuta. Kusimamishwa mara kwa mara kwa meli ya MV Umoja kutokana na kukosa mzigo kunakosababishwa na kupungua kwa mizigo inayosafirishwa kwa Reli ya Kati, kumeathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya kampuni.

Katika mwaka 2010/2011, Kampuni ya *MSCL* inatarajia kusafirisha jumla ya abiria 475,715 na mizigo tani 118,662, kuzifanyia matengenezo makubwa meli za MV Umoja, MV Victoria, MV Iringa, MV Songea na kukamilisha matengenezo ya MV Mwongozo iliyosimamishwa tangu mwaka 2008. Mpango mwingine wa Kampuni ni kuboresha usalama wa abiria na mali zao na kuweka bima za meli, abiria, mizigo na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Sekta Binafsi katika kutoa huduma za uchukuzi katika maziwa. Aidha, Serikali inazidi kuhamasisha Sekta Binafsi waendelee kutoa huduma kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Spika, Usafiri na Uchukuzi Baharini: Katika kipindi cha mwaka 2008/09, Kampuni ya Meli inayomilikiwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China ijulikanayo kama *SINOTASHIP,* ilikuwa na meli mbili zenye uwezo wa kubeba tani 31,000 kwa pamoja. Kusuasua kwa mwenendo wa uchumi duniani, pamoja na uchakavu mkubwa wa meli zake kulisababisha *SINOTASHIP* kuamua kuuza meli zake mbili ili kulinda mtaji na kupunguza hasara. Hivyo, katika kipindi cha kuanzia Juni hadi Novemba 2009, Kampuni ilikuwa haina meli baada ya meli mbili zilizokuwepo kuuzwa. Aidha, katika kipindi hicho, *SINOTASHIP* ilikuwa ikiendelea na mpango wake wa ujenzi wa meli moja mpya yenye uwezo wa kubeba tani 57,000. Ujenzi wa meli hiyo ulikamilika Oktoba 2009 na kuanza kufanya kazi Disemba, 2009. Katika kipindi cha kuanzia Disemba 2009 hadi Juni 2010, Kampuni iliweza kusafirisha jumla ya tani 150,000 ikilinganishwa na tani 148,590 zilizosafirishwa mwaka 2008 kwa kutumia meli mbili zilizouzwa kutokana na kuchakaa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa meli mpya ya pili yenye uwezo wa kubeba tani 34,000 unatarajiwa kukamilika mwaka 2011. Aidha, ili kuongeza mapato, katika mwaka 2010/2011, Kampuni itaelekeza nguvu zake katika kutafuta shehena inayosafirishwa kwa gharama kubwa na yenye masafa mafupi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003 kwa kuboresha ulinzi na usalama wa vyombo vya majini. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, jumla ya vyombo vidogo 43 na vyombo 435 vyenye uzito wa zaidi ya tani 50 vilikaguliwa katika mwambao wa Bahari ya Hindi ili kubaini ubora wake. Aidha, jumla ya vyombo 1,382 vilikaguliwa katika Ziwa Viktoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa. Vyombo ambavyo havikukidhi viwango vya ubora vilielekezwa kufanyiwa marekebisho kabla ya kupewa vyeti vya ubora na vyombo visivyotimiza kabisa masharti ya viwango vilivyowekwa vilisimamishwa kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Machi 2009 hadi Aprili 2010, Kituo cha kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji cha Dar es Salaam kilipokea taarifa za dharura za vyombo vya majini zipatazo 17 ambazo zilitokea eneo la Tanzania. Katika matukio yaliyotolewa taarifa, watu wapatao 278 waliokolewa na 12 kupoteza maisha. Aidha, maiti 28 waliopolewa kutokana na ajali ya ndege ya Shirika la Ndege la Yemen (Yemenair).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendelea na uratibu wa usalama wa vyombo vya uchukuzi nchini, SUMATRA pia imeendelea kudhibiti huduma za Makampuni yanayohudumia mizigo bandarini pamoja na Wakala wa Meli. Katika mwaka 2009/2010, kampuni 520 zinazoshughulikia huduma za mizigo bandarini zilisajiliwa ikilinganishwa na kampuni 588 zilizosajiliwa mwaka 2008/2009.

Jumla ya leseni 32 za Uwakala wa Meli zilitolewa mwaka 2009. Aidha, SUMATRA imeendelea kushirikiana na Wadau wa Bandari katika kuhakikisha kuwa huduma zinaboreshwa na ufanisi wa bandari unaongezeka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, SUMATRA itaendelea kukabiliana na ajali za majini kwa kuimarisha usimamizi wa usalama wa vyombo vya usafiri majini kwa kuvifanyia ukaguzi, kutoa elimu ya usafiri salama kwa wamiliki wa vyombo, waendeshaji wa vyombo vya usafiri majini, abiria na wadau wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* iliendelea na utekelezaji wa miradi mipya ya ujenzi wa miundombinu ya bandari na kufanya ukarabati wa miundombinu iliyochakaa ikiwa ni pamoja na kuibadilisha kulingana na mahitaji ya bandari. Lengo la kuboresha miundombinu na huduma za bandari ni kuweza kuhudumia shehena ya Tanzania na ya nchi jirani za Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda na Uganda kwa ufanisi zaidi. Sekta Binafsi imeendelea kushirikishwa katika kutekeleza miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Bandari ililenga kuhudumia tani za mapato milioni 6.98. Hadi Machi, 2010 jumla ya tani za mapato milioni 5.76 zilihudumiwa ikilinganishwa na lengo la kuhudumia tani za mapato milioni 5.32 kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 7.6.

Hadi Machi, 2010, TPA kupitia kitengo cha makasha kinachoendeshwa na TICTS kilihudumia shehena ya makasha (TEUs) 224,511 ikiwa ni pungufu ya lengo la kuhudumia makasha (TEUs) 249,300, upungufu huu ni sawa na asilimia 9.9. Sababu zilizochangia kushuka utendaji ni mlundikano wa makasha na msongamano wa meli uliokuwepo kati ya mwezi Julai hadi Disemba, 2009. Katika kukabiliana na hali hii, hatua za muda mfupi zilizochukuliwa ni pamoja na kuongeza vifaa vya kuhudumia meli na mizigo na kupanua maeneo ya kuhudumia mizigo ndani na nje ya bandari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali imeondoa kipengele cha ukiritimba katika mkataba wa TICTS na hivyo kuruhusu meli za makasha kuhudumiwa pia katika vitengo vingine. Hatua hii imepunguza msongamano wa meli zinazosubiri kufunga katika bandari ya Dar es Salaam kwani hivi sasa meli tano zinaweza kuhudumiwa kwa wakati mmoja ukilinganisha na meli tatu hapo awali. Aidha, Serikali imebuni mikakati yenye lengo la kutoa ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la msongamano wa mizigo bandarini. Mipango hiyo ni pamoja na kupanua bandari ya Dar es Salaam, kujenga bandari mpya za Bagamoyo na Tanga na kupanua bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa magati sita (Kalya, Karema, Lagosa, Kirando, Kagunga na Kibirizi) katika Ziwa Tanganyika iliyoanza kutekelezwa Disemba, 2009 na kubadilisha bomba la kupakulia mafuta ya aina mbalimbali *(Single Point Mooring – SPM)* lililopo ndani ya bahari eneo la Kigamboni zinaendelea.

Kazi ya ujenzi wa *SPM* inatarajiwa kuanza Julai 2010. Kazi nyingine zilizotekelezwa katika mwaka 2009/10 ni pamoja na uondoshaji mchanga *(maintenance dredging*) katika Gati Na. 1 - 11 na Gati la mafuta *(Kurasini Oil Jetty - KOJ)* katika Bandari ya Dar es Salaam, uondoshaji mchanga katika Bandari ya Tanga, ujenzi na upanuzi wa eneo la kuhudumia mizigo katika Bandari ya Tanga, kuongeza maeneo ya kuhudumia shehena ya kontena kwa kusafisha na kukarabati maeneo ya iliyokuwa eneo la AMI na maeneo yaliyokuwa yakitumika kutunzia shaba katika Bandari ya Dar es Salaam, uondoshaji mchanga *(maintenance dredging)* katika Bandari ya Kigoma na ujenzi wa ghala la kuhifadhia shehena Bandari ya Kasanga.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, miradi itakayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kituo kipya cha kuhudumia shehena ya makasha (Gati 13 & 14) bandari ya Dar es Salaam, kupanua na kuongeza kina cha lango la bandari na kuongeza kina cha Gati Na. 1 – 7 Bandari ya Dar es Salaam, mradi wa eneo la kuhudumia mizigo (CFS) Kisarawe, ujenzi wa kituo cha kuhudumia shehena ya mafuta cha SPM, ujenzi wa jengo la kuweka magari Bandari ya Dar es Salaam, mradi wa uendelezaji wa Fukwe, ujenzi wa gati katika Bandari ya Mafia, matengenezo ya eneo iliyokuwa NASACO, uboreshwaji wa Bandari ya Kasanga, ujenzi wa Jengo la Bandari *(One stop center*), ununuzi wa vifaa vya kuhudumia shehena na meli, ujenzi wa Gati la Kiwira na upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani na Bagamoyo.

Miradi mingine ni pamoja na kupanua Bandari ya Mtwara ili kuiwezesha kuhudumia mizigo ya kichele na kontena, kukarabati Bandari ya Kigoma, kuendeleza Bandari ya Mwanza na kukamilisha ujenzi wa gati sita katika Ziwa Tanganyika na ujenzi

wa mtandao wa mawasiliano kwa bandari kuu na maziwa. Aidha, TPA itaendelea kuhakikisha kuwa huduma na utendaji wa bandari unakuwa wenye ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2010/2011, Mamlaka inalenga kuhudumia jumla ya tani za mapato milioni 7.5 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.2 ya lengo la mwaka 2009/2010. Kitengo cha makasha (TICTS) kitahudumia makasha (TEUs) 340,100 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.9 ikilinganishwa na lengo la mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, TRL imekuwa ikitoa huduma ya usafiri wa abiria na mizigo kwa kiwango cha wastani. Kwa mfano, mwaka 2008/09, Kampuni iliweza kusafirisha tani 476,000. Hadi kufikia Novemba 2009, TRL iliweza kusafirisha tani 420,601 tu. Aidha, jumla ya abiria 59,000 walisafirishwa. Hadi kufikia mwezi Novemba 2009, jumla ya abiria 339,434 walisafirishwa. Hata hivyo, huduma za treni kuanzia Dar es Salaam na Dodoma zilizositishwa mwezi Disemba 2009 kutokana na mafuriko yaliyosababisha uharibifu mkubwa wa njia ya reli katika stesheni kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe. Kazi ya dharura ya kurejesha miundombinu hiyo ilikamilika katikati ya mwezi Mei 2010 na huduma za treni ya mizigo ilianza baada ya ukaguzi wa njia kukamilika. Huduma za abiria zinatarajia kuanza mwishoni mwa mwezi Juni, 2010 baada ya kukamilika kwa matengenezo madogo madogo ya mabehewa na kufanyiwa ukaguzi na SUMATRA.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, TRL imepanga kufanya ukarabati wa injini 11 na mabehewa 107 ya mizigo. Mpango mwingine ni kuboresha miundombinu ya mawasiliano, ununuzi wa vifaa mbalimbali vitakavyotumika katika shughuli za utunzaji na matengenezo ya njia ya reli, mabehewa na injini.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa kuboresha reli kati ya Dar es Salaam na Isaka ilikamilika Septemba, 2009. Reli za tani 12,000 zinazotosheleza kubadili km 150 za njia ya reli kati ya Dodoma na Tabora zimekwishapokelewa. Aidha, mataruma yanayotosheleza km 80 yamewasili nchini. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kununua mataruma ya km 70 zilizosalia.

Ujenzi wa vituo vya kuhifadhi makasha (ICDs) vya Ilala, Shinyanga na Mwanza unaendelea na mashine za kupakia na kupakua makasha *(Reach Stackers)* tatu zimewasili nchini na kupelekwa katika Vituo vya Ilala na Shinyanga. Mashine mbili za kupakia na kupakua mizigo zinatarajiwa kuwasili nchini mwaka 2010/11 kwa ajili ya Kituo cha Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, RAHCO imepanga kufanya usanifu wa kina *(detailed engineering design)* wa kuboresha Reli ya Dar es Salaam – Isaka na usanifu wa kina wa ujenzi wa reli mpya kati ya Isaka – Kigali/Keza – Gitega – Musongati kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni ubadilishaji wa kilometa 150 za reli kati ya Dodoma na Tabora, ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya kuhifadhi makasha vya Shinyanga na Mwanza, kutafuta mbia kwa ajili ya ujenzi wa mtandao wa mawasiliano *(Fibre Optic Cable Network)* kati ya Tabora na Kigoma na Tabora na Mwanza.

RAHCO pia ina mpango wa kuanzisha Mfuko wa Miundombinu ya Reli *(Railway Infrastructure Fund)* chini ya Sheria ya Reli ya Mwaka 2002 kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya reli nchini.

Mheshimiwa Spika, hali ya miundombinu ya Reli ya TAZARA kwa mwaka 2009/2010 ilikuwa inaridhisha ingawa utekelezaji wa mpango wa matengenezo ya reli ulikuwa duni. Katika kipindi cha nusu mwaka cha 2009/2010, kulikuwa na maeneo 23 yaliyowekewa tahadhari ya kupunguza mwendo wa treni. Sehemu nyingi za maeneo hayo ni zile zilizoharibika kutokana na ajali na mmomonyoko wa udongo. Aidha, vifaa vingi vya kufanyia kazi havikuwa katika hali nzuri kutokana na ukosefu wa fedha.

Kwa upande wa mawasiliano na ishara, TAZARA imeimarisha huduma hii kwa kutumia teknolojia ya nyaya aina ya *Microwave, Optic Fibre* na *High Frequency Radio.* Mamlaka imeendelea kukarabati njia za reli, mabehewa na injini ili kuimarisha usalama wa abiria, mizigo na vyombo vyenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA), ilipanga kusafirisha jumla ya tani 600,000 za mzigo. Hadi kufikia Mei, 2010, TAZARA ilisafirisha tani 474,832 za mizigo ambazo ni wastani wa tani 43,167 kwa mwezi sawa na asilimia 79 ya lengo. Mamlaka ilisafirisha abiria 695,867 ambao ni wastani wa abiria 63,260 kwa mwezi. Kiwango cha kusafirisha abiria kimeshuka kwa asilimia nne ya lengo kutokana na uhaba wa injini, mabehewa na fedha za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili TAZARA ni pamoja na uhaba wa fedha za uendeshaji.

Uhaba huu umeathiri utendaji kiasi cha kushindwa kufanya matengenezo ya injini za treni na mabehewa. Aidha, uhaba wa fedha umeathiri kwa kiasi kikubwa ukarabati wa miundombinu hususan upande wa Tanzania na hivyo, kusababisha kuwekwa kwa vidhibiti mwendo katika sehemu zilizoathirika.

Ili kutatua changamoto hizi, katika mwaka wa fedha 2010/11, Serikali za Tanzania na Zambia zitabeba jukumu la ukarabati wa miundombinu, injini na mabehewa kupitia bajeti za Wizara husika. Mpango mwingine ni kuirudishia TAZARA makato yanayofanywa na TRA kama kodi kutokana na ununuzi wa mafuta ya TAZARA, Serikali za Tanzania na Zambia kubeba madeni mbalimbali ya TAZARA hususan yale ya kisheria ili kuiwezesha kukopesheka na kufanya kazi kibiashara zaidi pamoja na kufanya tathmini ya kitaalam kwa ajili ya kushirikisha sekta binafsi kuendesha TAZARA.

Mheshimwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11, TAZARA inatarajia kubadilisha mataruma mabovu ya mbao 10,158 na kufunga mengine katika madaraja 322, kurudishia vyuma vya madaraja vilivyoibwa kutokana na kukithiri kwa biashara ya vyuma chakavu, kupaka rangi na kuchomea jumla ya madaraja 276 kwa upande wa Tanzania kutokana na kutu na kukarabati '*culverts*' zilizoharibiwa na mvua katika maeneo ya Kurasini na Yombo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, SUMATRA imeendelea kudhibiti na kusimamia usalama, ubora wa huduma na udhibiti wa kiuchumi wa usafiri wa reli nchini. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005/06 hadi 2009/10, SUMATRA ilifanya ukaguzi wa mabehewa 23 ya abiria na injini 6 zilizoingizwa nchini na TRL kutoka India. Aidha, SUMATRA ilifanya ukaguzi wa miundombinu ya reli, vifaa na huduma kutoka Dar es Salaam, Mwanza na tawi la kuelekea Mpanda. Upungufu uliodhihirika katika ukaguzi huo ni matengenezo yasiyoridhisha ya njia ya reli, baadhi ya maeneo kutokuwa na mawasiliano, uchakavu wa mabehewa na TRL kushindwa kutekeleza mkakati wa usalama. TRL walipewa maelekezo ya kurekebisha upungufu huo na SUMATRA iliandaa semina ya mafunzo kuhusu namna ya kukabiliana na makosa ya kibinadamu.

Kwa upande wa TAZARA, SUMATRA ilikagua mabehewa 100 yaliyoingizwa nchini kutoka China na kufanya ukaguzi wa miundombinu, vifaa na huduma za TAZARA kuanzia Dar es Salaam hadi Tunduma. Upungufu uliojitokeza ni hali mbaya ya mabehewa, mawasiliano mabovu, upungufu wa wafanyakazi wenye ujuzi na vitendea kazi. TAZARA walipewa maelekezo ya kurekebisha upungufu uliojitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, SUMATRA inatarajia kufanya ukaguzi na tathmini ya usafiri wa reli kwa ajili ya kuimarisha usalama na ubora wa huduma, kuendelea kudhibiti gharama za watoa huduma, kufanya tafiti kwa ajili ya kuboresha huduma, kutoa mafunzo ya udhibiti na usimamizi na kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kupitia Idara yake ya Huduma ya Uongozaji Ndege (ANS) ilifanikiwa kupata cheti cha Kimataifa cha Ubora cha ISO 9001:2008 na hivyo kuweka rekodi ya kuwa taasisi ya pili Kusini mwa Jangwa la Sahara baada ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Usafiri wa Anga ilikuwa inaendelea na ujenzi wa Jengo la Makao Makuu eneo la Ukonga. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2010 na Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga zilizokuwa katika majengo ya kukodisha katikati ya Jiji la Dar es Salaam zitahamia katika jengo hilo jipya.

Hii inatokana na juhudi zinazofanywa za kuwahamasisha watoa huduma hizo kufanya safari za kuja nchini kwetu. Mizigo mingi, hasa maua na samaki, bado husafirishwa kwa barabara kutoka Tanzania hadi Kenya, kabla ya kusafirishwa kwenye masoko ya Ulaya.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha usalama wa anga, mtambo unaosaidia Marubani kupata taarifa za mwelekeo na umbali wa ndege *(VHF Omni-directional Radio Range and Distance Measuring Equipment)* tayari umesimikwa katika

Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na umeanza kufanya kazi tangu Disemba 2009 na hivyo kuleta faraja kwa marubani wa ndege. Kuwepo kwa mtambo huu katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, kumeimarisha kiwango cha hali ya usalama katika anga kwenye kanda ya Ziwa Viktoria, hata kwa ndege zipitazo bila kutua katika Kiwanja cha Mwanza *(over fly)* kwenda nchi za Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo (DRC), Afrika Kusini, Sudan na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) imeendelea kutoa huduma za usafiri wa anga kwa kutumia ndege zake mbili aina ya Dash 8-Q300 na kurudisha ndege aina ya Boeing 737-200 iliyokuwa kwenye matengenezo makubwa nchini Msumbiji. Aidha, ATCL bado imeendelea kukabiliwa na matatizo makubwa ya kifedha na kimenejimenti kiasi cha kuathiri huduma zake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi 2009/2010, Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) umeendelea kutoa huduma za usafiri kwa viongozi wakuu wa kitaifa na Serikali kwa ujumla. Wakala wa Ndege za Serikali umehakikisha kuwa Ndege zake zote nne, zinafanyiwa matengenezo makubwa na ya kawaida hapa nchini na nje ya nchi.

Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Februari 2010, Wakala umeweza kukusanya madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 2.8 ambacho ni kati ya madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 7.9 inayodai. Wakala umeweza kufanya malipo mbalimbali yakiwemo ya vipuli vya ndege kwa asilimia 80 kulingana na fedha zilizotolewa kwa Wakala. Kwa mantiki hiyo wakala umekuwa na uwezo wa kukopeshwa *(credit worth)* kutoka kwa watoa huduma *(Manufacturers and Suppliers).* Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2005 hadi Mei, 2010, Wakala umeweza kupata mapato ya shilingi bilioni 22.0 yaliyotokana na ukodishaji wa ndege za Serikali ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 28.0 kilichokadiriwa kukusanywa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wakala ulikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa bajeti ukilinganisha na mahitaji na uhaba wa Marubani. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wakala uliendelea na mafunzo ya marubani na wahandisi pamoja na watumishi wengine.

Katika kipindi cha 2010/11, Wizara kupitia Wakala itaendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kuziandaa ndege zetu kuwa tayari kwa safari wakati wowote zitakapohitajika.

Wakala utaendelea kudumisha na kuboresha usalama wa ubora wa huduma kwa kufuata taratibu zilizopo kwenye mkataba wa huduma kwa mteja. Wakala pia utaendelea kuwapeleka watumishi katika mafunzo ya ndani na nje ya nchi ili kuwaongezea uwezo wa kufanya kazi zao kwa tija na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere Mamlaka ya Usafiri wa Anga imefunga mashine ya kisasa itwaayo *Multi-Channel Digital Voice and Data Logger,* ambayo husaidia kupata taarifa za uchunguzi wa kubaini kiini cha ajali za

ndege mara zinapotokea. Katika mwaka 2010/11, vifaa kama hivi vitafungwa katika viwanja vya ndege vya Arusha, Mwanza na Zanzibar. Ufungaji wa mitambo ya mawasiliano ya VHF ili kuimarisha huduma za uongozaji ndege utafanyika katika viwanja vya ndege vya Dodoma, Mbeya, Songea, Mtwara, Tabora na Arusha. Aidha, Mamlaka ya Usafiri wa Anga itatekeleza Mpango unaoratibiwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) ujulikanao kama *safety management system,* wenye lengo la kudhibiti na kuondoa vitendo vinavyoweza kusababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* iliendelea kuhudumia viwanja vya ndege kwa kuzingatia sera ya Taifa ya Uchukuzi ambayo inasisitiza viwanja vya ndege kujiendesha kibiashara, kujitosheleza kwa mapato na kujitegemea. Miongoni mwa mambo muhimu ambayo Mamlaka iliendelea kuyafanya ni pamoja na matengenezo ya kawaida ya viwanja vya ndege ili kuwezesha ndege kutua na kuruka kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka iliendelea na mkakati wa kuandaa mazingira mazuri ya kibiashara katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Julius Nyerere ili kiwe kiungo *(hub)* cha usafiri wa anga kitaifa, kikanda na kimataifa. Baadhi ya kazi zinazoendelea kufanyika ni pamoja na utekelezaji wa awamu ya pili ya ukarabati na ujenzi wa barabara za viungio na maegesho, barabara ya kuruka na kutua ndege, kuweka taa za kuongozea ndege, ukarabati wa maegesho ya ndege ya *Terminal I,* maegesho ya ndege za mizigo *(Cargo Apron)* pamoja na kazi/huduma zinazohusiana na masuala ya mazingira, ujenzi wa Jengo jipya la watu mashuhuri *(VIP Lounge)* eneo la *Terminal II* na usanifu wa ujenzi wa jengo jipya la abiria *(Terminal III),* usanifu wa ujenzi wa jengo jipya la mapokezi ya ugeni wa kitaifa *(State Reception Building).*

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuimarisha na kuboresha huduma za viwanja vya ndege nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini imeanza mchakato wa maandalizi ya awamu ya pili ya ukarabati na uboreshaji wa kiwanja cha Mafia kwa kiwango cha lami chini ya ufadhili wa *Millenium Challenge Corporation.* Kuhusu kiwanja cha Ndege cha Mwanza, Mamlaka inafanya mapitio ya mwisho ya usanifu wa uboreshaji wa miundombinu ya kiwanja hiki. Aidha, mchakato wa kutangaza zabuni umeanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanja cha ndege cha Arusha, Mamlaka imekamilisha ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maungio na maegesho kwa asilimia 95. Kazi ya ukarabati wa barabara ya kutua na kurukia itakamilika katika mwaka 2010/11. Serikali pia itakarabati barabara za kutua na kuruka kwa kiwango cha lami katika viwanja vya ndege vya Mpanda, Bukoba, Kigoma na Tabora. Katika kiwanja kipya cha Kimataifa cha Msalato Dodoma, Mamlaka imekamilisha kazi ya kuthamini mali, ulipaji wa fidia, upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja pamoja na kusawazisha eneo la kiwanja na kuweka mipaka ya eneo la kiwanja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ujenzi wa Kiwanja cha ndege cha Songwe, Mamlaka imeendelea na awamu ya tatu na ya mwisho ya kumalizia ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na viungio vyake kwa kiwango cha lami kujenga mfumo wa

kuondoa maji ya mvua kiwanjani *(drainage works),* ujenzi wa jengo la abiria (badala ya lile la awali ambalo litatumika kwa matumizi ya ofisi), ununuzi na ufungaji wa *X-ray machine* kwa ajili ya ukaguzi, Samani za jengo la abiria, Mifumo ya kurahisisha utoaji wa mizigo kutoka kwenye ndege *(conveyor belts),* mtambo wa umeme wa dharura *(generator),* mitambo ya hali ya hewa na *Public Address System;* na ujenzi wa miundombinu ya kuvuta na kusafisha maji *(Water Supply and Treatment Works).* Mamlaka inaendelea pia na juhudi za kupata hati *(Title Deeds)* kwa maeneo mapya kwa ajili ya viwanja vipya vya ndege. Maeneo hayo ni Bagamoyo (Pwani), Omukajunguti (Kagera), Kisumba (Sumbawanga), Msalato (Dodoma) na Ngungungu (Manyara). Aidha, Wizara kupitia TAA itafanya tathmini ya maeneo mapya yaliyoainishwa katika Mikoa ya Mara na Singida kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vipya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaendelea na ujenzi wa uzio wa viwanja vya ndege vya Mafia, Ziwa Manyara na Dodoma, kununua vifaa vya usalama, *X-ray machines* kwa viwanja vya JNIA (3), Mtwara, Dodoma, Mwanza na Arusha.

Kununua *Walk Through Metal Detectors* kwa Viwanja vya JNIA, Arusha, Mtwara, Tanga, Dodoma,Tabora, Kigoma, Mafia na Mwanza, kununua *Hand Held Metal Detectors,* pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali ya namna ya kukabiliana na vitisho vya kigaidi kwa viwanja vyote vya ndege vyenye ratiba maalum. Viwanja vya ndege vilivyobaki vitaendelea kuboreshwa na Mamlaka ya viwanja vya ndege kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio niliyoyataja hapo juu, Mamlaka ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa kifedha (bajeti) ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya ukarabati na uendelezaji wa miundombinu ya viwanja. Kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali, miradi mingi huchukua muda mrefu kukamilika na kwa gharama kubwa zaidi.

Changamoto nyingine ni vitisho vya matukio ya vitendo vya kigaidi na uhalifu dhidi ya usafiri wa anga duniani na hivyo kuhitaji umakini na gharama kubwa katika masuala ya ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege. Kukosekana kwa elimu na mwamko wa usalama wa usafiri wa anga kwa watumiaji wa viwanja vya ndege huleta misuguano mingi ya kiutendaji. Kukua na mabadiliko ya kasi katika matumizi ya teknolojia mpya katika usafiri wa anga duniani ambayo yanahitaji uwezo mkubwa wa uwekezaji katika miundombinu na huduma za viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizotajwa hapo juu, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inaendelea na juhudi za kushirikisha Sekta Binafsi (PPP) katika uendeshaji, uendelezaji, na upanuzi wa huduma za viwanja vya ndege. Viwanja vya ndege 16 vimepata kipaumbele katika Mpango wa Kitaifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi *(Transport Sector Investment Programme),* Viwanja hivyo ni JNIA, Arusha, Mwanza, Lake Manyara, Mafia, Mtwara, Tabora, Bukoba, Dodoma, Kigoma, Moshi, Shinyanga, Musoma, Tanga, Singida na Songwe. Jitihada

zinaendelea chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), pamoja na mashirika mengine ya kimataifa *(WB, BADEA, ORET, OPEC, JICA, ADB, IFC)* ili mpango huo uweze kupatiwa fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, huduma za hali ya hewa zimeendelea kuboreshwa ili zifikie matarajio ya watumiaji wa huduma hizo. Katika mwaka 2009/10, sekta zilizonufaika na huduma hizo ni pamoja na Uchukuzi, Kilimo, Maji, Mazingira, Ujenzi na tahadhari kwa Umma dhidi ya majanga yatokanayo na mabadiliko ya mwenendo wa hali ya hewa.

Katika mwaka wa fedha 2010/11, Mamlaka itaendelea kuboresha huduma za hali ya hewa ili kukidhi mahitaji ya Wananchi na pia sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Ujenzi wa Kituo cha Radar ya hali ya hewa ambacho kinajengwa Dar es Salaam kinatarajiwa kukamilika na kuanza kufanya kazi mwezi Agosti, 2010. Aidha, Mamlaka itanunua Radar ya pili ya hali ya hewa inayotarajiwa kufungwa Mkoani Mwanza na hivyo kuongeza usahihi wa taarifa za hali ya hewa pamoja na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa.

Mamlaka pia itaendelea kuboresha vituo vyake kwa kununua vifaa vya kisasa vya hali ya hewa. Katika kuhakikisha taarifa za hali ya hewa hususan utabiri zinawafikia walengwa, Mamlaka inatarajia kuboresha studio zake za kutayarishia taarifa hizo. Ili kufikia malengo ya utekelezaji wa mradi wa uhakiki wa ubora wa viwango vya kutoa huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa anga (*Quality Management System),* Mamlaka itanunua mitambo ya hali ya hewa ikiwemo *pressure calibration unit.*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka pamoja na kupata mafanikio hayo bado inakabiliwa na baadhi ya changamoto ikiwemo upungufu wa Bajeti, uchache wa vituo vya kupimia hali ya hewa, uhaba na uchakavu wa mitambo na vifaa, maslahi duni kwa wafanyakazi, ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka na Kituo Kikuu cha Utabiri, kukosekana kwa sera na sheria ya utoaji wa huduma kwenye sekta ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Serikali kupitia Wakala wa Majengo (TBA), iliendelea kutoa huduma za ushauri na kusimamia ujenzi wa nyumba za Viongozi na Watumishi wa Umma, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi za Serikali, kuweka samani katika nyumba za viongozi pamoja na kushughulikia migogoro na shughuli mbalimbali zinazohusu majengo, hususan nyumba na majengo ya Serikali.

Nyumba zilizoanza kujengwa ni kama ifuatavyo: Jijini Dar es Salaam (2), Tabora (1), Mwanza (1), Iringa (1), Arusha (1), Mbeya (1), Songea (1), Urambo (1), Tanga (1) na Dodoma (1). Nyumba za viongozi zilizoanza kujengwa ni Arusha (2), Ukerewe (2), Bahi (2), Kigoma (1), Sumbawanga (1), Mafia (1) na Mvomero (1). Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Wakala wa Majengo unaendelea na ukamilishaji wa majengo matatu ya ghorofa yanayojengwa kwa ubia Jijini Dar es Salaam kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kazi za ukarabati na uboreshaji wa makazi ya nyumba za viongozi nchini imeendelea kufanyika. Katika mwaka 2009/10, uboreshaji na ukarabati

wa nyumba 81 za viongozi zilizojengwa maeneo ya Mikocheni, Kijitonyama na Msasani Penninsular unaendelea kutekelezwa. Kazi nyingine za ukarabati zilizotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa ghorofa moja Ngano Street) lenye makazi 3 Jijini Dar es salaam. Nyingine ni majengo katika Miji ya Iringa (1), Tabora (1), Dodoma (1), Lindi (3), Mwanza (3), Lushoto (1), Tanga (1), Mafia (1) na Musoma (2).

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo umeendelea pia na kazi ya ujenzi wa nyumba kwa ajili ya Watumishi wa Serikali nchini. Miradi iliyoainishwa kutekelezwa katika mwaka 2009/10, ilihusu ukamilishaji wa nyumba 60 za watumishi katika mikoa yote Tanzania Bara pamoja na ujenzi wa majengo ya iliyokuwa NMC Mbezi Beach Dar es Salaam. Aidha, ujenzi wa Ofisi za TBA Makao Makuu, Mkoa wa Manyara na Pwani, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Bariadi, ujenzi wa Zahanati katika nyumba za viongozi Mwangaza Dodoma, ukarabati na uhifadhi wa Jengo la Boma la Kale Bagamoyo na ukarabati wa Ikulu Ndogo Mafia – Pwani unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wakala pia ulikamilisha umiliki wa viwanja 429 vilivyopatikana pamoja na eneo la eka 635 lililopatikana Mjini Dodoma litakalopimwa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Serikali kupitia TBA itaendelea na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba zilizokwishaanza kama zilivyoainishwa hapo juu pamoja na kuanza ujenzi wa nyumba mpya 16 kwa ajili ya viongozi nchini wakiwemo Waheshimiwa Majaji. TBA inategemea kuanza ujenzi wa nyumba nyingine tano katika kila mkoa Tanzania Bara kwa ajili ya watumishi wa umma, ununuzi wa nyumba za iliyokuwa NASACO, NIC, ujenzi wa nyumba 25 za Watumishi Bunju Dar es Salaam pamoja na kukamilisha upatikanaji na umiliki wa viwanja katika sehemu mbalimbali nchini kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, TEMESA imeendelea na majukumu yake ya msingi ambayo ni kutengeneza magari na mitambo, ukaguzi na ukarabati wa mifumo ya umeme katika nyumba za Serikali, elektroniki, viyoyozi na mabarafu. Wakala pia umeendelea kutekeleza miradi ya kutoa ushauri wa kitaalam (*Consultancy Services*) katika usimikaji wa mifumo ya elektroniki, viyoyozi na mabarafu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na mkakati wa kuimarisha vivuko katika maeneo mbalimbali yanayohitaji huduma hiyo. Katika mwaka wa fedha wa 2009/10, Wizara imekamilisha ununuzi wa Kivuko cha Mto Pangani (Tanga), ukarabati wa MV Kigamboni (Dar es Salaam) na MV Sengerema (Mwanza). Vivuko hivi vimekabidhiwa Serikalini na kuanza kutoa huduma chini ya uendeshaji wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA). Kukamilika kwa vivuko hivi ni hatua nzuri katika kuboresha huduma ya usafiri wa vivuko kwa wananchi katika maeneo husika hivyo kurahisisha utekelezaji wa shughuli zao za maendeleo. Aidha, Vivuko vya Utete (Rufiji), Rugezi-Kisorya (Mwanza) na Musoma-Kinesi (Mara) vinaendelea kujengwa na vitakamilika Septemba 2010.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilitojitokeza katika utekelezaji wa majukumu hayo ni pamoja na uchakavu wa karakana na ukosefu wa vitendea kazi vya kisasa. Wakala unaendelea na juhudi za kupunguza matatizo haya kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11, Wizara kupitia TEMESA imepanga kutengeneza magari 9,144. Aidha, Wakala utaendelea na Mpango wake wa ukarabati wa karakana na kuzipatia vitendea kazi vya kisasa na kuendelea kusimamia uendeshaji na matengenezo ya mara kwa mara ya vivuko vyote nchini ili viendelee kutoa huduma bora na salama. Pia Wakala utaendelea kutoa ushauri wa kiufundi kwa miradi ya matengenezo ya mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na mabarafu katika majengo ya Serikali ikiwa ni pamoja na ukodishaji wa mitambo na magari maalum kwa Viongozi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/11, Wizara imepanga kukamilisha ununuzi wa vivuko vipya vyenye uwezo wa tani 50 kila kimoja vya Msanga Mkuu (Mtwara), Rusumo (Kagera), Itungi Port (Kyela) na Kilambo (Mtwara) kitakachotoa huduma kati ya Tanzania na Msumbiji.

Wizara itaendelea kujenga maegesho *(ramps*) katika vivuko vya Nyakaliro-Kome, Msanga Mkuu na Rusumo ili kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko kwa urahisi nyakati zote za mwaka. Pia Wizara itafunga mashine za kukatia na kutambua tiketi zitakazotumia mfumo wa kompyuta katika Kivuko cha Kigamboni ili kurahisisha upatikanaji wa tiketi na utunzaji sahihi wa takwimu za mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Baraza la Taifa la Ujenzi *(NCC)* limeendelea kuratibu ushirikishwaji wa sekta binafsi ili iweze kushiriki kikamilifu katika masuala ya ujenzi nchini. Aidha, NCC imeendelea kutekeleza Sera ya Ujenzi kwa kupitia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2004 ambayo inatoa upendeleo katika utoaji wa Kandarasi na huduma kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Baraza limepanga kutoa msukumo katika utekelezaji wa Sera ya Ujenzi, kubuni na kutekeleza mikakati ya ukuzaji ubora na tija, kuandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria iliyoanzisha Baraza na kuboresha utendaji kazi wa sekta ya ujenzi isiyo rasmi. Aidha, Baraza limepanga kuratibu na kutoa mafunzo, kufanya ukaguzi wa kiufundi *(Technical Audit)*, kutoa ushauri wa kiufundi na kutatua migogoro katika sekta ya ujenzi na kufanya tafiti zitakazowezesha kubaini matatizo. Baraza pia litaendelea kutafuta kazi mbalimbali na kuendesha mafunzo na huduma za ushauri zitakazosaidia kuliongezea mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, Baraza litaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa 18 ambalo litatumika kwa shughuli za kiofisi na kibiashara kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* na mwekezaji binafsi, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kipindi cha mwaka 2009/2010, ilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 284.1 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14 ikilinganishwa na shilingi bilioni 249.1 mwaka 2008/2009.

Pamoja na ongezeko hilo la makusanyo, changamoto mbalimbali zilijitokeza ikiwa ni pamoja na kutokidhi gharama za matengenezo ya barabara. Kwa mfano, mahitaji halisi ya matengenezo ya barabara nchini kwa mwaka 2009/2010 ukijumuisha na mahitaji ya malimbikizo ya matengenezo ni shilingi bilioni 480 wakati bajeti kwa ajili ya matengenezo kwa mwaka 2009/2010 yalikuwa shilingi billioni 284.1 tu ambayo ni asilimia 59 ya mahitaji. Upungufu huo wa fedha uliathiri zaidi matengenezo maalum ya barabara.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kuongezeka kwa gharama ya kufanya matengenezo ya barabara kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta, vifaa na mitambo ya ujenzi. Aidha, malimbikizo ya matengenezo ya mtandao wa barabara yamesababisha barabara nyingi kuwa kwenye hali mbaya. Inakadiriwa kuwa, hivi sasa malimbikizo ya matengenezo kwa mwaka ni shilingi bilioni 113.0 kwa Barabara Kuu na za Mikoa na shilingi bilioni 70.0 kwa barabara za wilaya, ujazio *(feeder roads)* na za mijini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Bodi inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 286.9. Aidha, mchanganuo wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Matengenezo ya Barabara Kuu na Barabara za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ni kama unavyooneshwa katika Kiambatanisho Na. 5 (A-F).

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) hadi Mei, 2010, Bodi iliweza kusajili wahandisi wazalendo 541 na wageni 61 na kampuni za ushauri wa kihandisi 9, ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2008/09 ambapo ilisajili wahandisi wazalendo 461 na wageni 56. Haya ni mafanikio ya ongezeko la wahandisi la asilimia 17 kwa wahandisi wazalendo na asilimia 9 kwa wageni. Hadi kufikia Juni 2010, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa utaratibu wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi wote ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, Bodi imeendelea pia kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Juni 2010, Bodi ilisimamia mafunzo kwa wahandisi wahitimu 998 na kufanya jumla ya wahandisi wahitimu 1,496. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya wahandisi wahitimu 501 walihitimu na walisajiliwa kama Wahandisi wataalam *(Professional Engineers),* jumla ya miradi 285 ilikaguliwa, wahandisi wageni 61 walisajiliwa na 7 walikataliwa usajili kwa sababu hawakuwa na sifa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, katika kipindi cha 2009/2010, Bodi ilikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo; ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu, kufanya kaguzi za miradi nk, Wahandisi wengi kuikimbia taaluma kutokana na imani kwamba masilahi katika fani ya uhandisi ni madogo ukilinganisha na fani nyingine na ikizingatiwa kwamba, mafunzo huchukua miaka mingi kuhitimu uhandisi pamoja na uhaba wa ofisi ambao unasababisha upungufu wa wafanyakazi. Jitihada za kupata eneo la kujenga ofisi bado zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Bodi imepanga kusajili wahandisi 725, Mafundi Sanifu 200 na kampuni za ushauri wa kihandisi 20, kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya vitendo kwa wahandisi wahitimu 1,220. Bodi itafanya ukaguzi wa shughuli za kihandisi katika Halmashauri zote na miradi yote mikubwa.

Malengo mengine ni kuendelea kuwashawishi wahandisi wataalamu ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani. Kutembelea mikoa yote kuhamasisha utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Wahandisi namba 24 ya mwaka 2007 pamoja na kanuni zake na kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaamu wote.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(CRB)* katika mwaka 2009/2010, Bodi ilisajili makandarasi wapya 930 na hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa hadi Januari 2010 kufikia 5,698 ikilinganishwa na Makandarasi 5,125 mwaka 2008/2009. Hili ni ongezeko la Makandarasi 573. Aidha, jumla ya makandarasi 154 walipandishwa madaraja yao ya usajili baada ya kukuza uwezo wao na kukidhi vigezo vya madaraja ya juu. Idadi ya Makandarasi waliopandishwa madaraja ya usajili yaliongezeka kutoka 142 mwaka 2008/2009 hadi kufikia makandarasi 154 katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari - Disemba 2009 jumla ya miradi 1,765 ilikaguliwa. Miradi 1,235, ambayo ni sawa na asilimia 70 haikuwa na upungufu na miradi 530, sawa na asilimia 30 ilikutwa na mapungufu mbali mbali yakiwemo; kutokuzingatia afya na usalama kazini (11.6%), kutokusajili mradi (17%) na kufanya kazi zinazozidi daraja la usajili (2.6%). Makandarasi waliokutwa na upungufu walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Idadi ya miradi ya ujenzi iliyokaguliwa na Bodi na haikuwa na upungufu iliongezeka kutoka miradi 1,119 mwaka 2008/2009 hadi kufikia miradi 1,235 mwaka 2009/2010.

Katika mwaka 2009/2010, Bodi iliendesha kozi sita [6] kupitia mpango wake wa mafunzo endelevu kwa makandarasi *(Sustainable Structured Training Program)* katika Mikoa ya Kagera, Dar es Salaam, Ruvuma, Moshi, Morogoro na Tabora ambapo jumla ya washiriki 373 walihudhuria ikilinganishwa na washiriki 285 katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kukuza uwezo wa makandarasi wazalendo, kwani, ingawa makandarasi wa kizalendo ni asilimia 96, gawio la soko *(market share)* bado ni dogo (34%). Hii inatokana na makandarasi kuwa na uwezo mdogo kiutendaji. Ili kukabiliana na changamoto hii, Bodi imebuni Mkakati wa Makusudi wa Kuendeleza Makandarasi Wazalendo ili waweze kufanya kazi zenye thamani kubwa.

Uwezo wa makandarasi wazalendo unaathiriwa na kutokuwa na mitambo ya ujenzi. Ili kukabiliana na changamoto hii, Bodi imekamilisha utafiti ambao una mapendekezo ya kuwezesha makandarasi wazalendo kupata miradi. Baadhi ya mapendekezo hayo ni kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika vituo vya kukodisha mitambo *(plant hire pools)* na pia kuhamasisha asasi za kifedha kuwawezesha makandarasi kutumia *Lease Financing* katika kununua mitambo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Bodi imepanga kusajili makandarasi wapya 803 na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi 1,980. Aidha, Bodi inatarajia kuendesha kozi tano kwa ajili ya kujenga uwezo wa makandarasi ikiwa ni pamoja na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Makusudi wa Kuendeleza Makandarasi Wazalendo.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Bodi imeendelea kuwasajili Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ambapo katika mwaka 2009/10, jumla ya wabunifu majengo 21 na wakadiriaji majenzi 15 walisajiliwa na hivyo kufanya jumla ya wataalamu waliosajiliwa na Bodi kufikia 460. Usajili huu ni ongezeko la wataalam 27 ikilinganishwa na jumla ya wataalam 433 waliosajiliwa hadi kufikia mwaka 2008/2009. Aidha, Kampuni 8 za wabunifu majengo na kampuni 11 za ukadiriaji majenzi zilisajiliwa na kufanya jumla ya kampuni zilizosajiliwa kufikia 222. Hili ni ongezeko la kampuni 19 ikilinganishwa na kampuni zilizosajiliwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Bodi pia iliwasajili wataalam wa fani hizi wenye sifa za kati 25 na kufanya jumla ya wataalam wa sifa za kati waliosajiliwa na Bodi kufikia 62. Mafanikio haya katika usajili ni matokeo ya mpango unaogharimiwa na Serikali wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahitimu wa taaluma katika fani hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/10, ukaguzi wa majenzi ulifanyika katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara. Jumla ya sehemu za majenzi 999 zilikaguliwa ikilinganishwa na majenzi 610 yaliyokaguliwa mwaka 2008; hili ni ongezeko la sehemu za majenzi 389 zilizokaguliwa. Ukaguzi wa mwaka 2009 ulilenga katika kuhakikisha kwamba wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi wanahusishwa katika sehemu za majenzi na wanatoa huduma za kitaalamu zinazokidhi mahitaji ya jamii na mazingira. Aidha, Bodi ilihakikisha kwamba katika sehemu za majenzi kwa mujibu wa sheria kunakuwepo bango linaloonesha jina na anwani ya mradi, mwenye mradi, wataalam na mkandarasi wa mradi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, jumla ya majenzi 59 yalisimamishwa kwa muda, wakati waendelezaji na wataalam 72 walichukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kulipa faini kwa mujibu wa sheria kutokana na kukiuka taratibu za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali kupitia Bodi itaendelea kutafuta namna bora ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya mwaka 2010. Ili kufanikisha lengo hilo msukumo

mkubwa utakuwa kwenye kuimarisha raslimali watu na elimu kwa umma. Aidha, Bodi imepanga kuwasajili wabunifu majengo na wakadiriaji majenzi wapya 50, kuwasajili Wataalam wenye sifa za kati 28 na Makampuni ya ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi 28.

Mheshimiwa Spika, vile vile Bodi ina mpango wa kutembelea mikoa yote ya Tanzania Bara kuwaelimisha waendelezaji wa miradi ya ujenzi kuhusu umuhimu wa kutumia wataalam waliosajiliwa na Bodi katika miradi yao. Bodi pia itachukua hatua za kisheria kwa watakaokiuka taratibu za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Usambazaji wa Tekinolojia katika Sekta ya Uchukuzi *(Tanzania Transportation Technology Transfer (TANT$^2$ - Centre)* kilianzishwa mwaka 1997 kutokana na juhudi za Wizara yangu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam pamoja na msaada wa Shirika la Barabara la Marekani *(US FHWA).* Madhumuni ya Kituo hiki ni kuimarisha/kuboresha sekta ya uchukuzi kwa kutumia mbinu ya usambazaji wa tekinolojia katika sekta ya uchukuzi kwa wadau.

Kituo kilianza kwa kujihusisha na usambazaji wa tekinolojia katika sekta ya barabara tu. Hata hivyo kutokana na mapendekezo ya utafiti uliofanyika mwaka 2002 kuhusu uimarishaji wa Kituo na kuwezesha huduma zake kuwa zenye ufanisi mkubwa na endelevu, kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004, Kituo hiki kilianza rasmi usambazaji wa tekinolojia katika sekta ya uchukuzi kwa ujumla. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ina mpango wa kuendelea kukiendeleza Kituo hiki ili kiweze kusambaza tekinolojia kwa ufanisi zaidi katika sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, Vikosi vya Ujenzi vilianzishwa kwa Sheria ya Vikosi vya Ujenzi Na. 23 ya mwaka 1974 ili kufanya kazi za ujenzi pamoja na kubuni miradi yoyote ya kibiashara yenye mahusiano na kazi za majenzi. Vikosi vya Ujenzi vimeendelea kutekeleza kazi za kandarasi mbalimbali zinazopatikana kwa maelekezo ya Serikali au kupatikana kwa njia ya ushindani.

Katika mwaka 2009/2010, Vikosi vya Ujenzi vimekuwa vikitekeleza miradi ya ukarabati na uhifadhi wa Jengo la Boma la Kale Bagamoyo, ujenzi wa jengo la nane nane la Wizara ya Miundombinu Dodoma, ujenzi wa nyumba za viongozi Dar es Salaam na Mwanza, ujenzi wa kituo cha mabasi Mkata – Handeni, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Nyamagana, Ofisi ya Mtendaji Kata Enduimat Longido na ujenzi wa *Community Centres* za Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika vituo vya Mafia, Rufiji na Kilwa. Aidha, katika mwaka 2010/2011, Vikosi vya Ujenzi vinategemea kuendelea kukamilisha miradi iliyopo pamoja na miradi mipya itakayopatikana.

Mheshimiwa Spika, Kanda za Maendeleo *(Development Corridors)* Tanzania ina kanda nne za maendeleo; kanda hizo ni Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara; Ukanda wa Maendeleo wa Kati; Ukanda wa Maendeleo wa Tanga; na Ukanda wa Maendeleo wa Dar es Salaam. Katika jitihada za kuendeleza Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara, miradi kadhaa inaendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na maandalizi ya ujenzi wa barabara kutoka Bandari ya Mtwara hadi Bandari ya Mbamba Bay kwa kiwango cha lami. Ili

kuwezesha utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga, Serikali iko katika maadalizi ya ujenzi wa Barabara ya Itoni (Njombe) – Mchuchuma/Liganga – Manda (km 250) kwa kiwango cha lami. Aidha, Serikali inafikiria kujenga njia ya reli kati ya Makambako – Lindi – Mtwara kwa lengo la kufanikisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukanda wa kati, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya reli na bandari katika Ukanda huu. Upembuzi yakinifu wa mradi wa kujenga reli ya kutoka Dar es Salaam - Isaka – Kigali/Keza – Gitega – Musongati umekamilika. Utekelezaji wa mpango wa kupanua bandari ya Dar es Salaam na za Maziwa Makuu unaendelea ili kuhimili ongezeko la mahitaji ya matumizi ya bandari zetu na kurahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha Ukanda wa Maendeleo wa Tanga, ambapo miradi ya barabara, reli na bandari imependekezwa. Uendelezaji wa miradi iliyoainishwa utachochea ukuaji wa shughuli za maendeleo katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika Ukanda wa Tanga. Kwa upande wa barabara, Serikali inaendelea na jitihada za kuboresha barabara ya Tanga – Horohoro (km 65) kwa kiwango cha lami ambapo mkataba wa ujenzi ulisainiwa Disemba, 2009. Sambamba na mchakato wa kuanzishwa mradi wa kuvuna magadi katika Ziwa Natron, imependekezwa ijengwe Barabara mpya kwa kiwango cha lami kutoka eneo la mradi hadi Longido (km 99), reli mpya kati ya eneo la mradi na Arusha (km 164), uboreshaji wa reli ya Tanga – Arusha (km 437). Imependekezwa pia ijengwe bandari mpya katika eneo la Mwambani Tanga, ambayo itaongeza ufanisi wa bandari ya Tanga. Jitihada mbalimbali zinaendelea ili kuhakikisha kuwa mapendekezo hayo yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa Maendeleo wa Dar es Salaam unaendelea kuimarishwa kwa kuboresha miundombinu ya reli ya TAZARA, barabara na bandari ya Dar es Salaam. Miradi inayoendelea katika ukanda huu kwa upande wa bandari ni ujenzi na maandalizi ya maegesho ya magari katika bandari ya Dar es Salaam ili kupunguza msongamano bandarini. Miradi mingine inayoendelea ni ukarabati wa barabara kutoka Iyovi – Kitonga na Ikokoto – Iringa, pamoja na uimarishaji wa njia ya reli ya TAZARA eneo la Kitete – Mpanga.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano kati ya Serikali ya Muungano (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Wizara imeendelea kufanya vikao vya mara kwa mara katika ngazi ya Mawaziri na Watendaji Wakuu wa Wizara ya Miundombinu (SMT) na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ). Kikao katika ngazi ya Mawaziri kilifanyika tarehe 16 Novemba, 2009 Pemba ambapo tulijadili masuala ya utendaji wa kisekta. Aidha, tulipata nafasi ya kukagua miradi ya ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia mpya na nyepesi ya *Ro – mix,* bandari za Wete na Chake Chake pamoja na kujadiliana juu ya masuala mbalimbali yenye kero katika sekta zetu. Aidha, tumekuwa tukishiriki pamoja katika mikutano mbali mbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa inayohusu sekta ya uchukuzi. Tutaendelea kukutana mara kwa mara ili kuondoa kero mbali mbali katika

sekta ya Uchukuzi. Namshukuru sana Mhe. Machano O. Said Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi – SMZ kwa ushirikiano anaoendelea kunipa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushiriki kwenye mikutano mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuzungumzia masuala yanayohusu usafiri wa barabara, maji, reli, anga na masuala ya hali ya hewa. Katika ushirikiano huu, miradi mbalimbali ya miundombinu imeibuliwa na kufanyiwa maamuzi ya pamoja. Mradi mkubwa ni ule wa Mtandao wa barabara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African Road Network Project* – EARNP) pamoja na Mradi wa Uwezeshaji wa Kiuchukuzi na Kibiashara Afrika Mashariki (*East Africa Trade and Transport Facilitation Project* – EATTFP). Miradi hii inalenga katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa barabara za kikanda kwa kiwango cha lami pamoja na kuoanisha sera na mikakati mbali mbali kuhusu miundombinu kama kiungo muhimu cha kiuchumi. Jumuiya inakamilisha Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Uchukuzi na programu ya Barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga – Athi River umekamilika kwa takriban kilometa 29. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Arusha – Holili - Voi na Bagamoyo – Saadani - Tanga - Horohoro – Malindi inaendelea. Aidha, kituo cha pamoja cha Forodha cha Namanga (*One Stop Border Post)* kitajengwa chini ya mkataba wa ujenzi wa mradi wa barabara ya Arusha - Namanga – Athi River.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Makubaliano ya Itifaki ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa ya Nchi Wanachama wa SADC ya mwaka 1998 *(The SADC Protocol on Transport, Communication and Meteorology of 1998)*, Wizara imeendelea kushiriki katika vikao mbalimbali vya SADC kuhusu masuala ya uoanishaji wa tozo za ushuru wa barabara na uoanishaji wa viwango vya uzito na ukubwa wa magari, uendelezaji wa Kanda za Uchukuzi na ulegezaji wa masharti katika usafiri wa anga. Lengo ni kufungua njia za mawasiliano ya uchukuzi wa barabara na anga ili kuwezesha kukuza biashara kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utekelezaji wa masuala muhimu yaliyopo katika Itifaki ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa, Wizara bado ina jukumu la msingi katika uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi ili kuiunganisha nchi yetu na nchi wanachama wa SADC. Miongoni mwa miradi iliyopo katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara ni pamoja na ujenzi wa barabara za Mtwara – Mbamba Bay na Tunduma – Sumbawanga – Kasulu – Nyakanazi zitakazoiunganisha nchi yetu na nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia na DRC pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Daraja la Umoja linaloiunganisha nchi yetu na Msumbiji. Uboreshaji wa usafiri wa reli ya TAZARA na huduma za usafiri katika Bandari za Mtwara, Kasanga na Mbamba Bay utaendelea kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara imetekeleza muundo wake mpya na kujaza nafasi za Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi kulingana na Muundo huo. Wizara imeendelea kuwahudumia watumishi wake katika nyanja za kitaaluma na kijamii. Katika kipindi hiki, Wizara ilipeleka watumishi 97 katika mafunzo ndani na nje ya nchi. Kati yao, watumishi 19 walipelekwa mafunzo ya muda mrefu na 65 mafunzo ya

muda mfupi ndani ya nchi, na watumishi 13 walipelekwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 14 wa kada mbalimbali na kuthibitisha kazini watumishi 23. Wizara ilipata vibali 59 vya ajira za wataalam wa kigeni ambapo wataalam 29 walipatiwa vibali vya ajira mpya, na wataalam 30 waliongezewa muda wa kufanya kazi nchini. Wizara pia iliweza kuzindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kuwaelimisha wafanyakazi wote katika semina mbali mbali, kuhusu athari za Rushwa katika sekta yetu, makosa ya rushwa yanayoweza kutendeka na kuwahimiza kuepukana na makosa hayo. Aidha, Wizara iliendelea kuwasaidia watumishi waishio na virusi vya UKIMWI kwa kuwagharamia chakula chenye lishe bora kwa waliojitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/11, hadhi za Wakuu wa sehemu katika Idara ya Utawala na Utumishi; na Idara ya Sera na Mipango zimepandishwa na kuwa na hadhi ya Wakurugenzi Wasaidizi. Aidha, utaratibu wa kupeleka watumishi mafunzoni utaendelea kwa awamu kwa lengo la kuwaongezea ujuzi, ufanisi, na tija katika kufanya kazi zao. Watumishi 183 wamepangiwa kupewa mafunzo. Kati yao, watumishi 142 watakwenda kwenye mafunzo ya muda mfupi na wengine 41 watakwenda kwenye mafunzo ya muda mrefu. Aidha, Wizara itajaza nafasi 14 zilizo wazi baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Wizara itaendelea kuwasaidia watumishi waishio na virusi vya UKIMWI kwa kuwagharamia chakula chenye lishe bora kwa wataojitokeza na kuwahamasisha watumishi wengine kupima afya zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa miradi yote ya maendeleo ya miundombinu inatekelezwa kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira kwa kutumia Sera, Sheria, Kanuni na Mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa na Serikali. Katika 2009/2010, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 ikiwa ni pamoja na kupitia taarifa za Tathimini ya Athari kwa Mazingira (TAM) za miradi ya barabara 16 na mradi wa ujenzi wa Gati Na.1 katika Bandari ya Mtwara.

Katika ukaguzi wa barabara uliofanyika, imegundulika kuwepo kwa uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na vyombo vya usafiri. Kutokana na hali hii, Wizara kwa kuanzia inatarajia kujenga vituo vya kupumzikia katika maeneo ya Nangurukuru, barabara za Dar es Salaam – Lindi – Mtwara na Mkata katika barabara ya Dar es Salaam – Arusha. Aidha, Wizara iliandaa kanuni kwa ajili ya kuzingatia uhifadhi wa mazingira wakati wa ujenzi wa barabara. Kanuni hizo ni Mfumo wa Usimamizi wa Uhifadhi wa Mazingira, Mwongozo wa Kutathmini na Kusimamia Uhifadhi wa Mazingira ya Barabara na Kanuni za Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya Barabara.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilifanya mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari na Uhifadhi wa Mazingira ya barabara kwa Wahandisi 100 na Mafundi Sanifu 130 kutoka katika Halmashauri za Miji na Wakala wa Barabara (TANROADS). Kupitia Mradi wa

utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, Wizara ilishirikiana na wadau husika kutoa elimu ya kuhifadhi mazingira ya Bahari na Maziwa kwa Wadau wa vyombo vya Uchukuzi Majini katika Bandari za Mwanza, Mtwara, Ziwa Tanganyika na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa miradi ya miundombinu inatekelezwa kwa kuzingatia maendeleo endelevu ya uhifadhi wa mazingira, kuandaa Kanuni za ujenzi na uendeshaji wa viwanja vya ndege na bandari.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuelimisha Umma kuhusu shughuli za Sekta ya ujenzi, uchukuzi na hali ya hewa kupitia njia mbali mbali za upashanaji habari. Aidha, tovuti za taasisi zilizo chini ya Wizara ya Miundombinu zimeunganishwa katika Tovuti ya Wizara ili kumwezesha mtumiaji kupata Rejea za taarifa mbalimbali kwa urahisi. Wizara pia imeendelea kuratibu na kuandaa vipindi maalum kwenye televisheni kwa lengo la kuelezea matukio mbalimbali ya sekta, mafanikio yaliyopatikana na matarajio ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara itaendelea na kampeni za upashaji habari na utoaji elimu kwa Umma kupitia vyombo vya habari, mabango, vipeperushi na majukwaa mbalimbali yakiwemo matamasha ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inathamini mchango unaotolewa na vyuo vyetu vya mafunzo katika kutoa Wataalam wa kada mbalimbali kuhusu masuala ya ujenzi, uchukuzi na hali ya hewa. Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Miundombinu ni pamoja na; Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT),* Chuo cha Bahari Dar es Salaam *(DMI),* Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma, Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam, Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo Cha Matumizi ya Teknolojia Stahili ya Nguvu Kazi *(Appropriate Technology Training Institute – ATTI)* Mbeya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/10, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 269 wa kozi ndefu ikilinganishwa na jumla ya wanafunzi 248 waliodahiliwa katika mwaka 2008/2009. Hili ni ongezeko la asilimia 8. Kwa upande wa kozi za muda mfupi za aina mbalimbali, Chuo kiliendesha kozi kwa wanafunzi 1,701. Aidha, Chuo kimeweza kuboresha mitaala yake na kutoa mafunzo ambayo yanakidhi mahitaji ya soko la ajira na kujiajiri baada ya kupata ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Mafunzo hayo yanatolewa katika mfumo wa *Competence Based Education and Training (CBET)* katika ngazi ya Stashahada na Shahada ya Kwanza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Chuo kiliweza kutekeleza Mpango Mkakati wake ulioanza mwaka 2005 na kumalizika 2009 kwa asilimia 30 kutokana na ukosefu wa fedha pamoja na upungufu wa vitendea kazi kama vile maktaba, maabara za kufundishia, vifaa vya karakana, magari ya kufundishia, uhaba wa mabweni kwa wanafunzi na uhaba wa nyumba za wahadhiri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11, Chuo kimepanga kuendelea kuipitia mitaala yake na kuongeza idadi ya programu, kuimarisha uwezo wa wanataaluma wa Chuo, kuimarisha kozi za udereva wa kujihami, kuimarisha ukaguzi wa magari na utahini wa madereva, kuimarisha menejimenti ya Lojistiki ya Mizigo na kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike kutoka asilimia 20 hadi asilimia 35 ya wanafunzi wote.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kimeendelea kutoa huduma za mafunzo, utafiti, ukarabati wa vifaa vya kuokolea maisha na uwakala wa ajira kwa Wafanyakazi melini. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga katika kuendeleza rasilimali watu katika sekta ya usafiri majini. Katika kipindi hiki, Wanafunzi 378 wa kozi ndefu na 5,087 wa kozi fupi walijiunga na chuo ikijumuisha Wanafunzi wa ndani na nje ya nchi. Wanafunzi wa nje walitoka katika nchi za Kenya, Uganda, Comoro na Namibia. Aidha, udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu umekuwa ukiongezeka baada ya wanafunzi wa stashahada ya juu kupata udhamini wa Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo uhaba wa vifaa vya kufundishia, miundombinu na ugumu wa kupata ajira kwa wahitimu wa chuo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China zina mpango wa kutatekeleza mradi wa maendeleo wa chuo cha Dar es Salaam kupitia ushirikiano kati ya Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Usafiri Majini cha Dalian cha China; ambapo Chuo kikuu cha Dalian kitajenga tawi la chuo hicho ndani ya chuo cha Dar Es Salaam. Miundombinu itakayojengwa itakidhi mahitaji ya soko la elimu na mafunzo yanayohusu bahari. Aidha, Chuo kimepanga kununua *Engine Room Simulator* kwa ajili ya mafunzo ya vitendo ya wanafunzi Wahandisi wa meli.

Chuo kwa kushirikiana na SUMATRA, kitaelekeza nguvu zake katika kutafuta ajira kwa wahitimu wake katika meli za mataifa ambayo yatasaini mikataba ya ushirikiano na SUMATRA ya kutambua vyeti vya wahitimu kutoka chuo cha bahari. Aidha, Chuo kitaendelea kujitangaza ili kupata wanafunzi wengi zaidi wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usafiri wa Anga *(Tanzania Civil Aviation Training Centre)* kimeendelea kutoa mafunzo yahusuyo shughuli za usafiri wa Anga na uendeshaji wa viwanja vya ndege. Mafunzo hayo hutolewa kwa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2009/10, idadi ya wahitimu kutoka chuo hicho ilikuwa 110 ikilinganishwa na wahitimu 269 katika kipindi cha mwaka 2008/09 ikiwa ni pungufu ya asilimia 59.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Chuo katika kipindi cha mwaka 2009/10 ni pamoja na kuwaendeleza kitaaluma wakufunzi 20, Chuo kuendelea kupokea wanafunzi kutoka nchi za Botswana, Namibia, Uganda na Rwanda. Aidha, Chuo kilishinda na kupewa mkataba wa kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya kitaaluma kwa

ajili ya Mamlaka ya viwanja huko Msumbiji na hivyo kuendelea kuiingizia nchi fedha za kigeni na pia kutunukiwa cheti na Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Namibia cha kutambua ubora wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/11, Chuo kimepanga kuongeza idadi ya kozi zinazotolewa na chuo ikiwa ni pamoja na kuwa na majengo yake. Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imeendelea kuboresha Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kwa kujenga madarasa mawili. Jumla ya wanafunzi 227 walihitimu mafunzo ya awali na ya kati ya utabiri. Aidha, mafunzo ya muda mfupi na mrefu yamekuwa yakitolewa kwa wafanyakazi wa kada mbalimbali kulingana na mpango wa mafunzo wa Mamlaka. Katika mwaka wa 2010/2011, Chuo kinatarajia kuendelea kutoa mafunzo ya awali na ya kati katika fani ya hali ya hewa.

Mheshimiwa spika, Chuo cha Ujenzi Morogoro kilianzishwa mwaka 1962 kwa ajili ya kuendeleza taaluma za mafundi sanifu, stadi na Wahandisi wa Wizara za Miundombinu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, Chuo kwa sasa kinatoa mafunzo kwa mafundi sanifu na stadi wanaoshiriki kazi za ujenzi kwenye sekta zote za umma na binafsi. Hadi kufikia Mei, 2010, Chuo kimetoa mafunzo kwa Wanafunzi 346 kwa ngazi ya Ufundi Sanifu kwa fani ya barabara na majengo, 106, kwa fani ya Ufundi, madereva bingwa wa umma 40, madereva waanzaji 116 na mafundi stadi waanzaji 84.

Mheshimiwa spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/11, Chuo kimepanga kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la madarasa na karakana ya ufundi, kukarabati majengo manne, kununua samani, zana ndogo ndogo za kufundishia, kufundisha jumla ya wanafunzi 440 wa fani ya ufundi sanifu wa barabara, majengo na ufundi 120, madereva bingwa wa umma 50, madereva waanzaji 190, na mafundi stadi waanzaji toka fani za barabara, majengo na ufundi 80.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahili ya Nguvu Kazi katika ujenzi na matengenezo ya barabara *(Appropriate Technology Training Institute – ATTI)* Mbeya, katika mwaka wa fedha 2009/10, kimeendelea kutoa elimu ya matumizi ya teknolojia ya nguvu kazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara. Mafunzo hayo yametolewa kwa Makandasi wa Nguvu kazi, Wahandisi kutoka Halmashauri za Wilaya katika mikoa ya Tabora, Singida, Mbeya, Rukwa, Dodoma na sekta binafsi. Aidha, mafunzo yametolewa kwa wanawake wanaofanya kazi kwa kutumia teknolojia Stahili ya nguvu kazi na wanaotarajia kuanzisha kampuni za Ukandarasi kwa kutumia teknolojia Stahili ya Nguvu kazi.

Katika mwaka 2010/11, Chuo kitaendelea na usimamizi na utekelezaji wa mpango wa *Taking Labour Based Technology to Scale*, kutoa mafunzo ya teknolojia stahili ya nguvu kazi kwa Makandarasi, Wahandisi toka Halmashauri za Wilaya na sekta binafsi. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa Makandarasi wanaotumia teknolojia stahili ya Nguvu kazi na Wahandisi wa Halmashauri katika mikoa ya Iringa na Ruvuma kwa kugharimiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu, napenda kutoa shukurani za dhati kwa wadau wote wa sekta za ujenzi, uchukuzi na hali ya hewa ikiwemo sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutimiza malengo yetu. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na wadau wengine kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha wakati wa kipindi kigumu cha kukarabati na kurudisha katika hali ya kawaida miundombinu ya barabara na reli iliyoharibiwa na mvua kubwa zilizonyesha kati ya Disemba 2009 na Januari 2010. Shukrani zetu pia ziwaendee Washirika wetu wa maendeleo katika kutekeleza programu na mipango yetu ya Sekta. Washirika hao ni pamoja na mashirika ya kimataifa na taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji huduma na miundombinu ya sekta zetu.

Nchi na mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), Kuwait Fund, Jamhuri ya Korea, OPEC Fund, Umoja wa Nchi za Ulaya, Third World Organization for Women in Science (TWOWS), UNESCO, Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, Korea, India, China, Denmark, Norway, Ubeligiji, Ujerumani na wengine wengi. Tungependa waendelee kushirikiana nasi katika kuimarisha sekta yetu na kufanikisha malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru tena Kamati ya Bunge ya Miundombinu ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga (Mb), Mbunge wa Jimbo la Singida Kusini na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa michango na ushirikiano waliotupa katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara.

Mheshimiwa Spika, shukurani zetu pia ziwafikie wadau mbalimbali hasa wa sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya sekta zetu. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango na ushirikiano mlionipa katika kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara.

Mheshimiwa Spika, ninapofika mwisho wa hotuba hii sina budi kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje (Mb), Katibu Mkuu Mhandisi Omar Abdallah Chambo, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Wote kwa pamoja wamenipa ushirikiano mkubwa ambao umenisaidia kutekeleza majukumu niliyopewa ya kusimamia uendelezaji wa Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Hali ya Hewa. Michango yao ya mawazo na utendaji wao mzuri yamewezesha kufanya kazi yetu kuwa rahisi na yenye mafanikio. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ipasavyo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, naomba bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,164,983,227,000 Kati ya fedha hizo, shilingi 293,429,311,000 ni kwa matumizi ya kawaida na shilingi 871,553,916,000 ni kwa ajili ya

miradi ya maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida inajumuisha shilingi 56,743,044,000 za mishahara ya watumishi na shilingi 236,686,267,000 ni fedha za Matumizi Mengineyo *(OC).* Fedha za Miradi ya Maendeleo inajumuisha shilingi 370,880,081,000 za ndani na shilingi 500,673,835,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa mara nyingine nitoe shukurani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.infrastructure.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha majedwali ya miradi yote itakayotekelezwa katika mwaka 2010/2011 pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Miundombinu au mwakilishi wake ili atoe maelezo na maoni ya Kamati.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/11.

Naomba sasa nichukue fursa hii, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Miundombinu, naipongeza Wizara ya Miundombinu kwa maandalizi, ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hiyo mbele ya Kamati yangu kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya 2010/2011. Aidha, Wizara iliwasilisha pia Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati na Mipango ya Bajeti ya 2009/2010 na kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata pia fursa ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka 2010/2011 kama yalivyowasilishwa na Wizara ya Miundombinu mbele ya Kamati tarehe 2 - 4 na

tarehe 11 Juni, 2010. Baada ya kuwasilishwa kwa Mpango na Bajeti ya Wizara hiyo, Kamati yangu haikuridhishwa na Bajeti finyu na isiyotekelezeka na hivyo kuahirisha vikao hivyo ili kukutana na Serikali kupata maelezo ya namna Bajeti hiyo inavyoweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu ofisini kwake tarehe 4 Juni, 2010 na kujadiliana naye kuhusu Bajeti ya Wizara ya Miundombinu ya Mwaka 2010/2011, ambayo haikuzingatia madeni ya Wakandarasi yapatayo shilingi bilioni 305 pamoja na madeni ya fidia za Wananchi waliopisha maeneo ya kuendeleza miradi. Kwamba, Wizara haiwezi kuanza kutekeleza Bajeti mpya wakati kuna madeni hayo ya zaidi ya shilingi bilioni 305 katika miradi ya barabara pamoja na madeni mengine, ambayo kama yasingelipika yangekuwa na athari kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Fedha kukutana kwa maelekezo ya Waziri Mkuu, Kamati yangu ilikutana tena na Wizara hii tarehe 11 Juni, 2010 hapa Dodoma ili kukamilisha shughuli ya kujadili Bajeti ya Wizara hiyo. Taarifa iliyowasilishwa na Waziri wa Miundombinu baada ya Bajeti ya Wizara hiyo kupitiwa tena na Wizara ya Fedha na Uchumi kwamba madeni ya miradi ya barabara ya bilioni 305 yamehakikiwa na sasa madeni yaliyobaki ni shilingi bilioni 259.256 baada ya Serikali kutoa shilingi bilioni 35.7 zilizosalia katika Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Aidha, Serikali ilitoa shilingi bilioni 100 kulipia malipo ya awali kwenye baadhi ya miradi. Kwamba, deni lililobaki sasa lilikuwa shilingi bilioni 123.5. Katika hatua hiyo, Kamati yangu haikuridhika na hivyo kutopitisha Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na kuhitaji maelezo ya ziada ili kujua wapi fedha hizo zingepatikana, kwani kungeathiri miradi mingi ya barabara na Wakandarasi, ambao wameshaingia mikataba na Serikali wangeweza kudai fidia na hivyo kuwa tatizo kubwa zaidi. Serikali iliendelea kujadili namna ya kuweza kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Juni, 2010 Wizara iliwasilisha tena Bajeti yake mbele ya Kamati ya Miundombinu, ambapo baada ya kuhakikiwa tena na maagizo ya Waziri Mkuu kutekelezwa, Wizara iliweza kuainisha maeneo ya fidia kutoka shilingi bilioni 75.2 hadi shilingi bilioni 53.4; kupunguza mahitaji kwa shilingi bilioni 21.8 na hivyo kufanya deni la shilingi bilioni 123.5 kupungua na kuwa shilingi 101.7. Aidha, Serikali ilisema itakopa shilingi bilioni 50 kutoka katika mifuko ya pensheni na kwamba shilingi bilioni 51.7 zilizobaki Serikali itajibana kwa kupunguza matumizi yake yenye vipaumbele vya chini, kusitisha ununuzi wa magari na posho ili kumaliza deni hilo. Katika hatua hiyo, Kamati yangu iliridhika na kupitisha Bajeti ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika kikao kilichofanyika tarehe 29 Mei, 2009 baina ya Kamati na Wizara ya Miundombinu, jumla ya maagizo 41 yalitolewa kwa utekelezaji. Wizara iliyafanyia kazi maagizo hayo na hatimaye kufikia hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, yapo maagizo ambayo yametekelezwa kwa ukamilifu na yapo maagizo, ambayo utekelezaji wake ni wa muda mrefu na bado Wizara inaendelea kuyafanyia kazi. Kamati kimsingi imeridhika na hali ya utendaji wa Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka 2009/2010, Wizara iliweka malengo ya kukusanya Mapato ya shilingi 30,503,000. Mpaka kufikia Mei 2010, jumla ya shilingi 53,771,085 zilikuwa zimekusanywa na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 176. Ongezeko hilo limetokana na marejesho ya fedha za Serikali, ada ya ukaguzi na usajili wa magari ya Serikali pamoja na uuzaji wa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Wizara ilitengewa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida shilingi bilioni 270.85 ikiwa ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na ruzuku kwa Taasisi na Matumizi mengineyo; baadaye ziliongezwa shilingi bilioni 15.33 kulipia mishahara ya RAHCO na TRL na hivyo kufanya fedha zilizotolewa kwa mwaka 2009/2010 kuwa shilingi bilioni 286.18.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2009/2010, Serikali ilitenga shilingi bilioni 570.531 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 340.150 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 230.381 zilikuwa ni fedha za nje. Mpaka kufikia robo ya tatu ya mwaka 2009/2010 ziliongezwa shilingi bilioni 15.6 kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya miundombinu ya reli iliyoharibiwa na mafuriko. Hii ilifanya fedha zote za ndani zilizotolewa kwa mwaka 2009/2010 kufikia shilingi bilioni 355.75.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wizara imepata mafanikio katika utekelezaji wa mipango ya mwaka 2009/2010, kama ilivyofafanuliwa katika taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa mradi. Aidha, mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:-

- Kupitishwa kwa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya Mwaka 2010 *(The Architects and Quantity Surveyors Registration Act, 2010)* na kukamilika kwa Kanuni 12 za sheria mbalimbali zilizowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

- Usajili wa ndege 15 hapa nchini na 10 kati ya hizo zikiwa mpya pamoja na ongezeko la abiria kwa usafiri wa anga kutoka abiria 2,791,381 mwaka 2008/2009 hadi abiria 2,963,916 kwa mwaka 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la 6.1%.

- Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) ilitunukiwa Cheti cha Kimataifa cha Ubora na kuwa taasisi ya pili baada ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Afrika Kusini.

- Kukamilika kwa ujenzi wa miradi ya barabara 26 (zenye jumla ya km 2,237), kukamilika kwa ujenzi wa Daraja la Umoja, kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara mbalimbali, ukarabati wa barabara na ujenzi wa madaraja zaidi ya 50.

- Kukamilika kwa ujenzi wa Kivuko cha Mto Pangani, ununuzi wa vivuko vipya vya Utete, Rugezi-Kisorya na ukarabati wa MV Kigamboni na MV Sengerema

pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Magogoni, Pangani, Kigongo-Busisi na Kome.

- Kukamilika kwa utekelezaji wa Muundo wa Wizara na kujazwa kwa nafasi za Wakurugenzi na Wakurugenzi Wsaidizi na mafunzo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa Watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa mwaka 2009/2010 ni pamoja na:-

- Serikali kutokuwa na uwezo wa kifedha ikilinganishwa na mahitaji halisi ya miradi ya maendeleo.

- Uhaba pamoja na uduni wa mitambo ya kuwezesha Makandarasi Wazalendo kumudu utekelezaji wa kazi za barabara.

- Ujenzi holela katika maeneo yaliyotengwa kwa hifadhi ya barabara *(road reserves)* na ujenzi usiokidhi sifa na viwango vinavyotakiwa katika ujenzi wa majengo.

- Uwezo mdogo wa baadhi ya Wakandarasi katika kukamilisha miradi ya ujenzi kwa wakati na uwezo duni wa sekta binafsi katika ujenzi na matengenezo ya miundombinu.

- Mrundikano mkubwa wa madeni ya miradi ya barabara ambayo ulipaji wake uliathiri kwa kiasi kikubwa miradi ya ujenzi wa barabara kwa mwaka 2009/2010.

- Baadhi ya Wahisani kuwa na urasimu mrefu wa kutoa fedha wanazotoa kufuatana na ratiba iliyowekwa hivyo kuchelewesha miradi kuanza malipo kwa Makandarasi kwa muda uliokubaliwa katika Mikataba.

- Utaratibu mrefu wa kutoa Zabuni (hasa kwa miradi ya Wahisani) umekuwa ukichelewesha kuanza kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi.

- Ubovu wa miundombinu ya uchukuzi hususan Barabara, Reli na Bandari na hivyo kusababisha mrundikano wa mizigo na makasha bandarini.

- Washitiri kutoelewa lengo la kulipa ada ya ushauri kwa Wakala wa Majengo na kukwamisha malengo ya Wakala, Watumishi waliokopa nyumba za Serikali kutolipa madeni yao kwa wakati na kukwamisha ujenzi wa nyumba mpya.

- Kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi kutokana na mfumko wa bei na mtikisiko wa kiuchumi duniani.

- Ongezeko la ajali za barabarani, majini na reli pamoja na kuwepo kwa majanga ya mvua na mafuriko yanayoharibu miundombinu.

- Utekelezaji wa mpango maalum wa kufanya usanifu, upembuzi yakinifu na ujenzi wa baadhi ya barabara kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha za ndani.

- Ukarabati na ujenzi wa barabara za mikoa na wilaya, kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu maeneo ya hifadhi ya barabara na kuwajengea uwezo Wakala wa Barabara na Majengo kuongeza ufanisi katika sekta hizo.

- Kuimarisha karakana na kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa zana za ujenzi na kuhamasisha watu binafsi kuanzisha kampuni za kukodisha vifaa; pamoja na kukaribisha sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari na majengo ya Serikali.

- Kujenga na kukarabati vituo vya mizani na kuongeza mizani inayohamishika.

- Mafunzo kwa Watumishi ili kuongeza ufanisi, kujenga uwezo kwa Bodi mbalimbali na kutoa mafunzo kwa Wahandisi Washauri na Wakandarasi wa kizalendo waweze kusimamia na kutekeleza vizuri mikataba ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Malengo na Mpango wa Maendeleo wa Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2010/2011 ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005. Aidha, Mpango huu umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo *(Vision 2025),* Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Mkakati wa Kushirikiana na Wahisani *(Tanzania Joint Assistance Strategy),* pamoja na mikakati mbalimbali ya Kitaifa na Kisekta.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kwa kuzingatia Mwongozo wa Matayarisho ya Bajeti, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Mwongozo huo kwa upande wa Wizara ya Miundombinu ni pamoja na kutumia fedha za Mfuko wa Barabara katika matengenezo ya barabara, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara, vivuko na kusimamia utekelezaji wa miradi ya barabara. Aidha, katika mwaka 2010/2011, Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara zitatekeleza majukumu yake kulingana na malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa baadhi ya miradi, mbali na umuhimu wake katika kuendeleza uchukuzi na kukuza uchumi wa nchi kwa haraka, hayakuweza kutengewa fedha kutokana na ufinyu wa Bajeti. Kati ya miradi hiyo yenye thamani ya shilingi bilioni 298,625, ambayo haikutengewa fedha kwa Mwaka 2010/2011 ni pamoja na miradi ya barabara kama vile Bagamoyo – Saadani – Tanga, Makutano – Nyamswa – Fort Ikoma, Arusha – Minjingu, Mbinga – Mbambabay; madaraja kama vile Ruvu Chini, Lukuledi na Gulwe na Kilosa; viwanja vya ndege vya Musoma, Iringa, KIA); reli (reli ya Arusha – Musoma, Tabora – Kigoma); kutengeneza na kununua mabehewa mapya; ujenzi wa nyumba za Viongozi na za Watumishi wa Umma; miradi ya bandari na miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara kupitia Idara mbalimbali na Vitengo vyake, inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 36,272,000. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara imetengewa jumla ya shilingi 293,429,311,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 56,743,044,000 kwa ajili ya kulipia Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Aidha, shilingi 200,858,714,140 ni kwa ajili ya Mfuko wa Barabara na shilingi 35,827,552,860 ni fedha kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC).* Kwa mantiki hiyo, fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo zimepungua kwa shilingi 7,943,281,140 wakati gharama za ujenzi na uendeshaji zimepanda.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011, Wizara imetengewa shilingi 871,553,922,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 370,880,081,000 ni fedha za ndani na shilingi 500,673,841,000 ni fedha za kigeni. Bajeti ya Maendeleo iliyotengwa kwa mwaka 2010/2011 ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Wizara yanayokadiriwa shilingi trilioni 1.3. Wakati fedha hizo zinatengwa kulikuwa na madeni ya miradi ya barabara ya shilingi bilioni 285.9.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka 2009/2010 na kujadili Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka 2010/2011, Kamati ilibaini kuwa kulikuwepo na miradi ambayo haikuwa imetekelezwa au kukamilika. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza mipango ya kazi zake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi kama Dira ya Maendeleo kwa nchi yetu pamoja na kutekeleza ahadi za Viongozi Wakuu wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishukuru Serikali kwa kuthamini maoni na ushauri uliotolewa wakati wa vikao vilivyofanyika tarehe 2, 4 na 11 Juni, 2010 wakati wa kupitia na kujadili mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka 2010/2011; kwani kwa namna moja au nyingine, imesaidia kupatikana kwa fedha ambazo zimelipia madeni ya zaidi ya shilingi bilioni 300 ya miradi ya barabara, ambayo Serikali ilikuwa ikidaiwa.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ikijadili Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2010/2011; ilibaini kuwa, kuna ufinyu wa Bajeti, isiyokidhi Utekelezaji wa Mipango ya Miradi ya Maendeleo kama inavyostahili. Kwa kuangalia fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 871,553,922,000 hazilingani na mahitaji halisi yaliyowasilishwa, ambayo yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 1.3. Katika hali hii, miradi ya barabara na mingineyo haitaweza kutekelezeka. Kamati inaishauri Serikali kuongeza jitihada katika kupata vyanzo vya ziada vya mapato ya ndani hususan katika kutunisha Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Serikali imefanya jitihada za kupata fedha kwa ajili ya kulipia madeni ya miradi iliyokuwa imekwama kwa ukosefu wa fedha, Kamati inasisitiza kuwa ni vyema kuwa na vipaumbele katika kutekeleza miradi inayojipangia kulingana na fedha hasa za ndani badala ya kutegemea fedha za Wafadhili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zoezi la bomoa bomoa nyumba za wananchi ili kupisha upanuzi wa Barabara, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza zoezi hili kwa umakini ili kuepusha manung'uniko ya wananchi hasa pale wanapocheleweshwa kulipwa haki zao za fidia punde zoezi hilo linapokamilika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanza mara moja ujenzi wa miradi maeneo ambayo watu wamehamishwa, kwani kuchelewa kuanza kwa miradi hiyo, husababisha ongezeko la gharama za mradi tofauti na ilivyokadiriwa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka huu wa fedha imedhihirisha kuwa baadhi ya miradi ya barabara haikutengewa fedha kabisa. Miradi hiyo ni kama vile Barabara za Bagamoyo – Saadani – Tanga, Makutano – Nyamswa – Fort Ikoma, Arusha – Minjingu, Mbinga – Mbambabay; madaraja ya Ruvu Chini, Lukuledi, Gulwe na Kilosa. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mkakati utakaowezesha kupatikana kwa fedha za ndani, zitakazotumika kupanga Bajeti itakayokidhi kutekeleza mipango ya miradi ya maendeleo. Aidha, miradi ambayo haikutengewa fedha mwaka huu ipewe kipaumbele *(priorities)* kwa Bajeti ijayo kabla ya kuanza miradi mingine mipya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara zinazohitajika kujengwa ni nyingi; na kwa kuwa Serikali haina fedha za kutosha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutumia mpango wa *Build - Operate and Transfer (BOT), Build - Own - Operate and Transfer (BOOT)* na ule wa *Public Private Patnership (PPP)* kwa uwazi na kuharakisha kutunga Sera husika. Hii itahamasisha Wawekezaji wengi zaidi kujitokeza kushiriki katika ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Kamati ya Miundombinu pamoja na baadhi ya Wabunge mmoja mmoja, wamekuwa wakifuatilia na kuulizia Mradi wa Barabara ya Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa; pamoja na zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Pamoja na majibu yanayotolewa na Serikali, Kamati inashauri kuwa, Serikali sasa ifanye kila jitihada kuweza kukamilisha miradi hiyo na kuhitimisha kilio cha Wananchi wanaotumia barabara hizo. Aidha, Serikali ikamilishe ahadi yake ya Mradi wa *Mtwara Development Corridor* na kufungua barabara za mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka uliopita, Kamati hii iliwahi kushauri kuhusu ujenzi wa barabara katika Halmashauri zetu uendelee kusimamiwa na TANROADS. Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuangalia upya Sera ya Ujenzi wa Barabara ili kuiwezesha TANROADS kushughulikia miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara zote nchini (za kitaifa, mikoa na wilayani) kwa kuwa uwezo wanao na wataalam wa kutosha wapo. Hii itaokoa fedha nyingi, ambazo hupelekwa katika Halmashauri, ambako hakuna ufanisi kutokana na kutokuwa na wataalamu wanaokidhi sifa na viwango.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Serikali inaangalia uwezekano wa kuanzisha Wakala mwingine utakaoshughulikia barabara za wilaya ili kuleta ufanisi; suala hili

lifanyiwe utafiti wa kutosha kwani kuwa na Wakala mbili au zaidi ambazo zitafanya kazi ya aina moja na kusimamiwa na Wizara tofauti za TAMISEMI na Miundombinu linaweza kuleta mgongano kiutendaji. Kamati inashauri kuwa, ni vyema kuijengea uwezo TANROADS ili iweze kuwa na Wataalam wa kutosha na kusimamia vyema miradi ya barabara nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inasikitishwa na malumbano na mijadala inayoendelea kwenye vyombo vya Habari kuhusu Afisa Mtendaji Mkuu wa TANROADS. Pamoja na kuwa Kamati iliwakutanisha Watendaji Wakuu wa Wizara, Bodi ya TANROADS na Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala huo kubaini iwapo kulikuwa na tatizo; bado mijadala na malumbano hayo hayakuisha.

Kamati ilibaini kuwepo kwa makundi yaliyokuwa yakichagizwa na Wafanyakazi waliokuwa *TANROADS* na ambao wamesimamishwa kazi au kumaliza muda wao wa utumishi na wengine hawakuridhika na kuenguliwa kwao katika nafasi za uongozi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu kwa kutumia busara na ili kuepusha malumbano yasiyo na tija katika kipindi kinachopaswa kukamilisha miradi, iliishauri Wizara kukaa pamoja na Bodi ya TANROADs na Watendaji wake Wakuu kujadili masuala yanayowahusu hasa yale ya mchakato wa kujaza nafasi za Watendaji wa Wakala huo. Aidha, Kamati ilishauri kuwa ili miradi isisimame wakati mchakato wa kujaza nafasi hizo ukiendelea, Mtendaji Mkuu awateue wale wote wanaoshikilia nafasi hizo wakaimu hadi watakapopatikana wa kujaza nafasi hizo kulingana na Muundo Mpya wa Wakala huo (*Organization Structure*). Muundo ambao ulishakamilika na kuridhiwa na Idara Kuu ya Utumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato wa kujaza nafasi zilizo wazi za Watendaji wa Wakala huo ni wa muda mrefu; na kwa kuzingatia miradi mingi bado haijakamilika na nchi inaelekea kwenye uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, Kamati ilishauri kuwa mchakato wa kujaza nafasi zilizo wazi za Watendaji Wakuu wa *TANROADs* ukamilike mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu ili kuepusha mabadiliko yasiyo ya lazima kwa sasa hivi. Aidha, Serikali izisimamie Taasisi zake ili ziweze kutimiza majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa Sheria iliyoziunda bila kuingiliwa. Serikali itoe ushirikiano wa kutosha ili kuepuka malumbano na mijadala isiyo na msingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inasikitishwa sana na malumbano yanayoendelea katika magazeti kwa muda mrefu sasa kuhusu Mtendaji Mkuu wa *TANROADs*; kwa madai kwamba mkataba wake wa ajira *TANROADs* umekwisha. Lakini wakati malumbano hayo yakiendelea Serikali imekaa kimya bila ya kutoa ufafanuzi na ukweli wa madai hayo yanayoandikwa magazetini siku hadi siku. Kamati ingependa Serikali ieleze ukweli wa madai hayo, kwani inaathiri ufanisi na utendaji katika Wakala huo.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa Kamati yangu inampongeza Bwana Ephraem Mrema, Mtendaji Mkuu wa *TANROADs* kwa kazi nzuri aliyoifanya tangu alipoingia katika Wakala huo mwezi Juni, 2007 alipokuta Mikataba 10 tu na sasa kuna mikataba zaidi ya 40. Mabadiliko yalianza kuonekana kwa kasi kulinganisha na Mtendaji Mkuu aliyepita, kwani Bwana Mrema alipoanza kazi *TANROADs* katika mikataba 18 iliyokamilika, miradi minne alianza nayo yeye na kuikamilisha ambayo ni Kigoma – Kidahwe, Usagara – Sengerema na Masasi – Mangaka (2). Miradi mingine aliyoikamilisha tangu 2007 ni pamoja na barabara 18 za Nzega – Isaka – Tinde (2), Singida – Shelui (3), Tarakea – Kamwanga (1), Dodoma – Manyoni (1), Daraja la Ruvu (1), Barabara ya Sam Nujoma (1), Kyamyorwa – Buzirayombo (2), Kigoma – Kidahwe (1), Geita – Sengerema (1), Daraja la Umoja (1), Masasi – Mangaka (2), Nangurukuru – Mingoyo (2) na Morogoro – Dodoma (1).

Mheshimiwa Spika, pia, kulikuwa na miradi aliyoirithi 10 kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo aliyepita na miradi minne kutoka Wizarani. Leo hii ni zaidi ya miradi 54 ya barabara za kitaifa ambayo ameisimamia pamoja na miradi ya madaraja na vivuko kama vile vivuko vya Busisi, Kigamboni, Pangani, Kilombero, Utegi na vingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza *TANROADs* pamoja na Watendaji wengine wote wa Wakala huo kwa kukamilisha miradi iliyokuwa katika Ilani ya CCM pamoja na ahadi za Rais. Wakala umekamilisha ahadi za Mhe. Rais kwa asilimia 99.9%. Kamati ya Miundombinu imefanya kazi kwa karibu na Mtendaji huyu na inautambua mchango wake mkubwa hasa katika sekta hii ya miundombinu ya barabara. Kamati yangu inampongeza, asikatishwe tamaa na aendelee kuisaidia sekta hii bila kuvunjika moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Ujenzi na Majengo Kamati inaipongeza Serikali kwa kutungwa kwa Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ya mwaka 2010 (*The Architects and Quantity Surveyors Registration Act, 2010).* Sheria hii pamoja na nyingine zinazohusu ukandarasi na uhandisi zitasaidia kudhibiti ujenzi usiokuwa na viwango. Kwa watakaokiuka sheria hii, Serikali itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine wanaojihusisha na ujenzi usiokidhi sifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira mazuri kuanzia shule za msingi, sekondari na vyuo vya sayansi na ufundi, ili kutoa fursa ya kuwapata Wataalam wengi zaidi katika fani ya uhandisi, ukandarasi na utaalam mwingine.

Mheshimiwa Spika, Kamati vile vile inaishauri Serikali kutimiza ahadi yake ya ujenzi wa Daraja la Kigamboni kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Wananchi bado wana matumaini kuwa ujenzi wa daraja la Kigamboni litakuwa ndio mkombozi wao na kuwapunguzia kero za usafiri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama na udhibiti wa vyombo vya Usafiri. Serikali iliiunda Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) ili kusimamia sekta ya usafiri na usafirishaji nchini. Lengo kuu ni kudhibiti, kuwalinda watoaji na watumiaji wa huduma hii ili sekta hii ifanye kazi kwa ufanisi na kwa viwango.

Pamoja na malengo hayo mazuri sekta ya usafiri na usafirishaji imekuwa na changamoto nyingi zilizojitokeza hivi karibuni, hasa ongezeko la ajali zinazoua mamia ya Watanzania, upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu. Kamati inaishauri Serikali kupitia *SUMATRA* kujizatiti na kupunguza matukio ya ajali za barabarani na majini na kujiwekea mikakati endelevu ya kuvisimamia na kuvifanyia ukaguzi wa mara kwa mara vyombo vya usafiri ili kupunguza ajali.

Mheshimwa Spika, kwa vipindi viwili tofauti, Kamati yangu ilikutana na Wadau wa Usafirishaji ili kujadili kiini cha ongezeko la ajali za barabarani na kujaribu kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. Vikao hivyo viliwashirikisha Wizara ya Miundombinu, *SUMATRA*, Jeshi la Polisi (Usalama barabarani), *TANROADs*, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (*TABOA*), Chama cha Wamiliki wa Magari yanayosafirisha Mafuta (*TATOA*) na wengineo. Katika vikao hivyo wadau hao walijadili kwa kina vyanzo vya ongezeko la ajali za barabarani na kupendekeza njia mbalimbali za kupunguza na hatimaye kumaliza tatizo hilo kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wadau wa usafirishaji katika mapendekezo yao ya namna ya kupunguza ajali za barabarani, waliilalamikia *SUMATRA* kwa kushindwa kutimiza wajibu wao ipasavyo. Wadau hao hawakuridhika na baadhi ya maamuzi ya Watendaji wa Mamlaka hiyo; kwamba hawaijui vizuri sekta ya usafirishaji ndio maana baadhi ya maamuzi yao hayana tija. Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri wa Mamlaka hii, ili kusimamia vema huduma ya usafiri na usafirishaji.

*SUMATRA* kisheria wanapaswa kuratibu na kusimamia masuala yote ya usafiri; mizani, kodi na ushuru, Bidhaa Mtaji, matuta ya barabarani, muda wa kutembea usiku na kadhalika. Lakini masuala haya yanapopelekwa *SUMATRA*, hushindwa kuyashughulikia kwa madai kuwa hayo yapo chini ya mamlaka nyingine. Hili ni tatizo kubwa, Kamati inaitaka Serikali iliangalie suala hili na kuaninisha majukumu ya kila chombo ili kusiwe na migongano kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wamiliki wa mabasi ya abiria, ambao hupata usumbufu kutoka mamlaka tofauti wanapokuwa katika shughuli za utoaji wa huduma. Kwa mfano, basi linapoanza safari, watendaji wa Majembe hufika na kuanza ukaguzi kwa niaba ya *SUMATRA* kwa zaidi ya saa hata mbili; kisha hufika watendaji wa *SUMATRA*, ambao nao hutumia muda katika kukagua na kuhojiana; basi hilo hilo likipita kwenye mizani hukaa foleni kwa muda mrefu na pia hukutana na Askari wa Usalama barabarani nao wakifanya ukaguzi kama wa Majembe na *SUMATRA*.

Mheshimiwa Spika, vituo vingi vya ukaguzi bila mpangilio husababisha ucheleweshaji wa safari kwa saa mbili hadi tatu; ambapo sheria inamlazimu dereva afike aendako kabla ya saa sita usiku. Matokeo yake Madereva huenda mwendo kasi kufidia muda uliopotea na wakati mwingine kusababisha ajali. Kamati inaishauri Serikali kukaa pamoja na Wadau wa usafirishaji ili kuweka utaratibu utakaolenga kupunguza ajali na kupunguza kero kwa Wasafirishaji hao, ili waweze kuendelea kutoa huduma kwa Wananchi bila kubughudhiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa duniani kote huduma ya usafiri huendeshwa na Serikali au Mashirika ya Umma na kwa kuwa huduma hii nchini inaendeshwa na Sekta binafsi; Kamati inaishauri Serikali kuwa, kama ambavyo wawekezaji wengine chini ya mfumo wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*), wanafaidika na misamaha ya kodi, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Viwanda na Biashara na *TIC* iwaruhusu wamiliki wa vyombo vya usafiri wa abiria na mizigo kununua mabasi na magari ya mizigo kama "Bidhaa Mtaji". Hii itawasaidia wasafirishaji hawa wanaohudumia Watanzania milioni nane hadi 10 kwa mwaka kupata misamaha ya kodi. Misamaha, ambayo itawawezesha wengi kumudu kununua mabasi mapya na vipuri vyenye ubora na viwango na hivyo kupunguza ajali zinazotokana na kununua magari, matairi na vipuri vingine vilivyotumika *(second hand).*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ajali nyingi za barabarani zimekuwa zikipoteza maisha ya Watanzania wengi na upotevu wa mali nyingi; Kamati inaishauri Serikali kulichukulia kwa uzito wa juu tatizo hili. Serikali iwashirikishe Wadau wote wa Sekta ya usafiri na kufanyia kazi maoni yao, ambayo kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakiyawasilisha kwa vyombo husika bila utekelezaji wa kuridhisha. Serikali iangalie upya Sheria na taratibu zote katika Sekta ya usafirishaji na kuziondoa zile ambazo hazina tija kama vile; kuwepo kwa vituo vingi vya mizani na ukaguzi, vituo vya Wilaya kutoza ushuru kwa kulazimisha mabasi yaingie kwenye vituo vyao.

Mheshimiwa Spika, mabasi yanapoharibika yaruhusiwe kuvutwa na chombo maalum na si lazima kibali kitoke *SUMATRA*, Madereva wasiruhusiwe kunywa pombe hata chembe, maduka ya pombe kwenye vituo vya mabasi yaondolewe (hasa Ubungo) pamoja na vichocheo vingine vinavyosababisha ongezeko la ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa, katika kuratibu shughuli za sekta ya usafirishaji; ni vema Wamiliki wa vyombo vya usafiri wa abiria wawe chini ya kofia moja tofauti na ilivyo sasa, ambapo Wamiliki hawa wanasimamiwa na *SUMATRA*, Wizara ya Mambo ya (Polisi wa Usalama barabarani), Halmashauri za Wilaya, Majembe, Wizara ya Fedha na kadhalika. Utaratibu huu unaleta mkanganyiko na migongano isiyo ya lazima kana kwamba sekta ya usafirishaji haina umuhimu sana kwa jamii. Kamati inaishauri Serikali kuwa, *SUMATRA* ichukue na kutekeleza majukumu yake yenyewe na si kutafuta wakala wengine kama ilivyo sasa kwa kuwatumia Majembe. Hii itapunguza usumbufu na bughudha kwa Wamiliki wa mabasi wanayoipata kutoka kwa Watendaji wa Majembe wasioijua sawasawa sekta ya usafirishaji.

Mheshimewa Spika, suala la vibali vya kusafirishia mizigo mizito nalo limekuwa ni tatizo. Pamoja na kuwepo umuhimu wa vibali hivyo, Kamati inashauri Serikali kuliangalia suala hili kwa umakini mkubwa kwani limekuwa ni kero kwa Wasafirishaji na wakati mwingine huchukua siku mbili au zaidi kutolewa. Huu ni urasimu usio na tija yoyote kwani huchangia kwa kiasi kikubwa ucheleweshaji wa safari.

Aidha, Kamati yangu inashauri kuwa, suala la mizani liangaliwe upya hasa katika kupunguza msongamano maeneo hayo na mizani iwekwe karibu na bandari ili magari yakipakia mizigo yapite moja kwa moja kwenye mizani ili kupunguza foleni katika vituo hivyo. Utaratibu huu ukitumika utapunguza ucheleweshaji wa mizigo njiani na kutumia siku chache safarini. Ilivyo sasa, kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kuna vituo vya Mizani 4; kutoka Dar es Salaam hadi Tunduma kuna vituo zaidi ya 40, ambavyo ni vituo vya mizani, vituo vya *TRA* na Polisi. Huu ni mfano mmoja tu na zipo njia nyingi zenye usumbufu kama huo. Hili ni tatizo na ni kichocheo cha rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pamoja na Wadau tulijadili kwa kina kero nyingine kubwa kwa Wamiliki wa vyombo vya usafiri na watumiaji wa mafuta nchini, kuhusu tabia iliyoota mizizi ya kuchanganya mafuta ya taa na dizeli (maarufu kama "chakachua"). Tabia hii mbali ya kuharibu vyombo vya usafiri na kusababisha ajali; imekuwa pia ni chanzo kikubwa cha rushwa, kwani wenye tabia hii wamejenga mtandao mkubwa na Watendaji katika mamlaka husika kama vile *EWURA*, Polisi na katika vituo vya mafuta. Mtandao huo ambao unafaidika na tabia hii chafu, umeimarika na hata kusababisha wahusika kulindwa ili wasikamatwe. Kamati inaishauri Serikali kupitia *EWURA* na mamlaka nyinginezo kuwafuatilia Watendaji wake wanaohusika na tabia hii mbaya na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kuna magari makubwa yanayosafirisha mafuta nje ya nchi yapatayo 30 yalikamatwa Rwanda yakiwa yamechanganya mafuta ya Dizeli na mafuta ya taa. Kukamatwa kwa magari hayo, mbali ya kuipunguzia nchi pato la Taifa na kukosa soko; ni aibu na fedheha kwa nchi, kwa kuwa magari hayo yalitoka Tanzania. Kwa namna moja au nyingine hilo limeiathiri nchi yetu kwa kutoaminiwa na nchi za jirani na kupoteza nafasi ya kutumia fursa ya uchumi wa kijiografia. Kuna taarifa kuwa Rwanda na Burundi wameshaanza kupitishia bidhaa zao katika bandari ya Mombasa kwa kuhofia bandari ya Dar es Salaam. Waliohusika na kadhia hii watafutwe na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba unipe dakika mbili kidogo nisome angalau haya makadirio.

**SPIKA:** Makadirio ni muhimu, ila majina na nini itakuwa basi.

**MHE. JOYCE M MASUNGA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali ili kukomesha tabia hii ya "kuchakachua", ni vema mafuta ya taa yakawekewa kodi. Bei ya mafuta ya taa ikiongezeka itapunguza tatizo hili, kwani wanao "chakachua" hufanya hivyo kutokana na ukweli kuwa mafuta ya taa huuzwa kwa bei rahisi sana. Kamati inaishauri Serikali ifanye maamuzi magumu, kwani pamoja na ukweli kuwa mafuta ya taa ni nishati muhimu hasa vijijini, lakini matumizi yake ni kwa kiwango kidogo *(small quantity).* Serikali iirejeshe kodi ya mafuta ya taa kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali itaweka kodi katika bidhaa ya mafuta ya taa, mbali na kuondoa tatizo la "kuchakachua" itaokoa zaidi ya sh. bilioni 33 kila mwezi

katika mapato yake. Zaidi ya asilimai 99% ya matumizi ya mafuta ya taa hutumika vibaya na wanaochanganya dizeli na mafuta ya taa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuweka sheria itakayowabana madereva wasio waaminifu wanapokamatwa kwa kuchanganya dizeli na mafuta ya taa. Kwa sasa hakuna sheria inayowabana madereva hao na badala yake anayeshitakiwa ni mmiliki wa gari. Hili ni tatizo kubwa na halitakwisha kwa vile mhusika haguswi na sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuvifanyia ukaguzi vyombo vya usafiri mara kwa mara na kuwe na udhibiti katika utoaji wa leseni kwa madereva. Kabla madereva hawajapewa leseni Kamati inashauri wapimwe afya zao (akili) na kufanyiwa "*vetting*" ili madereva wazembe na wanaorudia makosa wanyang'anywe leseni zao. Kwa magari yanayokwenda umbali mrefu ni vema uwepo utaratibu wa kila gari kuwa na madereva wawili ili kupunguza uchovu, ambao unaweza kusababisha ajali. Serikali iweke utaratibu wa kuwa na maegesho kwa madereva na abiria kuepusha magari kuegesha barabarani yanayosababisha ajali. Aidha, *SUMATRA* ifuatilie kwa karibu suala la milango ya dharura kwenye mabasi ya abiria kuwa linatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la huduma ya kusafirisha abiria kwa kutumia pikipiki, maarufu kama "bodaboda". Pamoja na usafiri huu unasaidia kutoa ajira kwa vijana na kuwa kati ya usafiri rahisi na ambao wananchi wengi wanaumudu; Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka udhibiti katika utoaji wa leseni za pikipiki hizo ili kupunguza ajali. Aidha, hatua ziwe zikichukuliwa kuhakikisha usalama wa vyombo hivyo na abiria, sheria za usalama barabarani zizingatiwe na madereva na abiria wavae kofia maalum (*helmet*) kwa ajili ya usalama. Kamati inaishauri Serikali kupiga marufuku upakiaji wa abiria zaidi ya wawili kwenye pikipiki ujulikanao kama "mishkaki".

Mheshimiwa Spika, huduma ya usafiri wa Majini, Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi wa kivuko cha Mto Pangani, ununuzi wa vivuko vipya vya Utete, Rugezi-Kisorya na ukarabati wa *MV* Kigamboni na *MV* Sengerema pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Magogoni, Pangani, Kigongo-Busisi na Kome. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutawapunguzia adha ya usafiri Wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzitumia Bandari za Lindi, Mtwara, Tanga, Kasanga, Kigoma, Mwanza na Itungi kwa ajili ya kufungua fursa zaidi za kiuchumi ndani na nje ya nchi. Serikali ikae pamoja na wahusika kama vile Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Idara ya Uhamiaji na wengineo ili kuona namna ya kuweza kuzitumia bandari hizo katika huduma ya usafirishaji. Kwa kufanya hivyo pia kutaipunguzia mzigo bandari ya Dar es Salaam, ambayo nayo inaelemewa kwa kupokea mizigo na makasha mengi na eneo lao ni dogo. Aidha Serikali itamke sasa ni lini itaanza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, ambayo tayari upembuzi yakinifu umekwishafanyika ili kuondoa msongamano wa meli katika bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Zoezi la Ubinafsishaji au Uwekezaji. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika suala zima la kuingia mikataba au ubia na Makampuni, Wawekezaji na Wakodishaji wa kutoka nje ya nchi. Aidha, hatua kali ziwe zikichukuliwa kwa Watendaji wanaoiingiza nchi yetu katika mikataba mibovu inayolitia hasara Taifa pamoja na kulikosesha mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa zoezi la ubinafsishaji lisichukue muda mrefu kwani dhana hii huwaathiri wafanyakazi na kupunguza ari ya kupenda kazi kwa kujua ubinafsishaji unatarajiwa. Aidha, pale inapowezekana Serikali ijiwekee utaratibu wa kuwekeza kwanza katika Mashirika inayotarajia kuyauza au kuyabinafsisha ili yanapouzwa yawe katika hali ya kushindaniwa na kuuzwa kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Usafiri wa anga. Kwa kuwa Wateja wakubwa wa huduma za Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ni Serikali yenyewe na kwa kuwa kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikipatiwa huduma hiyo ya usafiri kwa Viongozi Wakuu wa Kiserikali; Kamati inaishauri Serikali kulipa limbikizo la madeni yake na kulipa madeni kwa wakati ili kuiwezesha *TGFA* kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia. Aidha, Serikali iwatengee fedha za kutosha. Mwaka jana waliomba shilingi bilioni 30 lakini walipewa shilingi bilioni nane tu, fedha ambazo hazikukidhi mahitaji ikiwa ni pamoja na kushindwa kukarabati karakana yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya vizuri kurejesha *ATCL* chini ya umiliki wa Umma. Lakini tangu kuundwa kwake baada ya kuvunja mkataba na Shirika la ndege la Afrika Kusini, *ATCL* imekuwa ikipoteza mwelekeo kadri siku zinavyoenda na kupoteza matumaini ya Watanzania kujivunia Shirika lake la ndege. Hali ya kifedha kwa Shirika hili haikuwa ya kuridhisha, hakukuwa na uwekezaji wa kutosha kuliwezesha Shirika kujiendesha na kuingia kwenye soko la ushindani. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kuanzisha na kufufua Mashirika yaliyoshindwa kufanya vizuri. Serikali ijipange vema na kuwa na mtaji wa kutosha ili kuepusha aibu kama ilivyokuwa kwa *ATCL*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Wafanyakazi, Menejimenti pamoja na Bodi ya *ATCL* tarehe 8 Aprili, 2010 kujadili mustakabali wa *ATCL*. Kikao hicho kiliombwa na Wafanyakazi wa *ATCL* kupitia kwako Mheshimiwa Spika baada ya juhudi zao za kukutana na Menejimenti iliyopo kujadiliana masuala ya Shirika lao kugonga mwamba. Katika kikao hicho, Taarifa pamoja na vielelezo vilivyowasilishwa mbele ya Kamati na Wafanyakazi wa *ATCL* ni aibu kubwa. Wafanyakazi walibainisha sababu zifuatazo kama ndizo zilizochangia kuifikisha *ATCL* hapa ilipo sasa:-

- Menejimenti kutokuwa wazi katika utendaji wake na kukosekana kwa dhana nzima ya ushirikishwaji wa Wafanyakazi katika masuala yanayowahusu. Wafanyakazi walishaomba zaidi ya mara mbili kukutana na Waziri mhusika bila mafanikio, Katibu Mkuu wa Wizara alishawahi kukutana na Wafanyakazi mara moja tu

wakati wa mchakato wa kupunguza Wafanyakazi *(redundance)* na ushauri wa Wafanyakazi kutozingatiwa na Menejimenti;

-  Matumizi mabaya ya fedha na raslimali za Shirika. *ATCL* imeuza eneo la maegesho ya magari kwa Hoteli ya *City Garden* kwa bei ya kutupa, umeme na *Genarator* la *ATCL* vinatumiwa pia na hoteli hiyo, Vikao vingi vya Bodi visivyo na tija ambapo Wajumbe hulipana kwa dola za Kimarekani, Marubani kulipwa sh. 400,000/= kwa siku wakati ndege za *Boeing* haziruki tena;

-  Ukodishaji tata wa ndege *(Airbus A320),* ambao umelitia hasara taifa. Ndege hiyo ilikodishwa ikiwa imeshatumika kwa miaka 12, ilipofika nchini ilifanya kazi kwa miezi 12 tu na ikahitaji matengenezo hata kabla haitoa faida;

-  Hujuma na ukiukwaji wa taratibu na Sheria ya manunuzi. *ATCL* ilinunua magari Dubai *(Second Hand)* na bila kutangaza tenda, ambayo hadi tarehe 8 Aprili, 2010 magari tisa yalikuwa yamezuiwa na *TRA (bonded)* tangu mwaka 2008 na yanadaiwa shilingi milioni 250, ukodishwaji holela wa magari na kukodisha Kampuni ya ulinzi isiyo na sifa; na
-  Bodi na Menejimenti ni dhaifu na Mtendaji Mkuu hana sifa za kushika nafasi hiyo. Ajira zimekuwa zikitolewa kwa upendeleo na kuwepo kwa tofauti kubwa ya ngazi za mishahara bila kuwepo vigezo vinavyotakiwa, kutotumia na kuthamini michango ya Wafanyakazi wa muda mrefu katika Shirika, Wafanyakazi kukatwa fedha za *NSSF* ambazo hazikuwa zikiwasilishwa kunakotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali pamoja na ukata unaoikabili *ATCL*, ni vema Serikali ikatumia vyombo vyake vya Dola kubaini ubadhirifu ndani ya Shirika la *ATCL* na watakaobainika kulihujumu wachukuliwe hatua za kisheria. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuwa makini katika kufanya uteuzi wa nafasi za Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zetu kwa kuwafanyia uchunguzi wa kina (*vetting*) kubaini uwezo na uwajibikaji wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mwekezaji China Sonangol haonyeshi nia thabiti ya kuingia ubia na Serikali ya kuendesha *ATCL*, ni vema kuanza juhudi za kutafuta mwekezaji mwingine ili Shirika hili lianze kufanya kazi mara moja. Kwa taarifa, ambazo Kamati ilipewa ni kwamba, Serikali ilishaanza mazungumzo na Kampuni ya China Sonangol ya kuingia ubia na Serikali ya Tanzania. Nini kilitokea baada ya hapo hata mazungumzo hayo yakaanza kusuasua na mwekezaji huyo kughairi? Kulikoni?

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*) kwa kazi nzuri inayofanyika ya uendelezaji na uboreshaji wa miundombinu katika viwanja vya ndege. Aidha, Kamati inapongeza juhudi za Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka hii kukamilisha zoezi la kuwahamisha wakazi wa Kipawa, Kigilagila na Kipunguni ili kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege. Aidha, pongezi kwa kukamilisha ulipaji fidia kwa Wakazi wa Kipawa na Msalato. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha malipo ya fidia kwa wakazi, ambao bado hawajalipwa ili kuepuka

usumbufu. *TAA* ifuatilie upatikanaji wa Hati miliki ya kiwanja cha Msalato Dodoma kutoka Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*).

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA*) inasimamia kikamilifu miradi ya viwanja vya ndege ambavyo vipo katika hatua mbalimbali; kuna miradi iliyokamilika, inayoendelea na inayokaribia kuanza kwa kutegemea fedha za Wafadhili na Mashirika ya nje. Miradi hiyo ni pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwl. Nyerere, Songwe, Mwanza na Msalato – Dodoma. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kihandisi kwa ajili ya kuboresha viwanja saba (7) vya Arusha, Bukoba, Kigoma, Mafia, Shinyanga, Sumbawanga na Tabora umekamilika. Kamati inaishauri Serikali kuwafuatilia kwa karibu Wafadhili hao ili miradi ikamilike kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza *TAA* chini ya Mkurugenzi wake Mkuu Mhandisi Prosper Tesha, kwa kutenga fedha za Mamlaka, ambazo zimetumika katika kutekeleza na kukamilisha miradi ya usanifu wa kina wa majengo ya abiria, minara ya kuongozea ndege *(Control Towers),* Vituo vya umeme (Power Stations), Ukumbi wa Wageni Mashuhuri *(VIP Lounges)* katika viwanja vya Arusha, Kigoma, Mafia, Tabora, Bukoba, Shinyanga na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyotumia fedha za Mamlaka ni ujenzi wa uzio km. 2 (JNIA), ujenzi wa uzio wa usalama km. 1.732 na kumalizia ujenzi wa kituo cha Polisi (Arusha); ufungaji wa taa za kuongozea ndege na ujenzi wa uzio wa usalama km. 5.605 (Dodoma); ukarabati wa barabara ya kurukia ndege (Tabora); matengenezo ya jengo la abiria na upanuzi wa ukumbi wa Watu Mashuhuri awamu ya kwanza na ya pili (Mtwara); ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege (Nachingwea); ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na maegesho ya ndege (Lake Manyara) na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege (Shinyanga). Kamati inaishauri Serikali kuiongezea fedha *TAA* hasa pale inapokwama kutekeleza miradi mikubwa inayogharimu fedha zaidi ya uwezo wa Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi wa Ukumbi mpya wa Watu Mashuhuri katika Uwanja wa Ndege wa Mwl. Nyerere (*JNIA*). Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga kumbi za abiria wanaosubiri kusafiri katika viwanja vingine vya Mwanza, Dodoma na Arusha; viwanja na kumbi vitakavyokuwa na hadhi ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena Kamati yangu inaishauri Serikali kuhusu makusanyo ya ada ya huduma za viwanja vya ndege inayokwenda hazina (*Passenger's service charges*), ambayo hukusanywa kupitia TRA, iwe ikirudi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (*TAA*) kwa asilimia 100% na kutumika kwa ajili ya huduma za viwanja vya ndege. kwa kuwa fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza miradi ya viwanja vya ndege hazitoshi kulingana na mahitaji halisi. Utaratibu huu umekuwa ukitumika pia kwa sekta nyingine kama ilivyo Maliasili, ambapo

makusanyo ya Ngorongoro huenda moja kwa moja kwao badala ya kupitia kwenye mfuko mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaipongeza kwa dhati Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (*TCAA*) chini ya uongozi thabiti wa Mhandisi Margaret Munyagi, kwa Mamlaka yake kutunukiwa cheti cha kimataifa cha ubora na kuwa taasisi ya pili baada ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Afrika Kusini. Kamati inautambua mchango mkubwa wa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hii na inaitaka *TCAA* kuongeza juhudi katika kuvisimamia na kuvikagua mara kwa mara vyombo vya usafiri wa anga ili viendelee kutoa huduma inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa reli. Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuvunja mkataba wa ubia na Shirika la *RITES* la India na hatimaye kununua hisa zote kuwa chini ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali kujipanga upya na kuwekeza vya kutosha ili kufufua huduma za usafiri wa reli, ambao ni tegemeo kwa Wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, wakati nchi yetu ipo kwenye maandalizi ya kuingia kwenye Soko la Pamoja la Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli kutoka Tanga hadi Musoma. Hii itatoa fursa ya kufungua njia za uchumi wa kijiografia na kuwawezesha wananchi wa maeneo husika kupunguza umasikini kwa kusafirisha mazao na bidhaa nyingine za kuwaongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuanzisha Mfuko wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Reli (*Railway Infrastructure Fund*), Kamati inashauri Serikali isitegemee sana fedha za kutoka nje ya nchi. Serikali itenge fedha zake za ndani na itoe kipaumbele hasa kwa reli ya Tabora – Mpanda, kwani wananchi wa eneo hilo hawana usafiri wa kuaminika unaoweza kupitika mwaka mzima, barabara zao ni mbovu na wanaathirika kiuchumi kwa kukosa miundombinu ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatoa pole kwa Wakazi wa Kilosa waliokumbwa na mafuriko yaliyowaacha wengi bila makazi, ambapo mali na miundombinu mingi iliharibiwa. Kamati yangu kwa dhati kabisa inatoa pongezi kwa Serikali kupitia *RAHCO, TRL* na Jeshi la Wananchi kwa juhudi na maarifa katika kusaidia ujenzi wa miundombinu iliyoharibiwa. Chini ya usimamizi wa Mtendahi Mkuu wa *RAHCO* Bw. Binhadad Tito zoezi hilo liliendeshwa kwa ufanisi mkubwa. Aidha, Kamati inalipongeza Jeshi la Wananchi kwa kufanya kazi kwa bidii wakati wote wa kuokoa watu na mali zao. Kamati inawapongeza wote waliojitolea kwa hali na mali kusaidia maafa ya Kilosa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko la mshahara kwa Wafanyakazi wa *TAZARA* la 5%, bado ongezeko hilo halitoshi na bado Serikali inapaswa kuangalia tena namna ya kuboresha mishahara ya Wafanyakazi hao. Thamani ya Dola ya Kimarekani inabadilika kila siku na hivyo kuondoa dhana ya ongezeko la mshahara kulingana na wenzao wa upande wa Zambia. Aidha, Kamati bado hairidhishwi na kusuasua kwa Serikali katika kuwalipa Wafanyakazi wa *TAZARA* wanaodai malimbikizo na

viinuamgongo baada ya kupunguzwa au kustaafu. Malimbikizo na mafao ya Wastaafu yalipwe mapema na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na karakana na Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Miundombinu. Kamati yangu inasikitishwa na fedha kidogo zinazotengwa kwa ajili ya Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*), Wakala unaoshughulikia matengenezo ya magari, pikipiki, mifumo ya umeme, mabarafu, ukodishaji wa magari, uendeshaji mitambo na vivuko. Tangu kuanzishwa kwa Wakala huu Serikali haijawahi kutoa kipaumbele ili kuwezesha Wakala huu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kupeleka magari yake *TEMESA* kwa ajili ya matengenezo badala ya kupeleka magari ya Serikali kwenye makampuni binafsi, ambako gharama zao ni kubwa na hivyo kuigharimu Serikali fedha nyingi na bila udhibiti wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, iwapo Serikali haitaitengea *TEMESA* fedha za kutosha kuiwezesha kununua vifaa na mitambo ya kisasa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao; na iwapo Serikali itaendelea na mtindo wa kutumia makampuni binafsi na kuinyima kazi *TEMESA*, ni wazi Karakana hii itakufa. Serikali inapaswa kuwa mteja namba moja wa *TEMESA* ili kuijengea uwezo. Suala la kuwa magari ya Serikali hayatengenezwi *TEMESA* kwa kuwa hawana mitambo ya kisasa kuhudumia magari kama *Land Cruiser* na mengineyo, halina mantiki kwani Serikali ndio inapaswa kuijenga *TEMESA*.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya taasisi zinazotoa mafunzo ya ufundi, usafirishaji, hali ya hewa na mengineyo ili ziweze kujiendesha. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya Chuo cha Usafirishaji (*NIT*), Chuo cha Mabaharia (*DMI*), Chuo cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma na Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam (*DIT*), zenye mahitaji makubwa kwa Wanafunzi, Waalim na Wafanyakazi hazitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na fedha zilizotengwa kwa ajili ya Taasisi hizi nilizozitaja, ambazo zimekuwa zikihitaji fedha kwa ajili ya kuongeza majengo ya ofisi, mabweni, karakana, maabara, maktaba na uendeshaji. Aidha, kuna Waalim na Wanafunzi wanaostahili kulipwa, lakini fedha za kuwalipa hakuna. Baadhi yao wapo nje ya nchi masomoni na Serikali imeshaingia gharama na kozi zao hazipaswi kusitishwa. Wapo pia Wazabuni wanaotoa huduma nyinginezo kama za vyakula katika Taasisi hizo na hawajatengewa fedha. Kamati inaishauri Serikali kuwa na mipango na mikakati ya kuziwezesha Taasisi hizo kutekeleza majukumu yake bila bughudha.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Ili kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka 2010/2011, Wizara ya Miundombinu inaomba iidhinishiwe jumla ya shilingi 1,164,983,227,000/=. Kati ya hizo shilingi 293,429,311,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 871,553,916,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na kupitia kifungu kwa kifungu na kuipitisha na sasa Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu kukubali kupitisha maombi hayo ya fedha kwa Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu. Nawashukuru pia Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Naibu Waziri wa Miundombinu; Mhandisi Omar Abdallah Chambo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha Taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa wa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha Taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. Kwa nafasi ya kipekee napenda kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati ya Miundombinu, ambao ni:-

Mhe. Alhaji Mohamed Hamis Missanga, Mwenyekiti; Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mjumbe; Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mjumbe; Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mjumbe; Mheshimiwa Paschal Costantine Degera, Mjumbe; Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mjumbe; Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mjumbe; Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mjumbe; Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mjumbe; Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mjumbe; Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mjumbe; Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mjumbe; Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mjumbe; Mheshimiwa Herbet James Mntangi, Mjumbe; Mheshimiwa Balozi Dr. Gertrude Ibengwe Mongella, Mjumbe; Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mjumbe; Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mjumbe; Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Phillemon Mikol Sarungi, Mjumbe na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Didimu Kashillilah; Makatibu wa Kamati hii Bibi Justina Mwaja Shauri na Bwana Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa uwezo wao wa kuihudumia Kamati ya Miundombinu kwa ufanisi mkubwa na kuandaa Taarifa hii. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Shinyanga napenda kuishukuru Serikali kwa kugawa Mkoa wa Shinyanga kuwa mikoa miwili ya Shinyanga na Simiyu. Hii ni fursa nzuri kwa mkoa weti kuongeza nafasi mbili zaidi za uwakilishi wa Wanawake Bungeni. Tunamuahidi Mheshimiwa Rais wetu, kwa mgawanyo huu Wanawake tutaitumia vizuri nafasi hii na tutampa Rais anachokitarajia, ategemee kura za kishindo. Aidha, nawaomba Wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini waniunge mkono katika uchaguzi Mkuu ujao kwani nina nia ya kugombea jiombo hilo. Namwomba Mwenyezi Mungu anijalie muda ukiwadia nitakuja kujaza fomu.

Mwisho naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda kwa miaka mitano niliyokuwa Bungeni. Shukrani za dhati kwa mume wangu mpenzi Meja Mstaafu Mohammed Ndaro kwa ushirikiano na uvumilivu wake alionionyesha kipindi chote cha miaka mitano. Niwashukuru pia watoto wangu Kuruthum, Ndaro na Mwanahawa bila kumsahau bibi yangu mpenzi Bibi Namate (Chiku Said) kwa kunilelea watoto wangu kwa takriban miaka 20. Namshukuru sana Dereva wangu Juma Lazaro, Mungu awabariki wote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi, naingia Shinyanga Mjini, naomba wanipokee na namwomba Mheshimiwa Dr. Mlingwa asiogope wala asihofu tutakuwa pamoja tu wanachama wataamua.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joyce Masunga na kwa kutenda haki msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani akiomba dakika za ziada nitampa. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Miundombinu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa kunipa fursa ya kusoma maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Wizara ya Miundombinu na bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Kwanza kabisa napenda nitoe pongezi za dhati kwa wanachama na viongozi wa Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa kumchagua Professor Lipumba kuwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Maalim Seif Sharif Hamad kuwa mgombea Urais wa Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa upande wa Zanzibar. Mchakato wa Chama changu cha CHADEMA bado unaendelea na naamini kabisa kwamba tutaweza kuangalia jinsi gani ambavyo tunaweza tukafanya kazi pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Miundombinu kwa kipindi cha takriban miaka mitatu sasa. Namshukuru kwa miongozo yake na kuiweka kambi katika uongozi thabiti akishirikiana na Naibu wake Dr. Willibrod Slaa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni katika Bunge la Tisa imefanya kazi kubwa sana ya kuwasemea Watanzania na hasa Watanzania wasio na sauti na hivyo kuleta mabadiliko makubwa katika uongozi wa Taifa letu. Kambi ya Upinzani Bungeni bila ya woga wala upendeleo imekuwa ikisema ukweli kuhusiana na jinsi Taifa letu linavyoongozwa na kuibua maovu yote kwa lengo la kuhakikisha kuwa mlipa kodi wa Tanzania anapata thamani ya kodi anayolipa. Kambi ya Upinzani Bungeni imetimiza wajibu wake wa Kikatiba wa kuwa Serikali mbadala kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na sasa tunatoa rai kwa Watanzania kutukabidhi Serikali ili tuweze kuiongoza kwa ufanisi zaidi kwa kuondoa ufisadi uliokithiri, kupambana na umaskini kwa kukuza uzalishaji mali viwandani na mashambani na kujenga miundombinu imara.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kigoma Kaskazini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kazi zangu. Katika kipindi cha miaka mitano tumefanya kazi kubwa sana ya kuleta maendeleo katika Mkoa wetu wa Kigoma na Jimbo letu la Kigoma Kaskazini. Mwaka 2005 kulikuwa kuna mtandao wa barabara za lami wenye kilomita nane tu Mkoa mzima wa Kigoma, leo kuna mtandao wenye kilomita 80 na ifikapo Oktoba mwaka 2010 kutakuwa na Mtandao wenye kilomita zaidi ya 100 baada ya kukamilika kwa barabara ya Mwandiga-Manyovu (asilimia 90 ya Mtandao huu wa barabara upo katika Jimbo la Kigoma Kaskazini). Mwaka 2005, kulikuwa na uwezo wa kuzalisha 4MW za umeme pekee, leo tuna uwezo wa kuzalisha 11MW.

Mwaka 2005 hapakuwa na Gati hata moja katika mwambao wa Ziwa Tanganyika, leo magati mawili yanajengwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania – moja Kigoma Kusini na lingine katika Kijiji cha Kagunga Jimboni Kigoma Kaskazini. Mwaka 2005 hatukuwa na Bweni hata moja la wanafunzi wa kike katika Shule za Sekondari, leo Kigoma Kaskazini peke yake imejenga mabweni matatu katika shule tatu tofauti ili kuhakikisha mabinti wa Kigoma Kaskazini wanasoma bila matatizo. Wakati Rais Jakaya Kikwete ametembelea Mkoa wa Kigoma, ukiachana na miradi ya kimkoa aliyozindua miradi mingine yote ilizinduliwa ni ya Kigoma Kaskazini peke yake. Watu wa Kigoma Kaskazini wanajivunia sana mafanikio haya ambayo yametokea ndani ya miaka mitano tu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Mwongozo, Kanuni.

**MHE.PETER J. SERUKAMBA:** Kanuni ya 68.

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kuweka *records clear* Rais alivyokuja Kigoma amefungua miradi yote pale Kigoma, Kasulu, Kibondo lakini pia kazi aliyoifanya ni kutekeleza Ilani ya Chama chetu ambayo tuliiahidi miaka mitano iliyopita. Kwa hiyo, yote yaliyofanywa yamefanywa na Chama cha Mapinduzi na ni kwa sababu Chama cha Mapinduzi ni Serikali ambayo inafanya yale iliyoyaahidi, sidhani imefanya kwa sababu rafiki yangu, mdogo wangu Zitto yuko kule, imefanya kwa sababu iliahidi kama Chama cha Mapinduzi.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Peter Serukamba, wewe unayoyasema ni kweli lakini usimtazamie Mpinzani asimame hapo halafu asifie sana, yeye naye kwa namna yake anasema, sasa wananchi ndiyo wataelewa nani ameyafanya, yeye anapoyatamka anayatamka hasemi kuwa hayakufanywa na Serikali, anasema yamefanywa na Serikali lakini yamefanywa kwenye Jimbo lake, nadhani yeye anasema ana mvuto maalum, ndiyo hoja yake hiyo, ndiyo anayosema tu ambayo sasa ni juu yetu upande wa Serikali kuangalia kwamba kuwe na uwiano basi, maana yake kama yote haya yamefanyika Jimbo la Kigoma Kaskazini na rafiki yangu Alhaji Msambya pale amepata sifuri sasa utekelezaji nao ni matatizo lazima Serikali iangalie, Mheshimiwa Zitto endelea. *(Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, sina cha kusema umemaliza.

Mheshimiwa Spika, napenda kurejea kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, narudia tena napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa niaba ya wakazi wote wa Kigoma, kwa kutusikiliza watu wa Kigoma na hususan kwa kunisikiliza mimi binafsi nikiwa Mbunge pekee wa Upinzani wa Majimbo kutoka Mkoa wa Kigoma. Maneno aliyoyasema Rais kuwa Serikali haibagui maeneo kulingana na itikadi za vyama, alipokuwa akizindua mitambo ya umeme Kigoma ndio maneno ya kiungwana katika demokrasia yoyote duniani. Bado kuna changamoto nyingi sana Kigoma na tutaendelea kuzisemea ili nasi watu wa Kigoma tujione kuwa tupo sehemu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa Mkandarasi wa kujenga kipande cha Kidahwe-Uvinza katika barabara ya Kigoma-Tabora tayari amepatikana. Nawashukuru sana watendaji wa *TANROADS* na hasa Mkurugenzi Mkuu na Meneja wa Mkoa wa Kigoma kwa kuwa wepesi katika kuhakikisha miradi ya Kigoma inakwenda haraka. Napenda kuwakumbusha kwamba katika ziara yake ya Kigoma, Mheshimiwa Rais alishauri kipande cha kutoka njia panda ya Mwandiga kwenda sokoni Mwandiga kiwekewe lami, lakini jana nimetoka Kigoma, bado juhudi hazijaanza. Kwa hiyo, nilikuwa nawakumbusha watu wa *TANROADS* waiangalie sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa Fedha zimetengwa katika Bajeti kwa ajili ya kipande cha Kidahwe-Kasulu katika Barabara kuu ya Kigoma-Nyakanazi. Nawashukuru sana Wizara ya Miundombinu kwa kutenga fedha hizi katika bajeti na kuwapongeza sana Wabunge wote kabisa wa Mkoa wa Kigoma bila kujali itikadi za vyama kwa ushirikiano mkubwa uliopo kuhusu miradi ya miundombinu katika Mkoa wa Kigoma. Naiomba Serikali na hasa Wizara ya Miundombinu iharakishe mchakato wa kumalizia malipo ya fidia kwa wananchi waliobomolewa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa Wabunge wa Kigoma tofauti na mimi na kwa michango yao ya kuchochea maendeleo ya Mkoa wetu wa Kigoma, Mungu atawalipa lakini siwaombei mrudi Bungeni kwani ni lazima kuimarisha demokrasia ya Vyama Vingi kwa kuchagua Wabunge wengi zaidi wa Upinzani na Mkoa wa Kigoma ni muhimu na lazima kupata Wabunge wengi kutoka Kambi ya Upinzani ili kupaza sauti ya Kigoma zaidi, jambo ambalo Wabunge kutoka CCM wanakwazwa. Hata hivyo, tutawakumbuka katika historia kama Wabunge mliokuwepo katika miaka muhimu ya mabadiliko katika Mkoa wa Kigoma na Mungu awajaalie huko mwendako.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya jumla. Sekta ya usafirishaji *(transport services)* ndio sekta inayoonekana ya kimkakati katika uchumi wa Tanzania. Nafasi ya kijiografia ya Tanzania inatoa upendeleo wa pekee wa sekta hii kuwa sekta chocheo kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Sekta hii ina mahusiano mazuri na chanya *(positive strong linkages)* na shughuli nyingine za kiuchumi, pia inagawa vizuri faida za ukuaji uchumi *(strongly supportive of broad based enabling environment)* na inaweza kutengeneza ajira nyingi sana. Sekta hii inajumuisha usafiri wa Reli, Barabara, Anga na Usafiri wa Majini. Sekta hii kwa Tanzania ni moja ya sekta zinazokua kwa kasi na mchango wake katika pato la Taifa, ni takriban asilimia saba, hii ni zaidi ya mara mbili ya mchango wa sekta ya madini katika *GDP* na zaidi ya mara sita ya mchango wa sekta ya umeme na gesi katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sekta ya Usafirishaji imegubikwa na changamoto nyingi sana na ni moja ya sekta ambazo licha ya umuhimu wake haipewi kipaumbele kabisa katika maamuzi ya Serikali. Iliichukua serikali zaidi ya miaka mitatu kupata suluhisho kuhusu kitengo cha makontena katika Bandari ya Dar es Salaam na kusababisha usumbufu mkubwa sana kwa wateja wa bandari yetu na hivyo kupoteza biashara kwa kiwango kikubwa sana. Imeichukua Serikali zaidi ya miaka minne kushughulikia suala la Ubinafsishaji wa Uwanja wa Ndege wa *KIA* na kuinunua kampuni ya *KADCO* na mpaka sasa bado menejimenti haijawa ya Shirika la Serikali. Imeichukua Serikali miaka mitano bila kupata suluhisho kuhusu ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania na hata kuweza kumaliza ubinafsishaji huo na kuua kabisa usafiri wa reli nchini. Inaendelea kuichukua Serikali miaka kadhaa kumaliza tatizo la Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*) na kuhatarisha sana biashara ya utalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu imekuwa ni Wizara yenye matatizo kuliko Wizara zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wakati gazeti la

*Sunday Citizen,* liliita Wizara ya Nishati na Madini *the most corrupt ministry of the year* 2008, Wizara ya Miundombinu imekuwa *the most incompetent Ministry* katika kipindi chote cha utawala wa miaka mitano ya Awamu ya Nne. Hii ni kutokana na hoja kuwa katika Wizara hii hakuna maamuzi yanayochukuliwa katika masuala mengi sana na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri wa Miundombinu alieleze Bunge na Taifa kwa ujumla juu ya utekelezaji wa Program ya Maendeleo ya Sekta ya Usafirishaji (*TSIP*). Huu ni mwaka wa tatu wa *TSIP*, Serikali haisemi hatua za utekelezaji ili tuweze kuipima. Kama rasilimali hazielekezwi katika *blue prints* ambazo tumezipanga wenyewe, ni kwa nini tunatumia muda na fedha kuweka mipango hii?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaaliwa na Mungu kwa kuzungukwa na Bahari ya Hindi na Maziwa makuu matatu ambayo ni Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Mungu angeweza kutunyima rasilimali nyingine zote na akatuacha na rasilimali hizi tu na tungeweza kukua kama Taifa kutokana na utajiri unaoweza kuzalishwa na Rasilimali hizi. Hata hivyo, Mungu ametujalia mengine mengi sana kama madini, mito yenye kuzalisha umeme na watu wapenda amani na wakarimu. Hata hivyo, bado hatujaweza kutumia rasilimali hizi kujiendeleza inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa reli ni usafiri muhimu sana kwa nchi na hasa kuhusiana na usafiri wa mizigo yenye uzito mkubwa. Hatuwezi kuendelea kamwe kwa kutegemea usafiri wa barabara kusafirisha mizigo yenye uzito mkubwa kama madini na bidhaa nyingine. Tanzania tuna reli mbili yaani ya *TAZARA* na ile ya Kati. Wabunge wamezungumza humu Bungeni kwa miaka mitano kuhusiana na adha ya usafiri wa reli. Kimsingi hatujapata jibu kuhusu reli ya kati. Wananchi wanaotumia reli kwa usafiri wanapata tabu kubwa. Usafirishaji wa mizigo umeporomoka kwa kiasi kikubwa sana kutoka tani 954 mpaka tani 570 ndani ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, reli zetu zote zinazosimamiwa na *TRL* na *TAZARA* bado zipo katika utaratibu ambao si wa kisasa. Ukiondoa uwezo mdogo wa kuhimili mizigo yenye uzito mkubwa zaidi, bado upishanaji wa treni unategemea kufika stesheni *(single track)*. Ni muhimu kuwa na treni zinazoweza kupishana bila kufika stesheni kwa kuongeza njia ili angalau ziwe mbili. Lazima pia uwepo mkakati wa makusudi wa kuzifanya reli zote ziwe katika mfumo wa kutumia umeme (*electrified railway system*) ili kuongeza ufanisi wa usafiri wa reli kwa kuongeza sana kasi, usalama na hata raha (*comfortability*) ndani ya mabehewa ya abiria.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mfumo wa reli za umeme kumezuia ujio wa wawekezaji walio makini zaidi kwenye sekta ya reli. Mifumo ya kizamani mno ya reli haivutii kuwekeza kwa faida na ni lazima kuachana nayo haraka. Treni zetu karibu zote zinatumia mifumo ya kizamani ya mawasiliano na ukiondoa simu za mikononi za abiria, wahudumu na madereva wa treni hizo, si rahisi kuona treni yenye mawasiliano bora ya redio au teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo viwanja vya ndege kwa usafiri wa anga, Stesheni za Reli zina umuhimu mkubwa sana kwa usafiri wa reli. Kwa muda mrefu sana Stesheni

za Reli zimekuwa ndio maofisi ya Shirika la Reli na pia zimekuwa zinamilikiwa kwa pamoja na Reli. Stesheni za Reli, hasa zile stesheni kubwa kama vile Tabora, Kigoma, Urambo, Mpanda, Kilosa, Dodoma, Morogoro, Tanga, Mwanza na Dar es Salaam zimekuwa hazitumiki kwa asilimia mia moja na kwa kweli stesheni nyingine zimekuwa chafu na hazihudumiwi ipasavyo. Nilizungumza suala hili katika hotuba zangu zote mbili zilizopita. Wizara imeweka mkakati gani wa kutumia Stesheni hizi kama vituo vya biashara na mahoteli?

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Tanzania kijiografia inatoa fursa kubwa kwa usafiri wa anga kuwa na manufaa kwa Taifa. Hivi sasa Taifa letu lina viwanja vya ndege viwili vya kimataifa yaani Julius Nyerere *International Airport* na Kilimanjaro *International Airport*. Kiwanja cha Songwe kinamaliziwa kujengwa. Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Kigoma, Tanga, Mtwara na Mafia ni viwanja muhimu sana kwa ukuaji wa sekta na uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, juzi alipokuwa Kigoma Rais wa Jamhuri ya Muungano alisema hadharani na mbele ya wananchi wa Manispaa ya Kigoma kuwa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kinajengwa kama Kiwanja cha Kimataifa ili kuhudumia nchi za Kongo – Kinshasa na Burundi katika eneo la Maziwa Makuu. Natumaini kuwa watendaji wa Wizara watakumbuka kauli hii ya Rais katika mradi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga: *TCAA* waliweka ushindani katika viwanja vyote vya ndege isipokuwa *KIA* katika suala la *ground handling* ambapo ni Kampuni moja tu ya *Swissport* inaruhusiwa kutoa huduma. Kwa sababu ya ukiritimba ni rahisi kwa kampuni hii kukataa kutoa huduma kwa makampuni mengine yenye wateja na hata kufanya huduma hizo kuwa ghali sana. Wizara iseme ni lini itaondoa ukiritimba huu ili kuongeza ufanisi katika huduma za usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la hanga pale KIA ambalo linaweza kutumika kwa ajili ya *hub* ya ndege binafsi katika eneo hili la Afrika Mashariki kwa ajili ya kuweka mafuta au kwa ajili ya kuhifadhi ndege kipindi ambacho wenyewe wapo katika mapumziko. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (*TAA)* imekodisha hanga hili kwa kampuni binafsi. Hata hivyo, kampuni hii haiwezi kupeleka ndege katika eneo hili na hivyo kupunguza matumizi ambayo yangeweza kuingiza mapato zaidi kwa nchi. Wizara iondoe vikwazo hivi ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inafaidika na uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa Hanga hii.

Mheshimiwa Spika, Kampuni yetu ya Umma ya *Air* Tanzania ambayo ilianzishwa baada ya kuvunjwa kwa mkataba na Kampuni ya *South Africa Airways* iliendelea kusuasua katika mwaka uliopita. *ATCL* ilisafirisha abiria wapatao 60,000 tu mwaka 2009 ikilinganishwa na abiria laki mbili na elfu saba mia tatu na tano mwaka 2008, abiria wanaosafirishwa na kampuni binafsi ya *Precision Air* mwaka 2009 walikuwa laki tano na elfu themanini na tatu ambao ni zaidi ya nusu ya abiria wote waliosafirishwa nchini mwaka husika *ATCL* hakuweza kufikia hata idadi ya abiria waliosafirishwa na kampuni ya *Costal Travel* ambao walikuwa ni takriban abiria laki moja na elfu arobaini na moja ni mategemeo ya Watanzania kuiona *ATCL* kama fahari ya Taifa *(The National Pride).* Hata

hivyo, hali ya *ATCL* inatia simanzi sana kwa sisi wapenzi wa sekta ya umma katika maeneo nyeti kama usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, shirika letu la ndege limekuwa katika wakati mgumu sana kwa kipindi kirefu kutokana na ukata na ukosefu wa fedha kutokana na hali ngumu ya kiuchumi ambayo inalikumba shirika hilo na hii inatokana na Serikali kutenga kiasi kidogo sana cha fedha ili liweze kujiendesha. kitendo cha *ATCL* kusafirisha nusu ya abiria waliosafirishwa na kampuni moja binafsi na robo tu ya abiria waliosafiri kwa ndege nchi nzima ni aibu kwa Shirika letu la Ndege kwani kama abiria wanaongezeka ilitegemewa kuwa ni Shirika letu la Ndege lingeweza kujiongezea faida na mapato zaidi kutokana na ongezeko hili la wateja, ila badala yake Shirika letu limekuwa na wakati mgumu zaidi kifedha.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Miundombinu aliunda Kikosi kazi cha kutazama jinsi ya kuokoa *ATCL* na taarifa yake tayari imekabidhiwa kwa Waziri. Hata hivyo, taarifa hii imefanywa siri kubwa na Utawala Bora unahitaji taarifa kama hii kutolewa kwa Umma ili wananchi waweze kujua hali ya Shirika lao, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri Bungeni kutoa taarifa haraka hapa Bungeni ili wawakilishi wa wananchi waweze kujua.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji wa mitaji ya Umma ya Juni 2009, Shirika la Ndege *ATCL* linadaiwa na kampuni ya ya *Celtic Capital* ya Miami *USA* kiasi cha shilingi 1.1bn kutokana na mkopo ambao haujulikani ulikuwa wa kiasi gani uliochukuliwa 15/12/2006 ili kukodisha ndege miwili *Boeing* 737-200. Dhamana ya Serikali imekwisha na deni halijalipwa. Shirika la *ATCL* pia linadaiwa na *Wallis Trading Company* ya Liberia USD 60,000,000 kwa kukodisha *Air bus* A320. Deni kwa mpaka sasa limefikia Tshs 13.3bn. Ndege hii ya *Airbus* ilipelekwa nchini Ufaransa kwa matengenezo na mpaka sasa haijarudi.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inalipa gharama za matengenezo kwa ndege hii, vile vile inatakiwa kulipa gharama za kukodisha ndege hii. Shirika limekufa na madeni yanazidi kuongezeka siku hadi siku. Naitaka Wizara ieleze kwa kina kuhusu madeni haya ya Shirika la *ATCL* na ni namna gani yatalipwa? Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu aeleze pia kwa nini ndege hii ya *Air Bus* haijarudi nchini baada ya matengenezo. Gharama za matengenezo zilikuwa kiasi gani na Serikali imelipa au inadaiwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, tafiti za masuala ya utalii zinaonesha kuwa kwa nchi zenye Shirika la Ndege la Kitaifa, asilimia 70 ya mapato yanayotokana na utalii hubakia ndani ya nchi husika ilhali kwa nchi ambazo hazina *National Carriers*, ni asilimia 30 tu ya mapato yanayotokana na utalii hubakia katika nchi zao. Ndio maana nchi kama Kenya inapata watalii zaidi na mapato ya utalii kubakia nchini humo kwa kiwango kikubwa. Hapa nchini kwa kuwa Shirika la Ndege la Taifa limekufa, ni theluthi moja tu ya mapato yanayotokana na Utalii hubakia nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kabisa kuona mahusiano haya na ndio maana imeshindwa kupata ufumbuzi kwa miaka mitano iliyopita. Kimsingi Shirika hili Serikali imeliua kwa miaka kumi sasa na kila mwaka linatokea katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwamba litaokolewa. Mwaka 2000, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ilisema *ATC* itabinafsishwa ili kuongeza ufanisi. Ilani ya mwaka 2005 ikasema Serikali italiondoa Shirika katika ubinafsishaji na kuliunda upya. Mwaka 2010, Ilani ya CCM itasema Serikali imeamua kulifuta Shirika hili iwapo kauli ya Waziri itazingatiwa kwamba Shirika litafutwa!

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kwa Serikali kwamba iwe na mwono tofauti katika suala la Shirika la Ndege la Taifa. Kwa kuwa Utalii unategemea sana usafiri wa ndege na kwamba sekta ya utalii itafaidisha zaidi nchi iwapo kutakuwa na Shirika la Ndege la Umma lenye nguvu.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ihusishe mashirika ya Umma yenye kuendesha shughuli za uhifadhi katika umiliki wa Shirika la Ndege. Serikali isitoze kodi kwa *TANAPA* na *Ngorongoro Conservation Area* (*NCA)* na badala yake mashirika haya yaruhusiwe kununua hisa za *ATCL* na kuwekeza mtaji. Sehemu ya mtaji ishikwe na Serikali na itakapofika Shirika kuanza kupata faida wananchi wauziwe sehemu ya hisa za Shirika.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji kutoka nje sio 'mwarobaini' wa matatizo yetu yote. Tunaweza kutumia mitaji ya ndani kimkakati ili kuimarisha Shirika la Ndege. Jambo la msingi ni Serikali kusafisha vitabu vya Shirika kwa kuchukua madeni yote na kuingiza uwekezaji kutoka Mashirika ya Umma ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Ndege ya *TGF* aina ya *Gulfstream* imezungumzwa sana hapa Bungeni. Kama wote tunavyofahamu, ununuzi wa ndege hii ambayo pia inayo hadhi ya kutumiwa na Rais wa Jamhuri, ulizua malalamiko mengi mno, hasa bei yake kubwa sana ikilinganishwa na umaskini mkubwa wa Tanzania, pamoja pia na gharama zake kubwa za kimatunzo na kiuendeshaji. Ni mara chache sana Rais wa Jamhuri yetu ameitumia ndege hiyo kwa safari zake nyingi sana za Kimataifa, ukiondoa zile za ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni nini kinachoendelea kuhusu uwepo mzima wa ndege hiyo na mchanganuo sahihi na wa kina wa faida zake za kiuchumi. Je, ni faida zipi za kiuchumi nchi yetu imezipata tangu ndege hiyo inunuliwe karibu miaka sita iliyopita. Ni kwa kiasi gani uwepo wa ndege hiyo umechangia kupungua kwa umaskini wa kupindukia wa wananchi wetu?

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Hali ya Uchumi inaonesha kuwa Tanzania ina mtandao wa barabara zenye jumla ya kilomita elfu themanini na tano (58,000) ambapo asilimia hamsini na tatu (53%) zipo katika hali nzuri na asilimia thethini na tatu(33%) ni za wastani, asilimia kumi na nne (14%) zipo katika hali mbaya sana. Mwaka 2008 kilomita elfu tano na mia tisa(5900) zilikuwa na hali nzuri mwaka 2009 jumla ya kilomita saba (7) zipo katika hali nzuri ongezeko hili limetokana na ukarabati wa barabara za

zamani na ujenzi wa barabara mpya. Hata hivyo, licha ya juhudi za Wakala wa Barabara nchini kujenga barabara zaidi, mtandao wa barabara za lami ni kilomita 5800 tu ambazo ni chini ya asilimia kumi (10%) ya mtandao wote wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la riba kwa makandarasi ambalo linaongeza gharama kubwa sana, kama nilivyoainisha katika hotuba ambayo nimeiwasilisha pamoja na *amendment* zake mezani, lakini pia *CAG* alifanya *Performance Audit* ya *value for money* ambayo Waziri hajaweza kuielezea ambayo iligundulika kwamba zaidi ya shilingi bilioni thelathini na sita zimelipwa zaidi kwa sababu ya mikataba kutokuwa imesimamiwa vizuri. Vile vile tumezungumzia kuhusu malumbalo ambayo yanaendelea kama jinsi ambavyo Kamati ilivyosema kati ya Wizara na Wakala wa Barabara. Ni malumbano ambayo hayasaidii, kwa sababu malumbano haya yalifikia hata kuhusisha maelekezo ya Kamati ya Bunge kwa Wizara kuhusu *TANROADS,* ambayo kimsingi ni *contempt of Parliament.*

Mheshimiwa Spika, nashangaa tu Mwenyekiti mwenzangu Mheshimiwa Missanga hakuweza kulisimamia hilo, kwa sababu inaonekana kabisa kwamba kuna barua ambazo zimetoka Wizarani zimelikishwa kwa Vyombo vya Habari kuhusiana na maelekezo ambayo Kamati ilikuwa imeyatoa, ambazo zilihusisha pia Maafisa wa Bunge ambao kimsingi inakuwa inaingilia uhuru wa Bunge kuweza kufanya kazi zake zinavyotakiwa. Kwa hiyo, kama jinsi Kamati ilivyosema ni vizuri Serikali iangalie jinsi gani ya kuweza kulimaliza suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kuhusu mjadala unaoendelea sasa kupitisha kilomita 60, barabara katikati ya hifadhi ya Serengeti. Kumekuwa na majadiliano makali kuhusu suala hili, ambalo wakati mwingine yamezaa hali ya uzalendo na pia uzalendo upofu yaani *Blind Nationalism*. Napenda kunukuu maneno ya Mwalimu Nyerere kuhusu uhifadhi kama alivyoyatamka katika Arusha Manifesto hapo Septemba mwaka 1961. *"In accepting the trusteeship of our wildlife we solomnly declare that we will do everything in our power to make sure that our children's grandchildren will be able to enjoy this riches and prestigeous heritage".*

Mheshimiwa Spika, maneno haya ya Mwalimu imekuwa ni dira ya wahifadhi wote nchini. Suala la barabara kupita hifadhi ya Serengeti lipimwe kutokana na lengo hili la kutunza uhifadhi. Swali muhimu la kujiuliza wakati tunafikiria kujenga ama kutokujenga barabara hii na hata kuweza kuhatarisha uhifadhi. Je, kama nchi tutafaidika au hatutafaidika na je kuna mbadala au hakuna mbadala wa barabara hii?

Mheshimiwa Spika, tusikimbilie kupeleka lawama kama ilivyo kawaida yetu kwa majirani zetu au kusema ni kuchagua kati ya watu na wanyama, kwani ni lazima tutambue kama Tanzania tunawajibu wa kiulimwengu wa kutunza utajiri uliopo Serengeti.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kurejea hitimisho langu la mwezi Julai mwaka 2007, Kambi ya Upinzani inatekeleza wajibu wake wa kidemokrasia wa kutoa maoni na hoja ili Kambi ya Chama Tawala ifanye kazi kwa maslahi ya Taifa. Nawatahadharisha wenzetu kuwa, hali ya kisiasa ya nchi imebadilika sana na kwa kasi, iwapo walio na Serikali watashindwa kutekeleza mabadiliko muhimu ya kisera ili kuendana na upepo wa mabadiliko ya kiuchumi, wananchi watawapumzisha. Sisi tunasubiri tupewe ridhaa na wananchi ili tutekeleze mipango hii ambayo wenzetu mmeshindwa kutekeleza. Mawazo mbadala tunayo, nguvu ya kutekeleza tunayo, nia pia tunayo na tunaweza! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii uliyonipa na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Waheshimiwa Wabunge orodha yangu ina wachangiaji 35, ni dhahiri kwa siku moja haitawezekana hawa wote. Ambao hawajachangia kama kawaida ya Kanuni zetu tunawapa kipaumbele ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Rita Mlaki na Mheshimiwa Eng. Laus Mhina.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia mara moja nitawataja watano tu wa kwanza ili wajiandae, nao ni Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Mohammed Missanga na Mheshimiwa Fuya Kimbita na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga.

Waheshimiwa Wabunge kwa mpangilio huo, nitamwita sasa Mheshimiwa William Shellukindo, atafuatiwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini wakati huo Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi ajiandae.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo kwenye hoja hii ya Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake pamoja na Wakuu wa Taasisi nyingine kwa kazi nzuri wanazozifanya. Wizara hii ni ngumu sana. Kama tunavyojua barabara zetu ziko katika hali mbaya, kwa hiyo, huwezi kutegemea kwa siku moja zote zikawa katika hali nzuri, lakini kwa hatua niliyoiona mimi kwa kweli wamejitahidi sana, wanahitaji pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo machache tu ambayo nilitaka kuchangia hapa, suala la kupandisha hadhi barabara nadhani Waziri anajua tuna barabara ya Bumbuli, Mayo, Mgwashi, Bagambelei kilomita 50. Barabara hiyo ni muhimu sana katika Jimbo la

Bumbuli, lipo katika maeneo ya kulima chai, maharage kwa wingi, viazi, vitunguu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kazi ambayo ilikwishafanyika kwenye mradi wa kuimarisha miundombinu ya mazao ambapo tulipata msaada wa shilingi milioni mia saba, sasa nguvu ile itapotea kwa sababu Halmashauri yetu haina uwezo wa kuweza kuitengeneza barabara hii. Tulitengeneza kilomita thelathini kati ya kilomita hamsini, tuliomba kwa muda mrefu sana toka mwaka 1998, tunaomba barabara hii ichukuliwe ili kuimarisha uchumi katika Jimbo hilo. Naamini Waziri katika kitabu chako cha Hotuba ukurasa wa 55 mnasema kwamba *The road reclassification Order* 2009 imeshatengenezwa ambayo nadhani mmeweka vigezo vipya, sasa ni vizuri vikatoka hivyo na sisi tuelewe kwa mfano mimi nijue barabara ya Soni- Bumbuli-Dindira kwa nini haikidhi vigezo, kwa sababu na mazingira ya mahali vilevile palivyo ni moja ya mambo ya kuangalia.

Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru sana Wizara pamoja na Serikali kwa kuiweka barabara ya changarawe ya Soni-Bumbuli-Dindira chini ya Mkandarasi kwa matengenezo ya miaka mitano tunashukuru sana barabara hiyo kwa kweli ilistahili kuwekewa lami kwa sababu ni muhimu sana kibiashara. Wakati wa ukoloni wa Ujerumani ilifikiriwa kwamba barabara ya kutoka Mombo kwenda Lushoto hiyo ni barabara ya Kiutalii kwa sababu inapita kwenye miamba na huwezi kuipanua. Barabara hii ndiyo ingekuwa barabara ya uchumi. Barabara inayotoka Lushoto kuja Soni, Bumbuli, Dindira halafu, Kwashenshi, Wilaya ya Korogwe. Hiyo ndiyo barabara ya kiuchumi ambayo inategemewa kwa sababu siku moja tu likiteremka jiwe moja katika eneo linaloitwa Vuga *road,* barabara ya Mombo- Lushoto basi itabidi pengine tukae wiki nzima bila kutoka katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho nataka kukizungumzia hapa ni kwamba baada ya kuweka barabara hiyo chini ya Mkandarasi, usimamizi wa mkandarasi uko mbali mno. Uko Dar es Salaam kwa *Chief Executive* wa *TANROADS*, pale Mkoani ni kama mahali pa kupitishia tu malalamiko kwamba kuna eneo limeharibika kwa hiyo Meneja wa Mkoa wa *TANROADS* apige simu Makao Makuu kumweleza kwamba kuna tatizo huku ili amfahamishe mkandarasi ambaye yupo kwenye *site* pale. Nadhani utaratibu wa kusimamia hizi kazi ungetazamwa upya ili maamuzi yasichelewe kutolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wetu wa Bodi ya Barabara Mkoa wa Tanga wa tarehe 17 Mei, 2010, hili suala tulilizungumza kwamba usimamizi ukiwa mbali mno kutakuwa na matatizo. Barabara ya Soni Bumbuli ilipata matatizo, kuna maeneo yalikuwa hayapitiki, ilibidi nimpigie simu Mhandisi Meneja wa Mkoa wa *TANROADS* halafu na yeye sasa amfahamishe *Chief Executive* ili na yeye ampe maelekezo huyu Mkandarasi ambaye yupo kwenye *site*. Nadhani utaratibu huu siyo mzuri. Usimamizi usogezwe karibu, wale Wahandisi wa Mkoa ni wazuri wanaweza kusimamia, wakifika mahali wamekwama ndiyo wanamtafuta *Chief Executive Officer.*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya kilomita chache tu katika kitabu cha Waziri ukurasa 237, Vuga Road-Vuga *Mission*. Hiyo barabara ina historia, ilifikishwa hapo Vuga *mission* kwa sababu wakati huo wa ukoloni pale palikuwa na Wazungu, kwa hiyo ikaishia hapo. Sasa Wazungu hawapo. Lakini Makao Makuu ya Kata hiyo ya Vuga yapo kilomita moja kutoka pale Vuga *mission*, tunaomba wachukue hiyo kilomita moja ili tuondoe ile fikira ya zamani kwamba barabara ilifika pale kwa sababu pale kulikuwa na watu weupe. Tumeipeleka kwenye Bodi ya Mkoa lakini Bodi haina madaraka ya kuweza kuongeza hiyo sehemu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri na usafirishaji hapa nchini, ningependa Serikali yetu izidi kupiga kichwa. Usafiri ambao nauona kwamba utaweza kuendeleza uchumi wetu hapa ni wa reli. Huu wa barabara ni ghali mno. Hayo magari mazito yanayopita kwenye barabara zetu za lami ambazo tunazitengeneza vizuri yanasababisha zisichukue muda kwa sababu uzito ule ni mkubwa sana unatakiwa ubebwe kwenye reli. Tuna mtandao wa reli hapa nchini, ni vizuri tukatazama upya. Kwa mfano ukitoka Dar es Salaam kwenda Ruvu, pale Ruvu kuna tawi linakwenda Mnyuzi inaungana na Reli ya Tanga, inakwenda mpaka Moshi- Arusha, halafu kuna sehemu ya Kahe inakwenda Voi, *network* moja.

Mheshimiwa Spika mwenzangu wa Upinzani Mheshimiwa Zitto nadhani alisahau kwamba tunazo reli tatu, tuna TAZARA, tuna reli ya Kati na tuna reli ya Kaskazini, hizi zote zikifufuliwa na kuimarishwa tutapunguza gharama kubwa sana ya kujenga barabara na kuzitengeneza kwa sababu uzito wa mizigo unaharibu sana barabara na vile muda unaochukuliwa na hata uchakachuaji pengine ingekuwa rahisi kuuzuia. Treni inasimama mahali ambapo inatakiwa kusimama haiwezi kusimama mahali popote pale, kwa hiyo unaweza kudhibiti uchakachuaji.

Mheshimiwa Spika, lori lililobeba mizigo, limebeba mafuta anaweza kulala mahali popote pale, wana vituo vyao, kwa hiyo uchakachuaji unafanyika. Kwa hiyo napendekeza kwamba, kipaumbele katika usafiri na usafirishaji kwa kweli tungeweka katika mtandao wa reli, tunazo ni za kufufua tu. Hata hizi mpya ziende taratibu lakini tungeweka umuhimu wa kwanza katika hizi ambazo zipo tayari ili tuweze kuziimarisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tukifungua ile ya Arusha-Musoma, huku hujatengeneza hii ya Ruvu kwenda Mnyuzi kuunganisha kwenda na ile ya Tanga utakuwa bado kuna kazi ambayo hujaifanya. Kwa hiyo, nadhani tungefanya programu maalum kabisa ya kukarabati reli na hiyo programu ingeletwa hapa, Bunge litaarifiwe japokuwa pengine wengine hatutakuwepo lakini Bunge litakuwepo, lakini nadhani wananchi wa Bumbuli wanaelewa tumetoka wapi, tupo wapi na tunaelekea wapi, watatumia akili zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo, naunga mkono hoja hii na kusisitiza hayo ambayo nimeyazungumza, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara hii muhimu ya miundombinu. Nianze tu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema

ya kuweza kuhudhuria Bunge lako Tukufu. Lakini vile vile niwashukuru sana na kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Mara kwa kuniteua kuwa Mbunge wao kwa kipindi chote cha miaka mitano. Niwaombe wasisite kuniteua tena au kunichagua tena kwani nimejipanga kuwatumikia kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo nichukue pia fursa hii kuwapongeza sana Wizara ya Miundombinu, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watalaam wote kwa hotuba nzuri sana ambayo wametuletea leo hii.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nikiisoma hotuba hii kwa mimi Mbunge wa CCM na wengine wenzangu wengi kutoka mikoa mingine watakubaliana nami kwamba kazi yetu wakati huu ni nyepesi sana, kwani kwa kiasi kikubwa miradi mingi sana imetekelezeka na hata ile ambayo haijatekelezeka inaendelea kutekelezwa. Mimi binafsi nitakuwa na pongezi zaidi lakini mambo machache ya kurekebisha hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kutujengea gati na hasa gati zilizokuwa zimeharibika sana kama gati ya Kisolya sasa hivi limekarabatiwa lakini vile vile gati ya Mwigobelo imekarabatiwa, gati iliyopo Shirati imekarabatiwa, kwa hiyo, tunaishukuru sana Wizara kwa ukarabati huu mkubwa uliofanyika kwenye gati hizi tatu.

Mheshimiwa Spika, vile vile nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mara na hususan Wilaya ya Musoma Vijijini kwa ujenzi wa barabara ya Kyabakari-Butiama. Sote tunaelewa kwamba Butiama ni eneo muhimu sana na tunashukuru sana Serikali kwa kuikarabati barabara hii yenye urefu wa kilomita kumi na moja kwa kiwango cha lami, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitoe shukrani zangu ingawa zitakuwa shukrani za furaha, lakini vile vile masikitiko kidogo kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara mbili kubwa ambazo zimefanyika kwa muda mrefu sana. Moja ni hii barabara ya Musoma- *Fort* Ikoma yenye urefu wa kilomita 140. Naomba kueleza masikitiko yangu kwa upande wa wananchi wa Mkoa wa Mara kwamba barabara hii tangu mwaka 2006, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika lakini mpaka hivi leo ninapoangalia kwenye vitabu hivi sioni pesa za kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo namwomba Waziri atakapokuwa ananijibu tangu mwaka 2006 ni kitu gani kimesababisha barabara hii ikwame na isiweze kuwekewa hata pesa nusu ya kuweza kuanza kujenga barabara hii ya Musoma- Fort Ikoma kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile barabara hii ambayo namshukuru sana Mheshimiwa Zitto ameizungumzia barabara ya Nata –Mugumu mpaka Loliondo. Kwa kweli Mheshimiwa Zitto siyo Mbunge wa Musoma lakini barabara hii kwetu Wabunge wa Musoma ni siasa. Wananchi wa Mkoa wa Mara wanasikitika sana na mpaka sasa hivi hatujui nini kinaendelea, tunasikia mambo mengi sana ya chini chini na hata sisi Wabunge tukiulizwa na wananchi tunashindwa kujua nini kinaendelea.

Kwa miaka mitano sasa barabara hii yenye urefu wa kilomita 452 imekuwa ikitengewa pesa, milioni mia tisa, milioni mia saba na bado tunaambiwa upembuzi yakinifu bado. Mimi kama Mbunge napata wasiwasi kidogo, kweli upembuzi yakinifu kwa miaka mitano na bado kuna maneno mengi kwamba haiwezi kujengwa na kama hizo kilomita tisini zinapita katikati ya Mbuga za Wanyama basi kuwe na mbadala.

Mheshimiwa Spika, tunao mbadala, tuna barabara nyingi, ni Wizara tu ingekaa na Wabunge na Mkoa kwa ujumla tukaweza kuamua basi kama hii barabara ya Nata-Mgumu-Loliondo imekuwa kikwazo tunayo barabara nyingine ambayo inatumika sana ambayo ni barabara ya Musoma-Makutano –Kiagata- Mugumu mpaka Arusha inaweza ikaishia Mugumu. lakini ukiijenga barabara hii ya Makutano-Kiagata-Mugumu ambayo ina urefu wa kilomita 120 sisi wananchi wa Mkoa wa Mara tutakuwa tumefarijika sana. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri kama barabara hii imekuwa kikwazo basi tupewe mbadala, hatuwezi kukaa Wabunge miaka mitano tunalilia barabara ya Nata – Mugumu – Loliondo na kila siku tunaridhishwa kwa kupewa milioni 900 bilioni moja ambayo haitufikishi popote.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo ni ahadi ya Rais, Rais ameisemea sana barabara hii. Sasa nachanganyikiwa kabisa kama Rais anakuja Mkoa mara tatu anaahidi barabara moja kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, barabara ya Nyamswa-Bunda – Kisorya yenye kilomita 90 lakini hatuoni chochote kinachoendelea. Mwaka jana nilisimama hapa nikauliza kuhusu barabara hii nikaambiwa inatengewa fedha mwaka huu wa fedha. Hakukuwa na fedha yoyote iliyotengwa. Sasa tuko katika mwaka wa uchaguzi, ahadi ya Mheshimiwa Rais haijatekelezwa na hatuna maelezo yoyote, wananchi wa Mkoa wa Mara. Ningependa Mheshimiwa Waziri anieleze barabara hii ya Nyamuswa-Bunda–Kisorya iko katika hatua gani? Kama inajengwa au Wizara imemdanganya Rais au ni vipi basi tuweze kuelezwa wananchi wa Mkoa wa Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ninayo mapendekezo, katika Mkoa wa Mara kuna barabara muhimu sana, sisi Mkoa wa Mara tunaziona kwa mfano, hii barabara ya Musoma–Majita mpaka Bukumi. Barabara hii inapita pembeni mwa Ziwa Victoria na shughuli zote za uchumi zinafanyika kwa mfano za uvuvi, lakini barabara hii ni mbovu ajabu. Mvua ikinyesha madaraja yote yanajaa na vile vijiji vyote vinafunikwa na maji. Kwa hiyo, ningeomba barabara hii iweze kupandishwa hadhi itoke kwenye Kiwango cha Mkoa ipelekwe kwenye kiwango cha Tifa tuweze kuwekewa lami.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza sana Wizara kwa kutuwekea kivuko cha Lugezi, Kisorya. Kivuko hiki kilikuwa kina hali mbali kinavutwa na kamba. Kwa kutumia Bunge hili nafikiri wananchi wa Mkoa wa Mara na hasa wananchi wa Bunda wamesikia kwamba tutapata kivuko kipya mwezi Septemba, 2010. Naomba Serikali ikamilishe kuleta kivuko hiki mapema.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pili, labda niseme kwamba tumezoea Watanzania kusema maji ni uhai. Lakini miundombinu ni uhai wa Taifa. Kwa hiyo, tunapozungumzia Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu katika nchi yetu ni lazima tujue kwamba tunazungumzia uhai wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, miundombinu kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza tunazungumzia Reli, Bandari, Barabara, Viwanja vya Ndege na bahari kwa ujumla. Vyote hivi ni vitu ambavyo vinatakiwa tuviweke katika mipango yetu ya muda mrefu. Sasa hivi inavyojitokeza ni kwamba tumeweka umuhimu zaidi katika barabara. Lakini tunapoangalia miundombinu mingine hasa Reli, Bandari kwa kweli Kitaifa hatujazipa uzito unaostahili. Sisi kama nchi tutaendelea kuwaona majirani zetu wanapiga hatua. Lakini Tanzania tutakuwa tunaendelea kubaki hapo hapo kwa sababu tumepuuza bandari zetu. Hata usafiri wa ndege *for that matter*. Kwa hiyo, ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba reli na hatuzungumzii tu Reli ya Kati, *TAZARA*, ya Tanga tunazungumzia na kuanzisha zingine. Ile ya *Mtwara Corridor* kutoka Mtwara kwenda Songea mpaka *Mbamba bay* tunaiweka katika mipango yetu, lakini mipango hii ya kuzungumza tu inaelekea kana kwamba inazidi kutukwaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bandari tunazungumzia bandari ya Dar es Salaam, lakini Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara, Bandari ya Mwanza, Kigoma, Kasanga, Kyela, Mbamba Bay hizi zote ni bandari zetu. Ni lazima nazo tuzipe umuhimu. Kama hatutazifungua hizi basi tujue kwamba mawasiliano na majirani zetu na nchi zingine za ulimwengu hatutaweza kufanikisha.

Mheshimiwa Spika, Viwanja vya Ndege sasa hivi tunazungumzia Dar es Salaam zaidi na Kilimanjaro. Lakini kuna Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Kigoma. Kigoma hata tufanyeje ni lazima tukubali kwamba kiwanja kile tupende tusipende ni lazima tutakijenga. Jinsi tunavyozidi kuchelewa ndiyo gharama za ujenzi wa viwanja hivyo inavyozidi kukua. (*Makofi*)

Nashukuru uwanja wa Songwe sasa inaelekea utakamilika hivi karibuni. Lakini Kanda ya Kusini inahitaji Kiwanja, Mtwara inahitaji, Songea inahitaji kiwanda. *Planners* wetu lazima waangalie masuala haya kwa sababu hii habari ya kuangalia tu viwanja hivi tulivyozoea *traditional,* kila mara Tanzania haiko Dar es Salaam peke yake, Tanzania ni Tanzania katika ujumla wake wote.

Sasa najua kwamba tutakapokimbilia ni kwamba fedha ziko wapi. Lakini mwaka uliopita nilisema hapa kwamba lazima tuwe jasiri kwenda kukopa ndivyo wenzetu wanavyofanya. Tusingonjee wafadhili. Wafadhili watatuwekea vikwazo vingi sana. Nchi yetu sasa inakopesheka. Hebu tukakope. Hakuna nchi yoyote ambayo itaipeleka Tanzania

mahabusu kwa kwenda kukopa. Lakini tukiweza kujenga miundombinu hii ndio itakuwa ufumbuzi wa matatizo yetu mengi ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nizungumzie suala lililojitokeza hapa, mapendekezo ya kuwa na wakala mbili za barabara,*TANROADS* na kwa ajili ya barabara za Wilaya. Hakuna kosa kubwa tutalifanya kama kuendelea ku-*duplicate* wakala wawili. wakala *TANROADS* tumpe muundo unaotosheleza na kusimamia hata kama tunataka aende kwenye barabara za Wilaya, lakini tusiendelee na kuunda *authorities* kila mahali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la uchakachuaji mafuta. Hili ushauri wangu kwa Serikali ni mdogo tu. Tatizo letu kubwa ni kwamba tuna sheria nyingi sana lakini usimamizi wa sheria zetu haupo. Mimi nasema kwamba wachakachuaji mafuta hawa ni wahaini. Hakuna jina lingine la kuwaita. Wachakachuaji mafuta hawa ni watu ambao ikibidi kama mtu atakutwa amepatikana na kosa hilo faini yake ianzie shilingi milioni mia moja siyo milioni moja. Afungwe miaka zaidi ya 10 kwa sababu hawa wanachofanya ni wahujumu wa uchumi. Wenzetu nchi zingine wanachofanya ni kuwapiga risasi hawa. Najua Watanzania ukianza kuzungumza suala la kupiga watu risasi tunastuka sana. Lakini wanachofanya ni kitu gani kama siyo kujaribu kuwaua Watanzania na juhudi za Watanzania katika kuleta maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoomba Serikali, ni kuwa wakali katika suala hili. Tunavyozidi kuwafumbia macho hawa maana yake ni kwamba tunawafanya wahalifu hawa wajione kwamba wao wana haki kuliko Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kwa ndugu zangu wa Jimbo la Mlalo, nawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Mlalo kwa jinsi ambavyo wamejiletea maendeleo yao kwa kupitia juhudi zao wenyewe katika kutekeleza Ilani ya CCM. Utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Jimbo la Mlalo kwa kweli umefika asilimia 98 na ukija kwenye sekta ya elimu wamechukua zaidi ya asilimia 180. Upande wa sekta ya afya nako vile vile tunapiga hatua. Najua watu wamezungumzia masuala kwenye kituo kimoja cha Mlalo kumetokea mambo gani, hizo ni siasa kwa sababu mambo ambayo yamejitokeza pale si ambavyo yalivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie kwa kusema kwamba *fuel levy*. Mwaka juzi tulivyopitisha suala la *fuel levy* kwamba tutoke 100 twende 200, wengine tulikuwa tumesema twende 300. Hata sasa hivi hatujachelewa zaidi, *fuel levy* ikibidi twende kwenye shilingi 300. Barabara hizi na sekta hii ya mawasiliano inahitaji fedha hizo. Watanzania tusiwe tunaogopa mno katika kufanya maamuzi. Maamuzi haya ni kwa ajili ya faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nizungumzie barabara ya Lushoto kwenda Magamba, ni kilomita sita tu, ilianza kuwekwa lami mwaka 2004, ilitakiwa ikamilike mwisho wa mwaka 2004. Matengenezo ya barabara ile yamekuwa yakifanyika kwa kilomita moja moja kama mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mnaweza kuwa mnahitaji kufuatilia mambo ya Serikali, napenda mtambue kwamba Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali hivi sasa ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu. Awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watalaam wote kwa kuweza kutuandalia bajeti hii ambayo nasema inazidi kutupa matumaini katika kuweka mawasiliano katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya pekee niishukuru Serikali. Utakumbuka kipindi kama hiki mwaka juzi nilisimama hapa nafoka na kupiga kelele juu ya kivuko cha Pangani. Nikisimama tu inaeleweka kwamba nitazungumza Kivuko cha Pangani. Lakini leo kauli yangu imebadilika nasimama hapa kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake kwa ujumla kwa kuweza kukamilisha ahadi ya Ilani ya Uchaguzi na hivi sasa niseme Kivuko cha Pangani ni kipya na kinatumika kama kawaida na tunategemea Mheshimiwa Rais wakati wowote aje kukizindua na hatimaye wananchi waweze kumsikiliza Mheshimiwa Rais katika uzinduzi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hiki ni kipindi kigumu kidogo kwa maana ya uchaguzi. Lakini kama Waheshimiwa Wabunge tumefanya basi tumefanya, tunayo maelezo ya kusema. Wanaokuja hawana maelezo, lakini maelezo yao ni fedha. Lugha ya fedha inajulikana. Lakini wananchi wanahitaji maendeleo kuliko fedha. Lakini fedha hizi tunazihitaji zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali vile vile kwamba sasa hivi mradi wa Horohoro Tanga umeshaanza na tunategemea sasa hivi baada ya kukamilisha barabara hiyo tutakuwa na mpango mzima kama hotuba ya Waziri inavyosema. Kuna mpango wa Bagamoyo-Sadan na barabara hiyo iendelee hadi kupitia Pangani na Tanga kukamilisha *network* mbadala ya kutoka Dar es Salaam kwenda Tanga iwe kuna njia mbadala ya kutoka huko kwa maana ya kupitia Tanga, Pangani, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mbele yetu kuna miradi mizito mikubwa ambayo kama nchi inahitaji fedha nyingi kwa ajili ya kukamilisha. Tuna sera ya *public private partnership* na sheria ipo njiani inakuja na naamini sera na sheria hiyo ndiyo itakuwa mkombozi wa kutatua matatizo mengi ambayo yatasababisha nchi yetu kuondokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninukuu baadhi ya miradi ambayo Serikali kwa kweli inaitilia maanani lakini kutokana na uwezo wa fedha inashindwa kuitekeleza. Suluhisho ni kuwa na sheria pamoja na sera tuliyokuwa nayo ya *public private partnership,* naamini hili ndio litakuwa suluhisho. Sasa tunachoomba ni kupunguza ule urasimu, wawekezaji

wanapokuja Tanzania kwa kweli tuwachangamkie, tusiwakatishe tamaa. Tuna mifano hai mingi, mtu anakuja Tanzania ana *interest* ya kutekeleza mradi mkubwa ambao Serikali haina uwezo lakini anakatishwa tamaa kutokana na urasimu uliopo miongoni mwa baadhi ya watalaam wetu.

Mheshimiwa Spika, pengine hata Mheshimiwa Waziri, hana habari kwamba hawa watu wamekuja na wanataka wamuone lakini wanamuondoa njiani. Miradi mikubwa baadhi yake nataka kusema, kuna bandari ya Mwambani Mkoani Tanga, tukiunganisha na reli kutoka Tanga kwenda Musoma na reli hii siyo tu italeta faida kwa nchi jirani lakini vile vile kusaidia ile *soda ash* ambayo iko pale *Lake Natron* ambayo inatakiwa duniani na hatimaye iweze kuinufaisha Tanzania na kupata kipato kikubwa hatimaye tuweze kunufaika na *soda ash* ambayo imekaa milioni ya miaka pale haina kazi. Sasa huu ni mradi mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa Bandari ya Mtwara. Bandari ya Mtwara ni Bandari tunaita *natural harbour,* huhitaji kuongeza kina. Kina kiko pale, *low tide* ni mita 12 mpaka 14, *high tide* ni mita 14 mpaka 22. Sasa huu ni mradi muhimu sana hasa kwa maendeleo ya uchimbaji wa gesi na mafuta ambao unaendelea kule Mtwara ni moja ya miradi ambayo tunaihitaji kwa nguvu kabisa katika nchi hii ili tuweze kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine *Stigler's Gorge* kwa upande wa umeme. Hii Serikali haina fedha lakini inahitaji mradi ule. Nyingine ni Mradi wa Mchuchuma na Liganga unahitajika kwa sababu ya kuongeza uchumi.

Mheshimiwa Spika, bado nina dakika tano. Hii yote ni miradi ambayo kwamba ….

**SPIKA:** Unazo dakika tatu. Huwa tunapiga dakika saba halafu dakika tatu. Kwa kuwa nimekusemesha basi naongeza moja. Kwa hiyo, utakuwa na nne.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo wapo wawekezaji, wako tayari na fedha hawajui wazifanye nini, wanatafuta miradi kama hii. Hivi sisi Tanzania tunakosa nini? Kumwambia kwamba njoo, lete fedha zako tutakupa eneo la *Stigler's gorge* utajenga miundombinu ya umeme pale tutapunguza gharama za umeme nchini ambazo wananchi wanazipigia kelele. Sisi *Tanzania Stigler's Gorge* haitaondoka Tanzania kwenda sehemu nyingine. Wale wawekezaji wakamaliza muda wao wataondoka, watatuachia *Stigler's Gorge* yetu, tutaendelea kuitumia milele mpaka hapo tutakapoona njia mbadala. Bandari zetu ni hivyo hivyo hazitaondoka. Leo Kenya wanajenga Bandari Lamu ili ku-*compete* na Tanzania. Tuna matatizo sasa hivi ya mafuta, wanataka kuhama waende Mombasa. Sasa haya yote ni matatizo lakini naamini *public private partnership* itakuwa ni mkombozi, lakini ni lazima sheria hii ieleweke vizuri iwe na utaratibu wa *win situation* kati ya Serikali na mwekezaji ili tuweze kumvutia yule mwekezaji aone hamu ya kuja kuwekeza Tanzania na hatimaye yeye asipate hasira vile vile katika mpango mzima.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasisitiza suala hili la *private partnership* basi wakati ukifika wa kujadili Muswada huo tutapata nafasi ya kuuona Muswada na jinsi

Serikali itakavyoweza kuusoma Muswada huu na sisi Waheshimiwa Wabunge tuweze kuchangia tuone kwamba tunapoingia mwaka 2010 basi tuingie na mipango mizuri ambayo kwa miaka mitano tujione kwamba tumepunguza kwa kiasi kikubwa matatizo yetu ya miundombinu Tanzania na hatimaye kukuza uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimshukuru tena Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na wataalam wote na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na niseme ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rished, hongera kwa Pangani kupata kivuko kipya. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Kabwe Zitto, nadhani kutakuwa na nafasi ya kumwita Mheshimiwa Rita Mlaki baada ya hapo. Mheshimiwa Kabwe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. Hotuba niliyosoma ilikuwa ni ya Kambi ya Upinzani, mimi nina masuala kama manne tu ya kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ambayo sikuweza kuyaingiza katika hotuba ya Kambi kama Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni barabara za Magharibi. Katika taarifa ya Serikali na hotuba ya Waziri, imeonyesha kuwa kuna hatua fulani fulani ambazo zimefikiwa kwa barabara za Magharibi na hasa Mikoa mitatu tu ambayo imebakia haijaunganishwa na barabara za lami.

**MBUNGE FULANI:** Minne.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Lakini Mikoa mitatu ni ya Magharibi. Kati ya Mikoa yote minne ambayo haijaunganishwa ni ya Magharibi tu ambayo ni Rukwa, Tabora na Kigoma. Barabara zote ambazo zitaweza kuunganisha Mikoa na hasa Mkoa wa Kigoma na Tabora, bado ziko katika hatua za chini sana. Katika maendeleo ya miundombinu ya nchi, huwezi ukapita juu ya Mkoa wa Tabora unapotaka kuiunganisha nchi. Kwa hiyo, Tabora ni Mkoa ambao upo *strategicaly positioned* na barabara zote ambazo ni muhimu za Mkoa wa Tabora zipo katika ama upembuzi yakinifu au Mkandarasi bado anatafutwa.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka mwaka jana kulikuwa na ubishani mkubwa sana hapa wa barabara ya Nzega - Tabora ambayo ni moja ya barabara mbaya sana kwa kweli. Nimepita juzi, nikikagua barabara kama Waziri Kivuli, nimeiona ile barabara ambayo mwaka jana tuliitengea shilingi bilioni 5.6, barabara ya Nzega – Tabora. Taarifa ya Serikali inasema barabara ile Mkandarasi bado anatafutwa, maana yake nini? Waziri anasema sehemu ya Nzega - Tabora kilomita 116, mchakato wa kumpata Mkandarasi upo hatua za mwisho. Maana yake ni kwamba shilingi bilioni 5.6 ambazo tulizitenga mwaka jana ama zimetumika kwa ajili ya kumtafuta Mkandarasi tu au hazijatumika kabisa na kwa sababu tunaanza mwaka mpya wa fedha tarehe 1 Julai, 2010 na mwaka huo mpya wa fedha zimetengwa takribani shilingi bilioni 6, yaani wameongeza shilingi bilioni 1,

maana yake ni kwamba fedha zote za mwaka ambazo zilitengwa kwa ajili ya barabara ya Nzega - Tabora na hazijatumika na tumetenga shilingi bilioni 6 tu kwa sasa hivi na ni kilomita 171, kwa nini isiwe shilingi bilioni 11, kwa maana ya mwaka jana na mwaka huu, kwa nini imewekwa shilingi bilioni 6 tu? Nahitaji kupata maelezo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni barabara ya Kigoma – Kidawe – Uvinza - Kaliuwa na Tabora. Kwanza imetengewa hela za kutosha yaani kwa kuanzia ni fedha nyingi sana, zimetengwa shilingi bilioni 86. Lakini jinsi ambavyo hii barabra imewekwa, ni tofauti na maeneo mengine ambapo barabara zilijengwa. Maeneo mengine tofauti na Magharibi walikuwa wanaanzia huku na huku. Kwa maana hiyo, barabara moja ingeweza kuanzia Kigoma na nyingine ikaanzia Tabora – Urambo – Kaliuwa, zikutane.

**SPIKA:** Hawataki. (*Kicheko*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, sasa zimetengwa shilingi bilioni 86, lakini mtiririko ni ule ule wanaanza Kigoma – Kidawe – Uvinza -Kaliuwa mpaka ije kufika Urambo – Tabora, inaweza kuchukua miaka mingine nane. Jambo zuri na la haraka ilikuwa ni kuanza kujenga kutoka Kigoma - Kaliuwa na kutoka Tabora - Kaliuwa. Hilo nalo naomba Waziri aliangalie na aweze kutueleza kama inawezekana kufanya hayo mabadiliko ili wananchi wa pande zote mbili wanufaike.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo ukiwa Kigoma utawaambia watu wa Kigoma barabara inajengwa ya kwenda Tabora kwa hiyo, biashara zitaongezeka tutapeleka chakula Tabora. Ukifika Tabora huwezi kusema hivyo kwa sababu hawaoni hizo juhudi ambazo zinafanyika. Kwa hiyo, naomba suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, la pili ni Reli ya Kati. Mipango yote ya Serikali inazungumzia kupanua Reli ya Kati, Dar es Salaam – Isaka - Kigali – Msongati. Maana yake ni kwamba ukishafika Tabora inapanda mpaka Isaka kwa hiyo, kipande cha Tabora kwenda Kigoma hakina *plan* yoyote, hakijafanyiwa *feasibility study*, haijafanyiwa sijui *detail design* maana yake ni kwamba tutaendelea kuwa na reli ile ile iliyojengwa na Mjerumani kipande hicho maana hakizungumziwi kabisa. Vipande vyote vinavyozungumziwa na sasa hivi fedha zinazotafutwa ni Dar es Salaam, *ofcourse* mpaka Tabora – Isaka - Msongati sijui Kigali - Msongati. Sasa nilikuwa nazungumzia hiki kipande cha Kigoma - Tabora na baadaye Kaliuwa – Mpanda, kinaangukia wapi katika mpango mzima wa hii *Central Corridor* na huo upembuzi yakinifu unafanywa lini?

Mheshimiwa Spika, lakini sio hivyo tu, hiyo inayozungumzwa ya Kigali - Msongati ni njia ndefu sana, njia nyepesi ya kuiunganisha Burundi na Reli ya Kati ni Msongati – Uvinza. Ni kakipande kafupi sana, lakini hakijafanyiwa chochote na ndio ilikuwa njia nyepesi sana na ingesaidia sana kukuza mji wa Uvinza na Uvinza sasa hivi

umekuwa Wilaya, Serikali imetangaza kuwa Wilaya, lakini ni njia nyepesi sana ya kwenda Burundi. Lakini hakuna kitu chochote kimezungumzwa kuhusu kipande hiki cha Uvinza - Msongati.

Mheshimiwa Spika, katika hili la reli naomba Serikali iangalie, nilishawasiliana na Waziri, nilikutana na watu wa *German Railways*, *DOTCHBAN,* wakaonyesha *interest* ya kusaidiana na Serikali ya Tanzania kwa sababu wao bado wanaji- *identify* na hii Reli ya Kati. Kwa hiyo, nimeongea na Waziri na naamini Waziri yuko analifuatilia suala hili kwa ajili ya kuweza kuangalia jinsi gani ambavyo tunaweza tukasaidiana. Wao walichokitaka, wanahitaji tu *interest* tu ya Serikali, yaani Serikali iwaandikie kwamba tunahitaji kusaidiana nanyi katika reli hii, ndio wanachokihitaji kwa sababu wao ndio *actually* hata *feasibility study* ya kutokea Dar es Salaam- Isaka kipande kile cha Isaka - Kigali wamefanya wao. Kwa hiyo, wana *interest* kubwa sana na wangeweza kusaidia, naomba Waziri afuatilie.

Mheshimiwa Spika, la tatu, kuna ukarabati wa majini, hapa nazungumzia Shirika la Marine *Services Limited* ambalo linamiliki meli katika maziwa yetu mbalimbali na mimi hapa *interest* yangu ni Ziwa Tanganyika na hasa MV Liemba. Tayari kuna kampuni ambayo iliitengeneza Liemba miaka 100 iliyopita, imeonyesha *interest* ya kuigeuza Liemba kuwa '*a floating tourist hotel'* na watuletee Liemba ndogo ndogo mbili kwa ajili ya ku-*float* ndani ya Ziwa Tanganyika na wataalamu wetu wa Tanzania wameshaenda kwenye ule mji ambao ile kampuni ipo panaitwa Papenburg na tayari Serikali ya lile Jimbo la Ujerumani ambayo ndio inataka kusaidia kupitia Serikali yao Kuu, imeshatuma *delegation* kuja Tanzania na walikutana na Mkuu wa Wilaya lakini sioni juhudi zozote wala hamna *reference* katika hotuba ambayo ameizungumza hapa. Kwa hiyo, naomba hilo nalo Waziri aweze kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ni suala la barabara hasa wakala upi uweze kutumika. Tulitoa mapendekezo kipindi fulani hapa kwamba tuwe na *Rural Roads Agency*, nchi nyingi zina *Road Agency* kwa ajili ya Barabara Kuu na Barabara za Mikoa na wana *Rural Roads Agency* kwa ajili ya Barabara za Vijijini. Kwa sababu ukirundika barabara zote za Vijijini na za Mkoa na za Taifa kwenye Wakala mmoja inaweza ikawa ni taabu sana katika ufuatiliaji wa ujenzi wa barabara fulani fulani.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Kenya wana *Rural Roads Agency* ambayo ni kwa ajili ya Barabara za Vijijini tu na fedha zote ambazo zinatengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara, ujenzi ule unafanywa na ile *Rural Roads Agengy* ambayo inaweza kuwa na matawi katika kila Halmashauri na inaweza ika-*pull resources* kwa pamoja na kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, aliyekuwa Waziri wa Miundombinu wakati ule, Mheshimiwa Chenge, alisema kwamba hatuna fedha maana yake *TANROADS* yenyewe ilianzishwa kwa fedha za wafadhili. Kwa hiyo, sisi hatuna fedha mpaka tupate mfadhili wa kutusaidia kuanzisha *Rural Roads Agency*? Nafikiria sasa ni wakati muafaka Serikali ingeweza kuliangalia suala hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe, unasema mambo ya maana sana kasoro yake umeng'ang'ania kukaa kwenye Upinzani, ndio tabu sana, lakini mchagiaji wangu wa mwisho mchana huu ni Mheshiwa Rita Mlaki. *(Kicheko)*

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hoja ya Waziri wa Miundombinu. Ninaishukuru sana Serikali kwa mikakati mingi na barabara nyingi sana walizojenga kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Ninaomba niongelee moja kwa moja Mkoa wa Dar es Salaam ambapo nitapenda kuongelea pointi mbili tu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetujengea kupitia *TANROADS* barabara nzuri sana katika Mkoa wa Dar es Salaam, barabara za pembezoni zikiwemo barabara kule Kigamboni, Kibada, Twangoma, Kilwa Road, barabara ya Kinyerezi, Segerea na Sam Nujoma kule Kinondoni, tunashukuru. Naiomba Serikali kwa kupitia fedha za *TANROADS* itusaidie katika Manispaa zetu. Manispaa hazina uwezo wa kujenga barabara ambazo zimewekwa chini yake kwa kiwango cha lami. Kwanza, tunashukuru kwamba Serikali itajenga barabara ya Ali Hassan Mwinyi mpaka Tegeta ambayo itasaidia sana kupunguza msongamano wa magari lakini ninachopenda kukileta hapa leo, Manispaa zetu katika Kata mbalimbali kuna mali za thamani kubwa sana, tungeomba *TANROADS* watusaidie kwa sababu zile mali au niseme nyumba katika maeneo hayo zina thamani ambayo ingeweza sana kusaidi uchumi wananchi. Hapa naongelea eneo la Mikocheni, eneo la *Mbezi Beach*, eneo la Tegeta, eneo la Makongo na maeneo mengi ambayo mnayafahamu katika Wilaya ya kinondoni.

Mheshimiwa Spika, nisiwe sina shukurani, tumejengewa barabara ya Oasis kutokea pale Afrikana, tungeomba basi *TANROADS* ifanye kama ilivyofanya, itujengee tena zingine kuikuta ile ya Mbezi vizuri na kutujengea maeneo kadhaa kama barabara inayokwenda Makongo. Barabara ya Makongo ni moja tu tunaiyomba ijengwe, Manispaa tunaona uwezo wake ni mdogo, tunaomba *TANROADS* muichukue hii barabara. Vile vile kuna barabra ya kwenda Salasala inayotoka pale Afrikana, eneo la Salasala lina watu zaidi ya 25,000 na barabara inaharibika sana zaidi kutokana na miundombinu hafifu ikiwemo mifereji. Watu wanatumia baiskeli, wanatumia pikipiki, wanawake wajawazito, watoto wagonjwa, tunaomba *TANROADS*, kilichobaki Mheshimiwa Waziri mtutupie pale

barabara ile ya Salasala, wananchi wamenituma, wanaomba sana pamoja na shukurani zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuongelea pointi ya pili kuhusiana na msongamano wa magari Dar es Salaam. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Waheshimiwa wananchi wa Dar es Salaam au mnaokuja pale kutembelea, nadhani mmeona ni tatizo kubwa sana kwa Dar es Salaam. Inakuchukua hata masaa matatu kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Huduma nyingi za Jiji la Dar es Salaam ziko katikati ya Mji, Kariakoo ambapo mnapafahamu, kufika pale inachukua masaa, watu wanachelewa kazini, wanachelewa katika biashara zao. Tumeambiwa kutajengwa *fly-overs* karibu tano, kutakuwepo na haya mabasi ya kwenda kasi, lakini tunaomba watekeleze kwa haraka kwa sababu ninasema au naamini na nyie mnaona baada ya miaka miwili kutokana na ongezeko la watu Dar es Salaam pamoja magari mji ule hautapitika kabisa.

Mheshimiwa Spika, huu mpango wa magari yaendayo kasi tangu nimeufahamu, kwa kuwa nimekuwa Mbunge Dar es Salaam miaka kumi, tumeuongelea kwa miaka saba na sasa hivi hatua ndio zinakwenda kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Tungeomba iharakishwe na isiwe hii barabara moja tu kuanzia Ubungo kwenda Mjini, iwe maeneo kadhaa ili tuweze kutatua tatizo hilo. Inawezekana vilevile tukawa tumepeleka magari kupitia *fly-overs* tukayaweka pale mjini, yatashindwa tena kutembea pale mjini. Nilikuwa natoa wazo kwamba labda iwekwe utaratibu kwamba magari kadhaa yasifike katikati ya mji au tukubaliane kwamba huu usafiri ambao ni *public* ndio tu utumike katika kusaidia kule katikati ya mji. Ikiwezekana watumie wataalamu maana kuna nchi nyingi ambazo zimepata matatizo kama hayo ikiwemo Nigeria na nchi kadhaa za Afrika na wameweza kutatua matatizo, tungeomba pia, Serikali kupitia Wizara hii wajitahidi kuweza kusaidia katika hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, usafiri pia wa majini kupitia *Indian Ocean*, kuanzia kule Kunduchi au tuanzie kabisa kule Bunju kwenda feri, tunaweza kuweka *fast boats* pale na zikafanya kazi, labda ningetoa hilo kama wazo kuweza kusaidia. Vile vile barabara za katikati ya Mji ziweze vile vile kupanuliwa ili tuweze kuondoa hilo tatizo. *Traffic* walioko Dar es Salaam kwa kupitia Serikali wawakamate wale wote wanaovunja sheria kwa sababu nao pia wanaleta msongamano mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kikwetu ukiwa na shida kubwa sana unapiga yowe, 'yeuwiiiiiiii', unapata msaada. Kwa hili la msongamano Dar es Salaam, naomba nipige mayowe japo nimeshatoa hizo pointi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumaliza kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Kawe kwa ushirikiano mkubwa sana walionipa kwa miaka kumi. Tumeweza kushirikiana kuleta maendeleo katika sekta ya elimu, afya, miundombinu na

huduma za jamii. Maji ambayo yalikuwa tatizo sugu lakini kwa sasa angalau tunapata. Ningeomba wananchi angalau tushukuru kwa hilo na tusilalamike kwa maeneo kadhaa ambayo bado hayajapata maji. Serikali yetu imejitahidi sana, Dar es Salaam ya sasa ni tofauti na Dar es Salaam ambayo tulikuwa tunaijua.

Mheshimiwa Spika, naomba nitamke leo rasmi kwamba sitagombea tena Ubunge katika Jimbo la Kawe, miaka kumi ambayo nimekaa katika Jimbo hilo nimeridhika na ninawashukuru sana wananchi, nitawaombea Mungu wapate Mbunge mzuri ambaye wataweza kufanya kazi nao ili kumalizia kazi ambazo zimebaki na Mbunge wa Chama cha Mapinduzi. Niseme kuwa sio kwamba ninaondoka katika kusaidia au kuchangia maendeleo ya nchi, nitagombea kupitia Taasisi zisizo za Serikali *(NGOs).* Kwa hiyo, Mungu akipenda tutakuwa tena pamoja kushirikiana na wananchi wa Jimbo la Kawe kutetea maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru wewe binafsi kwa kuniona kwamba sijachangia kabisa katika bajeti hii na kunikubalia kunipa nafasi za mwanzo katika bajeti hii muhimu ya miundombinu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kazi kubwa, Wizara hii haikuwa rahisi na yote mmejitahidi mpaka tukaweza kupata wafadhili na kufanya yote ambayo mmefanya kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rita Mlaki.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa kusitisha shughuli za Bunge umekaribia sana. Nina matangazo, la kwanza Mheshimiwa Elietta N. Switi, Katibu wa Umoja wa Wabunge Wanawake, ameniomba niwatangazie Wabunge wote wanawake kuwa Mwenyekiti wa Fursa Sawa kwa Wote, Mama Mkapa amekualikeni kutembelea Banda la Saba Saba linaloitwa *Women's Entrepreneurs,* tarehe 2 Julai 2010, saa mbili hadi saa nne. Basi wale wote ambao wangependa kwenda Dar es Salaam tarehe 1Julai 2010 ili wawepo kule tarehe 2 Julai, 2010 wajiorodheshe kwa Mheshimiwa Switi ili Ofisi ya Katibu iweze kuandaa mipango inayohusika kwa usafiri na kadhalika. Kwa hiyo, wanawake wote bila kujali itikadi, ni kuangalia mambo ya ujasiliamali Dar es Salaam, Saba Saba tarehe 2 Julai, 2010. Kujiandikisha ni kati ya sasa na kesho kutwa tarehe 1 Julai 2010 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, aliyesalia ambaye hajachangia kabisa ni Mheshimiwa Eng. Laus O. Mhina na niliwataja wale wachangiaji sita wa mwanzo pengine wanaweza kupata, lakini sifa ya kupata nafasi itakuwa ni kuwemo humu ukumbini saa kumi na moja kamili. Nitawaangalia wale ambao wataendelea kusinzia huko majumbani basi ina maana

hawana ile ari ya kutaka kuongea leo. Kwa hiyo, nitawaacha hata kama wameweka majina yao hapa, nitawateuwa wale ambao wanaonesha ari ya kuwepo hapa ndani ya muda.

Basi shughuli zimefikia hapo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kabisa orodha yangu hii ya wachangiaji 34 haitawezekana kuwafikia hata nusu yao. Kwa hiyo, tutajaribu kwa haraka haraka hadi saa 12.10 hivi. Kwa hiyo, ni kama watano tu au labda na dakika 20. Baada ya hapo, itabidi nimwite mtoa hoja, Naibu Waziri. Kwa hiyo, kwa sasa namwita Mheshimiwa Mhandisi Lous Mhina, atafuatiwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na wengine nitawataja kulingana na walivyowahi. Mheshimiwa Mhina.

**MHE. LAUS O. MHINA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza nataka nitoe shukrani, nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa leo ambaye yeye pekee ndiyo mwingi wa rehema, kwa kuniwezesha kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ya bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, pongezi zangu pia nataka nizipeleke kwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu pamoja na Naibu wake wakiungana na Katibu Mkuu wa Wizara hii. Vile vile nisingependa kuwasahau watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya hotuba hii. Lakini vile vile napenda pia nipeleke pongezi zangu za pekee au shukrani zangu za pekee kwa uongozi wa *TANROAD*, Mkoa wa Tanga hususan kwa *Engineer* Ndumbaro ambaye kwa juhudi zake kwa kweli matunda tunayaona jinsi gani barabara za Mkoa wa Tanga ambazo ziko chini ya *TANROAD* zilivyo leo hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nimeuoanisha katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza, ni barabara na ya pili ni reli. Nikianzia upande wa barabara, tuwe wa kweli na tuwe watu ambao tunajua shukrani ni nini. Mwenye macho haambiwi tazama. Leo hii ukilinganisha mtandao wetu wa barabara katika nchi yetu hii, utaona tofauti kabisa na miaka iliyopita. Mara nyingi tupende kulinganisha tunakotoka kama wenzangu walivyokwishakusema.

Mheshimiwa Spika, leo hii unaweza ukatoka Mwanza na leo hii hii ukaingia Dar es Salaam. Haya si mafanikio? Ukija upande wa Mikoa 20, Kusini ni vivyo hivyo, unatoka Lindi unalala Tanga leo hii hii. Haya si mafanikio? Tuna mabasi tunayaona ya wazi wazi yanalala Mbeya, ya Hood jioni yako Arusha. Haya si mafanikio? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenye kubeza, mwenye kusema, aah tuwaache waseme tu lakini ukweli unaonekana. Juhudi hizi siyo kwamba zimefanyika katika Barabara Kuu tu, mimi naona hata kwangu vijijini, Wilaya ya Korogwe Vijijini barabara zimeboreka sana hususan ambazo ziko chini ya *TANROAD*. Utakuta barabara katika Kata za Bungu, Dindira, Vugiri, Lutindi, Kerenge, Magoma, Mashewa, Kizara, Mnyuzi kwa Gunda, leo hii zinapitika nyakati zote za mwaka, iwe ni masika, iwe ni jua, barabara hizi zinapitika. Kitu ambacho kwa kweli kwa siku za nyuma ilikuwa kama ni ndoto ya mchana, haya ni mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenye kuibeza Serikali hii inayoongozwa na Chama cha CCM wana lao jambo. Lakini sidhani kama kweli wanabeza kutoka mioyoni mwao. Leo hii katika Jimbo la Korogwe Vijijini, Vijiji karibu takriban vyote, tuna usafiri wa mabasi, kitu ambacho awali sisi tulikuwa tunategemea sana usafiri wa malori na ma-*Land Rover* mabovu mabovu yale ya 109. Leo hii tunapanda mabasi tena mengine *luxury bus couches*. Haya ni mafanikio ndugu zangu, wale wenye kupenda kubeza wayaone, hawataki, waje Korogwe Vijijini waone barabara zilivyoboreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwe wa kweli, Serikali ya CCM ya Awamu ya Nne imefanya kazi na inastahili pongezi. Pongezi hizi pia ziende hata kwa Wabunge ambao wapo madarakani kwa sababu ndiyo waliowezesha haya na vile vile pia tusiwaruke Madiwani, wamesaidia mchango mkubwa sana katika uboreshaji huu na pia hususan wananchi wenyewe kule Majimboni wamefanya kazi kubwa kwani kama si usimamizi wao, aah, si ajabu makosa mengi yangeshindwa kurekebishwa. Kwa hiyo, tuna haki ya kuipongeza Serikali, tuna haki ya kujipongeza Wabunge tuliyopo madarakani, tuna haki ya kuwapongeza Madiwani na tuna haki ya kuwapongeza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeongelea labda mazuri tu lakini pia penye mazuri pana upungufu wake mdogo mdogo. Ningependa kudokeza tu machache ambayo labda ni vema yakafanyiwa marekebisho. Barabara zetu nyingi nimesema kwamba zimejengeka na zinapitika nyakati zote lakini kasoro ambayo nimeiona mimi mwenyewe binafsi kama Mhandisi hususan zile za Vijijini hazina mifereji ya maji ya mvua. Barabara bila ya mfereji wa maji ya mvua basi hata kudumu kwake hakutakuwa kwa siku nyingi. Barabara haina maana ya *carriage way* tu barabara pia inaunganisha na mifereji. Kwa hiyo, ninaomba juhudi kwenye upande wa mifereji ziongezwe ili matengenezo yetu haya ambayo tunayasifu leo yaweze kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, labda kwa uzoefu wangu wa miaka ya nyuma sana nilipokuwa mtoto, nakumbuka tulikuwa na vitu vinaitwa Kambi za Matengenezo ya Barabara, zilikuwa zinaitwa *PWD*. Kule kwetu mpaka leo yapo magofu hayo, ingekuwa vema Wizara ikaliangalia suala hili. Badala ya barabara zile mpaka mwananchi aone, apige simu labda *TANROAD*, Tanga ndiyo msaada uje. Vinginevyo labda kuwe na Wakandarasi waliowekwa kwa vipande vipande vya barabara wa kuangalia matengenezo haya madogo madogo ambayo itakuwa ni kazi ya kudumu kwa Wakandarasi hawa labda kwa mikataba maalum na kwa muda maalum.

Mheshimiwa Spika, upande wa barabara ningependa kidogo nitoe kasoro ambayo nimeona ya barabara hii ya Segera - Mkomazi. Barabara ile imeharibika sana, najua kuna matengenezo yanakuja lakini hebu ifanywe juu chini hali iliyopo hivi sasa kwa kweli ni mbaya sana. Wengi wa Wabunge hapa tunapita barabara ile kutoka Segera kuelekea Moshi, kuelekea Arusha, hali yake ni mbaya sana, mashimo yamezidi. Ukiangalia kilichoharibu barabara ile ni mifereji. Ukipita sehemu ya Msambiyazi kuna sehemu inaitwa Mugobe. Kila mara wanapotengeneza, wanatengeneza karibuni kila mwezi lakini hawashughulikii chanzo cha uharibifu huo, ukiangalia sana ni maji ambayo hayana njia ya kupita. Kwa hiyo hili litazamwe.

Mheshimiwa Spika, ningependa niongelee kwa juu juu tu suala la reli ya Tanga - Arusha. Naomba iangaliwe kwa jicho la huruma. Naona muda umekwisha, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru sana kwa kupata fursa hii ili niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tumeweza kufika siku ya leo hii na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii ya Miundombinu, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii, nipeleke pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi hiki cha miaka mitano. Lakini hususani naomba nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuweza kutangaza Jimbo la Kalambo kuwa sasa ni Wilaya. Pia nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kuhakikisha kwamba Jimbo la Kalambo, barabara ya kutoka Sumbawanga - Matai kwenda Kasanga na ile ya kutoka Matai – Kasesha, sasa imewekewa jiwe la msingi na yeye mwenyewe Rais na itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo barabara pia ya kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda ambayo nayo pia imeshaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Naomba apokee shukrani zetu kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa na wa Jimbo la Kalambo. Barabara hizi zinazojengwa katika Mkoa wa Rukwa na barabara zinazojengwa katika Mkoa wa Kigoma, nina uhakika sasa zinaufungua upande wa Magharibi mwa Tanzania ili tuweze kutimiza ndoto yetu ya uchumi wa kijiografia ili tuweze kusafirisha mizigo mingi iliyoko nchi ya Congo, Burundi na Zambia kuifikisha katika bandari ya Dar es Salaam ili kuweza kufikia masoko ya Ulaya na Mashariki ya Mbali.

Mheshimiwa Spika, barabara na reli ni sawasawa na mishipa ya damu katika mwili wa binadamu na uchumi wa Tanzania unategemea sana usafirishaji kupitia barabara na reli. Hivyo, tunashukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Nne kwa kuliangalia hili na kuanza kulitekeleza kwa vitendo. Wapo watu wanaobeza, wanasema hakuna kazi iliyofanyika lakini nasema kazi iliyofanyika ni kubwa sana na hasa kwa Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma ambao sisi hatukujua ni lini na wakati gani barabara za lami

zitaanza kujengwa ili kutuunganisha walau na Mikoa ya jirani ya Tabora na Mkoa wa Mbeya, mimi naomba wapokee shukrani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, haikuwa kazi rahisi. Lakini sehemu kubwa kama ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, inajionyesha waziwazi jinsi ambavyo barabara nyingi zimeguswa. Huu ni ushahidi wa kutosha kwamba nchi nzima kuna kazi zinazofanyika za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami na zile ambazo ni barabara imara zitakazoweza kutusaidia kuimarisha uchumi wetu. Tunachoomba ni ulinzi wa barabara hizi zinazojengwa ili zisiweze kuharibiwa na watu wenye tamaa ya kujaza mizigo sana na kuweza kuharibu barabara katika muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, naelewa ufinyu wa bajeti haukuweza kuwafikia wananchi wote na Majimbo yote katika nchi hii ya Tanzania, lakini kazi iliyofanyika ni nzuri kwa ujumla. Mimi naelewa kabisa watendaji wote wa Wizara na *TANROAD* wamejitahidi kadri ya uwezo wao kama Mwakilishi wa Kamati ya Miundombinu alivyoeleza, hakuna malaika katika nchi hii, sisi sote ni binadamu lakini tuwapime watu kutokana na kazi wanazozifanya. Mtendaji Mkuu wa *TANROAD* anatupiwa lawama nyingi sana lakini mimi nasema tuangalie kazi alizofanya kwa kipindi hiki ambacho ameingia katika madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi alizozifanya ziwe ni kipimo cha kusema kwamba amejitahidi kadri ya uwezo wake. Matatizo hayawezi kukosa na wale ambao labda pengine wangependa kuona kazi zile waangalie katika Jedwali lililoambatishwa katika kitabu hiki. Hata hivyo, panapokuwa na migogoro sisi kama Kamati ya Miundombinu, tulishauri viongozi wakutane ili waweze kuondoa tofauti zao. Lakini kama watu hawataki kuondoa tofauti zao na kuanza kulumbana kwenye magazeti na vyombo vingine, tunasema hilo si jambo la kujenga badala yake ni jambo la kubomoa.

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika barabara za Jimbo la Kalambo. Jimbo la Kalambo limeunganishwa na barabara nyingi tu mfano barabara ya Kaengesa - Mwimbi hadi Mbozi Custom, barabara ya Mwimbi - Matai, barabara ya Kaepula-Ilonga lakini barabara hii kwa upande wa Mbozi imeunganishwa na barabara ya Wilaya ambayo kwa kweli kiwango chake ni kidogo. Tunaomba Mkoa wa Mbeya uangalie jinsi ya kuboresha barabara hii ya Kakozi - Namchinka ili tuunganishe na Ilonga, barabara hii iwe ni ya *TANROAD* ili iweze kupitika na kuweza kufika Kasanga bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, barabara za Wilaya. Barabara za Wilaya zina matatizo makubwa kwa sababu ya utaalam unaotumika. Tunaomba kama ikiwezekana kutokana na mapendekezo yetu *TANROAD* iweze kuwasaidia hata Wilaya iweze kupata utaalam utakaosaidia kujenga barabara zilizo nzuri na imara.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha uwanja huu ni kama umetelekezwa, hakuna chochote kinachofanyika pale. Viongozi wa Kitaifa wanapokuja, wanalazimika kushukia Mpanda au kushukia Mbeya. Tunaomba sana kwa jicho la huruma waangalie jinsi ya kuweza kuboresha uwanja huu ili uweze kutusaidia na viongozi pia waweze kutumia uwanja huu badala ya kusafiri masafa marefu katika barabara. Tunaweza siku moja tukashuhudia balaa zinatokea kwa viongozi wetu kitu ambacho ni kilio cha muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana wewe mwenyewe. Nakutakia kheri katika uchaguzi ujao uweze kufanikiwa na kurudi hapa ili uweze kuendesha gurudumu hili kwa mafanikio zaidi. Lakini na wananchi wa Kalambo nawashukuru kwa sababu tumeshirikiana nao kwa kipindi hiki cha miaka mitano na wameona mafanikio makubwa, tumepata Wilaya, tumepata barabara, tumepata Kata mpya, Tarafa, Vijiji na maendeleo mengine wao wapime maendeleo hayo na kama ni ufanisi na mafanikio kwa ajili ya kusonga mbele badala ya kubeza na kuangalia mambo madogo madogo ambayo hayaleti tija.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwananzila na salamu zako hizo za kunitakia kheri nina hakika zimefika kule Mjini Urambo na Kata zote 12 za huko, basi ndiyo mambo yenyewe.

Sasa nitamwita Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Abdallah na kuna Mbunge ambaye alijitahidi sana kuwahi, nimepewa taarifa amefika saa kumi na moja kasoro robo, Mheshimiwa Zabein Mhita atafuatia. Mheshimiwa Mgana Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii ya Miundombinu. Niishukuru sana Serikali, kwa sababu kwa kweli kufutana na fedha inazopata inajitahidi sana kuboresha miundombinu ya nchi yetu ili iweze kupitika wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Kikwete, alitembelea Jimboni kwangu tarehe 4/5/2008, alipofika aliniuliza mafanikio ambayo Serikali imeyafanya na matatizo tuliyonayo. Nilimueleza mafanikio mengi ya maji, elimu, afya na vilevile nilimueleza juu ya matatizo, nilimueleza matatizo matatu. La kwanza, ni kupata Wilaya, la pili, barabara zetu sio nzuri sana na la tatu ni Daraja la Mto Sibiti. Kwa kweli aliposimama kuwahutubia wananchi wa Iramba Mashariki, sasa hivi Wilaya ya Mkalama, alisema Serikali itatekeleza haya yote kwa awamu. Mimi nishukuru na kuipongeza Serikali, kwa sababu sasa hivi tumeshapata Wilaya na sasa hivi Daraja la Mto Sibiti linajengwa, karibu mambo yote aliyoahidi Mheshimiwa Rais na yaliyokuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Iramba Mashariki, yanatekelezwa na mengine yameshatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na mambo ya barabara. Niishukuru sana Serikali kwa sababu iliipandisha hadhi barabara ya kutoka Kiomboi – Kisiriri – Kidaru – Mkalama – Matongo – Mkinto – Kidarafa, sasa hivi imekuwa ni barabara ya Mkoa na inatengenezwa. Kwa kweli, niipongeze sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Serikali ilitenga shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya Daraja la Mto Sibiti na mwaka huu vilevile imetenga fedha. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu katika madaraja ambayo alisema yataanza kujengwa mapema ni pamoja na Daraja la Mto Sibiti. Mheshimiwa Waziri, kule kwetu Mto Sibiti, unaanza kufurika mapema, mwezi wa 11 mwishoni mafuriko yanaanza, ningeomba wale waliopata tenda ya kujenga waanze mapema ili hata mvua zikianza wawe wamefikia kwenye hatua nzuri.

Mheshimiwa Spika, vilevile niipongeze sana Serikali, katika kuunganisha Mikoa na Mikoa, sisi wa Iramba Mashariki tumekuwa kiungo kati ya Mikoa ya Ziwa na nchi jirani na Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na nchi jirani upande wa pili. Serikali ilitamka hapahapa Bungeni kwamba itajenga barabara kutoka Shinyanga – Mwanuzi – Daraja la Sibiti – Mkalama – Haidom – Arusha, ambapo ni barabara ya kimataifa. Kwa hilo, ninaipongeza sana Serikali kwa kazi hiyo na kwa uamuzi mzuri ilioufanya kwa faida ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu, kwa kweli tusiwe watu wa kuilaumu Serikali, kwa hii miaka michache iliyopita, Serikali imejitahidi sana kujenga barabara nchi nzima. Kama walivyosema wenzangu, sasa hivi unaweza kwenda Kusini, Kaskazini, Magharibi, bila ya matatizo yoyote. Kwa hiyo, ni lazima tuipongeze sana Serikali kwa fedha ndogo inayoipata, tena hizi barabara nyingi zinajengwa kwa fedha za ndani, Jimboni kwangu karibia barabara nyingi ni barabara za Mkoa, Iguguno – Nduguti – Gumanga – Mto Sibiti, Msingi – Gumanga, Ilongelo – Nkungi – Kidarafa, kwa kweli hzi barabara karibu kila mwaka zinapata fedha na zinajengwa vizuri. Tatizo lililopo, nikitaja barabara moja moja, barabara ya kutoka Iguguno – Kinyangiri, kuna eneo linaitwa Muembeni, pale kila mwaka hiyo barabara inakatika mvua zikinyesha tu. Kwa hiyo mimi ningeiomba Serikali, ningemwomba Waziri wa Miundombinu, kwanza atembelee eneo hilo halafu watenge fedha wajenge daraja na kuinua tuta pale.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Nkungi – Kidarafa, barabara hii inapata pesa lakini kila mwaka wanaweka Mkandarasi asiye na sifa. Kwa sababu barabara nyingine zote zinatengenezwa zinadumu, lakini ile ya Nkungi – Kidarafa, kila mwaka ina matatizo na Nkungi – Kidarafa, kuna mto Ndurumo, lile daraja la pale limepitwa na wakati, liko chini, mvua zikinyesha maji yanapita juu yanaleta matatizo. Kwa hiyo, ninaomba hilo daraja liinuliwe. Vilevile daraja la Kidarafa kwa barabara ya Iguguno – Nduguti – Gumanga, kuna mito miwili, kuna mto Kamulungu, kuna *Drift* na mto Gumanga kuna *drift,* yale ma-*drift* yamepitwa na wakati, ile mito ina maji mengi sana. Kwa hiyo, ninashauri Wizara ijenge madaraja ya kudumu eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirudi upande wa Halmashauri, kwa kweli mimi ninaipongeza sana Serikali kwa sababu inatoa pesa ya kutosha kwa ajili ya barabara zetu.

Kwa mfano mwaka huu imetoa shilingi milioni 500 kwa barabara ya Iguguno – Kitumbili – Lyelembo – Iransoni – Msingi, barabara ambayo ilishashindika kwa miaka yote. Mwaka huu nina imani kabisa itatengenezwa kwa kiwango kizuri. Barabara ya Msiyu – Kidarafa imepewa shilingi milioni 60, barabara ya Ikolo – Indasiko imepewa shilingi milioni 70, barabara ya Mirade – Kaselya imepewa shilingi milioni 45, kwa hiyo kwa kweli mahali ambapo Serikali inafanya vizuri ni lazima tuipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri kwa mtindo ambao Serikali inaufanya wa kupandisha barabara, kwa mfano hii barabara yetu iliyopandishwa kutoka kwenye hadhi ya Halmashauri kwenda ya Mkoa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi inatengenezwa vizuri na itadumu na inapita kwenye mbuga ambazo kila mwaka huwa...

**SPIKA:** Kengele ya pili Mheshimiwa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, eeh! Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kabisa niiunge mkono hoja hii. Ninapenda kuwapongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Wataalamu wote, Katibu Mkuu na Mainjinia wote, *TANROADS,* kwa kazi nzuri ambayo imeonekana katika nchi hii katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, pili ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa maneno aliyoyasema. Kwa kweli, Zitto Kabwe, ameelezea uzuri wa utekelezaji wa shughuli ya Serikali ya CCM katika Jimbo lake na Mkoa wa Kigoma. Kwa kweli, yaani kutoka mdomoni mwake ninasema hii ni dalili kwamba kumbe kazi imefanyika. Lakini halafu huko kwingine anasema, ooh, lakini basi wao ndio waendelee. Sasa watawapeni kazi kwa kazi ipi ambayo mmeifanya? Maana kazi imeonekana na wewe umeisema, mimi ninakushukuru sana na ninakupongeza kwa hilo na ninawaomba watu wa kule Kigoma waelewe kwamba kazi ile imefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda sana kuipongeza Wizara kwa suala la Daraja la Umoja. Hili ni jambo ambalo limezungumzwa tangu wakati wa enzi ya Baba wa Taifa, Awamu ya Pili walijaribu, Awamu ya Tatu wameanzisha, Awamu ya Nne wamemalizia. Tunapenda kushukuru sana kwa kazi hii iliyofanywa. Lakini urefu wa mto Ruvuma, kutoka Ruvuma mpaka unapoingia Baharini Mtwara, ni urefu mkubwa sana na tunahitaji vivuko vingi zaidi ya hapo, ni zaidi ya kilometa 800, nafikiri 1000. Kule Songea, kuna daraja la Beile linasaidia na kule Mtwara kuna kivuko cha Kilambo, tunaomba vivuko vingi viwepo maana sio rahisi mtu asafiri masafa yote ili afuate hili Daraja la Umoja.

Tunashukuru kwamba hata barabara ya kutoka Masasi mpaka *Mbamba Bay* iko katika vitabu hivi na hili ninataka nilipongeze sana. Tumezungumzia jambo hili kwa miaka na miaka, kwa mara ya kwanza liko vizuri katika kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa ule wa 144 na hii inaenda sambamba na ujenzi wa *Mtwara Development Corridor,* tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema kwamba pamoja na juhudi hizi zote, sikuona mahali ambapo daraja la Nangoo limewekewa fedha. Daraja la Nangoo ni *baily bridge,* sidhani kama linachukua zaidi ya tani 10 sasa hivi. Sasa tumejenga daraja la Mtamba Swala, tunatengeneza barabara za lami, sasa hivi kutoka Masasi mpaka *Mbamba Bay,* bila kutengeneza daraja la Nangoo, barabara hii haina faida yoyote, kwa sababu tunajenga barabara hizi kwa ajili ya kusafirisha watu na kusafirisha bidhaa, sikuliona mahali popote. Ningependa liwekwe katika taratibu zinazojulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona katika ukurasa wa 160 wa hotuba hii ya Waziri, katika miradi itakayoangukia chini ya Mkoa wa Mtwara, kuna kitu kinaitwa *detailed design* ya barabara kutoka Mtamba Swala - Mangaka. Pamoja na pongezi na kazi nzuri mlizozifanya, lakini huu ni upungufu mkubwa sana. Kujenga daraja kwa muda wa miaka yote hii kwa fedha nyingi sana lakini ukishavuka kwenye daraja unaanza kupepesuka na vumbi mpaka Mangaka, kwa kweli hili ni jambo la ajabu sana. Halafu ufike Mangaka, ukutane na barabara ya lami, mtu unatoka Msumbiji, unavuka daraja zuri, unakwenda na barabara ya vumbi, halafu ndio unakutana na lami ya Mangaka kwenda Mtwara. Nafikiri utaratibu haukuwa mzuri sana, tulipaswa kuliangalia hili mapema. Sasa mwaka huu ni *detailed design,* sijui ujenzi ni lini? Kwa kweli hii itasababisha kwamba pamoja na daraja la Nangoo, barabara hii isitumike vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana mipango ya Serikali ya kujenga barabara kutoka Mangaka – Tunduru – Namtumbo – Songea – *Mbamba Bay,* kwa kweli ni kazi nzuri sana. Lakini ninachoomba ni katika ukurasa wa 75 wa hotuba ya Waziri, ameelezea habari za meli katika Ziwa Nyasa, *MV Songea* na *MV Iringa.* Hizi barabara, kama hakuna kiungo cha meli hizi, kwa kweli zinakwenda mpaka inafika mahali wanasema kwamba ni *blind* au *dead end,* hakuna mahali pa kuendea mbele. Hizi barabara zikitoka Mtwara na mizigo, zikifika *Mbamba Bay,* inakwenda wapi? Nia ya *Mtwara Development Corridor* pia ni kuusaidia ule mwambao watu waende mpaka sehemu za Malawi, sasa hivi hakuna usafiri wa namna hiyo. Hatujui sababu, lakini Waziri amesema zimeharibika, sasa jamani tangu mwaka wa 2008 sijui, sasa kuharibika huku miaka hii yote, wale watu wa mwambao huu wa Ziwa Nyasa, wanayo matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba hili suala la meli katika Ziwa Nyasa, *MV Songea, MV Iringa,* litazamwe vizuri na ziweze kufanya kazi zake sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kuelezea kwamba hotuba inazungumza juu ya viwanja vya ndege, lakini sikusikia upanuzi wala ukarabati wala matengenezo ya kiwanja cha ndege cha Mtwara. Mtwara, iko kule pembezoni tunapakana na Msumbiji. Kama nilivyosema, lile daraja linafungua ukurasa wa kwenda Msumbiji, lakini suala la usafiri wa ndege pia linafungua ukurasa vizuri na maendeleo mengi yanafanywa kwa

kufanya biashara ya nje, sasa sisi kule Kusini, nje yetu ni Msumbiji, kwa hiyo, tungependa vivuko vingi sana ili watu wawe wanakwenda Msumbiji na wa Msumbiji wanakuja, tufanye biashara kama vile wenzetu wa Kaskazini wanavyofanya na Kenya ama wenzetu wengine wanavyofanya na Uganda na wengine wanavyofanya na Rwanda na Burundi. Kwa hiyo, tunaomba jambo hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini nimeona vilevile katika hotuba ya Waziri na yeye nimshukuru, ameweka barabara ambazo mwenyewe amesema *border roads,* hizi ni barabara za mpakani katika Mkoa wa Mtwara. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa hili kwa sababu litafungua maendeleo na litafungua mawasiliano na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumpongeza sana Waziri, katika hotuba yake hii, ukurasa wa 73, ameeleza juu ya kuhamasisha wanawake kushiriki katika ujenzi wa miundombinu, kwa hili ninampa pongezi sana. Katika mwaka wa 2010/2011, amesema kwamba watawasaidia wanawake kuanzisha makampuni 15 ya ujenzi, mimi ninawapeni pongezi sana. Ningependa na Wizara nyingine zituambie zinafanya nini katika kusukuma maendeleo ya wanawake? Maana na mimi hapo ndio Jimbo langu, lakini hili ninakupongeza sana na ninakuomba wapewe kazi. Mnapotangaza kazi, mhakikishe hawa akina mama wamesaidiwa, ni watu waaminifu hawa. Kama walivyo wapiga kura waaminifu, mkiwapa kazi akina mama hawa ni waaminifu. Sasa sisi kisiasa tunasema, akina mama nendeni kwenye Majimbo, nendeni kwenye Kata mkagombee, hili ni jambo jema sana. Akina mama jitokezeni kuanzisha hizi kampuni ambazo Serikali iko tayari kutusaidia, tuingie katika kazi za ujenzi, za ukandarasi mbalimbali wa kinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Joyce Masunga; nilikuwa nimekaa hapa asubuhi, akitangaza nia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nikasema hili ni jambo la ufahari, jambo la ushujaa alilolifanya. Tarehe 16/7/2010, Bunge litakapovunjwa, Majimbo yale yako wazi, kwa hiyo kama akina mama waende wakagombee, wengine mwende kwenye ukandarasi. Ninaziomba Wizara nyingine mtuambie mna miradi gani ya kuhakikisha kwamba wanawake nao wanajitokeza kufanya kazi mbalimbali ambazo tunahitajika tuzifanye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kumbe ni ya pili Mheshimiwa Anna.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Vilevile ni kweli nilifika hapa saa 10.45 na nimeona faida ya kuwahi. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara, kwa bajeti nzuri ambayo wameiandaa na ambayo kwa kweli imeandaliwa kisayansi. Lakini vilevile nimpongeze kwa dhati Dokta Kijazi, ambaye ameteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa. Nina imani kabisa kutokana jinsi ninavyomfahamu mwanamama huyu, hatimaye atateuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu, hongera sana Dokta Kijazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuishukuru Serikali kwa dhati kabisa, kwa hatua ya kutengeneza barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati, kwa kuichonga kwa greda na kuishindilia. Waswahili wanasema ‘asiyeshukuru kidogo, hata kikubwa hatashukuru’, kwa hivyo tunashukuru. Barabara hii sasa inapitika vizuri na muda wa usafiri umepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zamani kutoka hapa mpaka Kondoa kilomita 160 tulikuwa tunachukua masaa zaidi ya manne, sasa hivi angalau masaa matatu, tunashukuru. Ukiachilia mbali hii kero ya vumbi, maana baada ya kupitisha greda, vumbi ni jingi, lakini hiyo tunaivumilia tukiamini pengine wataalam wataweza kujua jinsi gani wataweza kupunguza vumbi hilo lakini kwa kweli barabara inapitika tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya kutoa pongezi zote hizo kwamba barabara imepitishwa greda lakini kilio cha wananchi wa Kondoa kiko pale pale kwamba wanaomba barabara hii sasa ijengwe kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika kwa wakati wote, mwaka mzima na kurahisisha usafiri kati ya Dodoma, Babati, Arusha na maeneo mengine. Kilio hiki bado kiko, wananchi wa Kondoa nadhani mnasikia huko bado tunataka barabara hii itengenezwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2009/2010, ilipangwa shilingi bilioni 5.6 katika kutengeneza barabara hii. Lakini baada ya mjadala mrefu na mkubwa katika jengo hili, Serikali yetu sikivu iliongeza pesa kutoka shilingi bilioni 5.6 mpaka shilingi bilioni 45. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kuongeza hicho kiwango mpaka sasa hakuna chochote kilichofanyika. Taarifa tuliyonayo ni kwamba Mkandarasi amepatikana na amesaini mkataba. Sasa mgonjwa ukimwambia tumempata Daktari wakati anaumwa kwa kweli nadhani hutakuwa umemsaidia, mgonjwa yule anataka umwambie Daktari amepatikana, achukuliwe vipimo, ugonjwa ufahamike aanze kutumia dozi kama ni sindano ama ni vidoge. Sasa anaanza kujisikilizia kwamba baada ya kuchoma hii sindano pengine alikuwa hali, anaanza kula ndiyo tunachokitaka, kwamba Mkandarasi amepatikana, mkataba umesainiwa basi kazi pia ianze. Mwenye kiu cha maji ukimwambia tu maji yameletwa haitoshi mpe *glass* ya maji anywe. Naomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami, ndicho wananchi wa Kondoa wanachokitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu, Serikali imepanga shilingi bilioni 9.5 tu, kwa kweli bado pesa hii ndogo wala sijui itaweza kufanya kazi gani. Barabara hii ina umuhimu mkubwa sana kwani licha ya kuunganisha Mkoa wetu wa Dodoma na Mikoa mingine pia inaunganisha nchi yetu na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena, barabara hii ndiyo hiyo inayotoka Cairo - Misri hadi Capetown Africa ya Kusini, inafahamika kwa jina la *The Great North Road.* Kwa hiyo, ni dhahiri na wala hakuna ubishi wowote kwamba barabara hii ina umuhimu wa kipekee kabisa. Lakini tangu mwaka wa fedha 2008/2009 ilitengwa shilingi bilioni 12 hakuna kilichofanyika, mwaka 2009/2010 ilipangwa shilingi bilioni 5.6 ikaongezwa kuwa shilingi bilioni 45 hamna kilichofanyika zaidi tu ya kuambiwa Mkandarasi amepatikana na mkataba umesainiwa. Sasa mimi nauliza, je, Serikali ina dhamira thabiti ya kujenga baraba hii kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuzungumzia daraja lililoko Kolo, daraja hili lilivunjika tangu mwaka 1997, Dkt. Kijazi, kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa, wakati wa El-ninyo mtoto wangu kuna wakati aliumwa tukampeleka hospitali, akaulizwa umegua tangu lini? Akasema tangu wakati wa El-ninyo akiwa na maana toka wakati mvua ilipokuwa inapiga. Sasa daraja hili limevunjika tangu wakati wa El-ninyo mwaka 1997 mpaka leo daraja hili halijatengenezwa. Lakini tunajua Mkandarasi amepatikana, litengenezwe daraja ili liweze kupitika wakati wote. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha kusikitisha ni kwamba mwaka 2005 Mheshimiwa Rais mpendwa wetu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni alisema kabisa kwamba barabara hii ya kutoka Dodoma mpaka Babati itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini leo ni mwaka 2010 hata kilomita moja haijajengwa, hata jiwe la msingi halijawekwa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kondoa, Majimbo yote mawili, Kondoa Kaskazini na Kondoa Kusini kwa Mheshimiwa Pascal Degera, wanauliza Mheshimiwa Waziri barabara hii itaanza kujengwa lini. Swali ni moja tu barabara hii itaanza kujengwa lini, wanataka wajue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini na Kondoa Kusini wametusikia, kwa sababu kaka yangu Mheshimiwa Degera hakupata nafasi ya kuchangia.

**MBUNGE FULANI:** Na watawachagua.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Kilio chao jamani ndiyo hiki, barabara hii itaanza kujengwa lini na mimi nawauliza barabara hii itaanza kujengwa lini? Swali ni moja tu. Mheshimiwa Waziri barabara hii itaanza kujengwa lini? Jibu hilo ndiyo nalihitaji mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri Dkt. Shukuru Kawambwa na mdogo wangu umenisikia, Waswahili wanasema kizuri cha ndugu pia huliwa na mtu zake. *(Kicheko)*

**WABUNGE:** Alaaa Kumbe, tumekusikia.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anapofanya majumuisho, ninaamini kwamba atatoa majibu kwa hoja nilizozitoa. Kwa matumaini na imani kubwa niliyonayo, naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Bahati yako Mheshimiwa wewe una ndugu huko Miundombinu sisi tusio na ndugu Miundombinu sijui tutafanyaje, sijui. *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchango wangu katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ya Miundombinu, pamoja na taasisi na asasi zilizoko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ambayo yanaonekana matunda na mafanikio yake.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano ambao ameuonyesha kwenye Kamati, bajeti hii ilikuwa ni ngumu na nzito kama ilivyoelezwa kwenye taarifa yetu, lakini baada ya kushauriana naye mara kadhaa amekuwa msikivu na kujitahidi kurekebisha baadhi ya yale ambayo tumesema.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa niaba ya Kamati yangu ya Miundombinu, nalazimika kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa *intervation* yake katika bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu. Mafanikio haya ambayo yamefikia hapa tulipofika, kwa kweli ni kwa sababu ya kazi kubwa na ushirikiano mkubwa ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu ametupatia. Namshukuru sana, ahsante kwa kutujali na kutusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, niruhusu nimshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kutuletea maendeleo nchini. Lakini kwa sasa hivi, niruhusu nimshukuru kwanza kwa kutupatia Wilaya nyingine mpya. Sisi watu wa Singida, tumepata Wilaya ya Ikungi na tumepata Wilaya ya Mkalama, tumepata Halmashauri ya Ikungi, tumepata Halmashauri ya Mkalama. Muda mrefu tumelilia, tumeomba lakini sasa Mheshimiwa Rais wetu ametuondoa kwenye adha hiyo. Kwa dhati kabisa na kwa unyenyekuvu mkubwa, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia Wilaya ya Ikungi. Lakini mimi binafsi nimshukuru sana kwa kuligawa Jimbo langu na kuwa na Majimbo mawili sasa badala ya Jimbo la Singida Kusini, sasa lina Majimbo mawili Singida Magharibi na Singida Mashariki yote nina hakika kuna mkono wake na Mheshimiwa Waziri Mkuu ana mkono pamoja na Tume yetu ya Uchaguzi. Naomba nitoe shukrani sana juu ya hilo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema zaidi kuhusu hoja hii, nitoe masikitiko mawili tu au niseme maneno mawili. Katika gazeti la leo la Mtazania, ukurasa wa tano liko tatizo ambalo nilieleza wakati nachangia hotuba ya Waziri Mkuu, ni tatizo la muda mrefu na nimezungumza sana. Sasa hapa imeandikwa jinsi wananchi wanavyotaka kuuwawa, mashamba yao yameharibiwa, mazao yao yameharibiwa na tembo na wananchi wanalalamika kwamba hilo ni suala la muda lakini halishughulikiwi. Serikali ya CCM nasema ni sikivu, kuna tatizo gani kusikia juu ya kilio hiki cha tembo ambacho kinaathiri sana kilimo pamoja na maisha ya wananchi wetu? Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo ingawa kuna mtu anamsemesha nadhani analisikia jambo hili kwamba chonde chonde tembo wanauwa watu, wanaharibu mazao kule katika Jimbo la Singida Kusini kwenye Tarafa ya Ihanja na leo humu imeandikwa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nimuombe sana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu na hasa Mtendaji Mkuu wa *TANROAD*, nimepigiwa simu zaidi ya mara tatu kutoka jana na juzi kwamba kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa barabara moja inayoitwa barabara ya Singida – Mwakonko – Mdungila – Iyumbu, Serikali imefanya kazi nzuri, *TANROAD* wamefanya kazi nzuri na Mkandarasi aliyepewa barabara hiyo alianza kufanya kazi nzuri lakini sasa ama kasifiwa na pia kama mgema sasa anatia maji, barabara ile sasa badala ya kuweka kifusi anaweka mchanga sasa wananchi kule wamesema wataandama waende kwa Mkuu wa Mkoa. Sasa naomba sana nitumie nafasi hii kwa kweli kwa sababu nimepigiwa simu tena leo hii asubuhi, kumuomba sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na hasa huyu mtaalam bwana Mrema wa *TANROAD* azungumze na watu wake kwa kweli haiwezekani kuweka mchanga badala ya kifusi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi nimehusika sana kwenye Kamati yangu, kwa hiyo nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Joyce Masunga kwa uwasilishaji mzuri na yote aliyosema mimi nahusika nayo moja kwa moja, ni bahati mbaya hakupata nafasi nzuri ya kuyakamilisha yote ambayo angetakiwa kuyasoma, lakini nadhani kwa ruhusa yako yote yale yatakuwa yameingizwa kwenye *Hansard* ili yachukuliwe kumbukumbu kamili.

Mheshimiwa Spika, ziko sekta nyingine kadhaa ambazo hakugusia, hakugusia sekta ya *ATC* imo kwenye maandishi, hakugusia Bandari na nyinginezo. Kuhusu *ATC* tumehangaika nayo sana, tumezungumza na Mheshimiwa Waziri mara nyingi kwamba jamani ni lazima tufike mahali tupate ufumbuzi juu ya hii *ATC* na kama ubinafsishaji bado uko mbali basi hata hizi ndege mbili tulizonazo tuziweke sawasawa, tuziboresha, tunaweza kabisa tukaendesha Shirika letu la *Air Tanzania* kwa ndege zetu mbili, tatu kwa uzuri kama wenzetu wanavyofanya. Wenzetu wa Rwanda wameanzisha shirika juzi juzi hapa kwa ndege moja tu lakini sasa tayari wameshaanza kuja hata Tanzania na sisi tunaweza kabisa kwa ndege hizi mbili badala ya kung’ang’ania wawekezaji, sasa ni mwaka wa tatu tunazungumzia juu ya mwekezaji au huyu mwekezaji hajapatikana bado. Kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa kweli ni aibu kuona kwamba mashirika ya binafsi yanafanya vizuri, shirika letu halifanyi vizuri jitihada zote ambazo tumefanya kama Kamati, tumezungumza sana juu ya suala hili, naomba sana walipatie ufumbuzi juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, hapa tunalumbana juu ya kasugura kadogo na tatizo ni kwamba uwezo wetu kifedha wa ndani ni mdogo. Kwa muda mrefu tumesema ni vizuri sera ile ya *Public Private Partnership, PPP* ikafanya kazi, kwa sababu kama tungefanikiwa kukamilisha ile, nasikia unakuja hapa Muswada chini ya *certificate of Urgency,* nakubali lakini tu umechelewa sana kwa sababu ingefanikiwa barabara tungejenga nyingi, madaraja tungeyajenga mengi. Mwenzetu Mheshimiwa Rita asubuhi alikuwa anazungumzia *fly-overs,* hatuwezi kujenga *fly-overs* na barabara zote hizi kwa fedha zetu za ndani, haiwezekani. Sasa kama uwezekano upo wa kutumia fedha za wenzetu mbalimbali kutoka nje ambao wako tayari kuja na wanakuja lakini urasimu uliopo Serikalini ni mkubwa sana mpaka wengine wanakata tamaa wanaondoka? Hivi kuna tatizo kutokuikamilisha hii mapema, sasa maadamu Serikali imetanabahi jioni basi Muswada huu tuulete na wameleta hapa kwenye *Certificate of Urgency*, mimi nina hakika Waheshimiwa Wabunge tutaipitisha lakini basi isikae tena kwenye makabati zaidi ya miaka kadhaa. Tuipitishe na ifanye kazi ili tujikomboe katika barabara hata upande wa reli tunaweza kabisa na reli yetu ndiyo hiyo imeelezwa sina haja ya kuzungumzia tena tunadhani kabisa kwa kutumia utaratibu huu wa *PPP* basi tunaweza tukanufaika.

Mheshimiwa Spika, la pili, *solution* ya kuchakachua mafuta haya ya *diesel* na mafuta ya taa hakuna *solution* ya mkato zaidi ya kuoanisha bei ya mafuta ya taa na bei ya *diesel* hiyo ndiyo *solution*, mengine yote haya Mheshimiwa haya Serikali, itahangaika lakini haitapata *solution*. Mimi nasema tusiangalie tu mafuta ya taa bei ipande juu ili kusudi ioane na *diesel*, tuteremshe bei ya *diesel* ije chini ifanane na bei ya mafuta ya taa. Sababu unapoliangalia kwa maana ya kupandisha bei ya mafuta ya taa, unajua unawakomoa wananchi sawa, lakini tuangalie kwa maana ya kwamba bei ya *diesel* ishuke ifanane na mafuta ya taa ili kusudi tuondokane na aibu. Sasa nchi yetu uchumi wake unaharabika kwani watu wa Rwanda wamerudisha magari zaidi ya 60 wamesema hatufanyi tena biashara hiyo, wanataka kuisusa bandari yetu ya Dar es Salaam, sasa kitu kidogo hiki mpaka uchumi wa nchi hii uyumbe kwa sababu ya kushindwa kuainishwa hiyo bei ya mafuta ya taa na *diesel* kwa miaka nenda miaka rudi? Chonde chonde sana naomba Serikali kwa kweli katika hili ni aibu sana mpaka nchi jirani wanasema hawataendelea kututumia sisi, wataenda Mombasa na bandari zingine kwa kuwa tu tunashindwa kulishughulikia linavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, sitaki kugongewa kengele ya pili, narudia kukushukuru sana wewe mwenyewe, nakutakia kila la kheri lakini nadhani na wewe utaniombea na mimi kila la kheri ili nirudi hapa ili tukutane kwenye Bunge lijalo. Naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** *Inshallah*, Amina, Ahsante.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa jioni hii ya leo kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii muhimu. Nimshukuru Mwenyezi Mungu pia anayeendelea kutupatia amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia nimpe pole baba yangu mdogo, Mzee John Kimbita aliyefiwa na mtoto wake Awinia ambaye amezikwa mchana huu wa leo, nawapa pole sana ndugu, jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri na watendaji wengine wote, kwa kazi wanayoifanya. Jamani kwa sababu malalamiko haya yaliyopo sio malalamiko mabaya ni changamoto kwamba hawa watu wanahitaji maendeleo kwa kuamini kwamba barabara ni kiungo kimojawapo cha maendeleo lakini lazima tukubaliane kwamba kazi kubwa na nzuri imeshafanyika na tunaimani bado kazi inaendelea kufanyika ukisoma hiki kitabu mambo yako mengi sana na ni mazuri. Kwa hiyo mimi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote pale Wizarani kwa kazi kubwa wanayoendelea kufanya. Wala tusikatishwe tamaa na maneno madogo madogo, ni kawaida tu lakini kazi inaendelea kufanyika na bado kazi tunaendelea kuiona.

Mheshimiwa Spika, nisiwe mchoyo ya wafadhila, narudia kusema tena namshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, waliweza kutembelea barabara yetu ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa kujengwa kwa kiwango cha lami kutoka Kwa Sadala kwenda Masama ambako hivi tunavyozungumza nimeongea na yule Mkandarasi amenihakikishia kesho kutwa huenda kazi ikaanza, kwanza ile ya kufanya *clearance,* kuna vitu vidogo anakamilisha na baada ya mvua kusimama basi wananchi wa Wilaya ya Hai watashuhudia kwa macho yao kazi kubwa na nzuri ambayo itaanza hivi karibuni. Nashukuru sana na nazidi kuipongeza Serikali kwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza Wilayani Hai ziko barabara tatu tulizoomba zipandishwe daraja ambazo zinakidhi kabisa yale mahitaji ili kwamba barabara iweze kufikia kiwango cha kupandishwa daraja kutoka Halmashauri kwenda *TANROAD* nayo ni barabara ya kutoka kwa Sadala Masama, lakini kuelekea upande wa Mashua Masama Magharibi kwenda kuunganisha na barabara inayokwenda Sanya Juu kwa maana ya kuunganisha kuwa *ring road,* kwani barabara inakidhi viwango vyote vinavyohitajika katika kupandishwa daraja. Kutoka kwa Sadala kwenda Masama, Machame Barazani, barabara hii inakidhi viwango vinavyohitajika na pia itakuwa ni barabara mbadala endapo daraja letu la Kikavu litapata dhoruba yoyote, basi magari kutoka Moshi kwenda Arusha yataweza kupita hiyo barabara pia.

Lakini ipo barabara nyingine muhimu ambayo nayo inakidhi mahitaji ni barabara ya kutoka Bomang'ombe, Rundugai, Longoi hadi *TPC* kuja kutokea Moshi Mjini, nayo itatengeneza *ring*. Ni barabara ambayo inakidhi mahitaji. Kwa hiyo, tunaomba ipandishwe daraja. Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake na wale wataalamu waweze kwenda kuangalia tena vizuri vile vigezo na hatimaye hizi barabara ziweze kupandishwa hadhi na kuweza kuhudumiwa na *TANROAD* Mkoa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba tulishazungumzia kuhusu suala la *KIA*. Naishukuru Serikali kwa kununua zile hisa za zile kampuni za nje na kwamba ilikuwa imebakia kampuni ya kitanzania kutoka ile kampuni ya *KADCO*. Ili ule uwanja uweze kutumika, tunayo hazina kubwa kabisa kwani uwanja

wa *KIA* ni mkubwa sana na mzuri, lakini tunautumia chini ya matumizi yake, yaani tuna *under-utilize* ule uwanja. Wenzetu Kenya wanajenga uwanja mwingine karibu na Rombo sasa hivi. Maua yanayolimwa Arusha na Kilimanjaro yatasafirishwa kupitia Kenya. Hii ni aibu, kwani uwanja tunao mkubwa ambao tunaweza tukautumia kwa ajili ya biashara yetu ya maua, mbogamboga pamoja na vitu vingine ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watalii. Naomba sana ule uwanja wa *KIA* tuweze kuutumia vizuri ili kuongeza pato la Taifa na wananchi wa Wilaya ya Hai waweze kufaidika kutokana na uwanja huu wa *KIA*.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni mvua zimenyesha, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa matarajio mazuri ya mavuno. Lakini barabara zetu zimeharibika sana. Juzi tu nimesafiri kutoka Moshi kuja Chalinze hadi kufika hapa Dodoma, lakini kipande cha kutoka Moshi kufika Segera kusema ukweli kimeharibika. Nimeangalia kwenye kitabu huku naona kuna baadhi ya maeneo ambayo yamepata fedha, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie kwa jicho la huruma na kwa kuelewa kwamba barabara ya lami inapokuwa na vijishimoshimo ndiyo inaharibika haraka zaidi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake anijibu kuhusu hizi barabara tatu nilizozitaja ziweze kupandishwa daraja. Anijibu pia kuhusu utengenezaji wa hii barabara kutoka Moshi hadi Segera kwa sababu kipande cha kutoka Chalinze - Segera kinahudumiwa kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuipongeza Serikali yetu kwa uamuzi wa busara na hekima waliyoichukua kuhusu reli. Tunafahamu fika kwamba reli zetu zikiimarika pia tutaziponya barabara zetu kwa kiwango kikubwa kwa sababu ile mizigo mikubwa na mizito itakuwa inasafirishwa kwa kutumia reli. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa isitumie muda mwingi zaidi, ifanye maamuzi ya haraka katika kuboresha reli zetu na ikiwezekana kupata wabia. Lakini siyo lazima sana tukakazania kutafuta wabia kwa sababu ipo *PPP*. Wenzangu wameshazungumzia sana hii *Public Private Partnership*, labda ni hii sheria mpya tunayoisubiri ya manunuzi ili tuweze kufanya vitu vya maendeleo na vya makusudi.

Mheshimiwa Spika, nchi zote zilizoendelea zilikopa, kwa hiyo, nasi wala tusiwe wavivu kukopa maadamu tunakopa kwa ajili ya maendeleo yetu na pesa zile tukishazikopa tuzisimamie kwa uangalifu mkubwa. Natumaini tutapiga hatua ya maendeleo kwa kasi zaidi ili yale ambayo Watanzania wanayoyategemea waweze kuyaona na kushuhudia maendeleo makubwa kwa kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, nimesoma kwenye kitabu hiki, naona mambo ya *ring roads* za Dar es Salaam. Naipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla. Lakini naomba hizo kazi zifanyike kwa haraka zaidi kwa sababu wananchi wanaoishi Dar es Salaam wanapoteza muda mwingi sana katika foleni barabarani na pale mvua zinaponyesha ndiyo inakuwa shida kubwa zaidi.

Lakini pia haikuishia hapo, kama mabunge mawili yaliyopita nilimwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika maswali ya siku za Alhamisi kuhusu *congestion* ya magari mjini Dar es Salaam: Je, Serikali ingekuwa tayari kuja na wazo la kujenga

barabara za juu, yaani *fly overs*? Sasa nimeona kwenye kitabu nazo hizo *fly overs,* zitaanza mbili *TAZARA* na Ubungo. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake mzuri huo.

Lakini yapo mambo mengine ambayo tunayafanya kwenye barabara zetu tumeongeza mno matuta mengi barabarani kiasi kwamba muda wa kusafiri unakuwa mwingi sana, sijui kama tunatarajia tuoteshe viazi kwenye hizi barabara zetu! Nadhani suala la kufanya hapa ni kutoa elimu kwa umma, yaani matumizi bora ya barabara na sio kuongeza matuta kila mahali. Tunapoteza muda mwingi sana kusafiri na kusababisha ajali ambazo siyo za lazima.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri akakae na wataalamu wake wafikirie vizuri kwani barabara zetu karibu zote sasa hivi ukisafiri lazima uchoke na kupoteza muda mwingi sana kisa ni matuta. Lakini haya matuta badala ya kuokoa maisha ya wananchi sasa yanaleta misiba kwa sababu ajali zinatokea kwa wingi. Ninaomba tuwaelimishe wananchi wetu kuhusu matumizi ya barabara ili tuwe na nidhamu wakati wa kuvuka barabara na madereva pia wazingatie sheria za barabarani.

Mheshimiwa Spika, hii biashara ya mabasi mpaka karne hii wakati wa kusafiri yanasimama njiani kwa lengo la kuchimba dawa. Kuna tangazo muhimu la *Tigo* linaloonyeshwa na vituo vya televisheni, mtu kaachwa na basi kwa sababu ya kuchimba dawa. Ni kwa sababu hakuna vyoo katika barabara kuu. Ni mambo ya aibu sana! Watu wanapata maradhi mengi sana kutokana na huu utaratibu ambao siyo rasmi na wala siyo sahihi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri akakae na wataalamu ili waangalie uwezekano wa kujenga vyoo katika *high ways* zetu zote.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kuzidi kuwahakikishia Watanzania kwamba dalili za maendeleo zinaonekana. Hizi porojo nyingine za kwamba eti watu wengine ndiyo wapewe nafasi, bado hiyo nafasi haipo. CCM itaendelea kutawala na kule Hai wameniambia kwamba sasa hivi siyo Shambadarasa tena na siyo mahali pa kufanyia mazoezi, wananchi wa Hai wataendelea kuichagua Serikali yao ya CCM kwani kwa kipindi kifupi sana cha miaka mitano yapo makubwa na mazuri yaliyofanyika na wamezidi kuahidi kwamba wataendelea kuunga mkono Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninazidi kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa kazi kubwa na nzuri inayofanyika. Tuzidi kuombeana kila la kheri Waheshimiwa Wabunge wote ili tuweze kurudi hapa tukiendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye ametuongoza vizuri sana na mafanikio makubwa yanaonekana.

Naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Godwin Kimbita. Waheshimiwa Wabunge kadri tunavyoendelea na tuna mgeni nadhani atakuwa kwenye *Speakers Gallery* au sijui sehemu gani lakini ni mgeni wa Mheshimiwa Hezekiah Chibulinje - Naibu Waziri wa

Miundombinu, Mama Violeth Chibulunje, ni mkewe Mheshimiwa Chibulunje. Simwoni, basi labda ana udhuru kidogo, lakini nililetewa tangazo hili.

Tunaendelea na ninamwita sasa Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga na mchangiaji wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Bujibu Sakila.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami kuchangia hoja hii muhimu sana ya Wizara ya Miundombinu.

Nianze kwa masikitiko makubwa kwa kusema kwamba kwa mara ya kwanza katika kipindi cha changu cha kuwa Bunge, leo naanza kwa kusema siungi mkono hoja ya Wizara hii. Lakini huenda nitaiunga mkono pale nitakapopata maelezo katika maeneo ambayo yananipa matatizo.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha *Volume IV* tunaonyeshwa kwamba mwaka jana tuli-*approve* shilingi bilioni 6.7 kwa ajili ya barabara ya Manyoni-Itigi-Tabora. Mwaka huo huo tuka-*approve* pia shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya barabara ya Nzega-Tabora. Mwaka huu tunatakiwa tu-*approve* kwa Tabora – Itigi – Manyoni shilingi billioni 8.6 na kwa Nzega – Tabora shilingi bilioni 6.5. Kama mwaka jana pesa hizi hazikutumika, nina sababu gani ya kuamini kwamba mwaka huu pesa hizi tuki-*approve* zitatumika? Hilo ndiyo tatizo langu.

Lakini tatizo linakuwa kubwa zaidi wakati Serikali ilishazitangaza hizi barabara, ilizitangaza ili Wakandarasi wapatikane, *tender* zimeletwa na zimechambuliwa, lakini mpaka leo tunakuja kwenye bajeti hii Wakandarasi waliopewa barabara ya Tabora - Nzega, Tabora – Itigi - Manyoni hawajatangazwa. Sasa nina sababu gani mimi ya kuikubali bajeti hii? Ndiyo maana nasema sitaikubali mpaka nipate maelezo ya kutosha kwamba Serikali inafanya nini juu ya jambo hili?

Mheshimiwa Spika, kana kwamba hiyo haitoshi, kuna barabara ya kutoka Tabora kwenda mpaka Ndolo inatakiwa kujengwa. Katika kitabu hiki cha *Volume IV* haionyeshi barabara hii imepangwa kiasi gani, sasa kama haijapangiwa, pesa nina sababu gani mimi ya ku-*approve* bajeti ambayo haichukui maslahi ya eneo ambalo ninaliwakilisha?

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa tena, katika bajeti hii haielezwi kwamba baada ya Serikali kumalizana na *RITES* katika tatizo la uendeshaji wa kampuni ya reli, Serikali imejipangaje kutuondolea matatizo haya ya shirika hili la reli? Katika vitabu vyote viwili mimi natazama, yaani natazama *Volume IV* na *II* hakuna mahali unaona zimetengwa pesa kwa ajili ya kuifufua *TRL*. Hii *TRL* ndiyo inayochukua mizigo kuanzia Dar es Salaam mpaka Kigoma na nchi za jirani. Lakini leo hii tunazungumzia bajeti ya miundombinu, hakuna pesa za reli. Pesa za reli zilizopo ni kidogo sana, lakini mahitaji ya reli tukichukua sisi kama Serikali tunahitajika tuhakikishe kwamba injini zilizopo zinafanya kazi na zinahitaji vipuri, mabehewa yaliyopo yanayofanya kazi yanahitaji vipuri, reli yenyewe imechoka inahitaji kutengenezwa. Mambo haya ni mazito, hatuwezi kuja hapa tunapitisha bajeti ya Miundombinu ambayo haizungumzii namna gani na mkakati wa Serikali wa kufufua reli.

Kwa maana hiyo, sitaipitisha bajeti hii mpaka hapo nitakapopata maelezo yanayoridhisha kwamba Serikali imejipangaje kuondokana na tatizo la reli ya kati, tatizo la barabara ya Nzega-Tabora, barabara ya Tabora- Ndono na Tabora – Itigi? Tupate maelezo! Watu wa Tabora tumechoka jamani! Tumechoka kuwa wasindikizaji. Siku zote tunasema hapa na mimi naendelea kuipongeza Serikali yangu, imefanya kazi nzuri sana kinchi, lakini kwa Tabora haijafanya chochote. Nasikitika kusema hivyo kwa upande wa miundombinu. Kwa ajili hiyo, sitaunga mkono mpaka nitakapopata maelezo ya kuridhisha kwamba Serikali itafanya nini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mh! Habari ndiyo hiyo sasa! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mazuri ambayo yamefanya nisipate muda wa kuzungumza, lakini nizungumzie haya ambayo yananitinga sana. Lakini naishukuru Serikali kwa kumaliza utaratibu wa kujenga kiwanja cha ndege cha Tabora kwa lami, naishukuru Serikali.

Lakini vilevile Serikali bado ina tatizo kwenye shirika letu la ndege. Inasikitisha nchi nzima na Serikali nzima inashindwa kuendesha shirika la ndege wakati mtu binafsi au sekta binafsi ndiyo inayookoa nchi hii kwenye mambo ya usafiri wa ndege, iwakuwaje? Tatizo liko wapi? Mtu binafsi au sekta binafsi inaendesha shirika la ndege, Serikali nzima inashindwa. Labda tuambiwe alikuwa mwekezaji kutoka China hapa amenunua ndege mbili, *Dash 800* ndizo zinazofanya kazi. Huyu mwekezaji nasikia amekuwa *frustrated,* ameondoka na ndege katuachia, lakini ndiye mwekezaji huyu huyu ametujengea na *VIP lounge*, amejenga *VIP lounge* lakini sisi tumeshindwa kuwa naye. Sasa kama kuna matatizo yoyote, Shirika la Ndege ni lazima tulifufue, mkakati uwe hivi, atafutwe mwekezaji. Kiongozi akishapatikana, mwekezaji kiongozi, tulibinafsishe shirika hili kama tulivyobinafsisha benki ya *NMB. NMB* ni *good modal* ya kubinafsisha. Alipatikana mwekezaji kiongozi, wengine tukawa ni pamoja na wananchi wa Tanzania. Tufanye hivyo hivyo kwa *Air Tanzania*. Inawezekana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Shirika la Reli, lina historia yake. Reli hii ilijengwa na Mjerumani toka mwaka 1902 – 1905. Hao bado wanaweza kuwa na *interest* ya kuona reli hii inafanya kazi. Kuna tetesi kwamba Wajerumani wakiombwa wanaweza kuja, sasa kama tuliweza kuwaomba wawekezaji wengine hebu twende Ujerumani tuwaambie jamani eh, tuna Reli yenu imetushinda kuendesha, njooni tufanye mpango tuangalie. Sasa hivi kuna sheria mpya ya *PPP*, njooni Wajerumani. Tufanye hilo! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la Wizara hii vilevile ni kubwa mno kiasi kwamba utaona bajeti hii tunayozungumza leo hapa kwa kiasi kikubwa ndani ya vitabu vyote hivi takribani asilimia themanini na ziada tunazungumzia barabara tu. Lakini hii ndiyo Wizara ambayo ndani yake kuna bandari, viwanja vya ndege, reli, nyumba za Serikali na mambo chungu nzima yako huku. Wakati wa ukoloni, Shirika la Reli na Shirika la Bandari vilikuwa kitu kimoja. Wale walifanya vile kwa maana na ndivyo ilivyo hata kule *Senegal* sasa hivi. Kule Afrika Kaskazini, mashirika ya reli siku zote yanaendana pamoja na mambo ya bandari kwa sababu hivi ni vitu vina-*provide synergy*. Watu wa bandari

wanazo pesa. Kama reli hana pesa wanafanya *cross subsidies* wanasaidiana. Sisi kwa nini tusirudie utaratibu ule uliokuwepo? Shirika la Reli na Shirika la Bandari ifanye kitu kimoja halafu haya mambo mengine kama barabara, ikiwezekana iundiwe Wizara yake kwa sababu hapa leo tunazungumza habari ya barabara tu, mambo mengi yaliyomo humu ni barabara tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna suala zima la kuweza kujenga miundombinu yetu. Njia mojawapo ni kuwa na *infrastructure bonds. Infrastructure bonds* hizi zikitafutwa *specifically* kwa ajili ya miundombinu kama hilo ndiyo tatizo, maana yake kama matangazo yalitolewa wakandarasi waje kutengeneza barabara ya Tabora - Itigi na Nzega – Tabora, leo hii kwa nini hao wakandarasi hawapewi kazi? Kuna dalili kwamba hakuna hela. Sasa kama hakuna hela mbona sehemu nyingine kuna hela? Hela hazipatikani kwa ajili ya Tabora tu? Inapokuja Tabora, basi hakuna hela! *(Makofi) (Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kwa sababu umekuwa ukikatizwakatizwa na washangiliaji, basi nakuongeza dakika nyingine mbili. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Tabora kwenda Ndono kuelekea Urambo kwenda Kaliuwa, imefungwa ndani ya barabara ndefu kutoka Kigoma – Kidahwe - Uvinza na Malagarasi. Sasa hatujui, hizi hela za Tabora - Ndono zipo au hazipo? Maana yake njia ya kujua ni kuiona ile *portion* kabisa kwamba Tabora - Ndono ni shilingi kadhaa, tuambiwe hivyo. Lakini bado nimesimama pale pale, kwa nini mikataba ya Nzega - Tabora na Itigi -Tabora haisainiwi? Kwa sababu kama ni suala la wapigakura na watu kuona kwamba nchi hii ni yetu wote na watu wa Tabora nchi hii ni ya kwao pia. Sasa kwa nini wao siku zote ni wasindikizaji? Kwa nini? Inatia uchungu kusema kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iniwie radhi. Leo hoja hii mpaka tutakapopita kwenye vifungu ndiyo nitabadilisha mawazo nikipata maelezo yanayoridhisha, vinginevyo siungi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kaboyonga na una haki chini ya Kanuni 102 na 103 kwa hiyo, tutaishughulikia baadaye hii.

Sasa namwita Mheshimiwa Bujibu P. Sakila mchangiaji wa mwisho.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Nami ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia uhai mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Napenda

nichukue nafasi hii vilevile kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne hasa kwa mambo mengi ambayo yametendeka katika Jimbo langu la Kwimba.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, Jimbo la Kwimba tumefanikiwa kupandisha hadhi barabara mbili kutoka Halmashauri ya Wilaya kwenda Mkoani. Nashukuru sana. Lakini vile vile katika kipindi hiki cha miaka mitano, barabara kama tatu hivi zilitoka Halmashauri kwenda *PMR*, ni mradi mzuri sana. Ni barabara ambazo zilikuwa hazipitiki sana, lakini leo zinapitika. Barabara ya kutoka Mabuku kwenda Malampaka, barabara ya kutoka Jojina – Ngudu – Magu, hizo ni barabara ambazo ziko kwenye mradi maalum wa majaribio.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha miaka mitano, tunayo barabara ya Mwamala - Itongwitani. Mwanzoni mwa mwaka 2006 barabara hii ilikuwa haipitiki, lakini leo inapitika vizuri sana. Kutokana na hilo, kwa niaba ya wapigakura wangu wa Jimbo la Kwimba, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ya Miundombinu. Kazi hii ilikuwa ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani hizo, ninayo machache ya kuchangia kidogo. Napenda kutokana na hotuba hii na ninaishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga na kukarabati madaraja katika barabara nilizozitaja. Barabara ya Mwamala –Itongwitani kuna ukarabati wa madaraja na pia barabara ya Umbarwa – Ngudu kuna fedha ya madaraja.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kilichonishangaza, katika bajeti hii sikuona pesa yoyote hata ya ukarabati mdogo kwa barabara zote nilizozitaja. Wasiwasi wangu ni kwamba barabara ya kutoka Mwamala kwenda Itongwitani inapita kwenye maeneo ya mvua sana. Mvua ikizidi ile barabara itakatika. Barabara ile haina fedha hata kidogo, katika mchango wangu wa maandishi nimeiomba Serikali ijaribu kuangalia, itenge angalau fedha kidogo kwa ajili ya ukarabati mdogo mdogo, hii itaepusha barabara hizi zisije zikajifunga tena.

Mheshimiwa Spika, kitu hasa kilichonifanya nisimame pamoja na hayo niliyoyasema ni kuishukuru Serikali kwa mara ya kwanza kukukubali kutenga fedha kwa ajili ya lami. Hii ni lami ambayo inaendana na ahadi ya Mheshimiwa Rais, kwamba fedha ikipatikana barabara ya Ngudu - Magu itawekewa lami.

Mheshimiwa Spika, tumepata fedha kwa ajili ya kuweka lami, lakini ni kilomita moja tu katika barabara yenye karibu kilomita 60 na fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya kuweka lami katika barabara za Ngudu Mjini. Kimsingi tuliomba angalau tupatiwe fedha kwa ajili ya kuweka lami katika barabara yenye urefu wa angalau kilomita 3.4 tu ili barabara itoke kwa Mhandisi wa Wilaya kwenda kituo cha mabasi. Kwa bahati mbaya sana, badala ya kupatiwa fedha za kuweka lami yenye urefu wa kilomita 3.4, tumepatiwa fedha za kilomita moja tu. Barabara ile haifiki hata katikati ya mji, haifiki hata katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, wala kituo cha mabasi.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha ule urefu wa barabara ile na kilomita moja tuliyotengewa, inaoenekana kama ni kichekesho! Wananchi wa Ngudu wamefurahia lakini bado wamebaki na maswali mengi sana na kufikiri kwamba, huenda hii ikawa kama ni geresha tu. Nimeiomba Serikali ijaribu kuangalia tena upya na kuona kama inaweza kuongeza kilomita mbili ili angalau zifike kilomita tatu au zile kilomita 3.4. Mimi ninaamini kwamba inawezekana, Serikali haiwezi kushindwa kuongeza fedha ili badala ya kuweka lami katika kilomita moja, basi ziwe 3.4. Naamini kabisa Mtani wangu Mheshimiwa Kawambwa hapo na Naibu wake Mheshimiwa Chibulunje watakuwa wameongea na wataalam wao, na watakuwa wamekubaliana na ombi langu.

Mheshimiwa Spika, hasa hilo ndilo lilikuwa ombi langu kubwa kwamba ziwekwe fedha kidogo kwa ajili ya ukarabati mdogo mdogo wa zile barabara kwa sababu zinapita katika maeneo magumu sana. Ninaishukuru Serikali kwa ajili ya madaraja ambayo yamewekwa.

Mheshimiwa Spika, labda sasa nichukue nafasi hii na mimi kutangaza nia. Kwanza, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kwimba. Mwaka 2005 wakati wananichagua, baadhi yao hawakuamini kama ningeweza kumaliza miaka mitano. Wale ambao mliniona hapa mwanzoni mwa Bunge hili, hali yangu haikuwa nzuri sana, lakini ninawashukuru sana wapigakura wangu kwa kunifariji kwa kuwa karibu sana na mimi. Ule upendo walionionesha ndiyo unapelekea hali yangu kuendelea kuwa nzuri kila wakati, na kutokana na kazi nzuri ambayo nimeifanya wananchi wa Kwimba wamefarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwa sasa hivi kuna watu wanapitapita kule. Kwa bahati mbaya sana siwafahamu, huwa wanategea nikija huku ndiyo wanapitapita kule. Lakini ninapojaribu kufuatilia, nagundua kuwa baadhi yao wanakuja kuomba kutangaza majina. Inawezekana wamesikia kwamba labda ninakaribia kuachia ngazi baadaye, kwa hiyo, wanaanza kusogeasogea na mimi ninawaambia karibu, waje tu, kwani sina wasiwasi na wapigakura wa Jimbo la Kwimba hawana wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watu hawa wanakuja kujaribu, lakini Kwimba siyo maabara, siyo mahali pa kufanyia majaribio, Kwimba unaomba kazi, unafanya kazi. Hata wao ninapenda kuwaambia tu kwamba, viatu vyangu ni vipana sana, wanaweza kuja na wakajikuta wakipwelea. Hivyo ninawaomba sana wajitahidi waje, na wanaokuja kufadhili waje na wenyewe sijawakataza maana yake ndiyo utaratibu huo. Mtu kama una fedha nyingi, unasambaza kidogo na unapunguza umasikini. Kwa hiyo, ninawakaribisha sana na hao ninatamani waje wengi zaidi kwani bado tunahitaji msaada zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, ninatumia nafasi hii kutangaza nia, na kimsingi sitangazi nia ila ninatoa taarifa kwamba, kama nilivyokuwa nakuja safari zilizopita na sasa hivi ninakuja kutetea nafasi yangu. Bado yapo mambo ambayo tumeyaanza na tunakwenda vizuri. Masuala ya maji tunakwenda vizuri, na ndiyo tumeanza kusambaza katika vijiji mbalimbali na wananchi wanajua.Ttunasubiri mradi wa

umeme uanze, masuala ya barabara tunaendelea nayo vizuri sana na wananchi wanafahamu kwamba bado nitahitajika katika kukamilisha kazi hizo. Wananchi walikuwa na wasiwasi labda kwamba sitaomba Ubunge, lakini ninapenda kuwahakikishia kwamba nitaomba tena.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi hoja ya hotuba bajeti ya Wizara ya Miundombinu ya 2010/2011. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu kwa kazi kubwa inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina kazi kubwa ya kuhakikisha miundombinu inapewa fedha ya kutosha ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake. Ni ukweli usiopingika kwamba hivi sasa Halmashauri zetu zinajenga barabara zao hazina kiwango na kupoteza fedha nyingi za Serikali. Naiomba Serikali iweze kuzisimamia miundombinu ili tupate barabara bora.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya ujenzi wa nyumba za kuuziwa wananchi na nyumba za kukodi, pamoja na jitihada kubwa ya Serikali eneo hili linahitaji zaidi. Serikali itapata fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa pikipiki (boda boda) hivi sasa unasababisha wananchi kupoteza maisha kwa sababu ya ulevi wa saa zote, wakati wa kazi. Naomba Sumatra iangalie jinsi itakavyodhibiti hali hii.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbagala bora hivi sasa ni nzuri sana, unakwenda vizuri, lakini balaa ni pale unapofika Mbagala Rangi Tatu, msongamano unakuwa mkubwa, magari huchukua hata saa mbili kuingia njia moja. Ni vyema miundombinu ya eneo hilo iboreshwe hadi kiwanda cha Korosho, kuna maeneo ujenzi wake umeanza kubomoka irekebishwe, pia mifereji kwa zile sehemu ambazo wananchi wapo wengi ifunikwe na mifuniko iimarishwe badala ya wananchi kuweka mbao kwani ni hatari kwa kuwa huwa wanaitumia kama kivuko.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo gani *ATCL* hadi leo? Lilikodishwa ndege *(Air Bus A320)* kwa kuwa ndege ilikuwa tayari imeshatumika miaka 12 huko ilikotoka na hapa nchini ilitumika mwaka mmoja tu na leo tumeipeleka matengenezo, ningependa kupewa taarifa ya ndege hii hadi sasa. Pia kupata taarifa, mwekezaji China Senegal hadi sasa imefika wapi? Tufahamu hali hii na kikwazo kipo wapi?

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya Reli na Bandari, barabara ndio njia pekee ya ukombozi wa Taifa letu. Serikali na ikope pale tunapokopesha, Kenya inatuacha nyuma kuelekea shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nchi yetu inapata fedheha kubwa kwa tatizo la kuchakachua mafuta na hata kupelekea mafuta kutopelekwa nchi jirani ya Rwanda kurudishwa nchini, lakini jambo la aibu zaidi hapa nchini vituo vingi vinachakachua na kupelekea uharibifu mkubwa wa vyombo vinavotumia mafuta hayo. Ni vyema basi Serikali ilete sheria Bungeni ambayo itadhibiti hali hii. Faini ya shilingi milioni 10 ni ndogo sana. Kwa hiyo, ni vyema kufuta leseni sio chini ya miaka mitano. Wananchi sasa wanaona balaa hili Serikali itachukua hatua gani? Waziri aeleze hali hivi sasa ikoje na hatua zinazochukuliwa.

**MHE. ZULEKHA Y. HAJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri yenye kueleweka. Nimefurahishwa na nimefarijika kusikia hotuba hii imezungumzia na masuala ya watu wenye ulemavu kutokana na utaratibu wake na mipango yake ya miundombinu. Hivyo mipango hiyo na utaratibu huo uwepo sehemu zote mfano bandari, viwanja vya ndege, barabarani na vituo vya reli ili na wao wamudu kuzitumia hizo sehemu kama wananchi wengine.

Mheshimiwa Spika, vile vile ili kukuza uchumi wetu, napendekeza hivyo viwanja vya ndege viboreshwe kama vile Kigoma, Tanga, Mtwara, Dar es Salaam, Zanzibar, Kilimanjaro na kadhalika.

Pia bandari zetu nazo ziboreshwe kama vile ya Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Kigoma, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na kwingineko, na Reli ya Tazara, Reli ya Kati na Reli ya Moshi na Tanga. Ni imani kwamba hali ya uchumi itakua na umasikini utapungua na ajira zitapatikana kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, shirika letu la ndege lifikiriwe sana na litafutiwe ufumbuzi wa kuliwezesha. Kuhusu kuboresha hizi sehemu tunaweza kuzungumza na mifuko yetu ya jamii itukopeshe na kutusaidia kama ilivyofanyika Chuo Kikuu cha *UDOM* na nyumba za askari.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutengenezwa barabara ya Tabora – Ikembo – Kaliuwa – Kigoma kwa kiwango cha lami, sasa ni mwaka wa pili. Matengenezo ya barabara hii yameanza kidogo sana na hali hairidhishi. Serikali ieleze hapa Bungeni, barabara hii itakamilika lini? Kuanzia May, 2010 imenyanyuliwa kilometer chache kutoka Tabora mjini kuelekea Urambo, kama kilometer tano tu na kazi imesimama.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa kwa barabara ya Nzega – Tabora ni kidogo sana, hatuwezi kwenda kwa *speed* hii tukafika. Barabara yenye kilomita 116 imekuwa ni kikwazo kikubwa kwa uchumi wa Mkoa wa Tabora. Serikali ihakikishe mwaka huu wa fedha barabara hii muhimu inakamilika, pamoja na ile ya Itigi nayo ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Tabora na Singida pia.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 Serikali ilipandisha hadhi barabara ya Kaliua, kilomita 60, kilomita 90 hadi kwenda Mpanda na kuwa barabara ya Serikali kuu yaani *TANROAD*. Tangu hapo mpaka leo hakuna kazi au matengenezo yaliyofanyika kusaidia

barabara hii. Wakati wa mvua haipitiki kabisa, barabara hii ni muhimu sana kwa usafirishaji mazao ya biashara na chakula. Serikali itueleze nini inawaza kuhusu barabara hii?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe viwango vya utengenezaji wa barabara zetu hapa nchini. Wakandarasi wengi wanapewa fedha nyingi sana lakini barabara hazina viwango. Unakuta barabara inakamilika lakini baada ya muda mfupi inaanza kuonyesha kutitia na mashimo kibao mfano barabara Singida - Nzega imejaa mashimo tele! Barabara Morogoro – Dodoma kila leo utawaona *Tanroad* wapo kwenye matengenezo. Fedha yetu kidogo tuliyonayo tutumie vizuri siyo kucheza *marktime* kwenye barabara zile zile wakati mikoani barabara hazina lami.

Mheshimiwa Spika, barabara zote zinazotekelezwa kwenye Mikoa na Wilaya, ni lazima wahandisi wa barabara wa maeneo husika ili wawe wasimamizi wakuu, mikataba ya wakandarasi iwekwe wazi na nakala wapewe *engineers* wa Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, ajali nyingi zinazotokea maeneo ya Chalinze hadi Ruvu darajani zinasababishwa na ubovu wa barabara ambayo imebonyea, ina migongo na ukipita gari zinayumba. Serikali haioni hilo? Viongozi wote wanapita pale wanaona, lakini wanafumba macho au wote mnapanda ndege? Leo tunaona hospitali ya Kibaha kila leo inapokea majeruhi na watu wanaopoteza maisha Serikali ifanyie kazi sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Reli ya Dar es Salaam – Tabora – Kigoma ni mkombozi wa wananchi wengi na pia uchumi wa Taifa. Tukiamua tunaweza kuondea Reli zetu hapa nchini sisi wenyewe. Serikali ijipange, iweke mikakati ya kuboresha reli zetu bila kutengemea wawekezaji. Tujifunze yaliyotokea kwa *RITES* badala ya kutusaidia wametumaliza. Ahsante.

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ujenzi wa barabara ya Lushoto – Magamba kwa kiwango cha lami unakwenda polepole sana umbali wa kilomita 16 lakini ujenzi unatolewa kwa kandarasi ndogo mno kilomita moja. Barabara hii haipo mjini ni ya *rural.* Unapompa *contractor* ajenge anahitaji *mobilization* kwa ajili ya kilomita moja. Kwa nini tusimalize kilomita tatu zilizobaki badala ya kuzigawa?

Mheshimiwa Spika, pili, lipo ombi la kuongeza kilomita nyingine tatu kwa ajili ya kupitisha eneo la *University - SEKUCO*. *Tanroad* wanafanya kazi nzuri. Hebu wawezeshwe ili barabara hiyo ya Lushoto Magamba ikamilishwe kujenga kilomita tatu tokea mwaka 2004. Ni kinyume na mahitaji ya maendeleo.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati kabisa kumpomgeza Serikali ya Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Dr. JK kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2005.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Rufiji, tunatoa shukrani nyingi kwa Waziri wa miundombinu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu wake, Katibu Mkuu wake na watumishi wote wa Wizara hii.

Naomba kutaja barabara zifuatazo:-

- Barabara ya Kibiti – Mkongo – Utete – Nyamwage imejegwa vizuri hususan kipande cha Utete – Nyamwage. Aidha, tunasifu daraja kudumu lililojengwa katika kitongoji cha Kitundu mvumoni karibu na kivukoni Utete. Aidha, tunashukuru kwa Serikali kutekeleza ilani ya CCM ya mwaka 2005 kwa ununuzi wa Pantoni na ujenzi wa gati ya kivuko cha Utete.

- Ombi langu ni kwamba Serikali iendelee na utekelezaji wa kuiwekea lami barabara ya Utete – Nyamwage kuungana na barabara ya lami ya Kibiti – Lindi. Serikali ikubali kutimiza azima hii ili Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji, yaani Mji wa Utete iweze kufika kwa lami kama yalivyo Makao Makuu ya Wilaya ya Mkoa wa Pwani.

- Tunaipongeza Serikali kwa kuichukukuwa Barabara Barabara ya Ikwiriri – Mkongo – Mloka – Vikumburu – Kisarawe – Kibaha iwe inahudumiwa na *TANROADS* Mkoa wa Pwani.

- Ombi langu ni kwamba barabara hii haikupangiwa fedha wala kutamkiwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni leo. Naomba itafutiwe fedha ili ujenzi wa barabara hii uanze mara moja.

- Barabara hii ijengwe kiwango cha changarawe na kwa ufanisi unaofanana na ujenzi mzuri uliofanywa na wakandarasi wa ujenzi wa barabara ya Bungu – Nyamisati. Barabara hii ni mfano wa barabara ya changarawe iliyojengwa kwa ufanisi mkubwa.

- Barabara hii ina madaraja mawili korofi sana.

    (a) Daraja Mbambe katikati ya Kijiji cha Mbunju Mvuleni na Kijiji cha Ruwe.

    (b) Daraja la Kipo. Daraja hili lipo katika bonde lililopo katika Kijiji cha Kipo na Kijiji cha Kipugira.

Mheshimiwa Spika, tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kuwa barabara hii inapatiwa fedha za ujenzi wake pamoja na ujenzi wa madaraja ya kudumu katika barabara hii kama niliyoyataja hapo juu, yaani Daraja la Mbambe na daraja la Kipo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashukuru na kutoa pongezi nyingi kwa Meneja *TANROADS* Mkoa wa Pwani Bw. Gabriel Mwikola na Wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Jimbo langu. Ninawaomba wazidishwe bidii katika kazi zao na

kuangalia kuwa kandarasi zote ni zinazoleta faida ya fedha zinazotumika, yaani *Value for money*.

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutekeleza ilani ya CCM kwa vitendo na kazi wanayofanya inaonekana japokuwa bajeti inayotengwa haikidhi haja ya kumaliza kero zote zinazogusa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mikoa ya Kusini hasa Mtwara tushukuru sana na matunda ya Awamu ya Nne tumeyapata hasa kwa jitihada kubwa sana za kujenga barabara ya Kibiti - Lindi ambayo ilikuwa kero kubwa kwa wakazi wa Mikoa hii kwa kweli umekuwa ni ukombozi mkubwa sana. Lakini tunaomba Mheshimiwa Waziri achukue jukumu la kusimamia na kuhimiza mkandarasi anayejenga kilomita sitini zilizobaki aongeze kasi ili iweze kukamilika tuondokane kabisa na adha iliyopo katika kipande hicho.

Mheshimiwa Spika, shukurani nyingi pia kwa Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. Ni kazi kubwa iliyofanyika ya kujenga Daraja la Umoja katika Mto Ruvuma. Hii ni hatua kubwa ya maendeleo kwani kwa hivi sasa wananchi wameanza kunufaika kwa kusafiri bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imejitahidi kutafuta wafadhili na kupata pesa za ujenzi wa barabara ya Masasi - Mangaka ambayo ipo katika hatua nzuri sana, kwa kweli wananchi wa Mkoa wa Mtwara tuna haki ya kuishukuru Serikali yetu kwani kwa miaka mingi miundombinu ya barabara kwa kusini ilikuwa ni tatizo kubwa ambalo hatukutarajia kama litakwisha.

Mheshimiwa Spika, kila penye mafanikio hapakosi tatizo. Mkoa wetu wa Mtwara umekuwa na tatizo kubwa la barabara ya kiuchumi inayotoka Mtwara kupitia Tandahimbo – Newala – Masasi – Nanyumbu. Barabara hii ni muhimu sana, kwa ujumla tumeomba sana Serikal kuona umuhimu wa kutenga fedha ili kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili tuwe na uhakika kwa kipingi chote kusafirisha kwa urahisi mazao yetu na matumizi mengine. Je, hadi sasa Serikali ina mkakati gani wa kusikiliza ombi hili na kulifanyia kazi ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, ombi lingine ambalo ni la muda mrefu ni juu ya matumizi ya bandari yetu ya Mtwara ambayo ina kina kirefu na hivyo kuwa na sifa ya kuweza kutia nanga meli kubwa. Je, hadi sasa Serikali imelifikiria vipi suala hili?

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga mpango wa kujenga daraja katika mto Nangoo hili ni tatizo la siku nyingi sana. Kwa hiyo, naomba kujua ujenzi wa daraja hili utaanza lini na kukamilika lini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza kwa dhati waziri, naibu waziri, katibu mkuu na watendaji wote wa wizara kwa kuandaa bajeti nzuri na ya kisayansi, aidha naomba kushukuru serikali kwa kutengeneza barabara ya Dodoma – Babati kupitia Kondoa kwa kuichonga kwa grader. Hatua hii imesaidia barabara kupitika vizuri na kwa muda mfupi zaidi, kabla ya matengenezo haya muda wa kusafiri Dodoma –Kondao km 160 ilikuwa zaidi ya masaa 4 sasa ni masaa 3 tu, ukiachilia mbali kero ya vumbi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, bado kilio cha wananchi wa Kondoa ni barabara hiyo kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika wakati wote wa mwaka na kurahisisha usafiri kati ya Dodoma kupitia Kondoa hadi Babati.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali itenge shilingi bilioni 12, lakini hakuna kilichofanyika. Mwaka wa fedha 2009/2010 shilingi bilioni 5.6 zilitengwa, lakini baada ya majadiliano makubwa Serikali iliongeza bajeti hiyo hadi kufikia shilingi bilioni 45. Hata baada ya nyongeza hiyo hakuna kilichofanyika zaidi ya taarifa kuwa mkandarasi amepatikana katika bajeti ya mwaka huu 2010/2011 ni shilingi bilioni 9.56 tu imetengwa. Je, fedha hii itafanya kazi gani? Kwani ni chache mno.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri awaeleze wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Aidha, hatua za awali za ujenzi zitaanza lini? Ni matumaini yangu kuwa hoja zangu zitapatiwa majibu yenye matumaini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu. Hoja zangu ni kama zifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu shirika la Ndege *(ATC).* Inasikitisha kwa shirika kubwa na muhimu kama hili nchini kuendeshwa kwa kusuasua sana kama vile Serikali haipo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni utengenezaji wa barabara za pembeni. Mara ujenzi wa barabara unapoanza Serikali husahau kwamba kuna umuhimu wa kuwa na barabara mbadala ili usafiri uendelee kama kawaida. Kuna usumbufu mkubwa sana kwa wasafiri na hasa wakati wa masika. Shauri hili naomba lizingatiwe.

Kuhusu uchakakachuaji mafuta, kama kweli Tanzania tuna nia ya kuinua uchumi wetu, tunatakiwa kulivalia njuga kulipiga vita suala hili. Wale wote wahusika wasakwe, vituo vya mafutaa ya taa vifutwe katika vituo vya mafuta mengine visiwe pamoja.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kurejesha usafiri wa Reli ya kati toka Dar es Salaam hadi Tabora - Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba ari, nguvu na kasi ziongezwe ili pia reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza ianze kufanya kazi. Wananchi wana hamu sana kuona shirika lao linafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuitafuta asilimia 50 ya sehemu yoyote hapa nchini tunataka pia barabara ziitwe majina ya wanawake viongozi maarufu nchini kupewa heshima hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, hongera sana naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya kuweka lami barabara ya Iringa – *Ruaha National Park* yanaanzaje katika bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, nashauri barabara nyingine itengenezwe kwa kiwango cha lami toka Izazi, Mbolimboli, Pawapa, Mlowa na kuunganisha na barabara ya *Ruaha National Park*. Lengo ni kwamba watalii wanaotoka Kenya kwenda Ruaha isiwe lazima kupitia Iringa Mjini. Ni barabara muhimu sana, inaunganisha Jimbo langu lote na imepunguza umbali toka Dodoma kwenda *Ruaha National Park* bila kupitia Iringa mjini kwa kilomita zaidi ya 75.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, miundombinu ni sawa na mishipa ya damu katika miili yetu ambayo kimsingi inatupa uhai. Miundombinu ni nyenzo muhimu mno kwa maendeleo yetu. Bila miundombinu hakuna mawasiliano na bila mawasiliano tutaishi kisiwani peke yetu bila kujua wenzetu wanafanya nini. Tanzania ni nchi iliyojaliwa kuwa na bandari zinazosaidia katika si tu kuongeza kipato, lakini kusafirisha wananchi.

Tanzania vile vile imezungukwa na nchi sita zisizo na lango la bandari/bahari. Hali hii ingefanya Tanzania kuwa na pato kubwa sana kama ingeboresha reli ya kati na ile ya *TAZARA*. Hili limekuwa ni tatizo kwa mizigo mizito inayoingia katika bandari zetu, haiwezei kusafirishwa kwa njia nyingine zaidi ya reli. Tunajua nchi kama Zambia ina madini ya Shaba *(Copper)* ambayo ni mazito, hivyo reli zetu zingeweza kufaidika na zao hilo.

Mheshimiwa Spika, wakati wenzetu wa Singapore wameweza kusafirisha *(handling) 470 million TEU* kwa mwaka, Tanzania ni *seven milliom TEU*. Hii ni aibu hasa ikizingatiwa kuwa Singapore inategemea tu bandari yake kama rasilimali pekee na *oil refinery*, kwa bandari zetu pekee tungeweza kuinua pato la Taifa na kupunguza utegemezi wa wafadhili hasa kwa bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Msongamano Dar es Salaam ni jambo la kushangaza kuona Dar es Salaam inayoingizia nchi/Taifa zaidi ya asilimia 70 ya pato la Taifa inashindwa kusaidiwa na Serikali kuongeza pato hilo na badala yake kulishusha. Hii inatokana na msongamano mkubwa wa magari hali inayopelekea wafanyakazi wajasiriamali na kadhalika kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi mfano watu hutumia zaidi ya masaa matatu kufika kazini kutoka Tegeta hadi mjini ni kasheshe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilijua wazi haya yatatokea lakini wamekaa kimya, na jambo la kusikitisha ni mfumo wa barabara tatu ambao niliupinga ila kama kawaida tuliambiwa hata ulaya zipo. Swali ni je mbona sasa barabara tatu hazipo tena? Utaratibu huo sio tu ulisababisha ajali, bali pia uliongeza msongamano.

Mheshimiwa Spika, maamini mpango wa kuhamisha Makao Makuu kuja Dodoma ulikuwa na mantiki ya kupunguza msongamano Dar es Salaam, bado hapajakuwa na utashi wa kisiasa kuhamia Dodoma, kwani tunaona nyumba za Serikali zikiendelea kujengwa Dar es Salaam kama Brazil/Nigeria na Malawi wameweza, sisi tunashindwa nini? Nashauri viongozi wakuu wa nchi hii wahamie Dodoma, wengine wote watafuata.

Mheshimiwa Spika, nyumba nyingi sana za Serikali zinapojengwa na kukodishwa kwa watumishi wapangaji imekuwa ni tatizo kubwa kukarabatiwa, mfano mzuri ni nyumba za Dodoma *Site I Area D,* ni matatizo na balaa kubwa. Nyumba hukarabatiwa pale tu mpangaji anapohama mbali na hapo utakaa miaka! Utaripoti tatizo na wahusika hawaji, lakini ukichelewesha kodi utafuatiliwa kiasi cha kukerwa.

Tunaomba Serikali kupitia wakala wake wafuatilie kujua nyumba zao zilivyo na kufanya ukarabati kwa wakati kwani usipoziba ufa, utajenga ukuta.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena kupongeza hotuba yako na wafanyakazi wako wote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi mambo muhimu ili niyape uzito wake. Tatizo la Fidia kwa wananchi wa barabara ya Kilwa Road na tatizo la ujenzi wa barabara ya *Davis Corner* hadi *Jet Club.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la barabara ya *Kilwa Road,* wananchi wa *Kilwa Road* walifungua kesi mwaka 2004. Tarehe 15 Aprili, 2008 Mahakama ikaamuru wananchi hao walipwe fidia zao kutokana na ujenzi wa *Kilwa Road*, lakini hadi leo wananchi hao hawajalipwa. Kwa kuwa tatizo hilo Wizara inalijua, namwomba Mheshimiwa Waziri wananchi hao walipwe fidia zao ili kukinusuru Chama na mimi Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali pamoja na wananchi wa Temeke kwa kutujengea barabara ya *Davis Corner* hadi *Jet Club.* Pia tunashukuru sana kwa kuitembelea barabara hiyo. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Serikali iharakishe kulipa fidia kwa wananchi ambao mali zao na nyumba zao zinatakiwa zipishe ujenzi wa barabara kwa kuwa mambo haya tayari yapo Wizarani kwake. Kwa hiyo, tunamwomba yaharakishwe ili kupisha ujenzi wa awamu nyingine. Wananchi wa Temeke wanamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwajengea barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunamwombea Mheshimiwa Waziri afya njema, familia yake, Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara yake.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri. Nimesimama kuunga mkono hoja ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nimesimama tena kuishukuru Serikali kutupatia Mkoa wa Njombe na Wilaya ya Wanging'ombe. Tunapenda kuahidi kuwa tutajitahidi kutimiza wajibu wetu ili kukidhi lengo la Serikali la kuunda Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Njombe utakuwa katikati ya Mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Mbeya na Iringa. Barabara za kuunga ni Mkoa wa Njombe na Mikoa hii.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya maendeleo ya Mkoa wa Njombe, tunaomba Wizara hii ipange kujenga barabara zifuatazo:-

Barabara ya Njombe – Taweta kupitia Lupembe C, *Kilombero Valley* naomba iwe barabara ya Mkoa. Mlimba – Taweta (R), Kibena – Lupembe (R) na Lupembe – Taweta?

Barabara itaunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro na pia kuhamishia wakulima katika bonde la …. Tunaomba barabara ya Kibena – Lupembe iwe barabara ya lami, kwa sababu ya mizigo na magari mengi.

Nyingine ni barabara ya Madaba – Mlangali – Lupila – Tandala – Iwawa – Kitulo – Isonji *(Livingstone)* na Ruvuma – Njombe – Mbeya.

Mheshimiwa Spika, bandari zetu ni mgodi usioondosheka au kumalizika. Kwa hiyo, tuharakishe ujenzi wa barabara za muungano na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Njombe hujishughulisha na shughuli za mbao, viazi, mahindi, pareto, matunda, Mikutano, michezo na utalii.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa - Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza pia Naibu Waziri - Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka minne na nusu iliyopita Wizara hii imekumbana na uharibifu mkubwa wa mindombinu uliotokana na mafuriko yaliyotokea mwaka hadi mwaka, lakini Mheshimiwa Waziri Dr. Shukuru na timu yake walijipanga ipasavyo kukabiliana na hali hiyo pamoja na ufinyu wa bajeti. Nawapongeza kwa mafanikio makubwa waliyoyafikia.

Mheshimiwa Spika, nawapa pongezai wafanyakazi wa Wizara hii wote, kipekee kabisa pamoja na wanajeshi wa JWTZ kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa ustadi mkubwa wa kuijenga reli iliyosombwa na mafuriko katika Wilaya ya Kilosa na Mpwapwa katika kipindi kifupi.

Ujenzi huu umenusuru uchumi wetu kuporomoka vibaya zaidi kuliko ambavyo ungekuwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mikumi na kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kilosa, kwa ujumla tunaipongeza Wizara hii na wote walioshirikiana na kurejesha usafiri wa reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, dalili ziko wazi kwa Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu, imejitahidi sana kutekeleza ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu mradi wa usanifu na ujenzi wa barabara ya Korogwe – Handeni – Kilosa – Mikumi, hususani kipande cha Kilosa – Mikumi umefika hatua gani? Ni lini ujenzi wa kipande hiki chenye urefu wa kilomita 78 utaanza? Utagharimu shilingi ngapi na unakaribia kuchukua muda gani kukamilika? (ibara ya 44 wa ilani ya CCM, uk 53 na 54).

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha hoja yake awajulishe wananchi wa kata za Wilaya na Zombo iwapo madaraja ya Mto Miyombo ambayo yataunganisha mabonde makubwa ya walishaji mazao na barabara kuu mpya itakayojengwa yamesanifiwa na kujumuisha katika gharama za mradi mzima kama ilivyoombwa toka awali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo fununu kwamba baada ya barabara ya kutoka mikumi kupitia Kilosa, Kimamba hadi Melela kukamilika kwa kiwango cha lami. Barabara kuu ya mkato kutoka Melela kupitia Doma hadi Mikumi itatumika kwa magari yatakayolipa ushuru mdogo wa barabara. Je, hii ni kweli ? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara itokayo Mpwapwa kupitia Kinasi, Malolo, hadi Ruaha, Mbuyuni inaunganisha Wilaya za Mpwapwa Kilosa na Kilolo katika mabonde makubwa yanayozalisha vyakula mazao kwa wingi: Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa kwa vigezo hivi ni bora barabara hii ingewekwa katika kundi la kuhudumiwa na *TANROAD* hasa ukizingatia uimarishaji wa miundombinu itakayochochea ufanisi wa usafiri wa mazao chini ya utekelezaji wa miradi chini ya mpango wa Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Spika, mwisho, Waziri asilipuuzie wazo lililokwishatolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuwa pajengwe *dry port* kubwa ya kimataifa Ruvu ili kuibua matumizi ya bandari ya pili ya Tanga (baada ya kupanua huduma zake) ili kupunguza msongamano wa mizigo mingi Dar es Salaam na kupunguza *Dwel time* bandarini ya meli ya mizigo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na bajeti ya miundombinu iongezwe kwani ndio mtandao namba moja wa kukuza uchumi.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kutamka rasmi kwamba naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa ya Wizara hii, napenda kuchangia yafuatayo:-

Kwanza naipongeza sana *TANROAD* Mkoa wa Tanga kwa kazi nzuri inayofanya kwa kutengeneza Mkoa wa Tanga. Naipongeza *TANROAD* Makao Makuu kwa kufanya kazi nzuri nchi nzima. Napongeza Wizara kwa kunipatia kilomita tatu za lami Korongwe mjini. Kitendo hiki kimeweza kuipa hadhi Halmashari ya mji wa Korongwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri hayo, Mkoa wa Tanga na Korogwe tunazo kero zifuatazo :- Barabara ya kutoka Segera, Korogwe, Mombo, Same, himo inahitaji marekebisho makubwa. Hali ya mashimo ikiachiwa ilivyo sasa, barabara hiyo haitapitika kabisa. Jambo hili linahitaji udharura wa haraka.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kufahamishwa ni lini barabara ya *Old Korogwe* – Mashewa – Maramba hadi Mabokweni itatengenezwa kwa kiwango cha lami ili kuwepo ahadi kwamba barabara hii ndio mbadala wa kufikia Tanga hadi Korogwe iwapo itatokea dharura yoyote?

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi zinakufa kwa kukosa mifereji. Je, Wizara ina mikakati gani ya kulishughulikia suala la mifereji? Mimi ninaamini iwapo suala la mifereji litakuwa kama ajenda ya kudumu katika Halmashauri zote, barabara zetu zitapona.

Mheshimiwa Spika, kutokana na barabara mbovu ni ya Korogwe – Handeni pamoja na kuomba barabara hiyo kuwekwa lami, lakini sasa hivi inapitika kwa shida sana. Ninaomba juhudi za makusudi zifanyike ili barabara hiyo ipitike kwa wakati huu huku suala la wakandarasi likiwa linaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutoa hongera na pongezi nyingi kwa Wizara na *TANROAD*.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri - Mheshimiwa Chibulunje kwa kazi nzuri katika Wizara yao. Nawapongeza pia Watendaji Wakuu wa Wizara hii bila ya kumsahau Meneja wetu wa *Tanroads* Ruvuma Ndugu Kisumbo.

Mheshimiwa Spika, awali, Mkoa wa Ruvuma tuliwahi kupokea *riport* ya *Tanroads with reservation* ya barabara ambazo hatukuridhika nazo, lakini kwa sasa kwa kweli tunaiona ile *value for money*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, meli zinazotembea katika Ziwa Nyasa ziondolewe kutoka Hazina na ziondolewe katika mnada *(Specification)* na badala yake ziunganishwe na mamlaka ya Bandari ili sehemu ya faida hiyo itumike kuendesha meli hizo kama kichocheo cha uchumi katika Mikoa ya Kusini na vilevile itasadia kufanya kazi kwa karibu zaidi ukilinganisha na Bandari ya Mtwara/*Mtwara Corridor*. Meli ya *MV Songea* iko *service,* lakini nimeambiwa imedaiwa karibu shilingi bilioni 18 ili iweze kupata vipuri. Tunaomba isaidiwe ili *gate* za uchumi kusini zifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kutusikiliza, barabara ya Kipepe – Matuta – Mango – Kihagura ila pesa hizo zitumiwe mapema kabla ya mvua.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mbababay – kituli imepewa bajeti ndogo sana kuliko uhalisia wake. Mwaka ujao mlione hilo, kwani hiyo ndiyo barabara kuu ya Wilaya ya Ziwa Nyasa na ya mpakani muhimu.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa harufu ya barabara za lami Peramiho – Mbinga – Songea – Namtumbo na hatimaye Tunduru.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. EPHRAIM NEHEMIA MADEJE:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa hotuba nzuri na utendaji unaoridhisha.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwamba, wizara ijihusishe na upangaji, usanifu na ujenzi wa barabara katika Miji Mikuu ili kuepukana na mpangilio mbovu uliopo karibu kila mahali hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, wizara ihakikishe kunakuwepo mipango ya muda mrefu ya barabara kwenye miji yote ili kuepukana na msongamano wa vyombo vya usafiri kama ilivyo Dar es Salaam hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Barabara ya Dodoma - Iringa uanzie pande zote mbili, yaani mkandarasi mmoja aanzie Dodoma na mwingine aanzie Iringa.

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu, Engineer Chambo, pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Wizara hii kwamba, pamoja na hali ngumu ya uchumi, kwa mafanikio makubwa sana imeweza kujenga miundombinu mingi pamoja na kukarabati miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mkinga inafaidika sana na kazi nzuri ya Wizara hii. Takriban barabara zote za Halmashauri na za Kitaifa chini ya TANROADS zimekuwa zikipata matunzo mazuri na matengenezo mapya. Jambo la faraja kubwa ni pale Mheshimiwa Rais alipoliweka jiwe la msingi ujenzi wa Barabara ya Tanga – Horohoro na zaidi ya hilo, Mheshimiwa Rais kutoa idhini yake kwamba fidia ya kifuta

machozi itolewe kwa wale wote waliovunja nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara na hata wale waliovunja nyumba zao kwa kutii amri.

Mheshimiwa Spika, Wanamkinga tumefarijika sana kwa Barabara ya Mabokweni – Bombo Mtoni kwa utaratibu wa PMMR. Hata hivyo, ipo haja kubwa ya kuwafuatilia kwa makini wakandarasi chini ya PMMR ili wajenge na kutunza barabara kama inavyotarajiwa kimkataba.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunapata faraja kubwa kwa serikali kukubali kujengwa na kuipatia fedha ujenzi wa Barabara ya Kasera – Maramba kupitia Magodi, Mbambakofi na Mwele. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa barabara hii kiutawala na kiuchumi, nashauri barabara hii iongezewe fedha ili ujenzi wake uweze kukamilishwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa bandari mpya ya Tanga (Mwambani) na Reli ya Tanga – Musoma, kwa muda mrefu, jibu la serikali limekuwa uandaaji wa upembuzi yakinifu na usanifu bila kutoa uhakika wa lini hasa ujenzi unatarajiwa kuanza. Hali hii ni ya hatari kwa kuzingatia kuanza kwa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na hatua zinazochukuliwa na majirani zetu, kuboresha Bandari ya Mombasa na ujenzi wa Kiwanja kikubwa cha ndege maeneo ya Lamu. Tukumbuke nasaha za wahenga kwamba, "chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako." Ni muhimu sana kuharakisha uboreshaji wa miundombinu hii na mengineyo kama reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. MOHAMMED SAID SINANI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Wataalam wake kwa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuchangia hoja hii katika jambo moja kubwa nalo ni ujenzi wa miji kandokando ya barabara zetu kuu na ujenzi wa matuta ya barabarani.

Mheshimiwa Spika, ingawa Wizara imetenga na kuweka nguzo za mipaka ya barabara kuonesha mipaka ya barabara hizo, mimi naona kiasi kilichotengwa hakitoshi.

Mheshimiwa Spika, naishauri serikali iongeze mipaka hiyo walau mita 500 kutoka pande zote za barabara. Hatua hii itasaidida kwa kiwango kikubwa kupunguza ajali za barabarani na usumbufu wanaoupata madereva.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara inalazimika kujenga matuta ya kupunguza mwendo kila eneo la miji inayojengwa kandokando ya barabara. Baada ya muda si mrefu, miji hii itafika hadi Mwanza kutoka Dar es Salaam na hivyo hivyo kutapakaa kandakando ya barabara zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, athari nyingi ambazo zitatokea hapo baadae ni kwamba, serikali italazimika kulipa fidia za majengo yote ambayo yapo maeneo hayo iwapo itahitaji kujenga barabara nyingine sambamba na barabara iliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, tunashuhudia nguzo za umeme, viwanda, *petrol stations,* mkongo wa simu na kadhalika, kujengwa kandokando ya barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kuishauri serikali ichukue hatua madhubuti juu ya suala hili ambalo litaisumbua serikali kwa kiwango kikubwa hapo baadae.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Chimbuko la Uhuru nchi hii lilianza kwenye Barabara ya Kichwele ambayo sasa ni Uhuru – Ilala; je, kuna mpango gani wa kuifanya barabara hii iwe na hadhi ya Uhuru wa nchi hii?

Mheshimiwa Spika, serikali imefanya *audit* ya gharama za kutengeneza barabara mpya za lami, kutenganisha na nchi jirani, zipo taarifa nchi za jirani gharama huwa ndogo; kwa nini serikali inakuwa na kigugumizi kwenye kujenga barabara kwa mtindo wa *PPP* na *Road Toll* ikatozwa? Serikali inabeba mzigo mkubwa sana bila sababu kwa kujenga barabara yenyewe.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshiimia Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine wote wa Wizara, kwa kazi nzuri na za kutukuka wanazozifanya kila siku.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuipandisha Barabara ya Kiomboi – Kisiriri – Kidaru – Ibaga – Mkalalama – Matongo – Nkunto – Mwangeza – Dominiki – Kidarafa kutoka Barabara ya Wilaya hadi kuwa Barabara ya Mkoa na sasa hivi makandarasi watatu wako kwenye Barabara hiyo wanafanya kazi nzuri sana. Napongeza kupitia *Road Fund* kwa kutupatia Sh. 500,000,000 kwa Barabara ya Iguguno – Kitumbili – Lyelambo – Yulansomi hadi Msungi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana serikali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti. Pia napongeza sana kwa kuipandisha Barabara ya kutoka Shinyanga – Mwamizi (Meatu) – Sibiti (Iramba Mashariki) kwenda Arusha kupitia Mbulu kuwa Barabara ya Kimataifa. Huu ni ukombozi mkubwa sana wa kukuza uchumi kati ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa, nchi jirani Kanda za Kaskazini (Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Mkoa wa Tanga).

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana serikali kwa kukubali kujenga kwa lami barabara inayoingia Mji Mdogo wa Iguguno na kutokezea upande wa pili. Nashukuru sana kwa ahadi ya kumalizia kipande cha pili kuweka lami ili barabara yote inayoingia na kutoka Iguguno iwe ya lami, kuwezesha magari makubwa na mabasi kuingia na kutoka upande wa pili wa Iguguno.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuweka lami kipande kilichobaki, naomba sehemu ya kutoka Singida mahali barabara inapoingia Iguguno, kona iliyopo ni kali sana, pia

upande wa pili wa kutokea au kuingilia ukitokea Nzega. Kwa vile Wizara inasikiliza na kutekeleza maombi ya Wananchi kupitia kwa Wabunge, kazi hii itatekelezwa mapema.

Mheshimiwa Spika, kwenye Barabara ya Nduguti Gumanga pale Mto Kamulungu na Mto Gumanga miaka yote kuna *drifts*. Mito hiyo ni hatari sana, naomba sasa yajengwe madaraja.

Mheshimiwa Spika, kwenye Barabara ya Iguguno - Kinyangiri eneo la Mwembe mpaka leo hapo mahali wakati wa mvua huwa panakatika kwa sababu maji ni mengi sana na kuna *drifts* mbili; naomba painuliwe na pajengwe madaraja makubwa ya kudumu.

**MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote pamoja na Wafanyakazi katika Wizara, kwa kazi kubwa na ya kuridhisha mnayofanya. Ninayo maoni au maombi yafuatayo:-

- Tulifanye shirika letu la ndege lifanye kazi vizuri katika nchi yetu.

- Mtandao wa reli uimarishwe na uongezwe maana huu ni usafiri ulio rahisi na unachukua mizigo mingi. Tunapoongelea Kilimo Kwanza, jambo hili ni muhimu.

- Ni vyema Mikoa ya Iringa, Mtwara, Ruvuma na Rukwa ikaunganishwa kwa reli. Tuanze sasa kuiweka katika mpango.

Mheshimiwa Spika, ni wazi Mkoa wa Ruvuma uko mbali toka Dar es Salaam, wawekezaji wanayo hamu kubwa ya kutaka kufika Ruvuma na hasa Mbinga lakini umbali ni kikwazo. Naomba Wizara iyashawishi mashirika ya ndege nchini yaanze usafiri wa anga Dar es Salaam – Iringa – Songea – Mbeya – Mtwara. Hii itasaidia na itaokoa sana muda hata kwa Watumishi wa Serikali, Wabunge na Wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kigonsera – Matiri – Mbaha, siku zote matengenezo yanaishia Kilindi tu, Mbaha ni hadithi tu. Wataalam wanasema ni vigumu kupita mpaka Mbaha labda kuichepusha; tufanye hivyo ili Wananchi wasione kuwa wanadanganywa.

Mheshimiwa Spika, nafahamu juhudi za serikali za kuweka lami Mbinga – Mbambabay kwa vile Barabara ya Nyoni – Mkiha ni eneo la wakulima wazuri wa kahawa. Napendekeza sasa serikali ianze kutafuta fedha za kuweka lami kipindi hiki, pia kuokoa uzalishaji mkubwa ulioko katika maeneo hayo. Napongeza sana juhudi za Tanroad (R) kuiboresha barabara hii.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia serikali ifikirie kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Kitai – Ruanda – Lituhi – Mbambabay kwa sababu ni barabara ya ulinzi lakini pia kwa kuwa mkaa wa mawe uliopo Ruanda utaanza kuvunwa hivi karibuni, barabara hii itakuwa inatumika na magari makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa Mji wa Mbinga unakua kwa kasi kubwa sana, naomba mipango ya ujenzi wa kiwanja cha ndege ili kuimarisha utalii katika Mkoa wa Ruvuma.

**MHE. DR. ABDALLAH OMARI KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali kwa kuendelea kuiboresha kwa kiwango cha lami Barabara ya Mkata – Handeni, Korogwe – Handeni na ile ya Magole – Turiani. Kama mwakilishi wa Jimbo, ujenzi unaendelea vizuri. Aidha, niipongeze serikali kwa uamuzi wa kuifanyia ufembuzi yakinifu kwa kiwango cha lami Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto – Kondoa. Barabara hii itakuwa ni lango kuu kwa uchumi kati ya maeneo ya *East* na *West* ya nchi hususan kutoka Tanga.

Mheshimiwa Spika, tunaomba fedha za fidia kwa wananchi kwa Barabara ya Korogwe – Handeni na Handeni – Mkata itolewe/ilipwe ili taratibu za ujenzi ziendelee kwa kasi kubwa kuliko ya sasa.

Mheshimiwa Spika, wakati tukisubiri fedha, serikali iongee na mkandarasi, jukumu zima la kuboresha sehemu korofi kati ya Korogwe na Handeni, ili barabara iendelee kutumika kusaidia shughuli kubwa za kiuchumi na kijamii kwa eneo la Handeni.

Mheshimiwa Spika, fedha za Korogwe – Handeni na Handeni – Mkata zitolewe ili ujenzi uendelee kwa ratiba.

Naunga mkono hoja na nawaombea Waziri na Naibu Waziri kila la heri hususan katika kipindi hiki tunachoelekea.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia sehemu mbili tu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Tabora kilio kikubwa kwa Wananchi ni barabara. Tabora – Kigoma, Itigi – Tabora, Nzega – Tabora – Sikonge Mpanda. Kwa maana hiyo, naomba Waziri awaeleze Wananchi leo hii Bungeni kuhusu barabara hizo. Waziri Mkuu alifika Tabora na kuhakikisha barabara itajengwa. Mheshimiwa Rais pia alifika na kuahidi kuwa barabara itajengwa. Naomba leo uwaeleze Wananchi ujenzi huo utaanza lini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mizani; hivi Mtanzania mmoja anahitajika kuwa na kilo ngapi kwa sababu kwenye mabasi tunayopanda hupita kwenye mizani na huonekana uzito umezidi pamoja na kuwa abiria wote wamekaa hakuna waliosimama?

Mheshimiwa Spika, pia abiria hubaki na shida kuambiwa mizigo yao iwe na kilo 20 tu, wakati una mtoto. Sisi abiria wa mabasi tunajua, tunapata tabu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi kwa hili ndipo niunge mkono hoja.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu wa Wizara, Meneja wetu wa TANROADS, Singida na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo imeainisha vizuri vipaumbele vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, amekuwa makini na mwadilifu katika kusimama Wizara hii, ninamwombea Mwenyezi Mungu, yeye binafsi pamoja na Naibu Waziri wake, wapiga kura wawape kura za kishindo ili warudi kuendeleza majukumu yao. Vile vile nimemtaja Meneja wa TANROADS, ameingia Mkoani Singida, kweli utendaji wake katika kufuatilia utendaji wa barabara kwa wakondarasi umekuwa wa kiwango cha juu hata panapotokea eneo korofi hasa wakati wa masika hushughulika haraka, hajali uongozi mzima wa Mkoa wa Singida. Wananchi tunajivunia sana, tunaomba serikali isije kumhamisha mapema.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza sana serikali kwa kazi kubwa iliyofanya kwa kujenga Reli ya Manyoni hadi Singida. Vile vile ninaishukuru serikali kwa kuvunja mkataba wa mwekezaji aliyekuwa anaendesha Reli ya Kati pamoja na Reli ya Manyoni hadi Singida, kwani mwekezaji alishindwa kutoa huduma hii vyema. Hivyo, napenda kuomba serikali ifanye yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, serikali ihakikishe inavyorudisha magenge ya kwenye njia ya reli kwani yalikuwa yanasaidia sana kulinda reli na kufanya ukarabati pale palipoharibika na kutoa taarifa mapema. Vile vile magenge yalisaidia kutoa ajira kwa vijana na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, serikali ihakikishe reli hii ya Manyoni hadi Singida iwe na behewa la daraja la pili ili wale wenye uwezo waweze kupanda wakiwemo viongozi mbalimbali na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba serikali iweke mabehewa ya mizigo pamoja na behewa la mifugo ili kuwarahisisishia wafanyabiashara wa Singida na mikoa jirani kusafirisha bidhaa zao pamoja na mifugo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri serikali itamke lini reli hii sasa itaanza kazi baada ya serikali kuwaondoa wawekezaji utamkwe muda.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza serikali kwa kukubali kuzipandisha daraja barabara zifuatazo kuwa barabara za Mkoa. Barabara hizo ni Barabara ya Kiomboi – Kisiriri – Mkalama hadi Kidarafa (Iramba); Barabara ya Singida Mjini – Mgungira – Iyumbu (Singida Vijijini); na Barabara ya Sibiti – Matala (Km 15).

Mheshimiwa Spika, nipende kuikumbusha serikali kuwa, barabara hizi tangu zimepandishwa daraja kuwa za mkoa, hazijawahi kutengewa fedha. Hivyo, ninaomba nipewe majibu endapo zimetengewa fedha kupitia bajeti hii ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ahadi yake ya kujenga Daraja la Sibiti katika utekelezaji wake kupitia Ilani ya Uchaguzi. Napenda kufahamu kama fedha za kujenga reli hii kupitia bajeti hii zimetengwa? Nitashukuru kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, akinipa majibu wakati akijibu hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuikumbusha serikali, ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete ya kujenga barabara inayoingia Iguguno kutokea Mwanza, yenye urefu wa kilometa 2.5 kwa kiwango cha lami. Kwa kuwa muda wa Awamu ya Nne (miaka mitano ya kwanza), unakwisha; je, kupitia bajeti hii kuna fedha zilizotengwa kwa kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami? Nasubiri majibu ya serikali.

Mheshimiwa Spika, nimeona ni vyema kuikumbusha serikali ahadi ya Mheshimiwa Magufuli na Mheshimiwa Waziri Mkuu, juu ya kujenga barabara ya kuingia Manyoni Mjini na kutoka kuelekea Singida kwa kiwango cha reli, endapo fedha zake zimetengwa kwani muda wa ahadi ndiyo unaishia bajeti hii ya 2010/2011. Nitashukuru Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri akitamka neno katika ahadi hii.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza serikali kwa ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Singida Mjini ingawa bado hakina lami kwenye *Running Way*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Singida inakua kwa kasi sana na mkoa huu sasa barabara zake kuu zote zitakuwa kwa kiwango cha lami; ni wazi kuwa wawekezaji watamiminika kuja kuwekeza Singida tu. Hivyo basi, ninaiomba serikali ijenge kiwanja kikubwa cha Kimataifa ili ndege za biashara zitue Singida, kwani siku hizi hata usafiri wa anga ajali zinapatikana mara kwa mara, hata hali ya hewa kuharibika angani ndege kushindwa kuendelea na safari au kushindwa kutua ni rahisi kurudi kutua Singida kwani Singida ni mkoa ulioko katikati.

Mheshimiwa Spika, sina maana kwamba, fedha zitengwe kupitia bajeti hii, bali lengo langu ni kwamba, wazo hili la Mkoa wa Singida chini ya Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Dkt. Parseko Kone na Viongozi wote wa Mkoa kwa niaba ya Wananchi. Nitashukuru endapo Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, atapokea ombi hili.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kushukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri katika kuendeleza miundombinu.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Barabara ya Kagoma – Muleba – Kyamyorwa – Kasindaga – Biharamulo – Lusahunga, ujenzi wake unaendelea vizuri baada ya kubadilisha mkandarasi. Tunazo taarifa kuwa, ujenzi katika Pori la Burigi (kuanzia

Kasingaga hadi Biharamulo), unacheleweshwa, nahitaji tathmini ya mazingira *(Evironmental Ipact Asessment).* Je, nani anawajibika kwa ucheleweshaji huu? Kwa nini pori liwe na thamani kuliko manufaa yatokanayo na barabara ya lami? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Muleba – Nshamba – Kamachumu – Muhutwe ni muhimu sana. Nashukuru fedha imetengwa kwa ajili ya madaraja ingawa inaonekana kuwa kidogo. Namshukuru Meneja wa Barabara wa Mkoa, Daraja la Malahala limekamilika, lakini Madaraja ya Mugugu na Lwanjelu, karavati nyingi kati ya Nshamba na Kamachumu zinahitaji kujengwa upya haraka. Hasa eneo la Mugugu kwa sasa linapitika kwa shida sana baada ya kuharibiwa na mvua. Je, eneo hilo litarekebishwa haraka?

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Muleba Kusini halina magati pamoja na ahadi ya muda mrefu; je, lini gati litajengwa Katunguru, Kyofa na Nyakabango?

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Wizara na Serikali kwa ujumla kwa ujenzi na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Bukoba. Kwa niaba ya Wananchi, napenda kujua lini awamu ya kuweka lami itatekelezwa? Bukoba inapata mvua nyingi sana kwa mwaka, kwa hiyo, kuweka lami na kurefusha uwanja ni muhimu sana. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa barua yake nzuri kuhusu utaratibu wa kupandisha daraja Barabara za Kimeya – Mubunda – Nshamba; Kimeya – Mubunda – Kibanga – Kamishango - Ikondo – Luhanga; na Kimeya – Mubunda – Burungura – Rushwa.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kupandisha daraja baraba hizi ni kutokana na umuhimu wa kiusalama. Iwapo barabara kuu inayopita Mulemba Mjini itafungwa kwa sababu yoyote ile, magari yatakwama. Aidha, itakuwa ni kuunganisha Barabara za Mkoa za Kasindaga – Kimeya na Muleba – Nshamba – Kamachumu – Muhutwe. Tayari nimeongeza msukumo nikishirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba. Tunategemea ushirikiano wenu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atufikishie shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwa kufuatilia kwa karibu Barabara ya Kagoma – Muleba – Biharamulo – Lusanga na Uwanja wa Ndege wa Bukoba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, licha ya changamoto nyingi sana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nitoe masikitiko makubwa kwa Wizara kushindwa kuiwekea lami Barabara ya Tarime – Nyamwaga mara kwa mara kuliko kuweka kilomita moja kila mwaka. Ina maana kuwa, serikali itachukua zaidi ya miaka arobaini kukamilisha.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu serikali imetenga shilingi ngapi kwa Barabara hii ya Tarime – Nyamwaga? Je, serikali inakubalina nami kuwa kuna umuhimu wa kuiwekea lami barabara kwa mara moja ili ikamilike kwa wakati mmoja?

Mheshimiwa Spika, ili barabara zetu ziwe imara na za kudumu kwa muda mrefu ni lazima serikali iimarishe usafiri wa mizigo kwa kutumia njia ya reli, tunaweza tukawa na barabara nzuri lakini zitaharibika haraka kama mizigo yote itasafirishwa kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Spika, serikali imekuwa inaingia mikataba ambayo haina manufaa kwa nchi. Kwa mfano, Mkataba wa Serikali na Kampuni ya RITES ya India, Kampuni hii ilishindwa kufanya kazi licha ya Waheshimiwa Wabunge kuipigia kelele hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Naishauri serikali ifanye mabadiliko/maamuzi ya haraka ili kuepusha Taifa kupata hasara.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa Dar es Salaam ni shida sana, foleni ya magari ni kero sana kwa wananchi hasa wafanyakazi, wafanyabiashara na wanafunzi. Naishauri serikali kwa kuangalia foleni ya magari katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Arusha ili kuepusha foleni ndefu barabarani. Taifa (nchi), inapata hasara inayosababishwa na foleni barabarani.

Mheshimiwa Spika, serikali imeshindwa kulisimamia Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL).* Shirika linaendeshwa kwa hasara; ni aibu kwa nchi kutokuwa na usafiri wa anga ambao ni imara. Naishauri serikali iwe na shirika la ndege imara, lenye wafanyakazi wenye hekima, busara na wenye uzalendo. Pili, serikali inunue ndege za kutosha angalau hata tano ili tuweze kuimarisha usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, naishukuru serikali kwa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere. Serikali isimamie Mradi huu kwa karibu ili ukamilike kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naishauri serikali ipange na igawe kwa uwiano utaratibu wa kujenga na kukarabati barabara bila ubaguzi wa kimkoa wala itikadi ya chama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii.

**MHE. TATU MUSSA NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya kina kuhusu ujenzi wa barabara kati ya Itigi – Chaya – Kalongosi, Turo – Kizengi – Kigwe hadi Tabora. Kitabu hiki kinaeleza tu ujenzi wa barabara ya kutoka Tabora kupitia Urambo hadi Kaliua.

Mheshimiwa Spika, hii ina maana wanaokwenda Kigoma hawana haja ya kupitia Itigi – Tabora kwa kuwa Barabara ya Tabora – Nzega imo kwenye mpango wa ujenzi wa

lami, basi watu wanaokaa kati ya Itigi – Tabora watajua wenyewe au barabara hiyo iwekewe changarawe basi inatosha.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya kina yanayohusu ujenzi wa barabara hii ya Itigi – Tabora.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa *TANROADS,* watendaji wote wa Wizara na wahandisi wa mkoa wa Tanga kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa mchango wangu na kupata ufafanuzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya *PMMR East* na *West;* barabara zilizopo katika mpango huu Wilaya ya Muheza ni Pangani – Mkuza – Muheza na Muheza – Amani (Kibaoni). Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ukarabati wa barabara hizo? Katika kiambatanisho 5A ukurasa 184 inaonyesha hakuna mchango kwa wahisani kwa kuwa sasa mvua zimepugua na lini mkandarasi, *Y. N. Investment* ataanza ukarabati Muheza – Amani eneo ambalo limeharibika sana? Mapendekezo yafuatayo narudia kuomba yatekelezwe.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mlimani Amani kutoka eneo la Kituo cha Polisi Amani hadi Kibaoni magari ya mizigo yamekuwa yakihangaika mara kwa mara katika eneo hili. Eneo limejaa mawe makubwa na kona kali, eneo hili litapona tu kwa kuwekwa zege, tunaomba eneo hilo lianze na kufuatiwa na zege katika kona kali nyingine tatu zilizobaki kati ya kituo cha polisi cha Amani.

Mheshimiwa Spika, eneo la Muheza Mjini, eneo la mjini lipo daraja na upo mteremko mkali, kwa kuwa daraja ni jembamba tunashauri lijengwe eneo la wapita kwa miguu ili kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mbaramo – Bombani Lunguza, magari makubwa sana yanayobeba magogo kutoka msitu wa Lunguza - Muheza na yale yanayotoka Mkoa wa Morogoro kuleta magogo katika viwanda vya mbao eneo hilo yanachangia sana kuharibu barabara. *TANROADS* na halmashauri ya wilaya ya Muheza zinahitaji kukaa pamoja na kutafuta njia za kuzuia uharibifu huo, kwa kuwa barabara hiyo inasimamiwa na *TANROADS,* basi *TANROADS* itoe mapendekezo kwa halmashauri ya wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuikumbusha Wizara ya Miundombinu kuyakumbuka tena maombi niliyotoa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2009/2010 kuhusu yafuatayo, kwanza, kujenga mfereji upande wa pili wa barabara ya Pangani – Mkuzi, Kilulu - Muheza eneo la kutoka mjini Muheza barabara kuu ya Tanga kuelekea

Benki ya *NMB* -Muheza hadi kuelekea Kilulu nilisema mifereji ilijengwa upande mmoja wa barabara.

Pili, kwa kuwa Muheza imepata hadhi ya kuwa miji mdogo na kuelekea mji mwaka 2010/2011 tunaendelea kuomba lami angalau kilomita 0.5 kuwa eneo la barabara niliyotaka ijengwe mifereji upande wa pili Muheza – Mjini Kilulu hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TANROADS* Mkoa wa Tanga kwa jitihadi zinazoonekana wilayani Muheza na mkoa mzima wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa hotuba nzuri ya Bajeti na mipango mizuri. Ningependa hata hivyo kuchangia yafuatayo kuhusu barabara za Dar es Salaam na jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Spika, kwa anayejua vizuri tatizo la msongamano Dar es Salaam hawezi kuacha kutambua tatizo kubwa la msongamano toka maeneo ya barabara ya Tabata, Mandela kuelekea Buguruni na Tazara. Njia nzuri ya kupunguza msongamano katika njia hizi na kuunganisha barabara ya Mandela kupitia Tabata Dampo hadi barabara ya Kigogo inayojengwa kwa sasa. Barabara ya Kigogo inayojengwa kwa sasa barabara hii ni kilomita 2.25 tu na ilikuwa imepangwa kwenye orodha ya barabara za kupunguza msongamano lakini naona Wizara imeamua kuisahau katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 na pia Bajeti ya mwaka 2010/201. Naomba barabara hii iunganishwe kama mradi mmoja na barabara zinazojengwa sasa hivi za *Ubungo Terminal – Kigogo round about,* na *Kigogo round about* – Msimbazi – Twiga (Jangwani) ili hata hizo barabara zinazojengwa sasa ziwe na tija sana.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine itakayopunguza sana msongamano katika barabara za Tabata, Mandela na Nyerere ni ile ya Vingunguti – Barakuda – Chang'ombe (Segerea) *–Mabibo External.* Daraja la Vingunguti inajengwa lakini Serikali Kuu ingesaidia sasa kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahadi na agizo la Mheshimiwa Rais kwamba *TANROADS* imalize barabara ya lami ya Banana – Kitunda (kilomita 3) sasa imechukua miaka mitatu lakini ujenzi unakwenda taratibu sana (kilomita 0.5 tu kwa mwaka). Naomba ziongezwe fedha mwaka huu wa 2010/2011 ili agizo hili la Mheshimiwa Rais litimizwe mwaka huu kwa kukamilisha kilomita 1.2 iliyobaki fedha zilizowekwa mwaka huu hata kilomita 0.5 haziwezi kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ukonga (Mombasa) – Kitunda - Msongola pia iwekewe mkazo ili kuhudumia maelfu ya wakazi wa Ukonga, Kipunguni B, Kivule, Kitunda na Msongola. Fedha zinazowekwa kila mwaka hazitoshelezi hata kuitisha tenda.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iaze kuweka mkakati wa kurudisha/kujenga reli ya kutoka Mtwara hadi Mchuchuma na

Liganga. Mchuchuma na Liganga ndiko kunakotarajiwa kuchimbwa chuma na makaa ya mawe na iende *Mbambabay.* Suala hili liliwahi kuzungumzwa na Mheshimiwa Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, reli hii itatoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Mtwara sasa inashughulikiwa ambayo itatoa mchango mkubwa katika kusafirisha na kupelekea mizigo ya Tanzania, Malawi na hata Zambia, wenzetu wa China walionyesha dhamira ya kujenga reli hiyo.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na Katibu Mkuu kwa kuleta Bajeti hii wakati mgumu kama huu.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hoja hii naomba kuzungumzia mambo makuu matatu. Kwanza ni kuhusu Daraja la Mkapa katika Mto Rufiji, tumeijenga kwa kutumia fedha nyingi sana kiasi cha shilingi bilioni 35, hizi ni fedha nyingi na daraja hili ndilo mkombozi wa Kusini. Wizara ya Nishati na Madini ina mpango wa kupitisha *high voltage line* chini ya daraja hili. Hii ni hatari kubwa sana kuweka bomu lililojificha wakati wowote kama kuna *short* yoyote basi daraja hili ghali na mkombozi litaangamia, kuweka hizo *power line* ni sawa na kuweka *timed bomb.*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu ikatae kabisa utekelezaji wa mpango wa Wizara ya Nishati na Madini wa kupitisha *power line* zao chini ya mto yaani *underwater cable* ambayo hata Zanzibar tumetumia mpango huo. Iwe marufuku kabisa kutega nyaya hizo chini ya daraja.

Mheshimiwa Spika pili, naipongeza Wizara kwa kufanya kazi nzuri ya kuunganisha mikoa kwa barabara za lami, pamoja na haya nakumbusha juu ya ujenzi wa Daraja la Nangoo, Masasi linalounganisha Kusini na Kaskazini. Je, daraja hili litajengwa lini toka lilivyozolewa na mafuriko ya mwaka 1990. Pia kuna daraja la Nanganga ni lini litakamilika?

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu bandari na reli. Bandari ya Mtwara yenye kina kirefu kuliko vyote Afrika Mashariki haitumiki vyema wala kuwekezwa pamoja na ujenzi wa reli toka Mtwara mpaka Mchuchuma kuchukua makaa ya mawe, tukijenga reli hii tutainua sana uchumi wa nchi yetu na sasa ndio wakati tunapohitaji zaidi maendeleo .

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Miundombinu.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani kwa kupata fursa hii ili nami nichangie kwa maandishi. Kwanza nitoe pongezi kwa hotuba ya Waziri, pia nitoe pongezi kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa idara mbalimbali na watumishi wote katika Wizara hii, kazi kubwa ya miaka mitano ilikuwa sio safari rahisi kwani miinuko, mabonde na milima hadi leo tunaona mambo mazuri, Tanzania kwa upande wa barabara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani za dhati kwa niaba ya wananchi wa Singida na mikoa yote inayotumia barabara ya Dodoma - Singida, kweli tunatambua juhudi za Serikali kufika kutuletea maendeleo Wanasingida pia najua kuna kipande kidogo tu kilichobaki kati ya Manyoni na Mkiwa, tunaomba kusipunguzwe ili tuondokane na wimbo wa barabara ya Manyoni na Singida pamoja na hayo tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Manyoni – Tabora, barabara ya Mbeya - Rungwe, Itigi – Mkiwa hizi ni barabara ambazo zimetajwa sana tangu miaka mitatu iliyopita hivyo tunaomba hatua za awali zionyeshwe na zianze.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Singida – Babati, tunashukuru ilishaanza, ombi tu ni kuhakikisha mkataba unatekelezwa kama ulivyo kwani tatizo la barabara ya Dodoma - Singida lisije likajirudia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na kumpongeza kwa dhati Mkuu wa Mkoa na timu yake kwa kazi nzuri ya kuhakikisha barabara za vijijini Mkoani Singida zinapitika wakati wote hasa shukrani na pongezi hizi zimwendee Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa kwa kusimamia vizuri barabara hizi, ombi langu tu aongezewe fedha ili zile ambazo bado hazijatengenezwa zitengenezwe.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ituongezee fedha za kumaliza barabara ya Misigiri - Kiomboi kwani bado kilomita chache sana natambua kuwa kila mwaka zinatengwa fedha za kilomita tano tu, tunashukuru lakini angalau hizi zilizobaki tunaomba zimaliziwe.

Mheshimiwa Spika, mimi nilipata bahati ya kufanya ziara katika mikoa mingine hadi vijijini kuna mikoa barabara zake zinafurahisha kama Kigoma hasa Kibondo barabara nzuri sana lakini mikoa mingine ni hoi! Sijui kwa nini!

Naomba timu ya wataalamu au Mkurugenzi wa *TANROADS (T )* aanze utaratibu wa kuwatembelea vijana wake ili aone kazi wanayofanya, pamoja na hayo huwa kuna tatizo la watendaji wabovu kuhamishwa na kupelekwa mahali palipofanyiwa kazi nzuri na wale wazuri kupelekwa kwenye maeneo mabovu kwa kuwa ni mahiri ili wakaokoe jahazi, mimi naomba kama kuna mtendaji ameharibu (kushindwa kazi) asipate uhamisho wa kwenda kwingine, nashauri aondolewe kwenye nafasi aliyoshindwa apewe anayeweza kwani watu kama hao wanaiangusha Serikali sana.

Mheshimiwa Spika, je, kiwanja cha ndege cha Singida kimekumbukwaje?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA. J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Miundombinu kwa ushirikianao mkubwa sana hasa ukizingatia Wizara hii ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi, shukrani hizi

zimwendee Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ni sekta muhimu sana kwa ajili ya kuimarisha sekta zingine kwa umuhimu wake ndiyo maana napenda kuchangia hoja hii katika jimbo la Busanda tunashukuru sana kwa jitihada ya Serikali kuboresha baadhi ya barabara muhimu. Pamoja na shukrani hizi napenda kuzungumzia kero zinazosumbua sana wananchi wa Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Spika, kero ya kwanza ni ile barabara ya kutoka Katoro – Kaseme – *Bukombe boarder*. Barabara hii ni muhimu sana na ni barabara ya kiuchumi, mwaka jana ilitengewa fedha lakini mpaka sasa mwaka wa fedha 2009/2010 unaisha lakini barabara bado haijatengenezwa. Barabara hii iko katika hali mbaya sana na wananchi wanahangaika sana. Uchumi katika Kata ya Kaseme imeathirika sana. Jambo ambalo limenisikitisha mwaka huu kwenye kitabu cha Bajeti barabara hii haijawekwa kabisa. Hiki ni kilio kikubwa sana kwangu mimi pamoja na wananchi hivyo naomba kero yangu hii ipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni ile ya Katoro – Nyakagomba kupitia Inyala. Barabara hii ni kero kubwa wakati wa mvua wananchi wanateseka sana, wanahitaji ngalawa ili kuvuka ng'ambo ya pili. Barabara hii ni kiunganishi kikubwa cha kiuchumi, halmashauri imeshindwa kuihudumia barabara hii kutokana na ufinyu wa Bajeti. Hivyo naomba sana Serikali inisaidie kero hii ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa eneo la Tarafa ya Butundwe.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni ile ya Nyarugusu – Lwangasa, Busanda - Lwangasa. Barabara zote hizi ni muhimu sana kwa sababu zinarahisisha usafirishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali kwa ajili ya mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali inisaidie kuboresha barabara nilizozitaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, huu ni mchango wangu wa pili kwa maandishi kwa hotuba hii, pongezi na shukrani kwa Waziri na Wizara nzima nimezitoa kwa mengi mazuri yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa katika Jimbo la Kwimba.

Mheshimiwa Spika, Jimboni Kwimba ziko barabara tano ambazo ziko chini ya *TANROAD*S (Serikali Kuu) Mabuki Jojiro – Malampaka *(PMMR),* Jojiro Ngudu – Magu, Runele – Gatuli, Mwamhaya – Itongoitale, na Hungumalwa – Ngudu.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa barabara ambazo ni za *PMMR* barabara na tau, nne na tano zimetengewa fedha ya madaraja tu. Swali je, sehemu korofi za barabara hizo zitarekebishwa namna gani?

Mheshimiwa Spika, ombi naiomba sana Serikali ione uwezekano wa kutenga fedha hata kama ni kwa ajili ya *light grading* ziweze kutumika katika kurekebisha maeneo mbalimbali yatakayohitaji kurekebishwa katika kipindi cha mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii nikitegemea sana ombi hili litasikilizwa.

**MHE. *ENG.* LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, maendeleo ya matengenezo ya barabara zilizo chini ya *TANROAD*S yanaendelea vizuri katika jimbo la Korogwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Korogwe Vijijini wanalo ombi lao la siku nyingi ombi hilo ni kupandisha daraja baadhi ya barabara zake ambazo zinakidhi vigezo barabara hizo ni Mombo/Mseri huunganisha Wilaya za Korogwe/Handeni, Msambiazi/Ambangulu/Soni (Korogwe/ Lushoto), Kwameta /Dindira/Soni (Korogwe/Lushoto) Kwetonge/Kizara/Kizeru (Korogwe/Muheza) Kerenge/Kijango (Hali ya Hewa/ Magoma).

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupandisha madaraji umekwishapitia Wilayani *(DCC)* na Mkoani *(RCC),* maombi yalikwishaletwa Wizarani tunasubiri majibu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ya Wizara sikuona barabara ambazo ziko chini ya *TANROADS* katika Jimbo la Korogwe Vijijini iliyotengewa fedha kwa ajili ya matengenezo makubwa hili naomba litizamwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kwanza niunge mkono hoja mia kwa mia. Pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, naomba kueleweshwa mambo yafuatayo, kwanza *ATC* itafufuliwa lini? Pili, kuna mpango wowote wa kufufua Reli ya Kaskazini? Tatu, ni kwa jinsi gani msongamano wa magari Dar es Salaam utapunguzwa? Nne, kuna uwezekano wowote wa kuweka mizani pande zote za barabara mahali husika na mwisho kuna mpango gani wa kupanua usafiri wa kwenye mji kati ya Dar es salaam na Tanga?

Mheshimiwa Spika, je, haiwezekani kupunguza msongamano wa magari Dar es Salaam kwa kutumia usafiri wa baharini kutoka *town centre* kwenda pembezoni?

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuipongeza Serikali kwa ujenzi wa barabara zote za Mkoa wa Kilimanjaro. Ni matumaini yangu kuwa ujenzi wa barabara zote utakamilika wakati uliopangwa. Ahsante.

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia hoja hii naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Waziri wa Miundombinu, ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri wake pamoja na wataalamu wote wa Wizara kwa juhudi kubwa wanayofanya ya kuhakikisha kwamba kero za wananchi zihusuzo barabara zinakamilishwa kwa wakati wake.

Mheshimiwa Spika, kila wakati tulipokwenda kumuona Waziri na watalam na Wizara yake tulisikilizwa vizuri na kero zetu zilipata majibu ya haraka.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri pamoja na wataalamu wake waendelee na moyo huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zote ambazo nazitoa kwa Waziri lakini naomba nichangie kidogo hasa katika eneo la ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Ilembo kwamba naiomba Serikali kutenga fedha zaidi kwa vile barabara ile hasa wakati wa masika inapitika kwa shida, barabara ya Kikondo - Ifupa hadi Igulusi pia ijengwe kwa changarawe.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe unaendelea kujengwa, barabara ya Mbalizi – Mkwajuni pia inaendelea kuboreshwa isipukuwa naomba kuwa barabara hiyo ifikishwe kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kuunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kusimamia Wizara hii ambayo ni kubwa na ya kutegemewa na Watanzania wote katika kuinua uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii kuna mambo muhimu ya kipaumbele, barabara, bandari, reli, madaraja, magati, ndege pamoja na uwanja wa ndege, hali ya hewa na kadhalika. Haya yote na mengine ambayo sikuyataja ndizo shughuli katika Wizara hii lakini cha ajabu baadhi ya watendaji wanaonyesha wazi kutokuwa na uchungu katika nchi hii kwa kufanya mambo bila kuwa na umakini, sijui ni kwa maslahi ya nani? Mfano mtu aliyekwenda kufunga mkataba wa ndege aina ya *Air bus* akijua wazi kuwa haitoruka zaidi ya miezi sita, ni lazima itaenda kufanyiwa matengenezo makubwa, mtu huyu alikuwa na maana gani? Serikali haioni kama mtu huyu kaliingizia Taifa hasara kubwa kwa makusudi? Au alijali *ten percent?*

Je, Serikali imemchukulia hatua gani mtu huyu? Pamoja na wataalamu wote alioongozana nao kwenye kukodi ndege hii? Mheshimiwa Waziri naomba majibu utakapofanya majumuisho kwani kwa tabia hii na hawa watu wakiachiwa itakuwa ni kazi ngumu kwa maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea suala la *TEMESA* huu ni wakala chini ya Wizara ya Miundombinu lakini cha ajabu na cha kushangaza Serikali imeshindwa kuiwezesha *TEMESA* ili iweze kufanya kazi zake kwa uhakika kama Serikali ingekuwa makini magari yote ya Serikali yangetengenezwa *TEMESA,* kwa hivyo basi napenda kuishauri Serikali iweze kuiwezesha *TEMESA* vya kutosha, ili iweze kutengeneza gari zote za Serikali, na hii ndiyo maana kuu ya Serikali kuanzisha wakala huyu *(TEMESA).* Kama *TEMESA* itawezeshwa na gari zote za Serikali zitatengenezwa na *TEMESA* basi *TEMESA* inaweza kujiendesha kuliko hivi sasa imebaki na madeni matupu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara nchi yetu ijaribu kutafuta mkandarasi makini ili tuweze kupata barabara zenye ubora kuliko hivi sasa baadhi ya wakandarasi barabara zao si imara mfano *Kilwa Road,* mkandarasi huyu si mzuri kwani barabara imetengenezwa mwaka bado haijamaliza imeshaharibika, tunampongeza Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* kushughulikia miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara zote nchini. Hivyo tunaomba barabara zote nchini zingetengenezwa na wakala huyo kwani ni bora kuwa na wakala huyo mmoja atakayetengeneza barabara zote nchi nzima, kwa mfano barabara za Sabasaba hadi Busweru ni ya halmashauri kwa hiyo haijulikani hii barabara ni ya nani? Kama mtengenezaji wa barabara zote angekuwa ni *TANROADS* peke yake tusingeulizana barabara hii ni ya nani?

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumpongeza sana Mtendaji Mkuu wa *TANROADS.* Bwana Mrema na napenda kumshauri azibe masikio na azipuuze kelele zote za magazeti kwani kuishi na watu ni kazi ngumu, tunachohitaji kwake ni kuona barabara zinatengenezwa kwa hali aliyoanza nayo. Asimamie ubora wa barabara kwa umakini mkubwa, baadhi ya watu wameshaanza kuongozwa na watu ambao si Watanzania na kama akiwa Mtanzania majungu hayaishi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mdogo ukijikita kwenye maeneo machache. Kwanza niipongeze Serikali kupitia kwa Wizara ya Miundombinu kwa kazi kubwa sana iliyofanyika ya kufungua nchi haswa kwa upande wa barabara, lakini mwanga unaonekana.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kufafanua mikakati iliyopo juu ya uendelezaji wa uwanja wa ndege wa Bukoba kwa kutuhakikishia kuwa kuna mpango wa kuweka lami ili utumike wakati wote wa kiangazi na masika, kivuko cha kuunganisha Bukoba na Uganda kilichowekwa kijiji cha Rubafu katai ya Rubafu – Bukoba vijijini. Mradi huu chini ya Afrika Mashariki unasemekana umeanza kupungukiwa fedha. Tunapenda kuhakikishiwa kuwa mradi huu utakamilika. Pia kivuko cha Kyenyabasa kinachounganisha kati ya Bujugo na kata ya Kasharu kilichofungua injini ambayo wakati wote inaharibika haribika na kulazimika kuvutwa kwa mkono, je, lini tatizo hili litamalizika?

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Wizara na *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe maombi yangu ya fedha kwa ajili ya kukarabati daraja lilibomoka, nilileta rai hiyo asubuhi lakini hapakuwa na saini yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba makandarasi wanaojenga barabara ya Minjingu – Singida waende kwa kasi inayotegemewa. Natoa pongezi na shukrani.

**MHE.JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, hoja ni kwa nini mwaka huu 2010/2011 wa fedha barabara muhimu sana ya Mkiwa – Itigi – Rungwa haikutengewa fedha?

Mheshimiwa Spika, nilijenga hoja tangu mwaka 2005/2006 kuwa barabara hii iliharibiwa vibaya na *El-Nino* ya mwaka 1998 na miundombinu yote kuharibiwa. Serikali ikaahidi kwamba ingetenga fedha za kuikarabati barabara hiyo kwa kiwango cha lami na tokea hapo imekuwa ikitenga fedha 2008/2008 shilingi milioni 400, mwaka 2009/2010 shilingi milioni 350, je, mwaka 2010/2011? Je, ni kwa nini wakati maeneo toka Kirumbi – Mwamagembe bado hayajatengenezwa?

Mheshimiw Spika, barabara hii ina urefu wa zaidi ya kilomita 200 si barabara ya kutengewa fedha za *routine maintenance* inahitaji fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba shilingi billion moja na nawasilisha.

**MHE.KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia masuala mawili muhimu ili kufafanua hoja kadhaa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa *ATCL* imilikiwe na Mashirika ya Umma ya ndani kwa kiasi cha 40% na 50 %, nilizungumza na *TANAPA* na *Ngorongoro Conservation Authority (NCA)* kuhusu uwezekano wa wao kuwekeza katika Shirika la Ndege. Inaonesha iwapo Serikali ikiwaruhusu watafanya, kwa mfano iwapo Serikali itawasamehe makato ya kwenda Hazina na kodi ya mapato na kuelekeza waweke mtaji wao *ATCL,* Serikali itaweza kupata mtaji wa *ATCL* zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa mwaka na hivyo kidogo kidogo tunaweza kuboresha Shirika.

Serikali iwe na hisa kati ya 20% na 30% ambazo itashika kwa niaba ya wananchi na baada ya *ATCL* kuanza kupata faida inaweza kuuza hisa hizo kupitia soko la hisa. Kiasi kilichobaki cha hisa anaweza kutafutwa mwekezaji kutoka nje *(strategic investor)* mwenye uzoefu wa muda mrefu katika sekta au mwenye mtaji wa kutosha. Kwa mfano ile Kampuni ya *Ras Al- Khaimali (RAW AIR)* inaweza kuobwa kushirikiana na *ATCL. Route* za mbali zaweza kurejea kupitia *strategic partnership* kama hizi. Tunaweza kutafuta *money manager contractors* na kuwapa malengo maalumu chini ya *Board of director* iliyo imara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TRL/RAHCO,* juhudi zifanywe kuhakikisha kuwa tunapata *management contract* kutoka kampuni kubwa duniani kama *DB* ili pia tupate msaada kutoka Serikali ya Ujerumani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *marine services,* Serikali itoe msimamo kuhusu ubinafsishaji wa *MSCL* ili kuliondoa shirika katika *specification*. Serikali iweke nafasi ya uwekezaji katika shirika hili. Mradi wa *MV. Liemba* tayari Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KFW)* wamefanya kazi ya kufanya *feasibility* na zimetengwa paundi milioni tisa kwa ajili ya mradi huu, Serikali ishirikiane na Serikali ya Ujerumani kufanikisha mradi wa *MV. Liemba.*

**MHE.DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake hapa Bungeni leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri zinazoendelea katika ujenzi wa barabara ya Singida – Babati - Minjingu. Nashukuru kwa kujenzi wa daraja la Mto Magara, barabara ya Dareda – Dongobesh na daraja la Basharet, ujenzi wa barabara ya Babati – Orkesment, ujenzi wa barabara ya Mbuyu wa Mjerumani (Mwada) – Mbulu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya barabara ya Babati – Dodoma – Iringa hususani kipande cha Babati – Dodoma lini hasa kazi *(physical works)* zitaanza?

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu ni matumaini gani tunayo kwa shirika letu la ndege la *ATCL* na tunayo matumaini gani kwa Shirika la Reli?

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na tuhuma nyingi kwenye magazeti juu ya uongozi ndani ya *TANROADS.* Je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi *to clear the air?* Ifahamike kwamba siku zote ni vyema kuondoa au kupunguza matatizo kuliko kuyaahirisha ni muhimu kuyatatua, vinginevyo naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. VITA RASHID KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Naibu Waziri Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa ushirikiano waliotupa sekta hii Halmashauri yetu Namtumbo na wananchi wake kwa kutukarabatia barabara zetu zinazopitika mwaka mzima kwa usimamizi wa *TANROADS* Mkoa Ruvuma ulio na uongozi mahiri chini ya viongozi wa meneja wake Mkoa wa Ruvuma Mr. Kishimbo.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara imekua ikitutengea fedha za Mfuko wa Barabara kila mwaka ambao fedha zake zinatusaidia kukarabati barabara na madaraja ya njia zilizo chini ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Namtumbo – Songea kilomita 67. Naishukuru Serikali kwa ku-*sign* mkataba wa barabara Namtumbo – Songea kilomita 62 kwa kiwango cha lami na mkandarasi ameshakabidhiwa *site*. Huu ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Namtumbo, kazi ya kutathmini na kulipa mali za wananchi zitakazoathirika na ujenzi wa barabara hii imefanyika vizuri bila malalamiko. Tunawashukuru sana waliofanya kazi hiyo toka mwanzo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Namtumbo – Tunduru kilomita 194, tunaishukuru Serikali kwa kuomba mkopo fedha za kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami kutoka *ADB* na *JICA* ya Serikali ya Ujapani.

Mheshimiwa Spika, katika barabara hii ya Tunduru–Namtumbo kumetokea malalamiko katika zoezi la tathmini kwa maelezo ya wananchi walio katika maeneo hayo maafisa waliokwenda hawakufanya tathmini kwa kuwashirikisha, kilichotokea wao walikwenda na fomu na kuwaambia wasaini fomu hizo na baadaye wakaja kuona fomu zao zimewekwa viwango ambavyo hawakuona mtu kuja kuzikagua nyumba zao kwa kufanya tathmini kilichofanyika ni kuwaita na kujikuta wengine nyumba zao kuwa na thamani ya Shs.450,000/= (laki nne na nusu).

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ilitazame tatizo hili haraka ili haki itendeke ili isije kutukwamisha na kuchelewesha utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuweka mawe ya msingi kama ishara ya kuanza kujenga barabara za lami Mkoani Rukwa kama ilivyopangwa ndani ya ilani. Kwa niaba ya wana-Rukwa namshukuru Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Kikwete; Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Kawambwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Chibulunje kwa kuthibitisha kuwa sasa nayo Rukwa itaiona lami kwa maendeleo yao, tangu dunia iumbwe! Hongera kwa watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nimekwishaomba mara kadhaa barabara ya lami kwa barabara ya Kaengeza - Mwimbi – Ulumi – Manamba – Mtula. Barabara hiyo inaunganisha Tanzania na Zambia na kwa kiasi kikubwa sana itakuza biashara ya Mkoa wa Rukwa na kuleta maendeleo endelevu na makubwa kwa Sumbawanga na maeneo ya pembezoni ya Kaengesa, Mwazye, Mwimba, Ulumi, Legeza Mwendo, Mambwe – Nkoswe, Mambwe Kenya na Katazi. Maeneo ambayo yako nyuma mno kimaendeleo (inatisha na hata namna ya kuuza mazao yao ni kwa kulanguliwa tu wakati soko lao liko wazi huko Zambia, *DRC* (Nyasa), Malawi kwa kupitia barabara hiyo ninayoitaja.

Mheshimiwa Spika, naomba watu hawa waonewe huruma wapate kufurahia matunda ya uhuru. Ilani ya CCM ni yetu sote tufaidike nayo. Si sahihi mtu kusema barabara ya Kaengesa-Mwimbi-Ulumi-Mnamba- Mtula isubiri zijengwe barabara za Tunduma-Nyakanazi na Sumbawanga-Kasanga. Naomba maandalizi ya barabara hiyo ya Kaengesa-Mwimbi-Ulumi-Mnamba-Mtula yaendelee kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tayari Ulumi wamepata mradi wa umwagiliaji wa thamani ya Tshs.800,000,000/=, ukimalizika watu wa huko watahitaji barabara. Soko wanalo huko Zambia, DRC, Malawi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Kawambwa pamoja na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Chibulunje kwa kazi zao nzuri na nzito sana kwani Wizara hii ni kubwa na ndiyo roho ya nchi hii katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii matatizo ni mengi tena sana na yote yanatokana na bajeti ya Wizara hii kuwa finyu sana, kwani inashindwa hata kujiendesha katika miradi ambayo imejipangia. Lakini pamoja na hayo lazima tunachoona tuseme, kwani bila kusema hatutakuwa tunawatendea haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kulisemea suala la ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mwanza, kwani imekuwa ni hadithi tu katika vitabu na kumbukumbu za Serikali kwani kila mwaka husikia hadithi hii na utekelezaji ni duni kabisa. Hivyo, tunaiomba Serikali iangalie zaidi Uwanja wa Nege wa Mwanza na pia ichukue hatua ya ujenzi huo, kwani tunapoingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, uwanja huu unaweza kuingiza pato la Tifa,kodi ya ziada ambayo ilikuwa haipo, pia ikawa ni kiunganishi kwa Jumuiya hiyo. Naomba tuache maneno na sasa tunahitaji vitendo. Uwanja huo ambao unaweza kuwa tegemeo wakati wa mvua na hasa nyakati za masika. Hakuna namna ambayo mtu anayetaka kupanda ndege asitoe yeye na mzigo wake, hakuna jinsi ya kufanya hata kama ni dharura kwa wakati huu, ina maana *TAA* hailioni hili au ndiyo kasi mpya? Naiomba Srikali iwe na maneno machache na iwe na vitendo vya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Spika, pia barabara ya Mwanza Shinyanga kuelekea Dar es Salaam eneo la Mwabuki hadi Kona ya Misasi ni kero ya muda marefu, ni vipi hali hii iendelee bila matibabu? Tunaiomba Serikali kutupatia ufumbuzi wa barabara hiyo, tunaisihi Serikali kuchukua hatua kwa barabara hiyo na ifanye juu chini ili eneo hilo lipitike bila wasiwasi. Je, mjenzi wa barabara hiyo ni nani na yuko wapi? Haoni usumbufu anaowapa wasafiri bila sababu?

Mheshimiwa Spika, tusipate misaada ya kutufunga kwa kufanya mambo bila hali ya eneo. Tazama barabara ya Dar es Salaam – Dodoma, ni barabara isiyo na muda mrefu na tazama ilivyokwisha bomoka na kuweka mifereji katikati ya barabara, hili ni tatizo kubwa na si suala la kufumbia macho kabisa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua hivi Serikali ilikosana nini na mkandarasi ambaye alijenga barabara ya Chalinze – Morogoro, kwani ni barabara imara na ni ya muda, ukilinganisha na barabara ambazo zimekuja nyuma yake, ni kwa nini tusimtumie mkandarasi huyo ambaye ni madhubuti sana. Hebu tutafakari hili kwa ukaribu zaidi na sio kukubali miradi ambayo inaweza kutupotezea hali nzuri ya barabara.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimia Spika, napenda kuwapongeza Rais Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kusimamia vizuri sana utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi hususan ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi zake za kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Serikali ikiwemo miundombinu. Yeye amekuwa mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwa uadilifu mkubwa sana. Nawatakia kila la heri katika uchaguzi wao.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri. Nawatakia baraka za Mungu katika utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri wanazozifanya napenda kuzungumzia changamoto chache ambazo zimegusa sana Wilaya ya Morogoro Vijijini kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Morogoro-Kisaki, barabara hii ni ya *TANROADS* lakini hali yake (yaani ilivyo) haionekani kama kweli inahudumiwa na taasisi yenye wataalam kama *TANROADS*. Hali ya daraja la Mto Ruvu, katika eneo la Kibangile ni hatari kwa watumiaji. Naomba hilo daraja lijengwe kwa *design* iliyo imara zaidi. Vile vile kuna maeneo korofi katika maeneo ya Dutumi na Mngazi pamoja na eneo la katikati ya Kiloka na Mkuyuni. Naomba maeneo haya yapatiwe suluhisho la kudumu.

(ii) Mheshimiwa Spika, barabara barabara ya Kinole ni mbaya sana. Mvua ikinyesha magari mengi hayapiti, hivyo wananchi wanashindwa kuuza mazao hata kushindwa kufikia huduma za kijamii kama hospitali. Naomba barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami au simenti (zege) katika maeneo korofi. Aidha, barabara ni nyembamba sana na haifanyiwi usafi pembeni mwa barabara ili kupunguza ajali zinazotokana na kutokuona magari au pikipiki zinatokea upande wa pili kwa sababu ya uwepo wa kona na majani marefu yanayoziba barabara.

(iii) Barabara ya Ngerengere kwenda Mkulazi. Barabara hii ni mbaya sana mpaka imesababisha nauli za magari na pikipiki kupanda mpaka Tshs.15,000/= kutoka Ngerengere kwenda Mkulazi badala ya T.Shs.3,000/=. Haya ni mateso kwa wananchi. Naomba barabara hii ifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

(iv) Madaraja. Mheshimiwa Spika, naomba *TANROADS*, iangalie uwezekano wa kusaidia madaraja na makaravati katika barabara zinazochimbwa na wananchi wa Tegetero, Mbehuwi, Amin, Lukenge na Nyange.

Mheshimiwa Spika, kwa njia ya pekee naomba *TANROADS* isaidie daraja la Zigzig katikia Mto Mbezi. Daraja hili litasaidia wananchi wasiopungua 10,000 ambao

mto ukifurika wananchi wanashindwa kwenda sokoni, hospitali hata kwenda mashambani. Naomba hii kero itazamwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara izingatie kero za Morogoro Vijijini kwani maendeleo ya eneo hili yamedumaa kutokana na matatizo ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi zangu kwa Waziri pamoja na Wizara kwa mkandarasi wa kutengeneza barabara ya Muleba-Lusaunga, pamoja na kuchelewa hali sio mbaya sana. Pili, ukarabati wa uwanja wa ndege Bukoba pamoja na wananchi wa Kata za Kashainyamkazi, Kahorora ile barabara ya muda iliyowekwa ina msongamano mkubwa sana na kusababisha ajali za mara kwa mara kwa sababu ni finyu sana.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini isipanuliwe? Uwanja wa ndege wangeharakisha kabla ya mvua za masika, ikianza ninavyojua hali itakuwa mbaya sana. Swali lingine, kuhusu matengengezo ya uwanja wa Kajuguti na ukilinganisha tunaingia Soko la Pamoja tuna nchi jirani ambazo zina miundombinu mizuri. Sisi bila kuwa na miundombinu hasa uwanja ambao ni wa kibiashara tutatwangia maji kwenye kinu. Je. Serikali pamoja na Wizara inatufikiriaje hata sisi pamoja na nchi kuingiza kipato, uchumi, ajira inaweza kuondokana na umaskini? Ukilinganisha na Kajunguti ni katikati nimeona Uwanja wa Mbeya nimefurahi sana, ukiisha watu wa Mbeya watafaidikaje na Kagera inawezekana.

Mheshimiwa Spika, matatizo yanayotokea kuhusu upanuzi wa miundombinu yoyote inakuwa na migogoro ya kuvunja vunja makazi ya wananchi pamoja na sehemu za biashara, je, Wizara pamoja na Serikali ina mipango gani kupunguza migogoro mapema. Kwa wananchi kuwaandalia makazi kabla ya yote?

Mheshimiwa Spika, matatizo ya ukarabati wa barabara zetu, mara kwa mara tumalaumu madereva kwa ajali lakini na wanaokarabati wanachimba mashimo barabarani wanayaacha bila kuyafunika, yanaweza kumaliza siku mbili hadi tatu. Je, si yanasababisha ajali?

Mheshimiwa Spika, utengenezaji au ukarabati wa barabara za mitaani hasa Dar es Salaam zinapunguza foleni. Je, Wizara imeishaliona na je, inalifanyia kazi kupunguza foleni?

Mheshimiwa Spika, matatizo ya (*VIP*) nimetembea sehemu nyingi tuna matatizo sana ukiangalia nchi jirani *VIP* zao na za kwetu aibu, hata ya kwetu Bukoba. Tumepanua uwanja lakini *VIP* hairidhishi hata kidogo, je na yenyewe inapanuliwa?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilichangia kuhusu barabara ya Kanazi kwenda Katoro Bukoba Vijijini, hiyo barabara ni muhimu sana ambayo inaahidiwa na ya kivuko ninacholalamikia kila siku. Kyenyabasi tukipata kivuko au kutengenezewa daraja itasaidiana na barabara hiyo lakini sasa vyote vina matatizo barabara mbovu, pamoja na daraja la Kalebe. Ombi, je, tuwe na tegemeo mwaka kesho?

Mheshimiwa Spika, bandari Mkoa. Tuna matatizo angalau tuwe na bandari moja japo ya Bukoba Mjini. Kemondo tuwe na cha kujivunia pamoja na ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa bandari ukiangalia kwa sasa mabasi yamepunguza kipato, Mwanza, Bukoba abiria wanapanda mabasi.

Mheshimiwa Spika, matatizo katika Kituo cha Mabasi cha Ubungo, nimepanda mabasi, nimeona kinachosababisha ajali. Mabasi yanapanga foleni eti yanakaguliwa *SUMATRA* yanachukua muda mrefu sana yakishaondoka yanakuwa na spidi yanakwenda kwa kasi yanasababisha ajali. Je ni kwa nini ukaguzi wasibadilishe mabasi yaendayo mikoani yakalala yamekaguliwa ili kupunguza ajali zinazotokea?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi kushindwa kuendesha Shirika muhimu la Ndege *(ATCL)*. Utambulisho wa nchi katika nchi nyingine ni ndege. Leo kwenda nchi nyingi za Afrika na Ulaya na duniani kote utaona utambulisho wa Kenya kwa sababu tu ya ndege yao. Hivi ni laana gani ipo Tanzania mpaka Shirika letu la ndege linakufa au lmeufa? *ATCL* inadaiwa na kampuni ya *Celtic Capital* ya Miami *USA* Shilingi bilioni 1.1. Huo ni mkopo uliochukuliwa tarehe 15/12/2006 ili kubadilisha *boeing* 2 737-200. Mbaya zaidi mkopo huo haujulikani ulikuwa wa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, *ATCL* pia inadaiwa na *Wallis Trading Company* ya Liberia *USD* 60,000,000 kwa kukodisha *Air bus* A320, deni limefikia bilioni 13.3 wakati ndege haifanyi kazi, ipo Ufaransa kwenye matengenezo na haijulikani pesa zitalipwa vipi na ndege itarudi lini. Serikali ieleze ni vipi italipa madeni haya na mpango ukoje wa kulifufua shirika hili.

Mheshimiwa Spika, reli ya kati, hili ni tatizo lingine. Reli ilijengwa kipindi cha Ukoloni, lakini matengenezo ya uboreshaji wa reli uliendelea kusuasua matokeo yake reli haiaminiki, usafiri unakuwa wa adha kubwa. Ni jambo la kawaida usafiri kusitishwa kila mara. Ingawa sasa safari za reli ya kati zimeaanza lakini bado *route* haitoshi. Sasa reli yatumika mara moja kwa wiki kwa kuwa na treni ya abiria. Bado mabehewa hayatoshi na yamechakaa sana.

Mheshimiwa Spika, stesheni za reli, zimedorora, Srikali ione umuhimu wa kuwekeza au kutafuta wawekezaji, ziwekwe ofisi na hoteli au migahawa ya kisasa. Serikali itupe mikakati yake ya kuboresha reli, treni na stesheni zake.

Mheshimiwa Spika, barabara ni sawa na mishipa ya fahamu na ya kupitisha damu mwilini. Kwani ndizo zinazotumika kupeleka huduma, chakula, mafuta, malighafi na kadhalika kutoka sehemu moja ya nchi mpaka eneo lingine la nchi. Lakini nchi yetu bado inategemea wahisani kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa barabara zetu na ndio maana hatufanikiwi kujenga barabara zetu kwa wakati, matokeo gharama huzidi mara mbili zaidi ya gharama ya awali iwapo wahisani wanachelewesha pesa.

Mheshimiwa Spika, mfano, mwaka 2010/2011, bajeti ya maendeleo ni 871,553,916,00. Kati ya hizo 370,880,081,000 ndio za ndani, 500,673,835,00 zategemewa zitoke nje. Wasipozitoa maana yake ni kwamba miradi mingi haitatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigoma–Nyakanazi kupitia Kibondo na Kasulu bado inasuasua, tunaomba ijengwe kwa kiasi cha lami ili treni inapokosekana wananchi wapate uhakika na raha ya safari. Vile vile Serikali isiisahau barabara ya Itigi Tabora kupitia Nzega ili safari mpaka Kigoma iwe ya lami pote kama ilivyo *route* ya Arusha toka Dar es Salaam.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wakuu na wengine wote walioandaa hotuba hii nzuri yenye kuonesha tulikotoka na tunakoelekea.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niipongeze Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, hasa kwa kusimamia ujenzi wa barabara za lami changarawe na hata barabara za vijijini zinazosimamiwa na Halmashauri zimetengenezwa vizuri na zinapitika vizuri. Kwa sisi wananchi wa Mkoa wa Dodoma tunafarijika sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua inayochukua kwa kuandaa ujenzi wa barabara ya Dodoma – Kondoa –Babati na Dodoma-Iringa. Tunaiamini Serikali kwa kauli zake, tunachoomba ni Serikali kuwaambia wananchi ni lini ujenzi wa barabara hiii itaanza kujengwa.

Mheshismiwa Spika, naamini Serikali inajua uzito wa barabara hii Kimkoa, Kitaifa. Vinginevyo tunaomba ujenzi huu uanze kabla ya kampeni vinginevyo tutapata tabu ya kujibu maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu Serikali inavyojitahidi kuunda upya Shirika la ndege la Tanzania. Kwa ujumla shirika hili ni muhimu kwani kwa kukosa Shirika la Ndege tunapoteza mapato mengi hasa kutoka kwa watalii matokeo yake tunapoteza. Dodoma tuna eneo ambalo limetengwa kujenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa. Naomba nirudie tena kuuliza kwamba Serikali ina mpango gani wa ujenzi wa Kiwanja hiki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu wa kujenga nyumba za kuwauzia watumishi, jambo ambalo ni la kulinda heshima za watumishi ambao wengi wanapostaafu huwa hawana nyumba. Naishauri Serikali badala ya kuwauzia, kuwepo na chombo kama vile bima na watumishi wawekeane mkataba na Serikali kwa kuwakata kidogo kidogo ili nyumba hiyo apewe hata kabla ya kustaafu na akiba yake imsaidie kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliangalie suala la usafirishaji kwa njia ya mabasi hasa yale yanayoanzia Mikoani na Wilayani kwani yanajaza abiria, suala ambalo ni hatari kwa abiria.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isimamie kikamilifu suala la kuchakachua mafuta ili lifutike kabisa. Naiamini Serikali ina uwezo mkubwa wa kusimamia kazi hiyo, tendo hili ni la aibu na Serikali inaweza kabisa kuwajua na kuwashughulikia. Kwa hiyo, nawatakia Waziri na Naibu Waziri ushindi mkubwa katika Majimbo yao na warudi hapa Bungeni na namwomba Mwenyezi Mungu ili Mheshimiwa Rais awarudishe tena katika nafasi zenu, kwani kazi mlizofanya katika Wizara hii ni kubwa na zinastahili kuigwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukurani nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa taasisi za miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa, Wizara hii ndiyo kioo cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu itengewe fedha za kutosha na nyingi kwa sababu umuhimu wa safari ni miundombinu, bila ya miundombinu hakuna maendeleo.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa Wizara kwa kuipandisha barabara ya Lugoba-Ubena kuwa ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya usanifu wa barabara ya Bagamoyo Saadani hadi Tanga, ahsante sana. Barabara hii ikikamilika itasaidia sana wananchi wa Matipwili, ambao hulazimika kusafiri kwa umbali wa kilomita mia moja kwa kuzunguka badala ya kilomita nane hadi kumi kutoka Matipwili Bagamoyo.

Pia, Mheshimiwa Spika, kama usanifu utakuwa na mushikeli basi rudisheni Kivuko cha Mto Wami.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuondoa msongamano wa magari Dar es Salaam. Magari ya mizigo yaishie Ruvu, Vigwaza na Chamakweza. Kurudisha huduma ya reli, ni njia tosha ya kupeleka au kusafirisha mizigo hiyo hadi maeneo niliyotaja. Pia kutopatikana ajira kwa vijana, kusafisha mapori yaliyo maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa kipaumbele barabara ya Msata–Bagamoyo, naomba Serikali tunaelekea kwenye uchaguzi, naomba Wakurugenzi watoe tamko kwa Bunge letu Tukufu, ili wananchi wetu wa Bagamoyo na Chalinze wasikie, najua kulikuwa na matatizo, tunaomba ifikie tamati kwa barabara hii, ni mtihani mkubwa kwangu na Mheshimiwa Waziri. Tunaomba mtuokoe.

Mheshimiwa Spika, najua ndugu yangu Mrema ana majukumu mengi ya barabara nyingi, namwomba jicho lako litazame barabara hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bagamoyo pamoja na Jimbo la Chalinze ni kitovu cha kati na ni muunganisho wa mikoa yote, kwa hiyo barabara hizi ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wote watendaji wa Wizara, *TANROADS* kwa kazi zenu.

Mheshimniwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo niwaombe sasa nichangie machache kuhusu hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Iringa – Dodoma – Babati, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha ya kuridhisha kwa kipande cha barabara hiyo toka Iringa hadi Dodoma (bilioni 51,575). Kitendawili kipo katika kipande cha Dodoma hadi Babati. Barabara hii imetengewa bilioni 9.5645/= tu. Kiwango hiki ni kidogo mno kwa kazi zilizopangwa. Pia napenda kuikumbusha Serikali ahadi yake ya mwaka jana 2009/2011, ya kutenga bilioni 40/= nje ya bajeti kwa ajili ya barabara ya Dodoma hadi Babati. Napenda kuonesha wasiwasi wangu kuwa ahadi hii inawezekana haitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura wangu naomba Serikali itekeleze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Handeni–Kiberashi-Kijungu-Kibaya-Njoro-Olboloti-Mrijo Chini-Chandama-Chambalo-Chemba-Farkwa-Kwamtoro–Singida. Naipongeza Serikali kwa kuamua kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Naomba Serikali iharakishe upembuzi yakinifu, usanifu na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka kumbukumbu sahihi naomba niifahamishe Serikali kuwa barabara hii katika Wilaya ya Kondoa inapita katika Vijiji vya Olboloyi-Mrijo Chini-Mrijo Juu-Chandama-Soya-Cambalo-Chemba-Farkwa-Kwamtoro-Ovada-Kinyamshindo hadi Singida na siyo Olboloti–Mrijo Chini–Dalai–Bicha–Chambalo–Chema–Kwamtoro–Singida kama inavyooneshwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 182.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba za Wakala wa Majengo (*TBA*). Napongeza Wakala wa Majengo kuamua kujenga nyumba moja Mjini Kondoa, hata hivyo ujenzi hivi sasa umesimama. Naomba Wakala wa Majengo ikamilishe ujenzi wa nyumba hii haraka maana inahitajika sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache natamka kuwa naunga mkono hotuba hii.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba niseme na kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi na ahsante nyingi kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa juhudi zake za kujenga barabara za lami Mkoa wa Kigoma. Barabara za Kigoma/Kidahwe, Kigoma-Manyovu na sasa Kidahwe-Kasulu na Kitahwe-Uvinza zimeinua ari mpya kwa wakazi wa Mkoa wa Kigoma. Mheshimiwa Rais na Wizara ya Miundombinu tunasema ahsante sana. Tunaomba juhudi zaidi katika kusimamia kazi mpya zinazoendelea na hasa barabara Kidahwe–Kasulu-Tole.

Mheshimiwa Spika, kupandisha hadhi barabara kutoka hadhi ya Mkoa na kuwa barabara kuu (*Trank road*). Napendekeza barabara zifuatazo zifikiriwe tena kupandishwa hadi, *road board* ya Mkoa wa Kigoma imezipitia barabara hizi na kuona zina sifa zote za kupandishwa hadhi, barabara hizo ni zifuatazo:-

(i) Barabara ya Kasulu-Manyovu ipandishwe hadhi na kuwa barabara kuu. *Tank road* kutoka hadhi yake ya sasa ya *Regional Road*.

(ii) Barabara ya Makere, Heruushingo-Kitanga, Burudi *Boarder*, nasisitiza ipandishwe hadi na kuwa *regional road* kutoka hadhi yake ya *district road*. Maoni yaliyotolewa na tume iliyotumwa kuja Kigoma, pamoja na kwamba kwa mshangao wa wengi hawakuweza kutembelea barabara hiyo yamezingatiwa, hasa kuwasiliana na upande wa pili wa Mto Malagarasi ambao ni Mkoa wa Rutana nchini Burundi.

(iii) Barabara ya Rusesa–Zeze–Nyanganga Kazula Mimba hadi Kandaga/Uvinza – *trank road*. Barabara hii ina sifa zote na za kuwa regional *road*. Kigoma *regional road board* nimependekeza mara mbili, kwa hiyo, naomba Waziri apandishe hadhi barabara hii, ni barabara ya kiuchumi – *from a point of trank road to trank road* Kigoma/Kasulu *road junction to* Kandago-Uvinza. Barabara hii kuendelea kuwa *district road* si tu haipendezi, bali ni kinyume cha hata sera yenyewe ya barabara. Kigoma inahitaji kuongeza mtandao wake wa barabara za *regional roads*. Kigoma *has least regional road network in the country*. *Kindly take note*.

(iv) Daraja la Kitanga Wilaya ya Kasulu kwenye Mto Malagarasi, ni vyema *studies* zifanyike. Naomba *TANROADS* wasaidie utalaam Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu (ujenzi) ili kuanza mchakato wa ujenzi wa daraja hili muhimu.

Mheshimiwa Spika, nyumba zilizouzwa na Serikali Wilaya ya Kasulu, nilishatoa hoja hapa Bungeni nikisema kwamba nyumba za Serikali zilizopo Kasulu ziliuzwa, bila shaka kwa makosa, maana:-

(i) Nyumba ya Hakimu wa Wilaya iliuzwa.

(ii) Nyumba ya *OCD* Kasulu iliuzwa.

(iii) Nyumba ya *DED* na *Planning officer* zote ziliuzwa na kadhalika. Zaidi ya nyumba hizi zipo bomani eneo ambalo ni *strategic* kiulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa sijapata kusikia Wizara au *TBA* wamefanya nini kwa Kasulu na lini nyumba hizi zitarudishwa Serikalini. Nataka maelezo.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege, Kigoma, nimefurahishwa sana na juhudi za kujenga Uwanja wa Ndege Kigoma kwa lami. Anzeni kazi hiyo sasa. Tunasubiri sana, tena kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ENG. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji na wafanayakazi wa Wizara hii kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 – 2010 ya CCM katika kuendeleza miundombinu nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba Tabora (Mji wa Tabora na mkoa kwa ujumla) bado haijaunganishwa kwa lami na barabara inara zinazoweza kupitika kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano (2005-2010) kumekuwa na matamko mengi kuhusu kujengwa kwa barabara za Tabora – Urambo – Kigoma, Tabora – Nyahua – Manyoni na Tabora – Nzega (pia Tabora – Sikonge). Barabara hizi ni muhimu sana katika kufungua uchumi wa eneo pana la katikati ya tanzania na pia ni muhimu katika kuendeleza kwa vitendo sasa uchumi wa kijiografia, hasa kuelekea na kutoa mizigo *DRC* na nchi zingine jirani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi na matamko ya serikali juu ya barabara hizi, naamini wananchi wa eneo husika watajiandaa vizuri zaidi katika kunufaika na barabara hizi kiuchumi, kiutamaduni na kijamii pia kama matamashi ya serikali yataimarishwa kwa mikataba itakayowekwa kuthibitisha matamko ya serikali na baadaye ujenzi wenyewe. Tumesubiri sana, imetosha.

Mheshimiwa Spika, kweli serikali imejenga tayari barabara nyingi sana kwa kiwango cha lami. Lakini pia Mheshimiwa Spika, uimara wake umekuwa wa kutia mashaka, ama usimamizi wa matumizi nao unatakiwa kuboreshwa zaidi. Haya nayasema Mheshimiwa Spika, kutokana na kubonyea na hata kubomoka kwa maeneo mengi ya barabara hizi. Inawezekana magari yanazidisha sana uzito kuliko inavyostahili, kama siyo pia haisababishwi na uduni wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kubonyea kwa barabara ya Dar es Salaam Morogoro katika eneo la Mizani pale Kibaha, kubonyeas na kuchimbika kwa barabara baina ya Kibaha na Chalinze (Mkoa wa Pwani) na pia uduni wa aina hiyo pale Chalinze penyewe kunaleta mashaka yote ya uduni wa ujenzi na pia uduni wa usimamizi wa matumizi bora ya barabara zetu. Wizara inafanya nini katika udhaifu katika maeneo yote haya mawili?

Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana pia nionapo tunajaribu kufidia mapungufu ya umahiri wa madreva wetu na pia waenda kwa miguu kwa kuongeza matuta, tena pasi na mpangilio maalumu, katika barabar zetu. Hivi ni kwa nini hatuchukui hatua za kuboresha weledi wa madreva wetu, kwanza kwa kuwatambua madreva hawa kama "professionals" muhimu sana katika uchumi wa usafirishaji nchini kwetu? Tumefanya udreva kuwa ni kazi ambayo tunavumilia watu kupata leseni daraja zote, na hasa daraja "C", kwa namna za udanganyifu na tunataka kupata majibu ya ongezeko la ajali barabarani kwa kukwepa hili!

Mheshimiwa Spika, ukipata takwimu za uingizwaji wa magari makubwa yanayohitaji kuendeshwa na madreva wenye leseni ya daraja la "C", ukalinganisha na leseni halali za daraja hilo zitolewazo katika mwaka ndipo utakapoona udhaifu wenyewe na sababu kubwa ya ajali barabarani.

Mheshimiwa Spika, kuweka matuta barabarani haiwezi ikawa mbadala wa weledi wa madreva wetu hata siku moja. Inatakiwa kazi kubwa ya kuimarisha weledi was madreva wetu. Pia elimu kwa Watanzania wote itolewe waweze kujua namna bora na salama ya kutumia barabara zetu. Tafadhali sana juhudi hizi zionekane.

Mheshimiwa Spika, kujenga matuta barabarani siyo tu kuharibu barabara zenyewe, bali pia kunachelewesha usafirishaji na kuongeza gharama za usafirishaji nchini.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya mafuta yanaongezeka sana katika kulifikia na kuondoka baada ya kuruka tuta. Lakini pia uchakavu wa gari unaongezeka, pamoja na kupondeka kwa barabara katika maeneo hayo. Matuta haya yanapunguza sana "man hours" katika uchumi wetu. Tuseme Mheshimiwa Spika, matuta haya ni tatizo kubwa sana katika uchumi wetu wa usafirishaji hapa nchini. Utafiti utaonesha hivyo na, kwa hiyo, uchumi makini utataka kuondokana na hilo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara zetu mijini ni duni hasa ukizingatia kasi ya ongezeko la wakazi mijini. Msongamano inaongezeka kwa kasi kubwa kuliko uwezo wetu wa kuleta masuluhisho. Hii inafanya pia gharama za kuishi na kufanya biashara mijini ziongezeke sana. Lazima tupate ufumbuzi. Tena wa kudumu. Pia tuanze kuendeleza njia zingine za usafiri mijini, ikiwemo ujenzi wa treni za chini ya ardhi (metro au subway). Bora tuanze sasa kwani hilo halikwepeki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeza sana Waziri mhusika kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu wizara yake.

Mheshimiwa Spika, pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100%. Pamoja na kuunga mkono naomba kuchangia maeneo yefuatayo:-

(1) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara ya kutoka Manhyali – Chalinze-Kiegea – Nghambi-Njia Panda ya Kongwa. Je, fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

(2) Je serikali imetenga fedha kiasi gani 2010/2011 kwa ajili ya matengenezo makubwa ya barabara ya kutoka Mbande-Mjini Kongwa – Nghambi – Chunyu – Mpwapwa – Lupeta – Mbori – Suguta- Mlali hadi Pandambili hata hivyo naipongeza serikali kwa kazi nzuri ya kuifanyia ukarabati mkubwa barabara ya kutoka Nghambi – Chunyu – Mpwapwa.

(3) Kwa kuwa bodi ya barabara ya mkoa ni muhimu sana je katika bodi hizo kwa nini wahandisi wa wilaya ujenzi wasiwe wajumbe wa bodi hizo za mikoa ili waweze kusimamia pia barabara zinazotengenezwa na mkoa katika wilaya zetu *(Regional Roads)*

(4) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondoa makandarasi ambao wanashindwa kutengneza barabara kwa kiwango kinachotakiwa kwa kukosa vitendea kazi na uwezo wa kifedha. Je katika mwaka, 2008/2009 na 2010/2011 ni makandarasi wangapi wamefutwa kutokana na sababu hizo.

(5) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti ujenzi holela wa magorofa yanayohatarisha maisha ya watu hasa katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam.

Nawapongea Mheshimiwa Waizri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti.

(6) Je, ni fedha kiasi gani zinadaiwa kwa ajili ya kulipa madeni ya makandarasi. Je serikali itakubaliana nami kwa mba kutowalipa makandarasi kazi ya kutengeneza barabara zitasimama.

(7) Kwa kuwa barabara nyingi zinahitaji matengenezo makubwa na hasa barabara za vijijini. Je kwa nini fedha zinazotengwa ni kidogo.

(8) Je, ni fedha kiasi gani zinatumika kwa ukarabati wa reli ya kati na kwa nini stesheni ya Msagali imefungwa na treni ya abiria haisimami Msagali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. JENISTA JOAKIM MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa utendaji mzuri wa serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza wizara kwa utendaji mzuri wenye uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nichukue pia nafasi hii kuwashukuru viongozi wote na wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa jinsi walivyonisaidia na kunifariji wakati wa kuuguza na hatimae kumzika mume wangu mpendwa Leonard Mhagama aliekuwa mtumishi wa Wakala wa Barabara Tanroads – Ruvuma Mungu ailaze Marehemu mahala pema peponi – Amein.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kifungu 4132 kina fedha za matengenezo ya barabara za mikoa na ukweli kazi nzuri imekuwa inafanywa na wakala wa mikoa wa barabara. Ninasshauri sana sasa mpango wa matengnezo hayo uangalie misimu ya mvua na kiangazi, mara nyingi barabara hasa za changarawe zingekuwa zinatengenezwa mara tu baada ya mvua kuisha wakati unyevu bado upo zinapunguza barabara gharama na huwa angalau zinadumu, pamoja na kuangalia suala la aina ya udongowake.

Mheshimiwa Spika, kifungu 4137 kinatenga fedha fedha za "Unity Bridges". Ningependa kufahamu kama unity bridges zitakazotumia fedha hizo ni zote mbili yaani daraja la Mtambaswala na la Mkanda – mitomoni Muhukuru Ruvuma

Mheshimiwa Spika, kifungu namba 4197 Masasi – Songea-Mbambabay. Kifungu hiki kinahusu barabara ya Masasi – Songea – Mbambabay. Ningependa kufahamu kwanza kama fedha hizo zinahusu pia mradi wa MCC – pia ningependa kufahamu kama barabara hiyo kwa sasa haitambuyliki kama Songea Peramiho Mbambabay na kama MCC hawafiki Peramiho tena kama ilivyokuwa mwanzo. Pia ningependa kufahamu mradi wa MCC katika barabara hiyo ya Songea – Peramiho – Mbambabay.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Likuyufusi – Mkenda inayounganisha Tanzania na Msumbiji kupitia mkoa wa Ruvuma, Muhukuru – Mkenda mwaka 2008 Mheshimiwa Rais alipokuwa anakagua ujenzi wa daraja la umoja kati ya Msumbiji na Tanzania kupitia Kijiji cha Lukenda aliahidi barabara hiyo sasa iingizwe katika mpango wa kuwekwa lami ili kuendana sambamba na maendeleo ya barabara kwa upande wa Msusmbiji. Mwaka 2009 niliuliza swali la msingi la kujua maendeleo ya mpango huo na serikali ilijibu tayari iko katika mpango. Ningependa kufahamu kama sasa barabara hiyo iko katika mpango wa kuwekwa lami.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwakilisha naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri na pia uendelezaji mzuri wa miundo mgbinu nchini./

Mheshimiwa Spika, wizara imefanikiwa kutekeleza miradi yake hasa kwa Mkoa wa Pwani na mategemeo yetu maendeleo haya yataleta tija kwetu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba/bajeti ya Waziri Mkuu nilichangia na kuomba nipatiwe majibu ya baadhi ya hoja zangu, ambapo nilisema, kuna mpango gani kwa serikali kuzipatia kibali mashirika ya hifadhi ya jamii (NSSF, PPF, PSPF, LAPF na kadhalika) wajenge barabara zetu, kwani mashirika hayo yana uwezo mkubwa wa kifedha na wapewe kwa mtindo wa B.O.T. Pia niliuliza juu ya hatua ya ujenzi wa daraja la Kigamboni ambalo ni kiungo kwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

Mheshimiwa Spika, suala la foleni katika Jiji la Dar es Salaam ni kero na tatizo hilo linakuwa siku hadi siku ni lini serikali itaanza kuweka miundo mbinu ya tahadhari kwa miaka inayokuja kwa kuweka tahadhari ya foleni na kujenga barabara za kisasa katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, kuna mpango gani wa kurudisha/kuweka Road Tol kwa barabara zetu ambpo fedha hizio zinaweza kusaidia kutunza barabara zetu kwa kuwa bajeti ya wizara kila mwaka inakuwa haitoshelezi, kutokana na sungura ni mdogo na walaji ni wengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ni mategemeo yangu wizara itatekeleza yale yote wanayokusudia kwa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH**: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dokta Shukuru Kawambwa (Mb), Naibu Waziri, Hezekiah Chibulunje (Mb), Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara ya Miundo mbinu kwa kuandaa bajeti ya 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali ya Awamu ya Nne (4) kwa kazi nzuri ya barabara za Mkoa wa Singida nashukuru kwa maana barabara zinazounganisha Singida na Mikoa mingine kwa kiwango sasa zinaendelea kutengnezwa ama simekamilika kabisa. Barabara ya Dodoma hadi Manyoni imekamilika kabisa, Manyoni hadi Isuna zimebaki Km 15 na Isuna hadi Singida hadi Shelui imekamilika tatizo lilolopo ni kutofautisha kwa viwango, viwango vya Dodoma hadi Manyoni inaridhisha sana, Isuna hadi Sijgida nayo inaridhisha sana,m iweje ile ya Singida hadi Shelui viwango vyake ni hafifu?

Barabara hii sasa imesaanza kubomoka baadhi ya maeneo hasa eneo la Mlima Sekenke kwa takribani miaka miwili tangu kumalizika kwa barabara hii imeshaanza kuwekwa viraka jambo ambalo linaonesha thamani ya fedha (value for money) kutokuzingatiwa kimatumizi naomba pia maeneo ya madaraja yale sita zile kingo zilizoharibiwa na magari yanayopinduka zirejeshwe ili hadhi na heshimia ya barabara ikarejea kama ilivyokuwa awali,

Mheshimiwa Spika, barabara ya Singida kwenda Babati serikali iongeze kasi katika kuwaondolea kero wananchi wanaotumia barabara hii. Maishukuru serikali kuipandisha daraja barabara ya Kiomboi Kibiriri, Kidatru hadi Kidarafa yenye urefu wa

Km.92.8, naomba maelezo ni lini utekekezaji wa barabara hii utaanza kutekelezwa kupitia TANROADS.

Kadhalika naomba waziri juu ya vigezo vinavyotumika katika kupandisha madaraja barabara kwani zipo barabara ambazo kwa kiwango kikubwa zinaonesha zinafaa kuwa za mikoa mfano mzuri barabara ya Shelui – Mtoa – Kisonga – Mtekente (Lunsanga) – Kimbayi – Urughu Mnadani hadi kiungani cha barabara ya Mkoa Kibaya. Barabara hii inazo Km.65.5 maeneo inayopita barabara hii zipo kata tano (5) idadi ya watu wanakadiriwa kufikia 50,000 kwa hali ya sasa barabara hii kuiacha kuendelea kuhudumiwa na Mfuo wa Barabara Wilaya ni kitendo cha kuwaumiza wananchi kuendelea kupata huduma mbovu ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya kuwajengea uwezo halmashauri kuhusu masuala ya usimamizi wa barabara kwani wataalamu hawatoshelezi katika kukabiliana na matatizo ya kuzihudumia barbara zilizopo wilayani naomba TANROADS ipanue wigo kwa kushirikiana na wahandisi wa wilaya wa masuala ya barabara kiutalamu kwani kufanya hivyo kutaongeza tija na ubora wa matengenezo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba serikali ikamilishe Km 10 za barabara kwa lami Doubl surface dressing ile ya Misigiri hadi Kihambelu.

Mheshimiwa Spika, mwisho matengenezo ya drift eneo la mto Kyenka ng’ombe baina ya Sekenke na Nkonkilangi barabara ya Mkoa meter 250 ukamilishwe haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu katika maendeleo ya miundombinu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Barbara ya Mbeya - Lwanjiro Km.36. baada ya mkandarasi Kundan Singh kushindwa kutekeleza majukumu yake ya ujenzi wa barabara hii, serikali ilimsimamisha kwa ahadi ya kumaliza kazi hii kwa kumpata mkandarasi mpya. Aidha zipo taarifa kuwa Kundan Singh aliishitaki serikali na kushinda kesi hiyo, ukweli ni upi juu ya hili? Na nini mikakati ya serikali katika kuhakikisha kipande hiki cha barabara ya Mbeya – Makongorosi kinaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege – Songwe, naipongeza serikali kwa ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kiwanja hiki kinakwisha kwa wakati. Hata hivyo bado sijaona maendeleo ya upanuzi wa jengo la kufikia abiria, ambacho tulielezwa ni sehemu ya ujenzi wa kiwanja cha Kimataifa cha Songwe. Je ni lini hasa, tunatarajia kiwanja hiki, kinaanza kutumika na kuziibua fursa za kiuchumi zilizopo katika ukanda wa nyanda za juu kusini na Mkoa wa Mbeya kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, fidia ya wahanga wa Barbara ya Mbeya – Lwanjilo – Km 36. napenda kutoa pongezi zangu za pekee kukupongeza wewe waziri kwa kutenga muda wako wa kutembelea Mbeya na hatimaye kuongea na wahanga wa barabara hii. Ni faraja

kubwa kwangu. Naomba serikali, inieleze ni lini watawalipa wahanga wa barabara hii, kwa fidia ya marejeo kwa wale waliosahauliwa awali.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mzunguko/makutano ya barabara kuu ya *TANZAM* eneo la Mafiati – Jijini Mbeya. Eneo hili ni makutano ya barabara kuu itokayo kati ya Jiji kuelekea kiwanja cha ndege na barabara kuu toka Mwanjelwa kuelekea Mbalizi – eneo hili la Mafiati limekuwa likiitwa machinjio ya binadamu kwa sababu ya ajali zinazotokea mara kwa mara. Tanroads walitoa ahadi ya kujenga mzunguko eneo hili. Naomba kujua hatua za kutekeleza azma hii itaanza lini ili kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja ya Waziri wa Miundombinu na kuwatakia yeye na Naibu Waziri uchaguzi mwema.

**MHE. JOB YUSTINO NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa ni muhimu sana na inaunganisha Wilaya za Kongwa na Mpwapwa. Ahadi zilishatolewa za kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Je, kuna juhudi gani za kuanza angalu na upembuzi yakinifu?

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Mkutani Wilayani Kongwa kuna korongo kubwa linalohitaji daraja la gharama kubwa. Wizara inaweza kusaidia vipi halmashauri ya Kongwa kujenga darja hilo ili kufungua barabara ya eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, fungu la barabara za mkoa wa Dodoma ni dogo sana liongezwe.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ya simu za mkononi Wilayani Kongwa kwa kampuni za TIGO, VODACOM, ZANTEL, TTCL si mazuri kwa sehemu kubwa ya wilaya kutokuwa na huduma za makampuni hayo. Hongera kwa ZAIN angalau wanajitahidi. Serikali ihimize hizo kampuni nyingine kuleta huduma Kongwa Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuna maboresho makubwa kwa barabara za vijijini Keep it up, hongereni wizara.

**MHE. MARGARETI SIMWANZA SITTA:** Mheshimiwa Spika, reli ya kati ni muhimu sana kwa kusafirisha watu na mizigo.

Mheshimiwa Spika, barabara zitadumu reli ikiimarishwa. Nawapongeza kwa kazi nzito mnazofanya. Hongera sana.

**MHE. JANETH MAURICE MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliochini ya Wizara ya Miundombinu kwa kazi nzuri waliofanya kwa kipindi cha miaka mitano cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Mwaka 2005/2010. pamoja na pongezi nina maoni yafuatayo:-

Maoni na/ushauri, barabara ya Kilwa ambayo mkandarasi wake ni KAJIMA kazi yake haiko katika kiwango kilichotegemewa au kiwango bora kinachotakiwa. Je wahusika wa ukaguzi wa barabara hiyo wakiwamo Bodi ya Wakandarasi, Tanroad na Mhandisi Mshauri wanasemaje juu ya barabara hii ambayo imeharibika kabla ya kufunguliwa? Mifereji, kingo za barabara na mzunguko katika barabara (round about) zote zimebomoka hali hii inaiabisha serikali yetu kwa wananchi. Fedha zinatumika kazi chafru. Tunaulizwa majibu hatuna. Sababu kubwa ni nini?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Chanika mpaka Chamazi kupitia Msongola kwa kiwango cha lami itamalizika kujengwa lini?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tabata/Segerea/Kinyerezi mpaka Majumba Sita (hasa maeneo yaliyoharibika) kama eneo la Segerea Migombani kona (shell) inahitaji tuta maana kuna kovu kali sana ambayo husababisha ajali za mara kwa mara na wananchi wnaomba wajengewe matuta ili kunusuru roho za watu wasio na hatia. Na katika eneo hilo liendane na ujenzi wa barabara katika maeneo yaliyoharibika katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wingi/msongamano wa magari hasa wakati wa asubuhi na jioni katika maeneo ya Majumba Sita, Banana, Ukonga mpaka Pugu. Je serikali ina mpango gani wa kupanua barabara hii kuanzia Airport mpaka Pugu ikizingatiwa kuwa kuna idadi ya watumiaji magari wengi?

Mheshimiwa Spika, viwango vya ndege vya Mpanda, Mwanza, Sumbawanga, Musoma. Tabora, Songea, Iringa, Mbeya na maeneo yenye mvuto kwa uwekekezaji wa kilimo, viwanda na utalii kwa maeneo kama Katavi National Park( Mpanda), Serengeti National Park, (Musoma, Ruaha National Park na Kilulo National Park maeneo haya yanahitaji viwanja vya ndege ili watalii wa ndani na nje waweze kufika kwa urahisi na serikali itaweza kupata mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, bandari iliyoko Kyela iboreshwe ikizingatiwa eneo hilo ni kivutio cha biashara kwa wakazi wa eneo hilo na zaidi ni kivutio cha utalii wa majini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA;** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Shukuru, Mheshimiwa Naibu Waziri Chibulunje, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote hapo wizarani kwa kutuletea hotuba hii pamoja na ufinyu wa bajeti tulionao mwaka hadi mwaka lakini jitihada zenu wenye macho tumeziona, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa serikali (wizara) kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujengwa kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Kwasadala – Masama ambapo hivi sasa mkandarasi yupo site tayari kwa kuanza kazi kesho kutwa. Kwa niaba ya wananchi wa Hai ninawashukuru sana sana.

Mheshimiwa Spika, niombe kukumbushia maombi ya kupandishwa kwa daraja kwa barabara zetu zifuatazo kutoka halmashauri ili zihudumiwe na Tanroads kwa kuwa zinakidhi vigezo vinavyotakiwa, barabara hizo ni:-

(i) Kutoka Kwasadala – Mashura, Kwenye Jiwe, hii itakuwa ni mwendelezo wa ile inayojengwa kwa ahadi ya Mheshimiwa Rais na itakuwa ni Ring kwa maana ya kuunganisha na barabara iendayo Sanya Juu (Siha)

(ii) Kwasadala – Masama – Machame Barazani, hii pamoja na kujengwa sehemu moja kwa lami kutokana na ahadi ya Rais itakuwa ni ring kwa kuunganishwa na ile ya Kilimanjaro Machine Tools pia itakuwa ni barabara mbadala endapo tutapata hitilafu katika daraja la kikavu, barabara kuu iendayo Arusha.

(iii) Shirinjoro – Makoa, hii ni kutoka Maili sitas na kuunganisha na KMT na inapita taasisi muhimu ya Utafiri wa Kahawa (Tacri). Wafadhili wa EU walionesha nia ya kusaidia.

(iv) Bomang'mbo – Runadugani – Longoi – *TPC*,, hii ni ring itakayo/iunganayounisha kutoka Bomang'ombe hadi *TPC* – Moshi Mjini.

Mheshimiwa Spika, nikumbushie sheria ya majengo ni muhimu tuwe nayo, je ni lini italetwa bungeni?

Mheshimiwa Spika, nitoe masikitiko kwa tabia inayoendelea ya mabasi kusimama porini na abiria kujisaidia hovyo eti kuchimba dawa!! Haifai.

Mheshimiwa Spika, naunga hojo mkono.

**MHE. LUCY FIDELIS OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara kwa kuandaa hotuba hii, napenda pia kumpongeza Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, *TEMESA*, ilianzishwa ili magari ya serikali yaweze kutengenezwa kufanyiwa *service* kule. Sasa hivi magari ya serikali yanapelekwa kwa wakala *(TAMESA)* halafu wao ndio wanapeleka wenye *garage* za watu binafsi yatengenezwe ambapoo yanakuwa ghali sana.

Mheshimiwas Spika, je, Serikali ina mikakati gani ya kuifufua TEMESA hata kama mitambo ile ni ya zamani lakini inaweza kubadilishwa kwa sababu *TEMESA* ipo karibu mikoa yote nchini"?

Mheshimiwa Spika, pale Dar es Salaam *(TEMESA)* uwanja wao unatumika kuhifadhi magari yanayokamatwa na "yono" kwa makosa mbali mbali. Ni kiasi gani kilichopatikana kwa "Yono" kukodishiwa viwanja vile?

Mheshimiwa Spika, je, *TEMESA* inabadilisha matumizi yake ya awali?

Mheshimiwa Spika, hali za barabara. Barabara kubwa ya Dar es Salaam – Chalinze haswa kipande kutoka Mlandizi – Chalinze barabara ile ina mabonde, inanepa haijatengenezwa kwa uimara.

Mheshimiwa Spika, je, mkandarasi anavyopewa kazi ya kujenga barabara huwa hatoi guarantee barabara itadumu kwa muda gani?

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Pamekuwepo na msaongamano mkubwa sana wa magari katika Jiji letu lakini zipo barabara nyingi za *(feedes road)* ambazo zikikarabatiwa zitapunguza kwa kiasi kikubwa. Je, Serikali ina mikakati yoyote ya kukarabati hizo *feedes roads*?

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndega *ATC*. Kwa mara nyingine tena naulizia hatua ya *ATC*? Itafufuliwa au Serikali ina mikakati gani na shirika hili?

Mheshimiwa Spika, *ATC* ina madeni ya kiasi gani?. Je ili *Air bus* bado inalipwa fedha ya kuikodisha?. Mpaka sasa tunazo ndege ngapi za *ATC*?.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi shirika hili la *ATC* pale Makao Makuu Dar es Salaam wanayo magari mengi sana? Magari yale ni kwa ajili ya shughuli gani? Na kwa nini wanunue magari mengi hayo? Kwa kuwa magari yale hayatumiki kwa nini yasipigwe mnada na fedha zile zikasaidia katika matumizi ya ofisi?

Mheshimiwa Spika, naipongeza serikali kurudisha safari za treni kwa reli ya kati. Kwa kuwa pamekuwepo na ajali nyingi za barabara na watu wengi kupoteza maisha na usafiri ni ghali sana katika safari za kwenda Moshi – Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mikakati gani ya kufufua safari za treni kwa abiria kutoka Dar es Salaam mpaka Moshi?

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Spika, mchakato wa ujenzi wa barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya – Tabora, umechukua muda mrefu sana. Naomba maelezo hatua zimefikia au zimekwama wapi na lini ujenzi wa barabara hii muhimu utaanza?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkiwa – Itiga – Rungwa – Makongolosi ilipimwa *(surveyed)?* Naomba kujua programu ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami itaanza mwaka gani?

Mheshimiwa Spika, Reli ya Kati iliyojengwa enzi za dola ya Ujerumani (1905) imechakaa sana na ni reli ya kizamani na hata *engine* na mabehewa ni ya kizamani hayavutii watu kusafiri na treni. Nashaurui Serikali iijenge upya Reli ya Kati. Majadiliano na Serikali ya Ujerumani yaendelee ili yafikie muafaka wa kuijenga upaya kwa *gauge* kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia reli ya Manyoni – Singida sasa ijengwe upya kukidhi viwango vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara ya Ukiwa – Manyoni inaenda vizuri. Napendekeza Kampuni ya Ujenzi ya *CGC* inayojenga barabara hii, wapewe barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya - Tabora kwa sababu wana uwezo. Nawasilisha.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, katika suala la ujenzi katika maeneo mbalimbali udhibiti wake unafanywa na aidha na Manispaa au Mamlaka ya Majengo Tanzania *(TBA).* Kuna mgongano mkubwa baina ya *TBA* na Manispaa katika suala zima la ruhusu ya ujenzi katika Manispaa. Tatizo hilo limetokea katika Halmashauri ya Manispaa ya Tanga na Kinondoni. Nataka nieleweshwe ni nani hasa mwenye Mamlaka ya ruhusa ya ujenzi katika maeneo hayo?

Nchi yetu imepakana na nchi kadha ambazo hazina bandari. Sisi tumebahatika sana kuwa na Bandari ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar. Wingi wote huo wa bandari bado tumeshindwa kuzihudumia ipasavyo nchi zilizotuzunguka. Bado utendaji wa Bandari zetu ni mdogo na zina urasimu mkubwa, inachukuwa siku nyingi wateja kupata mizigo yao. Usafirishaji wa mizigo kwa kukosa reli yenye uhakika ni tatizo na kwa kupitia kwenye barabara kuna usumbufu mkubwa ukiwemo vituo vingi vya gari hizo kusimama kwa visingizio mbalimbali. Bila ya kuziboresha Bandari zetu, reli na huduma kwenye barabara zetu, nchi zinazotuzungunguka zitaelekea nchi nyingine kupata huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, ni aibu sana nchi yetu kuwa na Shirika la Ndege *(ATCL)* lisilo na uhakika na usafiri zake za nje ya nchi lakini hata kwa safari za ndani. Kila bajeti Wizara inaeleza kuwa wataliimarisha shirika hilo lakini inavyoonekana ni maneno tu. Nchi yetu ina vivutio vingi vya utalii lakini biashara ya utalii haiwezi kuimarika bila ya kuwa na Shirika letu la Ndege. Ni lini Shirika hili litaweza kukidhi haja inayokusudiwa badala ya maneno ya kawaida yanayosemwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, watu wengi wanapoteza maisha yao aidha kwa kusafiri kwenye Bahari yetu au kwa uvuvi lakini hakuna chombo maalumu cha uokoaji wa maisha ya wananchi hao. Nadhani umefika wakati kuanzishwa kikosi maalum cha uokoaji badala ya kutegemea Kikosi cha Polisi cha Bahari, Kikosi cha Bandari ni watu binafsi. Ninashauri kiundwe Kikosi cha Ulinzi wa Ukanda wa Bahari *(Coast Guard)* kazi yake iwe ni ulinzi wa Ukanda wa Bahari yetu na uokozi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa 74 wa Hotuba ya Waziri, kifungu cha 94, abiria waliosafirishwa kwa meli katika Maziwa Makuu kwa mwaka 2009/2010 ni 474,252 na kifungu 95 kwa mwaka 2010/2011 ni abiria 475,715 wataosafirishwa na meli katika Maziwa Makuu. Ni dhahiri tofauti iliyopo ya abiria watakaosafirishwa kwa mwaka 2009/2010 na 2010/2011 ni 1,464, hili ni ongezeko dogo. Ongezeko hilo dogo limetokana na changamoto zinazolikabili Shirika la *MSCL*. Ipo haja changamoto hizo zitafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutamka kwamba ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha miundombinu hasa ya barabara katika maeneo mbalimbali ya nchi. Aidha, ninaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza ahadi ya Rais ya kujenga walau barabara moja ya lami katika Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Spika, barabara ya lami ya urefu wa Km.5 ya Mjini Kahama imeanza kujengwa na ninaamini itaendelea kukamilishwa katika bajeti ya 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, suala la Reli ya Kati ni nyeti na linalohitaji maamuzi makini. Kuendelea kuiacha reli hii kama ilivyo sasa, ni kutowatendea haki wananchi wa Mikoa ambayo reli hii inapita lakini pia ni kutoitenda haki sekta ya uchumi ambayo inahitaji reli hii ili iweze kukua.

Mheshimiwa Spika, ninayo masikitiko makubwa kuona kwamba zoezi la kujenga barabara ya lami kupita ndani ya Serengeti linafanywa kisiasa zaidi kuliko kisaikolojia. Ni kwa nini suala hili linafanywa kisirisiri? Ninataka kujua barabara hii inajengwa kwa kiwango gani na ku-*facilitate* kupita kwa urahisi magari ya aina gani? Nitaiunga mkono Serikali kama barabara hiyo imejengwa kwa madhumuni ya kukuza na kuendeleza utalii lakini pia kama Access Road kwenda Mugumu kwa *light tracks* na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mashaka, kujengwa kwa barabara hii kwa kiwango cha kupitisha magari hadi tani 40, itakuwa ni kuinua Serengeti. Huo utakuwa mwisho wa "*Serengeti shall not die"* na itakuwa ni mwisho wa kauli mbiu ya utalii hivi sasa *"Tanzania the Land of Kilimanjaro, Serengeti and Zanzibar"*.

Mheshimiwa Spika, umaarufu wa Serengeti ni *migration* na eneo linalopitishwa barabara hii ni jembamba kwa maana nyingine msongamano wa wanyama katika eneo hili huwa mkubwa wakati wa *migration*. Swali barabara hii ikikamilika ni nani atakayesimamia upitaji wa magari na wanyama katika eneo hili?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Naunga mkono 100%.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. Nawaombea Mwenyezi Mungu awaongoze na kuwabariki ili warudi tena katika Bunge lako Tukufu kwa kishindo katika Uchaguzi huu Mkuu wa mwaka 2010 katika Majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, Waswahili husema "mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni". Nasema hivyo kwa sababu nimeisemea sana barabara T3 ambayo inatoka Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Igunga hadi Nzega, ni ya lami ila ikifika Nzega

*(Round About),* inakuwa si ya lami, ya changarawe. Ubao upo unaonesha mwendelezo wa T3 ila si lami tena toka Nzega kwenda Bukoba/Kagongwa ambayo ni Kahama kupitia Itobo.

Mheshimiwa Spika, kipande hiki ni cha 66 kms tu. Ni kipande kidogo ila inasikitisha sana kwa maonevu haya. Kwa kweli tumeonewa, hatujatendewa haki, ndio maana nimesema, mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Kwa misingi hiyo, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa S. Kawambwa (Mb) na Mheshimiwa E. Chibulunje (Mb) na Naibu Waziri, wote ni watani wangu wa jadi na watani ndio watendaji wakuu kwenye shughuli zote. Kwa misingi hiyo, mimi naamini jungu kubwa halikosi ukoko, basi nawaomba tena na tena, kama nilivyowaomba ana kwa ana, naomba wanitafutie vijisenti vya kutosha kumalizia hiki kisehemu cha kilomita chache tu, kilomita sitini na sita (66) tu.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa tu nyumba zilizo kandakando ya barabara zilishawekewa 'X' miaka mingi sana na wananchi wanashangaa, kwani hakuna kinachoendelea. Barabara hii kwa hivi sasa ni mbaya sana, afadhali ingekuwa nzuri kwa kiwango cha changarawe. Barabara hii ni maendeleo, ni uchumi na inahitajika kijamii pia. Naomba basi kama tunatafuta ukoko wa jungu kuu, basi itengenezwe vizuri kwa kiwango cha changarawe, kwani hii ni ahadi ya Rais.

Mheshimiwa Spika, barabara niliyoielezea hapo juu T3 inapitia Itobo kwenda Kahama, lakini tukiwa tunatafuta pesa kidogo ya hizo kilomita 66, naomba tusisahau kipande kidogo tena toka Itobo kwenda Makao Mkuu ya Jimbo yaani Bukene. Itakuwa maajabu sana kama lami ikifika Itobo na isifike Bukene. Naomba nayo iwe lami.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini penye nia pana njia, hiki kipande kitapatiwa au kitatendewa haki kuwa cha lami. Nitafurahi sana kama nitapatiwa jibu leo, lini itatekelezwa? Wapiga kura wangu masikio yao yako kwenye barabara hii. Nawaomba waseme neno moja tu ili watani zenu wafurahi.

Mheshimiwa Spika, lingine mimi naamini Wizara hii itatengeneza reli na mabehewa kwa Reli ya Kati, yaani Dar es Salaam/Tabora, Tabora/Kigoma na Tabora/Mwanza, ni muhimu sana. Hebu chakarikeni kuokoa usafiri kwa walalahoi, naomba sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kuipongeza Serikali ya CCM kwa kazi nzuri ya kutengeneza miundombinu ya usafirishaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Miundombinu awaeleze wananchi wa Dodoma – Manyara, ni kwa nini Serikali haisemi ukweli kuhusu barabara ya Dodoma – Babati? Mwaka jana barabara hiyo ilitengewa Shs.45 bilioni, hata hivyo katika Kitabu

cha Bajeti pesa hizo hazionekani? Pamoja na kutengwa kwa Shs.45 bilioni katika mwaka 2009/2010 hakuna kinachoendelea. Naomba Mheshimiwa Waziri awaeleze wanachi ni nini kilichokwamisha ujenzi wa barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, mwaka huu barabara hiyo imetengewa Sh.9.5 bilioni, je, kiasi hicho kidogo kitasaidia nini kama Sh.45 bilioni, hakikusadia kitu? Ombi langu Sh.45 bilioni za mwaka jana zijumuishwe na Sh.9.5 bilioni za mwaka huu 2010/2011 kujenga barabara ya Dodoma – Babati.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aeleze hatma ya ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Daraja hili limezungumziwa na Wabunge tangu Bunge hili lianze na Shirika la *NSSF* walikuwa tayari tangu miaka minne iliyopita kujenga daraja hilo. Tatizo lilikuwa ni Serikali kuidhamini *NSSF* tu, je, Serikali inasemaje kuhusu hilo?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza katika aya ya 62 kuwa Serikali imenunua hisa 51 za *RITES* lakini ikajikanyaga kuwa mazungumzo yanaendelea na *RITES* kununua hisa hizo. Je, ukweli ni upi? Hisa za *RITES* zimeshanunuliwa au bado? Usafiri wa reli ni muhimu kwa wananchi wanyonge na usafiri wa reli husaidia sana katika kutunza barabara kwani mizigo mingi itasafirishwa kwa reli, hivyo kuna umuhimu wa Serikali yetu kuweka umuhimu katika kutengeneza miundmbinu ya reli.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kuwa *ATCL* ni mdau wa usafirishaji wa anga kwani *ATCL* ni kama imekwishakufa. Serikali iweke mikakati madhubuti ya kufufua *ATCL*. Nchi iliyo huru haiwezi kukosa ndege zake. Atafutwe mbia wa kueleweka kuendesha Shirika la *ATCL*. Wananchi hawafurahishwi na Shirika hili kutofanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE.IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, kutokana na msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, napenda kufahamu ni lini upanuzi wa barabara ya Bagamoyo toka Kawawa Jet hadi Tegeta utaanza kutekelezwa? Pia naomba kufahamu ni lini nyumba zilizojengwa kwenye eneo la barabara hiyo zitaanza kuvunjwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mvua zilizonyesha katika Jiji la Dar es Salaam zimeharibu sana barabara zetu hasa Jimbo la Kinondoni, naomba Wizara iwaagize Wakurugenzi wa Halmashauri waanze kuzitengeneza barabara hizo na zile za changarawe zianze kuchongwa kwani hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, pia nakumbusha ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara ya Kagera hadi Mburahati, lini nayo itaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri mnazofanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kuipongeza Wizara kwa juhudi wanazofanya kuimarisha sekta ya miundombinu nchini.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa kukabiliana na changamoto kubwa za unyofu wa bajeti na changamoto nyingine mbalimbali. Mimi ninapenda kuchangia kiujumla juu ya *Air Tanzania* au Shirika la Ndege la Taifa. Matatizo ya *ATCL* kwa kiwango kikubwa yanatokana na ubadhilifu na hujuma iliyoanzia kwenye mikataba ya awali na sasa na baadaye usimamizi mzima wa *ATCL* baada ya kuvunjwa mkataba huo. Serikali ilikuwa na jukumu kubwa la kuwekeza pesa za kutosha kufufua Shirika kwa kupata ndege za kutosha kuendelea kuhudumia zile njia ambazo *ATCL* bado inamiliki za nje na ndani, bila hivyo tutakuwa tunafanya mzaha. Vilevile wafanyakazi wa *ATCL* kuanzia ngazi ya juu wamekua kwa muda mrefu wakilihujumu Shirika katika manunuzi, malipo mbalimbali, wizi wa moja kwa moja na mahusiano mabaya na wateja, hulipotezea hadhi Shirika na nchi. Menejimenti ya *ATCL* izingatiwe katika mfumo wowote ule utakaoundwa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara ni lazima iboreshwe mara dufu ili kuhakikisha kuwa gharama kubwa za usimamizi na urekebishwaji wa miundombinu ya reli zote muhimu, barabara za kuunganisha nchi na nchi jirani na barabara zinazounganisha sehemu za vijijini na mijini kurahisisha usafiri wa bidhaa na watu na kuleta maendeleo ya haraka zaidi. Ni afadhali Serikali ijinyime kwenye sekta nyingine ili kukamilisha miundombinu hii ili hata hayo maendeleo ya sekta nyingine yatafanyika kwa urahisi zaidi baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, rai, ni muhimu Wizara ikasimamia kwa ufanisi fedha inayotolewa ili utekelezaji wa miradi iwe kwa ufanisi zaidi kwa kuzingatia utawala bora. Wizara iguswe na shutuma na tuhuma zilizopo miongoni mwa watenda kazi wake wa ngazi zote na kuwachukulia hatua wote wanaojihusisha na tuhuma na matendo ya uhujumu na rushwa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusikia Wizara inaweka mikakati gani mahususi kuhakikisha mambo hayo hapa juu yanatekelezwa yaani kuna mipango gani baada ya kupata maoni yetu? Mnajipanga vipi kushughulikia matatizo haya ambayo yako ndani ya uwezo wa Wizara?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, narejea kukumbushia juu ya umuhimu wa kufungua barabara zinazoingia na kutoka Tabora. Tangu bajeti ya mwaka 2006/2007, Serikali mara zote imekuwa ikitoa ahadi ya kutekeleza. Wananchi katika Mkoa wa Tabora wamepokea kwa shangwe kupata Wakandarasi, wanachosubira kwa shauku na hamu ni kuona makandarasi barabarani. Ninatumaini leo atawapa kauli ya kuwatangazia lini mikataba itafanywa na kazi ya ujenzi itaanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Nzega ulishaleta maombi ya kupewa lami za mitaa ya Nzega Mjini kilomita 15.

Mheshimiwa Spika, *ATCL*, kila nchi ina Shirika lake la Ndege *"National Carrier"* inayobeba utambulisho wa Taifa. Shirika la Ndege la Tanzania ni muhimu sana katika kuinua uchumi na kuimarisha utalii. Nina shaka na hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa kutaka kulifufua Shirika hili, kwa sasa limedorora kiasi cha kuathiri huduma za usafirishaji ndani na nje ya nchi. Je, kuna hatua gani za makini zinazochukuliwa ili kulibadili ili shirika hili muhimu lianze kazi yenye tija? Kwa nini huduma zimekwama za kunusuru madeni ya ndani na nje?

Mheshimiwa Spika, *TRL/TRC*, ni muda mrefu sasa Kampuni/Shirika la Reli nchini limedorora hasa katika usafiri wa abiria na mizigo.Uwezo mdogo wa kubeba mizigo na hasa ile ya nchi za Kanda ya Maziwa Makuu. Ukijenga reli utaokoa barabara.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali iamue kwa dhati, kufufua Shirika la Reli, kuimarisha Reli ya Kati iwe ya kisasa na ni vema Shirika la Reli na Bandari iunganishwe ili kuleta "*linkage*" (fungamanisho).

Mheshimiwa Spika, nawatakia kazi njema, msichoke Wizara hii ni injini ya maendeleo kwa nchi.

**MHE. EMMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, nimpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa *TANROD* na Watendaji wote kwa pamoja, kazi inayoendelea nchini inaridhisha na suala la miundombinu linaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuweka Wakandarasi barabara la Isaka – Ushirombo – Lusahunga, ni kweli hali yake ilikuwa mbaya sana, tunaamini ujenzi ulioanza unatia moyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kwa kutenga fedha za Barabara zifuatazo Runzewe – Buseresele na Ushirombo – Mjikonga. Naamini Serikali itasimamia vizuri sio kulipua kazi.

Mheshimiwa Spika, ninayo maombi ambayo ni muhimu yafanyiwe kazi. Barabara la Ushirombo - Nyikonga ni kwa nini isiwekwe kwenye mpango wa kuweka lami kwa kuwa inaenda Makao Makuu ya Mkoa wa Geita?

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliahidi kuweka lami barabara ya Runzewe – Buseresere ni lini itawekewa lami?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali izungumze na Wakandarasi wanaojenga barabara ya Isaka – Ushirombo - Lusahunga waweke lami barabara za kuingia *stand* ya Ushirombo (Bukombe).

Mheshimiwa Spika, suala la *ATCL*, Mheshimiwa Balozi wa Tanzania nchini Dubai alifanya mazungumzo na mmiliki wa Emirate. Mmiliki huyu alikubali kuikwamua

*ATCL*. Inavyoonekana ndani ya watendaji wa *ATCL* hawakukubali. Ni nini kilisababisha mawazo ya Mheshimiwa Balozi na mmiliki wa Emirate yapuuzwe?

Mheshimiwa Spika, nampongeza tena kwa dhati Mheshimiwa Waziri jinsi anavyosimamia shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, taasisi zilizo chini ya Wizara hii na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya maendeleo ya miundiombinu nchini.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ikamilishe haraka Barabara Kuu zinazounganisha Makao Makuu yote ya Mikoa yetu kabla ya sherehe ya miaka 50 ya uhuru wetu. Aidha, barabara za Dar es Salaam, naomba ziboreshwe.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Shinyanga unatajwa katika Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Uwanja huu umeendelea kutajwa katika hotuba za nyuma za bajeti ya Wizara hii, hata hivyo hotuba ya bajeti ya mwaka huu 2010/2011, Uwanja wa Ndege wa Shinyanga haujatajwa kabisa, sasa umefutwa katika mipango? Maana kuna wananchi waliotoa ardhi yao kwa upanuzi wa uwanja bila fidia kulipwa hadi sasa, hivyo hawatumii tena ardhi hiyo pasipo fidia pia.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo mahususi kuhusu uwanja huu katika maana ya mipango ya kuupanua/kuuboresha.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani kwa niaba ya wananchi wa Makete, kwa Serikali kuboresha barabara zote za Mkoa zilizopo Makete kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea katika babaraba ya Njombe – Makete.

(ii) Matengenezo ya barabara ya Makete – Bulongwa – Kikondo ambayo yamewezesha barabara hii kupitika mwaka wote.

(iii) Matengenezo ya barabara ya Nkenja –Kilolo na kuweza kupitika majira yote ya mwaka.

(iv) Matengenezo ya barabara ya Kitelo – Matamba - Mfumbi, ambayo pia inapitika majira yote ya mwaka.

(v) Kupandisha hadhi barabara ya Tandala – Lupila – Mlangali (Ludewa) kuwa ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe - Makete – Mbeya, baada ya kutangazwa Mkoa mpya wa Njombe, barabara hii sasa inaunganisha Mikoa miwili yaani Mbeya na Njombe, hivyo, tunaomba Serikali ijenge kwa kiwango cha lami hadi Mbeya.

Hii ni barabara ya kiuchumi inayoweza kuongeza kasi ya kujenga uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbeya (Isyonje) – Makete – Tandala – Ludewa – Madaba (Songea) inaunganisha Mikoa mitatu yaani Mbeya, Njombe, Ruvuma na pia ni barabara inayopita kwenye Milima ya Livingstone hivyo inaweza kukuza utalii na uchumi. Tunaomba Serikali ijenge kwa kiwango cha lami kipande cha barabara hii yaani Tandala – Lupila – Ludewa kilichopandishwa hadhi, haijetengewa fedha kwenye bajeti ya mwaka huu yaani 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibena – Lupembe – Taveta (Kilombero), sasa inaunganisha Mikoa ya Njombe na Morogoro na ni barabara ya kiuchumi sana katika Mkoa huu mpya. Tunaomba Serikali ianze kuona namna ya kutengeneza barabara hii ili fursa zilizopo ziweze kutumika.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja na kumtakia Mheshimiwa Waziri na Kikosi chake chote ufanisi wa kiutendaji pamoja na kwamba kiasi kilichotengwa kwa shughuli za Wizara hakitoshi kushughulikia majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali na hususan Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa jinsi ambavyo suala la ujenzi wa barabara za kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tabora hadi Dodoma kwa upande mmoja na Kigoma hadi Nyakanazi (Kagera) kwa upande mwingine linavyotekelezwa. Kadhalika Wizara kwa kusimamia ujenzi wa barabara ya Mwandiga – Manyovu, imeweka mazingira muafaka ya kiuchumi wa Tanzania hususani wana Kigoma na nchi jirani ya Burundi kupitia Manyovu.

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza hatua ambazo Mheshimiwa Rais Kikwete na Serikali yake inachukua za kuendelea kutafuta fedha za nje na ndani kwa ajili ya ujenzi wa barabara za kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine ya Kagera na Mwanza, Kigoma na Tabora hadi Dodoma na Dar es salaam na pia Kigoma na Rukwa hadi Mbeya, Iringa, mpaka Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Mheshimiwa Rais zimewezesha kuweka mkazo wa ujenzi wa Daraja la mto Malagarasi kuelekea Tabora, pamoja na barabara za Kigoma hadi Tabora. Napenda kuipongeza Serikali kwa hatua ilizoonyesha za ujenzi wa barabara Simbo, Ilagala hadi Kaliya, umbali ambao barabara hii imefikia ni wa kuleta matarajio na matumaini kwa wananchi waishio mwambao wa Ziwa Tanganyika Kusini. Hata hivyo, naiomba na kuishauri Wizara ione umuhimu wa kuijenga barabara hii hadi mwisho ifikapo Desemba, 2011 kama ahadi iliyotolewa na uongozi wa *TANROAD* kwenye vikao vya *RCC* mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutaka kuhimiza kumalizika kwa barabara ya Simbo – Ilagala – Kaliya, nashauri suala la Daraja la Mto Malagarasi pale Ilagala ili

kuunganisha Ilagala na Kaliya kwa daraja badala kivuko duni kilichopo pale Ilagala lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa hatua inazochukua kulinusuru Shirika la Reli Tanzania *(TRL).* Hata hivyo, tukiri kuwa uamuzi wa ubinafsishaji haukuwa makini, tusirudi huko. Tuhakikishe chombo hiki kinaendeshwa kiufanisi ili kujenga uchumi wetu. Nchi jirani za *DRC*, Burundi, Rwanda na vilevile Zambia, wanategemea reli hii, ufanisi wa reli hii pia ni kichocheo cha ajira ndogo kwa wakazi wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara za kulipia, tusilalamikie umasikini, hivi Wizara imejielekeza katika kutafuta wawekezaji wa kujenga barabara za kulipia ili kiwe kichocheo cha ujenzi wa barabara nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege/Shirika la Ndege, nashukuru sana juhudi zinazofanywa na Serikali za kupanua na kuupa uhai Uwanja wa Ndege wa Kigoma na hatimaye kuwa pia na Shirika la Ndege imara ambalo litafanya safari kwa uhakika. Hivi hatua za kuimarisha Shirika la Ndege ni zipi kwa lengo la kuwa *"National Carrier"* yetu?

Mheshimiwa Spika, mwisho, natamka naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Siha, naomba kuchukua fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa asubuhi ya leo.

Nampongeza pia Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, kwa msaada mkubwa anaoutoa kwa Mheshimiwa Dr. Kawambwa na hivyo kuleta ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kilio changu ni kile kile cha barabara itokayo Bomang'ombe – Sanya Juu hadi Kamwanga iliyopo ukurasa wa 140 katika jedwali lililoambatanishwa. Pamoja na jitihada zote za kukumbushia suala hili mara kwa mara na kuonana na Mheshimiwa Waziri bado naona kipande hiki cha hii barabara hakikutengewa chochote kile nimesikitika.

Nakumbusha kuwa barabara hii ilishafanyiwa *"feasibility study" ,"preliminary design"* na *"detailed design"* ili kuondokana na tatizo la hii barabara hasa wakati wa mvua. Bado sijakata tamaa, naamini Serikali itazidi kufuatilia suala hili na hatimaye ufumbuzi utapatikana. Ukiangalia jedwali lililopo ukurasa wa 140 barabara hiyo ndiyo peke yake ambayo haikugawiwa fedha yoyote ile iwe ya ndani au ya nje.

Mheshimiwa Spika, nilikwishamwomba Waziri akubali walau tuanze na kilomita tatu halafu tuendelee na hizo nyingine zitakazobakia lakini naona imeshindikana, chonde chonde Waziri Kawamba, watu wangu wanakumbusha kila siku kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Sanya Juu akiwahakikishia kuwa barabara ili itajengwa kwa kiwango cha lami ili kukamilisha ile *"ring road"* kuzunguka Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Siha naye alisisitiza kuwa Serikali ilikwishaahidi kwa hiyo barabara hiyo itajengwa.

Mheshimiwa Spika, nitafurahi kusikia neno moja tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Kawambwa na roho yangu itapoa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, najua wengi hawakuweza kupata nafasi, lakini ndiyo hivyo. Sasa ni zamu ya Serikali kuweza kutoa maelezo na mpangilio nilionao hapa ni kwamba, Mheshimiwa Waziri anazo dakika 25 na Naibu Waziri anazo dakika 15 kwa hiyo, jumla yake wanazo dakika 40. Dakika 10 za kawaida za uchangiaji ambazo zingekuwa za Naibu Waziri na dakika 30 za Waziri, jumla 40. Wamegawana dakika 15 kwa 25. Namwita sasa Naibu Waziri wa Miundombinu kwa ajili ya ufafanuzi wa baadhi ya hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa bafasi hii nami niweze kuchangia hoja hii ya Makadirio ya Wizara yetu ya Miundombinu iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa shukurani kwanza kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa heshima aliyonipa na kuniamini na kuniteua mara nne katika kipindi hiki cha muhula wake wa kwanza wa Serikali ya Awamu na Nne kutumikia kwa wadhifa huu wa Naibu Waziri katika Wizara mbalimbali zikiwemo Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na hatimaye Wizara hii ya Maendeleo ya Miundombinu. Kwa unyenyekevu mkubwa, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani aliyoonesha juu yangu na wapigakura wangu wa Jimbo la Chilonwa wanamshukuru sana. Mimi na wapigakura wangu wa Jimbo la Chilonwa tunamuunga mkono katika harakati zake alizokwishazianza za kutafuta ridhaa ya kutuongoza kwa muhula wa pili na tunamtakia kila la kheri Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru sana Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa uongozi wake mahiri na maelekezo yake kwangu juu ya utekelezaji wa majukumu ya kazi zangu katika Wizara mbalimbali. Sisi wana-Chilonwa tunamtakia kila la kheri na kuwaomba wapigakura wake wa Jimbo la Mpanda Mashariki, wamrudishe tena hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa kwa jinsi alivyonishirikisha katika majukumu ya kuiongoza Wizara hii ya Miundombinu. Nimefarijika sana pia kwa ushirikiano nilioupata kutoka kwa Watumishi wote wa Wizara ya Miundombinu, pamoja na Taasisi zilizopo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Eng. Omar A. Chambo kwa kunipa msaada wa kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu na ninaomba waendelee na moyo huo wa ushirikiano kwani kwa kufanya hivyo, mafanikio yanaweza kupatikana. Ninawashukuru sana Watumishi wote wa Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nimshukuru sana mke wangu mpendwa - Vailet ambaye alikuwepo hapa asubuhi lakini bahati mbaya nadhani taarifa za kuwepo kwake hapa hazikukufikia, lakini ulipomtangaza nimefarijika sana. Nashukuru sana pamoja na familia yangu kwa msaada ambao wameendelea kunipa kwa kunifariji na kunipa moyo wa kuweza kutekeleza majukumu ya kazi zangu zote za Ubunge na hizi za Wizara kwa utulivu na amani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie shukurani zangu kwa kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Chilonwa kwa imani waliyoonesha juu yangu kwa kunipa fursa ya kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni kwa kunichagua kwa vipindi vitatu mfululizo. Nawashukuru kwa jinsi walivyonipa ushirikiano katika kutekeleza mipango mbalimbali ya Jimbo letu. Napenda niwakumbushe tu kuwa bado tunazo changamoto nyingi mbele yetu katika kujiletea maendeleo katika Jimbo letu na mimi mtumishi wao bado niko tayari kushirikiana nao katika kukabiliana na changamoto hizo. Kwa unyenyekevu mkubwa, naomba niwaahidi kuendelea na azma yangu ya kutii na kutimiza wajibu wangu kama nilivyotekeleza kwa vipindi vitatu vilivyotangulia. Naomba tushikamane na tusonge mbele pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nianze kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwanza kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tuunge mkono hoja hii ili mipango ya miradi mbalimbali iliyoombewa fedha hizi iweze kutekelezwa.

Pili, nieleze tu kwamba, kwa ujumla hoja za Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kupitia hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi, hotuba ya Waziri Mkuu pamoja na hii yetu ya leo, zote tutazitolea majibu kwa maandishi katika kipindi hiki kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Bunge hili. Lakini, kama ilivyo kawaida, Mheshimiwa mtoa hoja atawatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kwa kuzungumza kwa kuwataja.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kuanza kujibu hoja mbalimbali, naomba nipokee kwa mikono miwili shukurani na pongezi nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa utekelezaji mzuri wa Wizara yetu na Serikali kwa ujumla katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo ni ishara ya wazi kabisa kwamba, ushindi wa CCM mwaka huu ni dhahiri.

Mheshimiwa Spika, sasa nipitie baadhi ya hoja kwa sababu hoja ni nyingi na muda ni mfupi. Nianze kwa hoja ambayo ilikuwa inasema Serikali iboreshe miundombinu ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano. Hoja hii ilichangiwa na wachangiaji wengi kidogo katika hotuba zilizopita na hata hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja hii ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Azan Zungu,

Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na wengine waliochangia leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, nijibu tu kwamba ili kukabiliana na msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* imekamilisha utafiti wa mpango kabambe wa kuboresha barabara za Jiji la Dar es Salaam *(Dar es Salaam Roads Master Plan Study)* ambao umeainisha maeneo ya kipaumbele katika kuboresha miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kupitia mpango huu, Serikali imeanza ujenzi wa baadhi ya barabara zikiwemo za kupunguza msongamano, upanuzi wa barabara ya Mwenge – Tegeta na barabara ya pete *(Dar es Salaam out ring road).* Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kuboresha makutano ya barabara kwa kujenga barabara za juu, mazungumzo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, yako maombi ya kupandisha madaraja baadhi ya barabara nchini na hii imechangiwa na wachangiaji wengi. Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Luka Siyame, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa William Shellukindo.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba suala hili la kupandisha barabara madaraja ni zoezi linaloendelea, kwa hiyo, tunapopandisha barabara madaraja bado mchakato unaendelea kwa kuzifanyia uchunguzi barabara nyingine ili kuona kama zinatimiza vigezo na kama zinatimiza vigezo, basi zinapandishwa madaraja, na zikishapandishwa madaraja mwaka wa fedha unaofuatia ndiyo zinaingia katika kuhudumiwa na *TANROADS* kwa sababu ukipandisha barabara daraja, siku hiyo hiyo tu haiwezekani fedha zake zikawa zimeshatengwa katika ngazi inayostahili.

Kwa hiyo, ningependa wale Waheshimiwa wote ambao wametoa hoja hii ya barabara kupandishwa madaraja wazingatie hii kwamba, kwanza kuna utaratibu ambao unatutaka tupitishe kwenye Halmashauri zetu za Wilaya, Vikao vya Bodi ya Barabara *(RCC)* na hatimaye mapendekezo yamfikie Mheshimiwa Waziri, lakini kwa kutum**ia** ile Kamati yake ambayo inamshauri, utaratibu huu unaendelea na hauna kikomo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianze ujenzi wa daraja kama alivyoeleza Mheshimiwa Msindai. Maelezo ni kama alivyoelekeza yeye mwenyewe kwamba, ujenzi umekwishaanza.

Mheshimiwa Juma Kilimbah wa Iramba Magharibi amesema kwamba barabara za Shelui – Mtoa – Kisonga – Mkunde hadi katika kiungo cha barabara ya Mkoa haikupanda. Nimeishatoa maelezo.

Mheshimiwa Abdallah Kigoda anazungumzia habari ya fedha za fidia kwa miradi ya barabara za Mkata - Handeni na Korogwe – Handeni zilipwe ili kuruhusu ujenzi wa barabara. Fidia italipwa kwenye maeneo ambayo ujenzi utaanza katika mwaka huu wa

fedha wa 2010/2011. Lakini, vilevile mkandarasi atahimizwa kufanya matengenezo kwani fedha zote za malipo ya awali zimekwishalipwa.

Mheshimiwa Tatu Ntimizi – Mbunge wa Igalula anaomba maelezo ya kina kuhusu ujenzi wa barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora. Pengine hili niliache, Mheshimiwa Waziri atakuja kulitolea maelezo kwa kirefu kwa sababu tayari baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine kutoka Tabora akiwemo mtani wangu Mheshimiwa Kaboyonga wamelizungumzia hili kwa uzito unaostahili. Hivyo pengine niliache ili lijumuishwe katika maelezo hayo ya jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Pascal Degera - Mbunge wa Kondoa Kusini na dada yangu Mheshimiwa Zabein Mhita wameulizia barabara hii ya Dodoma – Kondoa – Babati na niseme tu kuwa na mimi ni mdau katika barabara hii. Swali kubwa ambalo aliuliza hapa Mheshimiwa Mhita ni kwamba, barabara itaanza kujengwa lini? Nami nataka tu nimweleze tu kwamba, awamu ya kwanza itahusu sehemu ya Babati – Bonga na barabara za Kondoa Mjini ambapo Mkataba wa Ujenzi ulitiwa saini mwezi Mei mwaka huu. Kwa sehemu ya Dodoma - Mayamaya yenye urefu wa kilomita 43, Mkataba wa Ujenzi umetiwa saini jana tarehe 28 Juni, 2010.

Aidha, mchakato wa kumpata mkandarasi wa kujenga daraja la Kolo unaendelea. Lakini kwa uhakika kabisa nikijibu swali la Mheshimiwa Mhita ni kwamba ujenzi utaanza rasmi mwezi Septemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ephraim Madeje - Mbunge wa Dodoma Mjini, ujenzi wa barabara ya Dodoma/Iringa uanzie pande zote mbili. Jibu ni kwamba kwa kurahisisha utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu tatu. Iringa - Migori kilomita 95, Migori - Fufu kilomita 93 na Fufu - Dodoma kilomita 70 na ninavyozungumza sasa hivi mchakato wa kutafuta makandarasi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, orodha ni ndefu, Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mbunge wa Mpwapwa anauliza Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara ya Manchali – Chalinze – Kiyegeya - Ng’ambi mpaka Pandambili. Katika mwaka wa fedha 2010 Serikali imepanga kuifanyia barabara hii matengenezo ya muda maalum na kiasi cha shilingi milioni 169, zimetengwa na vile vile hoja hii ilikuwa imeletwa na Mheshimiwa Job Ndugai.

Mheshimiwa Masilingi ametupongeza na sisi tunashukuru kwa pongezi hizo, ni ishara tosha kwamba tutakwenda pamoja kwenye uchaguzi na pongezi hizo zitaendeleza ushindi wa Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Mwera, barabara ya Tarime - Nyamwaga inajengwa kwa kiwango cha lami kidogo kidogo. Kutokana na ufinyu wa bajeti Serikali imejenga kila mwaka kadri ya bajeti inavyoruhusu. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 shilingi milioni 120 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah amependekeza Serikali iendeleze bandari ya Mtwara kwa ajili ya kuchochea maendeleo ya sekta ya uchimbaji gesi. Serikali kupitia *TPA* imeanza kutekeleza mradi huu kuendeleza bandari

ya Mtwara likiwemo eneo la Msangamkuu ili kuhudumia sekta ya uchimbaji gesi unaoendelea Mtwara. Benki ya Maendeleo ya *ADB* imeshirikishwa katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, eneo la *road safety,* Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali anazungumzia matatizo kwamba wanapata abiria wa mabasi kwa kuambiwa wanatakiwa kusafiri na mzigo wa uzito usiozidi kilo 20. Kama ilivyo utaratibu katika vyombo vya usafiri ikiwa ni pamoja na usafiri wa ndege na treni vile vile usafiri kwenye mabasi wanaruhusiwa kuwa na kilo 20 tu kwa tiketi moja. Kwa hiyo, hilo ni utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba hoja nyingi zitajitokeza katika maelezo yetu kwa njia ya maandishi. Pengine nimalizie kwa kujibu hoja za usafiri majini. Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Joyce Masunga alisema Serikali ijitahidi ili kupunguza ajali zinazotokana na vyombo vya usafiri kwa kufanya ukaguzi wa vyombo hivyo mara kwa mara. Hiyo ndiyo kazi inayofanywa sasa hivi na *SUMATRA*.

Msemaji wa Kambi ya Upinzani - Mheshimiwa Zitto Kabwe - Mbunge wa Kigoma Kaskazini sekta ya usafirishaji ipewe kipaumbele na Serikali katika kutetea maamuzi yanayosema yaendelee kisekta. Hiyo ndiyo kazi inayofanywa sasa hivi na *SUMATRA*. Brig. Jen. Hassan Athumani Ngwillizi sekta ya reli, bandari na viwanja vya ndege vipewe kipaumbele na umuhimu unaostahili. Ushauri unazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hoja ni nyingi kwa kuziorodhesha hapa moja moja na wakati wenyewe hautoshi ni kama nilivyoahidi tu kwamba tutazitolea majibu kwa umakini sana na kila Mbunge ataondoka na majibu yake kabla ya Bunge hili halijavunjwa na kwa hiyo, nimwachie Mheshimiwa mtoa hoja aje kuhitimisha hoja yake na nirudie kusema kwamba naiunga mkono hoja na naomba wenzangu wengine wote pamoja na Mheshimiwa Kaboyonga na Aziza Sleyum Ali wote tuiunge mkono hoja hii ili kazi zetu ziweze zikatekelezwa na hayo mengine mliyoyaomba yaweze vile vile kupatiwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa ili aweze kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwako wewe binafsi kwa jinsi ambavyo umesimamia majadiliano ya Bajeti ya Wizara yangu, hekima, busara na upeo wako mkubwa ambao umeutumia katika kusimamia kwa umahiri mkubwa majadiliano haya. Hii inaonesha ni jinsi gani Chama cha Mapinduzi kilivyo na hazina kubwa ya viongozi katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu - Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga - Mbunge wa Singida Kusini kwa maoni aliyotoa ya Kamati yake. Ni wajibu wangu kuishukuru sana Kamati hii ya Bunge kwa ushirikiano ambao amenipa mimi binafsi na kwa Wizara kwa ujumla katika kufanikisha shughuli za Wizara katika kipindi cha miaka mitano ya utendaji wa Wizara hii. Mapendekezo ya Kamati ni ya kitaalamu na yenye upeo wa kisera ambayo kwa ujumla wake yatasaidia sana kuboresha sekta hii kwa wakati huu na wakati ujao.

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu sekta ya miundombinu kwa maoni na mapendekezo yake kuhusu bajeti ya Wizara ya Miundombinu. Napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Zitto kuwa Serikali inathamini mchango wa Kambi ya Upinzani na itazingatia katika mipango ya utekelezaji wa mipango yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao waliyoitoa kwa maandishi na kwa kuzungumza hapa Bungeni wakati wakijadili hoja ya Wizara yangu. Naomba nimshukuru sana Naibu Waziri - Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza walikuwa 16 na waliochangia kwa maandishi walikuwa 73. Michango yao iliyojaa busara itatusaidia sana katika kusimamia utekelezaji wa bajeti hii pamoja na kuboresha sekta ya miundombinu katika siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwatambua waliochangia hotuba yangu kwa kuzungumza kama ifuatavyo:- Kwanza Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Brig. Jen. Mstaafu Hassan Athumani Ngwillizi, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mheshimiwa Arch. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga na Mheshimiwa Bujiku Sakila. *(Makofi)*

Naomba pia kuwatambua waliochangia hotuba yangu kwa maandishi kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Margareth Sitta, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Arch. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Tatu Ntimizi,

Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Lucy Nkya, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa James Daudi Lembeli na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Felister Bura. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Emannuel Luhahula, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Zulekha Yunus Haji, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Athumani Ngwilizi, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa na Mheshimiwa William Lukuvi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Milton Mahanga, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu. Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Nazir Karamagi na Mheshimiwa Damas Nakei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwatambua Waheshimiwa hawa waliochangia na pengine labda nitakuwa nimeacha jina, naomba radhi kwa yule ambaye sikumtaja jina lakini yule ambaye sikumtaja jina lake naomba niletewe jina ili niweze kulitambua na niombe radhi kwa wale ambao pengine kwa namna moja au nyingine sikutamka majina yao vizuri sio kwa kuwadharau isipokuwa tu "Waswahili wanasema ulimi hauna mfupa".

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakubaliana na maoni ya Kamati kuhusu haja ya kuongeza vyanzo vya mapato vya ziada ya ndani kwa lengo la kutunisha Mfuko wa Barabara, kuangalia upya utaratibu wa utoaji wa vibali vya kusafirisha mizigo mizito, kupunguza msongamano kwenye mizani na kuboresha usafiri kwa kudhibiti utoaji wa leseni za usafirishaji wa pikipiki. Aidha, Serikali imepokea ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vyake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Mtendaji Mkuu wa *TANROADS*. Wizara ilikutana na Bodi ya *TANROADS* na Mtendaji Mkuu kama vile Kamati ilivyoagiza. Katika kikao hicho ilielekezwa ifuatavyo kwamba wafanyakazi waliokuwa na mikataba waendelee na kazi zao hii iliwahusu Mameneja wa *TANROADS* wa Mikoa 10 ambayo ni Ruvuma, Dodoma, Iringa, Morogoro, Arusha, Kagera, Shinyanga, Dar es Salaam, Mwanza na Tabora ambao wote walitakiwa kuachishwa kazi.

Aidha, Wakurugenzi waliokuwepo *TANROADS* ambao wote aliowateua Mkurugenzi Mtendaji kabla ya muundo mpya wa *TANROADS* wabakie badala ya

kuwaondosha ikiwa ni mchakato wa kujaza nafasi hizo kwa mujibu wa taratibu za kujaza nafasi hizo kwa Wakala wa Serikali. Suala hili linaendelea kusimamiwa na Bodi ya *TANROADS* na sisi Wizarani tunalipa umuhimu mkubwa kwa sababu ufanisi wa *TANROADS* ndio ufanisi wa Wizara ya Miundombinu na suala hili la ujenzi wa miundombinu wa barabara Tanzania ni kero kubwa kama ambavyo Mheshimiwa Spika ulivyoliona limeleta joto kubwa katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda wa utendaji kazi wa Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* Serikali bado inalifanyia kazi suala hili na muda muafaka ukifikia basi tutalitolea maelekezo. Ni kweli kwamba kuna utata kati ya barua na mikataba ambayo Mtendaji Mkuu yule anayo na hili ni suala la kisheria na ushauri wa kisheria lazima upatikane na Mwanasheria Mkuu wa Serikali lazima alitolee maelekezo suala kama hili. Kwa hiyo, si suala lile ambalo Serikali inaweza kukurupuka tu na kufanya maamuzi ambayo hayana ushauri wa kisheria kutokana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Itakapofikia mwisho wa ufafanuzi wa jambo hili Serikali haitakuwa na kigugumizi ya kuweza kulitolea kauli na kuchukua hatua zile muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya barabara ambayo ni hoja pia ya Kamati ya Miundombinu, miradi ya barabara hupangwa na Serikali kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Pia ahadi za viongozi wakuu na kutekeleza mpango wa uwekezaji katika miundombinu ya usafirishaji *(TSIP),* kama nilivyoeleza mwanzoni katika hotuba yangu, utekelezaji wake hufanywa na *TANROADS* na kusimamiwa na Wizara ya Miundombinu na hii kazi inafanywa kama ni kati ya timu kati ya Wizara ya Miundombinu kama msimamizi mkuu na mwenye mali na pia wenzetu *TANROADS* ambao wanafanya kazi ya kila siku. Hii wala sio kazi ya mtu mmoja mmoja ni kazi ambayo wote tunashirikiana kwa pamoja kuweza kuifanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni ya Kambi ya Upinzani, baadhi ya masuala yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ni pamoja na umuhimu wa uharakishaji wa maamuzi ndani ya sekta. Hata hivyo, maamuzi mengi yanahusisha mikataba ambayo inahitaji uchambuzi wa kina, umakini na mashauriano ya kutosha kabla ya kufikia maamuzi. Uharaka tunauhitaji, lakini lazima kazi hii ifanywe kwa kina, kwa sababu mikataba hii bila ya kufanyiwa kazi kwa kina na kwa umakini inaweza ikatuletea matatizo. Kwa mantiki hiyo kama maamuzi husika yatafanyika kwa pupa na jazba yanaweza kuliingiza Taifa letu katika gharama kubwa na migogoro ya kisheria.

Kuhusu suala la utekelezaji wa programu ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi *(TSIP),* tathmini iliyofanywa mwaka 2009 kuhusu utekelezaji wa programu hii imeonesha kwamba asilimia 40 ya miradi iliyopangwa kutekelezwa katika awamu ya kwanza ya *TSIP* tayari imetekelezwa. Changamoto kubwa tuliyonayo ni ongezeko kubwa la gharama ya ujenzi wa barabara na ongezeko hili sio ongezeko ambalo tungependa litokee, lakini nje ya uwezo wetu, ongezeko hili limetokea mwaka 2006 wakati Serikali ya awamu ya nne inaanza kazi barabara ya lami tulikuwa tunaijenga kwa gharama ya Dola 3,500 kwa kilomita na hivi sasa tunaijenga barabara hiyo hiyo kwa wastani wa Dola 800,000 kwa kilomita moja ongezeko ambalo ni zaidi ya maradufu. Kwa maana hiyo ni

kwamba kwa kadri Serikali hii ilivyojitahidi kuongeza fedha hata ikiongeza fedha zake katika bajeti maradufu, bado haiwezi kujenga barabara zile zile ambazo ilikuwa inajenga katika mwaka 2006 wakati Serikali imeingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali katika utekelezaji wa programu hii ni pamoja na kutoa kipaumbele kwa sekta binafsi kushiriki katika kujenga miundombinu ya uchukuzi kupitia mpango wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Mikakati ya uboreshaji wa reli ya kati ni suala linalopewa kipaumbele na Serikali kwa lengo la kuimarisha mfumo wa reli nchini ikiwa ni pamoja na kuboresha njia ya reli, mawasiliano na kuboresha miundombinu ya stesheni za reli kwa lengo la kuwavutia wawekezaji.

Kuhusu utoaji wa huduma ama *ground handling services* katika kiwanja cha ndege cha *KIA*, kimsingi Serikali imeshaondoa ukiritimba katika huduma hii tangu mwaka 2007 na Makampuni ya ndege yanaruhusiwa kujihudumia yenyewe. Hata hivyo, katika Kiwanja cha Kilimanjaro bado *Swisspot* inaendelea kutoa huduma kutokana na ukweli kwamba miundombinu ya *KIA* hairuhusu Makampuni zaidi ya moja kutoa huduma kwa wakati mmoja. Miundombinu pamoja na *volume* ya wasafiri haijaweza kuruhusu kuwa na watoa huduma zaidi ya mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Ndege la *ATCL*, Serikali inaandaa mkakati wa kuliunda upya ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji. Niseme kwamba Serikali inaandaa mkakati lakini hili ni tatizo ambalo limetokea baada ya Serikali kufanya juhudi kubwa sana kuliondosha Shirika la Ndege la *ATCL* kutoka kwenye matatizo ya kiuendeshaji. Mwaka jana tarehe 11 Juni, 2009 Serikali ilikuwa imeshafikia makubaliano na mwekezaji wa Kichina kwa ajili ya kuingia ubia na Serikali kuendesha Shirika la Ndege la *ATCL*. Ni kweli mwekezaji huyo alikuwa na nia thabiti na aliweka vigezo vingi ambavyo vilionesha kwamba ana nia ya kushirikiana na sisi.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya hapo, tukaingia katika tatizo moja baada ya lingine ambalo haliko kwenye uwezo wa Serikali, ni wabia hawa au wawekezaji hawa wana vigezo vyao chungu nzima vya kuingia kwenye biashara na mara mambo yakibadilika kama tunavyofahamu mwaka jana dunia iliingia katika matatizo ya kiuchumi ambayo Mashirika mengi na wawekezaji wengi walibadilisha mipango yao kiuwekezaji. Hatuna njia ya kuweza kuyabadilisha hayo. Kama isingetokea hivyo kwamba tarehe 11 Juni, baada ya kufanya makubaliano ya mwisho na mwekezaji leo tusingekuwa na kauli ya kuuliza kuhusu *ATCL* kwa sababu mipango yote ilikuwa mizuri na watu ambao walikuwa wawepo kama waendeshaji ni Kampuni nzuri na wenyewe walikuwa wameweka nia ya kuweka fedha ya kutosha ya kuendesha Shirika hili.

Lakini kwa vile haikutokea kwa ajili ya kuliendesha Shirika hili, lakini kwa vile haikutokea hata baada ya pale tulipofikia hatua ya mwisho basi leo ndiyo kubwa na kadhia hii ya kulizungumzia Shirika la *ATCL*. Lakini niseme tu kwamba Serikali bado ina mkakati maalum na wa hakika wa kuhakikisha kwamba Serikali hii au Taifa hili linarusha bendera yake Kimataifa tofuati na nchi nyingi ambazo hata zinazotuzunguka nyingi zingine hazina Mashirika yao. Uganda haina Shirika lake la Taifa, Zambia haina Shirika lake la Taifa na nchi kadhaa ambazo zinatuzunguka. Hata Kenya ni chini ya

asilimia 13 ndani ya Shirika la Kenya, kwa hiyo huwezi kuita kwamba ni shirika ambalo linamilikiwa kwa asilimia kubwa na Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Spika, naomba nipitie hoja za Wabunge baada ya kuzungumzia hoja za Kamati ya Miundombinu na Kambi ya Upinzani. Sasa naomba nitoe ufafanuzi kuhusu michango ya Wabunge waliochangia hoja yangu kwa maeneo makuu. Kwenye maeneo makuu yaliyojitokeza kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge, kabla sijafanya hivyo naomba nirudie ujumbe wa Wabunge wengi ambao wamekwishatoa kwamba miundombinu ya uchukuzi pamoja na huduma zake ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa letu na kuleta maisha bora kwa wananchi wote. Miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na vivuko.

Naomba kuchukua fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imepokea kwa moyo mkunjufu michango hiyo ya Waheshimiwa Wabunge na niahidi kwamba tutaifanyia kazi michango hiyo ambayo kwetu itakuwa dira katika utendaji wetu wa kazi wa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuanza kutoa ufafanuzi kuhusu hoja zilizotolewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye eneo la barabara ambalo Waheshimiwa Wabunge walisemea sana na kwa hisia kubwa inahusiana na uboreshaji wa mtandao wa barabara katika nchi nzima. Michango hiyo ni ya msingi kwa kuzingatia umuhimu wa barabara katika uchumi wa Taifa letu. Hata hivyo changamoto kubwa tuliyokabiliana nayo kama nilivyosema awali ni kwamba tumekabiliana na changamoto ya upandaji wa gharama za ujenzi wa barabara lakini pia uhaba wa fedha zetu za ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara. Tungependa tuwe na pesa zaidi na tusiwasaidie wahisani lakini hatuna pesa zile ambazo zingeweza kujenga barabara ambazo tunazihitaji. Serikali inafanya jitihada za kutafuta vyanzo mbalimbali vya kukidhi mahitaji ya Kibajeti katika sekta ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano ambayo sasa inamalizika mwaka 2010 miradi ambayo tumeitekeleza Tanzania nzima imeweza kujenga jumla ya kilomita za barabara 1,398.6 na bado tunapoenda katika miaka mitano ijayo tumepanga ujenzi wa kilomita zinazozidi 6,000 hii ni shauku yetu au ni kiu yetu ya maendeleo ya barabara. Lakini haitaambatana na uwezo wetu wa kifedha wa fedha za ndani ya barabara hizi. Kazi hii ni kubwa lazima tuiwekee nia thabiti na lazima tuelewe mzigo mkubwa ambao umetukabili na ni kweli tunataka maendeleo lakini maendeleo hayo hayateremka kama mvua isipokuwa inategemea jasho letu la kuzalisha fedha za ndani na zile ambazo tutapata kwa wahisani kuweza kujenga barabara hizi ambazo tunataka kuzijenga.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuimarisha barabara nchini, Serikali inaendelea na jitihada za kushirikisha sekta binafsi katika uboreshaji wa miundombinu. Jitihada hizi zinapewa msukumo baada ya kupitishwa kwa sera ya Taifa ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ama *PPP*.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inakamilisha mchakato wa kutunga Sheria ya *PPP* ili kuweza kuwavutia wawekezaji katika sekta hii. Sheria hii imeshasomwa kwa mara ya kwanza ndani ya Bunge hili mwezi wa Juni. Kwa hiyo, tunatarajia kwamba kwa juhudi za Waheshimiwa Wabunge Sheria hii itapitishwa mapema iwezekanavyo ili iweze kufungua njia kwa ajili ya ushirika ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo mafupi kwa baadhi ya barabara zilizozungumzwa na baadhi ya Wabunge wakati wakichangia hotuba yangu. Kwanza barabara ya Iringa –Dodoma. Serikali tayari imeingia makubaliano ya mkopo wa fedha na Serikali ya Japan na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Iringa hadi Dodoma. Mchakato ulikuwa mrefu, kazi haikuwa nyepesi, barabara ni ndefu na kama nilivyosema uwezo wetu wenyewe wa fedha za ndani si mkubwa sana kwa maana hiyo tumeenda kukopa katika Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na Serikali ya Japan na tunawashukuru kutukopesha pesa na sasa tunatarajia kwamba ujenzi wa barabara hiyo ya Iringa – Dodoma utaanza rasmi mwaka mpya wa fedha 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Dodoma – Babati, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Dodoma – Mayamaya, mkataba wa ujenzi umesainiwa mwezi Juni, 2010 na *specifically* ni wiki iliyopita. Pia mkataba kwa ujenzi wa barabara ya Babati – Bonga na mchepuo wa barabara ya kuingilia Kondoa kwa maana ya Dicha hadi Kondoa nao umeshasainiwa Mei 20, 2010. Mradi huu tumeuanza wenyewe, ni mradi mkubwa, barabara ndefu ina jumla ya kilomita 287 gharama yake ni kubwa sana lakini tumesema kwamba hata kama kabla hatujapata fedha za wahisani au fedha za wahisani wengine au pesa za wafadhili wengine basi au tuanze na pesa zetu wenyewe za Tanzania na wenzetu wahisani wanatupatia pesa kwa *grant* ama kwa kutukopesha lakini kwa vigezo vyao.

Mheshimiwa Spika, tumehangaika na barabara hiyo hatuna namna ya kuwalazimisha vigezo vyao vitakavyokuwa havikutimia ni kwamba wameicha mpaka hivi leo, lakini tumesema kwamba tuna matumaini makubwa baada ya Serikali kuweka juhudi kubwa kuhakikisha kwamba tunazipata pesa za kuongeza juu ya pale ambapo Serikali imeshindwa. Kazi hii dada yangu Mheshimiwa Zabein Mhita ameuliza itaanza lini?

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri ameitolea majibu kwamba itaanza mapema mwaka wa fedha 2010/2011. Niseme kwamba kwa sababu wakandarasi hawa wameshasaini mikataba ndani ya utaratibu wa mikataba hii, mkandarasi anapewa miezi miwili mpaka mitatu ku-*mobilize* au kujiandaa kwa ajili ya kuanza kazi kwa maana ya kwamba alete vifaa kwenye mradi ule na kuanza kusafisha barabara na kuwa tayari kwa ajili ya ujenzi. Kwa hiyo, tutegemee kwamba kwa makisio hadi mwezi Septemba, 2010 ujenzi katika barabara hii muhimu ya Dodoma hadi Babati kwa kiwango cha lami utakuwa umeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara zingine ambazo ningependa kuzitolea maelezo ni zile za Manyoni – Itigi - Tabora, Nzega – Tabora na Tabora – Urambo. Napenda

kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaingia mikataba ya ujenzi wa barabara hizi mwezi Julai, 2010. Mchakato wa kuwapata wakandarasi wa ujenzi uko katika hatua za mwisho kabisa. Mchakato huu si mwepesi sana na kazi hii imefuata baada ya kazi zote zingine kukamilishwa ikijumuisha kazi ya usanifu. Kwa ukarabati wa barabara kuu na za mikoa nchini, naomba niwasihi Waheshimiwa Wabunge waangalie kwenye majedwali ya kitabu cha Bajeti ya Wizara ya Miundombinu ili waone barabara zao zimetengewa kiasi gani kwa ajili kazi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba barabara ya Tanga – Horororo, Tunduma – Sumbawanga, Songea(Peramiho) – Mbinga na Tunduru hadi Namtumbo ambazo zinajengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia *MCC* zitajengwa kama ambavyo imepangwa. Fedha za ujenzi za barabara hizi zipo kwenye kitabu cha maendeleo *volume four,* Fungu la 50 Wizara ya Fedha na Uchumi, ukurasa wa 108. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari katika barabara za Jiji la Dar es Salaam ni kero kubwa kwa wananchi. Tatizo hili limeanza kutafutiwa ufumbuzi kwa kuanza kuongeza mtandao wa barabara za jiji kwa kutumia fedha za ndani. Aidha, tatizo la msongamano kwenye makutano ya barabara limeanza kutafutiwa ufumbuzi katika mpango wa ujenzi wa barabara zinazopita juu ama *fly-overs*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la usafiri majini, katika kuimarisha miundombinu ya huduma za mizigo katika bandari zetu, Serikali kupitia Mamlaka wa Usimamizi wa Bandari itatekeleza mpango kabambe wenye lengo la kuendeleza bandari na kuongeza ufanisi na tija katika shughuli za huduma kwa meli za sheheni ili kuhakikisha kuwa bandari zetu zinakuwa vivutio vya ndani na nchi jirani katika kupitisha biashara za Kimataifa na hivyo kuongeza mchango wa sekta katika Pato la Taifa. Aidha, Serikali inafanya juhudi za kuboresha usafiri wa majini katika Maziwa Makuu ili kuchochea maendeleo ya jamii na kiuchumi katika ukanda wa maziwa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa eneo la usafiri wa reli, suala la uboreshaji wa huduma ya miundombinu ya reli nchini imepewa kipaumbele katika miradi ya maendeleo kutokana na umuhimu wa reli hizi katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo sekta hii imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha na mizigo hasa katika eneo lile la reli kati ya Dar es Salaam hadi Arusha. Reli hii itapata msukumo zaidi wakati wa kuimarisha reli ya Tanga hadi Moshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itabidi nifupishe baadhi ya maeneo kwa sababu muda hautoshi. Naomba nizungumzie kidogo kuhusu eneo la usafiri wa anga. Pamoja na changamoto zinazolikabili Shirika la Ndege, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za usafiri wa anga ikiwa ni pamoja na kazi ya kuwavutia wawekezaji. Hali kadhilika Serikali inafanya mazungumzo na wawekezaji walioonesha nia na kuwakaribisha wengine ili kuwekeza katika Shirika hili la Ndege. Kuhusu viwanja vya ndege, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa viwanja vinaimarishwa kulingana na viwango vya Kimataifa na kuvifanyia matengenezo ili vitoe huduma wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha naomba nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafuatao, kwanza kwa Rais Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua kuwa Waziri wa Miundombinu, pili kwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, kwa kunipa ushirikiano mkubwa na miongozo mizuri iliyoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi zaidi.

Tatu, ni kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nguzo kubwa kwangu katika kuweka masuala ya sekta ya miundombinu kwenye muelekeo mzuri wa kuliletea Taifa hili maendeleo. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunipa maoni ambayo mara zote yamekuwa ni msaada mkubwa si tu kwa sekta yetu bali pia kwa sekta yetu kwa ujumla. Nawashukuru sana, nawatakia wote ushiriki mzuri wa mchakato wa uchaguzi wa Oktoba, 2010 na kumwomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe sote turudi tena hapa Bungeni baada ya Uchaguzi Mkuu na kuendelea na kazi za kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru tena Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Katibu Mkuu Mhandisi Omar Chambo, Wakuu wa Idara na Taasisi zilizochini ya Wizara pamoja na watumishi wa Wizara ya Miundombinu kwa msaada mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu yangu kwa kipindi chote nikiwa Waziri wa Wizara ya Miundombinu na hii ni Wizara ambayo imekuwa na changamoto nyingi sana na ndiyo Wizara ambayo nimekaa kwa muda mrefu kuliko Wizara nyingine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Bagamayo kwa kunipa ushirikiano mkubwa sana katika kipindi chote ambacho nimekuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Tumefanya kazi kubwa za kimaendeleo Jimboni Bagamayo na ni mategemeo yangu kwamba wananchi wangu watanipa nafasi nyingine ya kushirikiana nao tena katika kipindi kijacho, nawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu nyingi sana na za dhati kwa mara nyingine kwa mke wangu mpendwa na watoto wetu kwa kunipa moyo na ushirikiano na kwa kunivumilia kwa kipindi chote ambacho nilikuwa nikitekeleza majukumu mbalimbali ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua sikujibu hoja zote kama ambavyo vile ningependa lakini muda haupo na mimi, lakini niwaahidi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba hoja zote ambazo zimesemwa ama zimeandikwa tutazitolea ufafanuzi kimaandishi na tutaziwasilisha Bungeni kwa kila Mbunge na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa jitihada za kuzijibu hoja. Waheshimiwa Wabunge ingawa hoja imetolewa na kuungwa mkono. Utaratibu wa Kanuni ya 100 unahitaji tuwe katika hatua nyingine tena. Namwita Katibu ili tuingie katika hatua hiyo.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

**MWENYEKITI:** Katibu tupitishe kwenye vifungu.

### Fungu 98 – Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu

Kifungu 1001 - *Administration and General* … ... Sh. 2,160,676,100

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Ellieta Switi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Mussa Zungu na Mheshimiwa John Lwanji. Tunaanza na Mheshimiwa Lwanji. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza, mimi napenda kupata maelezo au ufafanuzi kuhusu barabara hii ya kutoka Itigi kwenda Rungwa. Tulikubaliana kwamba walau kila mwaka wangeweza kutenga fedha kwa ajili ya kuikarabati hiyo barabara ambayo mwaka 1998 ilizolewa na maji wakati wa mvua za *El-Nino.* Sasa siioni kwa sababu nimeangalia siioni. Mwaka juzi 2008/2009 walitenga shilingi milioni 400, halafu mwaka huu wametenga milioni 350 na barabara hiyo inapitika vizuri isipokuwa kuna maeneo kutoka Kihungi mpaka Mwamambege bado na kuna sehemu ambazo bado hawajakamilisha. Sasa naona fedha ambazo hazijatengwa na ninavyoona huko mbele tunakokwenda kama Mkoa mpya wa Katavi utaundwa barabara hii ndiyo itakuwa *outlet* ya Mkoa, sidhani kama watazunguka tena kwenda Mbeya itabidi waje huku kupitia hiyo barabara. Nashangaa hao wataalam wameisahau barabara hii ni muhimu sana. Napenda kupata maelezo kuhusu hilo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa John Lwanji, kama ifuatavyo:-

Sifahamu kama Mheshimiwa Lwanji ameangalia kwenye kitabu kipi, inawezekana ameangalia kwenye kitabu cha nne ambacho ni miradi ya maendeleo cha Bajeti hii na ameikosa. Lakini niseme kwamba pesa za matengenezo pia zinaonekana katika hotuba yangu ya Bajeti kwa maana katika barabara zile ambazo pesa zake tumezitenga kutoka kwenye mfuko wa barabara bila shaka tukiangalia kwenye Singida tunaweza kuikuta kule. Mimi sijaiangalia na nategemea kwamba kwa umuhimu wa barabara hii itakuwa imetengewa fedha za matengenezo kutoka fedha za Mfuko wa Barabara na taarifa ambayo ninayo hapa ni kwamba bila shaka itakuwa imetengewa fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niangalie kwenye kitabu lakini kama itakuwa haipo tutahakikisha kwamba tunapata namna ya dharula ya kuifanyia matengenezo. Ila nimuhakikishie Mheshimiwa John Lwanji kuwa barabara hii kwa umuhimu wake ni kwamba tumeiweka katika kuifanyia usanifu na upembuzi kwa maandalizi ya ujenzi wa kiwango cha lami ili iweze kuwa katika hali nzuri zaidi kushinda hiyo ya matengenezo ya kawaida. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nataka niungane na wasemaji walipopita kuhusu mkakati wa kuimarisha reli ya kati Kibajeti. Nilikuwa naangalia kwenye Kitabu cha *Development* naona hakuna mkakati mahususi wa Kibajeti wa ku-*rehabilitate* reli ya kati na wewe unajua kwa sababu ni mtumiaji wa reli hii ni kwamba tutakuwa tunahangaika na barabara kubeba mizigo mizito, hili jambo litatugharimu kama Taifa kwa muda mrefu nilikuwa nataka kujua ni kwa nini mkakati mkubwa usijielekeze kuvua hii reli ya kati kwa maana ya kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma na zaidi ya hayo katika hoja hizi kama wasemaji wengine walivyosema vitabu vyote vinazungumzia juu ya reli Dar es Salaam, Dodoma, Tabora inachepuka inakwenda Isaka, Kasongati mpaka Kigali, nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri hiki kipande cha Tabora, Kaliua na Kigoma maana kimeachwa na kama kimeachwa maana yake ni nini. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, kama ifuatavyo, kwanza kwa ujenzi na uboreshaji wa miundombinu, Serikali imetenga pesa unajua tungependa tutenge pesa zaidi kuliko ambazo tunamudu kufanya hivyo. Lakini kwenye *sub vote* 270845 kuna pesa za *TRL* jumla yake ni shilingi 15,470,952,900. Lakini pia tumeitengea *RAHCO* pesa ambayo iko katika *sub vote* 4270847 jumla ya shilingi 6,861,441,900 ni pesa nyingi zaidi kuliko ambavyo tulimudu kutenga fedha mwaka jana wa fedha, mwaka jana tulitenga bilioni moja moja lakini safari hii tumetenga fedha nyingi zaidi na hasa kwa kuzingatia kwamba ni hivi juzi tu tumetoka kumaliza kutumia bilioni 15,700,000,000 katika Miundombinu ya reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Serikali hii imewekeza hela nyingi pamoja na kwamba tunakiri kuwa hizi pesa hazitoshi na tunafanya mkakati mwingine kwa ajili ya kuhakikisha tunapata pesa za kuweza kuboresha miundombinu ya reli ya kati. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kupata maelezo kuhusu Shirika la Ndege la *ATCL*. Pamoja na maelezo mazuri ya Waziri kwamba tumeongea na mfadhili lakini mimi nilidhani tungekuja na mkakati, nilitaka sasa Waziri aniambie kuna mkakati gani kwanza kama nchi tusafishe madeni ambayo tunadaiwa, tulipe baada ya kufanya biashara miaka miwili, mitatu tunaanza kupata faida ndiyo tuanze kwenda kuongea na mtu wa kuja kuingia naye mkataba kama *partner,* sasa ukienda wakati vitabu ni vichafu hata namna ya ku-*negotiate* huwezi ku-*negotiate* kwa sababu unakwenda wewe *almost* kampuni imekufa, matokeo yake utafanya anachotaka yeye yule unayemuita kuja kuingia naye ubia. Mimi nilitaka Waziri aniambie kwenye kitabu cha maendeleo hapa sioni pesa yoyote kwa ajili ya *ATCL* na kweli watu wengine kama sisi ndege hiyo kwa watu wa Tabora na Kigoma ni ya muhimu sana, moja ninachotaka kujua mkakati wa Kibajeti wa kwetu kwanza kabla ya huyu Mchina au mwingine ukoje kwenye suala hili?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwenye hoja ya Mheshimiwa Peter Serukamba kama ifuatavyo, baada ya matatizo haya ya ubia pamoja na mwekezaji ambayo nimeyaongelea katika majumuisho yangu Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunapata mwekezaji mwingine ambaye tutashirikiana naye kwa ajili ya kulifufua Shirika hili. Lakini labda nirekebishe tu kuwa siyo kulifufua Shirika hili, mkakati uliopo hivi sasa ni kuunda upya Shirika la Ndege la Taifa kwa maana ya kwamba tuaanza mkakati wa kuunda upya, thamani ya kuweza kuwa na Shirika ambalo linafanya biashara vizuri ni kisio la jumla ya dola milioni mia tano na ishirini na moja hii ni zaidi ya shilingi bilioni mia sita ya kuweza kuwekeza ili tuweze kuwa na Shirika ambalo ni jipya na kuweza kurusha Bendera ya Taifa. Hizi siyo pesa chache tungependa kama tungeweza sisi wenyewe tuweke sisi wenyewe pesa hizo lakini tuna mengi ya kufanya lakini hatutoweza kutafuta pesa hizo na kuwekeza kwenye Shirika la Ndege kwa vile bado tuna miundombinu chungu mzima ambayo inahitaji fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa mantiki hii kwa nchi kama za jirani ambazo nazo ziliamua baadaye kwamba ni bora waachane kuwa na Shirika la Ndege la Taifa sisi tunasema kwamba hatuna uamuzi huu. Bado sera yetu na maamuzi yetu ni kuunda Shirika la Ndege la Taifa litakalo peperusha bendera ya nchi hii na baada ya kushindikana kuingia katika makubaliano na mwekezaji huyu wa Kichina sasa hivi tunajiweka vizuri ili tuweze kumpata mbia mwingine na Serikali itawekeza pesa kwa ajili ya kuunda Shirika jipya. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:**Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina haja na mshahara wa Mheshimiwa Waziri kwa mambo ambayo anayoyafanya. Nilikuwa nahitaji ufafanuzi kuhusu barabara ambayo yeye mwenyewe aliitembelea ya Igawa, Madibira, Lujewa na Kinyanambo kwa maana ya Mafinga mwaka jana ilipewa shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa madaraja lakini kwenye taarifa ya kikao cha barabara cha Mkoa kulikuwa na taarifa kuwa karibu shilingi milioni 650 zimetumika kwenye usanifu wa kina na mwaka huu nimeona kwenye Bajeti kuna shilingi bilioni mbili na milioni mia sita kwa ajili ya ujenzi wa madaraja tena, je, hizo zilizobaki mwaka jana zilikuwa *committed* kwa

ajili ya hiyo barabara au hii Bajeti inaanza tena upya na ujenzi wa barabara hii unaanza lini kutokana na ahadi ambayo alitoa wakati ametembelea Wilaya ya Mbarali?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Estherina Kilasi. Barabara ya kuanzia Rujewa kwenda Madibira hadi Kinanyambo pale Mafinga ni moja kati ya barabara muhimu ambazo zijengwe kwa kiwango cha lami. Mchakato umeanza na ndiyo ambao tumeutengea pesa mpaka mwaka uliopita wa fedha ambao ndiyo huu 2009/2010 kwa ajili ya kukamilisha taratibu zake za maandalizi kwa ajili ya usanifu.

Sasa kazi hiyo imekamilika na tumeimaliza na kwamba katika kumaliza kazi hiyo ya usanifu kwamba hatua nyingie tunayokwenda sasa katika mwaka mpya wa fedha ni ujenzi na tumepanga kwamba katika mwaka huo mpya wa fedha utakapoanza kujenga barabara hiyo tuanze na madaraja kwanza ili madaraja yakae vizuri ambayo yatawezesha usafiri katika barabara hiyo uwe unaendelea bila matatizo wakati tunajenga nguvu kwa ajili ya kuwekea lami barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa katika mwaka uliopita wa fedha zimetumika katika kazi hizo za maandalizi na kama tunavyofahamu kila fedha ambayo inatumika inaidhinishwa tena Bunge lako Tukufu na hakuna hela ambayo tunaiweka ili iweze kurundikana na pesa nyingine ambayo inakuja katika mwaka mwingine unaofuatia. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi naomba kuzungumzia suala la Daraja la Mkapa. Daraja hili tumelijenga kwa gharama kubwa ya zaidi ya shilingi bilioni 35. Wizara ya Nishati na Madini inataka kupitisha *high voltage wire* chini ya daraja hili hiyo ni sawa na kuweka bomu, hitilafu yoyote ikitokea pale...

**MWENYEKITI:** Hukusikika vizuri, ni sawa na kuweka?

**MHE.RAYNALD A. MROPE:** Ni sawa na kuweka *timed bomb*, hitilafu yoyote ikitokea daraja lile litalipuka na ndiyo mwisho wa Daraja la Mkapa na hatutakuwa na mawasiliano yoyote kati ya Kusini na Kaskazini. Sasa nilitaka kumuuliza Waziri Katika Bunge hili yeye kama mwenye lile daraja kweli anaweza kuruhusu watu wa nishati wapitishe nyaya zao pale? Mbona Zanzibar tumepelea chini ya bahari mpaka kule Zanzibar kwa nini wasifanye vile pale Rufiji? Kwa nini wanataka kutuweka katika hatari na sisi watu wa Kusini tuwe roho juu kila wakati kufikirie kwamba linaweza kulipuka wakati wowote?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Raynald Mrope. Kumtoa hofu Mheshimiwa Mrope katika hili yeye ni mtu wa Mtwara na mimi ni wa Pwani wote tuko katika ukanda wa Pwani kwa hivyo, wote tunaogopa mambo ya umeme kwa hali ya juu sana, suala hili kwa kweli lilileta ugomvi mkubwa Serikalini kwa maana ya Wizara mbili, Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Miundombinu na uvushaji wa nishati ya umeme pale ulichukua muda mrefu na hata ikafikia wakati ambapo

maelewano yalikuwa madogo sana kati ya Wizara hizi mbili kwa maana ya Miundombinu ikikataa na Nishati kusema tupitishe katika daraja hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa taratibu zilichukuliwa, wahandisi washauri yaani *consultancy* zaidi ya moja yaani makampuni mawili yalifanya tathmini na wataalamu kutoka pande zote mbili za Wizara hizi mbili. Baada ya kuwa ugomvi mkubwa wamekutana kwa ajili ya kufanya mapitio katika stadi zile ambazo zimefanywa na hawa *consultant* na hapa nisemapo ni kwamba tumefikia makubaliano kuwa hakuna madhara makubwa ambayo tunaweza kuyapata kwa kupitisha umeme katika njia hiyo ambayo imefanywa hivi sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nitumie Kanuni ya 104 ili tuongeze muda usiozidi dakika 30 baada ya saa mbili kasoro robo ni dhahiri tutaendelea hivyo, na pili nitatumia Kanuni ya 4 kuwaita zaidi ya mmoja ili tuwe na mtiririko mzuri na ufanisi zaidi. Sasa nitawaita Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Mheshimiwa Elietta Switi.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hilo hilo naomba tu nipate mchanganuo wa matengenezo ya hii barabara ya Itigi - Tabora kwa sababu uchambuzi yakinifu umeanza toka mwaka 1998 katika barabara hii. Kila baada ya miaka miwili wanaongeza pesa wakisema uchambuzi tena yaani kila baada ya miaka miwili uchambuzi tena, wana Igalula wamechoka kusikia kuhusu uchambuzi wa barabara hii, je, hizi shilingi bilioni 8 kweli zitafanya kazi yoyote ile ambayo ionekane na watu wa Jimbo langu kuona kuwa barabara hii inatengenezwa?

**MHE. ELLIETA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ni *vote* hiyo hiyo, programu hiyo hiyo. Katika maandishi yangu nimeiomba Serikali au nimemuomba Waziri ikiwezekana basi ile barabara inayotoka Kaengesa kwenda Mwimbi, Ulumi, Mtula iwekewe lami ili kuwasaidia watu wale wanaoishi mahali pale maana maendeleo yao ni duni kwa sababu hawana *infrastructure* nzuri ya namna yoyote si ya lami, si ya maji, si ya anga japokuwa nichukue fursa hii pia kushukuru kwa sababu sasa Mkoa wa Rukwa umetizamwa kwa maana ya *infrastructure*. Naomba Waziri anipe maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Tatu Ntimizi kwamba katika pesa zile ambazo zimetengwa nikiri kuwa katika baadhi ya maeneo pesa hizi zina upungufu kiasi. Lakini tumeweka mkakati Serikalini kuhakikisha kwamba tutadai pesa ambazo wafadhili walikuwa wameziahidi kwenye Bajeti ya mwaka 2009/2010 ambazo jumla ya shilingi bilioni moja na sabini hazikutoka nadhani kwa mkakati wa Serikali pengine tunaweza tusipate fedha zote hizo walau nusu yake tutazipata kwa maana hiyo ni kwamba tutaweza kujazia kwa hiyo, itabidi turudi tena kwenye *Supplimentary Budget* ama kwa njia nyingine ili kuhakikisha kuwa tunaijazia pesa miradi hii ili iweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa barabara hii ya Itigi, Tabora tuna Tabora - Nyahua na tuna Manyoni – Itigi - Chaya ambazo zabuni zake zimeshatangazwa na

tumezitengea pesa tumeweka nia thabiti kuwa tutaanza ujenzi ndani ya mwaka wa fedha wa 2020/2011 mwaka huu mpya wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mheshimiwa Ellieta Switi naomba niseme kuwa sikuipata barabara aliyoizungumzia Mheshimiwa Mbunge. Lakini niseme kwamba kama haimo katika vitabu vyetu niseme tu kuwa naomba radhi sana kwamba haitowezekana Serikali kutimiza miradi yote, katika Mikoa yote kwa wakati mmoja kwa sababu barabara tunazozijenga ni nyingi sana barabara kuu peke yake ina jumla na ni zaidi ya kilomita 5,000 na zile ambazo tulizipandisha hadhi peke yake zina zaidi ya kilomita 2,000 kwa hiyo, kama haipo nimhakikishie tu Mheshimiwa Ellieta Switi kwamba katika Bajeti zinazofuata tutafanya ufikirio wa barabara ambayo umeitaja lakini tumeshaweka nia thabiti kwamba Mkoa wa Rukwa nao ufunguke na kazi zinaonekana tumeshaanza na Mheshimiwa Rais alikuwa huko ameweka mawe ya msingi kwa hiyo kasi itakuwa ni hiyo hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Diana Chilolo leo umevaa kilemba sijakuona na kilemba hata siku moja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilisema mengi lakini nataka ufafanuzi juu ya jambo moja tu la Daraja la Nangoo. Tumejenga Daraja la Umoja, tumetengeneza barabara za *Mtwara Development Corridor* kwa pesa nyingi kabisa hivi sasa tunataka barabara hizo zipitishe magari madogo ya tani 5 hadi 10 tu?

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimezungumzia kuhusu reli ya kutoka Manyoni kwenda Singida kwamba kabla hajachukua mwekezaji Reli ya Kati pamoja na Reli ya Manyoni Singida kulikuwa na magenge njiani katika reli hiyo ambayo yalikuwa yanasaidia kukaa waangalizi wa reli hiyo wakati reli ikiwa na maharibiko wanatoa taarifa au wanafanya matengenezo jambo ambalo lilikuwa linasaidia sana kuzuia ajali, lakini baada ya mwekezaji kuchukua reli hiyo magenge yote yalivunjwa na watumishi wakaachishwa kazi sasa kwa kuwa Serikali imechukua reli hiyo, je, magenge hayo yatarudishwa na hao watumishi watarudishwa? Ningeomba kupewa maelezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya kwa hayo mawili daraja la Nangoo na reli ya Singida - Manyoni.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Anna Abdallah kama ifuatavyo, kuwa Serikali imejipanga vizuri kwa ajili ya kujenga Daraja hilo la Nangoo katika barabara hii ya kuanzia Mtwara kwenda mpaka Masasi, Songea na *Mbambabay* ambayo ina *save* ukanda wa maendeleo wa Mtwara, Serikali imejipanga vizuri kwamba iifungue hii barabara ijengwe kwa kiwango cha lami ili iweze kuleta maendeleo au iwe kichocheo cha maendeleo ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumeanza ujenzi wa Daraja la Nanganga na limeshafikia hatua kubwa, mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Daraja la Nangoo, kwa hiyo tumelitengea pesa ujenzi wa Daraja la Nanganga linaendelea na Daraja la Nangoo mwaka wa fedha 2010/2011 ili barabara hiyo sasa ukiunganisha na ujenzi wa Tunduru na Namtumbo, Namtumbo-Songea, Songea kwa maana ya Peramiho mpaka Mbinga kwamba sasa barabara hiyo iwe inapitika kwa kiwango na magari makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba tuna mpango huo wa kurudisha magenge ya ujenzi katika Reli hii ya *TRL*. Hili ni moja katika mambo yalidhoofisha sana utendaji mzuri wa reli yetu ya kati. Kwa hivyo, sasa wakati tunachukua wenyewe kwa ajili ya kuiendesha tumeweka nia thabiti ya kuhakikisha kwamba matengenezo katika reli hii yanafanywa kwa ufanisi mkubwa.

**MWENYEKITI:** Nitawaita watatu sasa Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Zaynab Vulu na Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, kwa mpangilio huo nitaanza na Mheshimiwa Kirigini.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, mimi pia nilitaka kupata ufafanuzi katika mchango wangu nilipochangia asubuhi nilionyesha wasiwasi kuhusiana na barabara yetu ya Nata - Mugumu mpaka Loliondo na nilitegemea Waziri katika majibu yake angetuondolea sisi wananchi wa Mkoa wa Mara wasiwasi huu. Pesa iliyotengwa ni shilingi bilioni moja na milioni mia saba ambayo naiona ni ndogo sana kwa barabara hii. Nilitaka kupata ufafanuzi; je, barabara hii itajengwa kama alivyotuahidi Mheshimiwa Rais?

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi sina haja ya kuchukua mshahara Waziri, ila katika mchango wangu nilikuwa nataka nipate ufafanuzi, nilizungumzia suala la foleni zilizokithiri katika Jiji letu la Dar es Salaam ambalo ni Makao Makuu ya kibiashara, uchumi wa nchi yoyote ile unategemea na miundombinu ikiwemo barabara. Barabara za Dar es Salaam zimekithiri kwa foleni, hakuna muda wowote unaweza ukasema unaweza ukapita labda saa hizi hakuna foleni na sisi Mkoa wa Pwani tuna maeneo makubwa tu ambayo yanaweza yakajengwa barabara na kama barabara za Dar es Salaam zimejaa maana yake zitasogea kuja katika Mkoa wetu wa Pwani. Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi kwa Waziri na hasa aliposema kwamba Bajeti ya Serikali pesa zake ni ndogo kwa maana kwamba sungura ni mdogo walaji tupo wengi, je, Waziri anaweza akatueleza ana mkakati gani wa kuyashirikisha mashirika yenye uwezo au taasisi zenye uwezo ili waweze kujenga barabara kwa mtindo wa *build operate and transfer (bot)?*

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma naomba Waziri apokee shukrani nyingi sana kwa ajili ya ujenzi unaotarajiwa kuanza wa barabara hizi za kutoka *Mbambabay* mpaka Tunduru kwa ujumla. Lakini baada ya shukrani hizi, kwa kuwa wote tunaguswa na tatizo la msongamano wa abiria Dar es Salaam na kwa kuwa kuna reli ambayo ingeweza kupunguza tatizo hilo kutokea Pugu mpaka mjini na kuwaacha wananchi

wanaotumia reli ya kwenda Bara waanzie Pugu kwenda Bara, je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ufumbuzi rahisi kama huu ambao nadhani hauhitaji hata mikakati mingi sana ya kipesa ili kuweza kuondoa tatizo hili?

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Zungu Mbunge wa Ilala pengine na wewe unajilekeza huko huko, basi tulimalize.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kweli tumeona kuna mpango wa kupunguza msongamano wa magari katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini kwa masikitiko makubwa sana mpango huu haugusi barabara ya Uhuru ambayo kwa kweli ina msongamano mkubwa sana kutoka mnazi mmoja mpaka barabara ya Mandela inakuchukua masaa zaidi ya manne. Ninataka kujua tu mpango wa Serikali katika hili, kwanini barabara ya Uhuru imetengewa shilingi milioni mia moja peke yake?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri sasa kuna maswali manne hapo, kuna swali la Mheshimiwa Rosemary Kirigini kuhusu barabara ile inayotoka Musoma Vijijini kupita Serengeti, kuna swali la Mheshimiwa Zaynab Vulu kuhusu msongamano Dar es Salaam ambalo limerejewa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwamba pengine reli inaweza kuwa ni ufumbuzi, lakini pia Mheshimiwa Mbunge wa Ilala yeye anasema barabara ya Uhuru ni mbovu na ina msongamano zaidi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo, nikianza na Mheshimiwa Rosemary Kirigini kuhusu barabara ya Nata - Mugumu na kwamba inatengewa shilingi bilioni moja na inaweza isitoshe. Lakini naomba niseme kwamba barabara hii siyo Nata mpaka Mugumu, barabara hiyo ni kwamba inaanzia Makutano - Nata, Nata - Mugumu inaenda Loliondo - Engasero inateremka mpaka Mto wa Mbu- Arusha. Tumeanza muda mrefu kuifanyia *studies* kwa maana ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hiyo na ujenzi wake tutaijenga kwa awamu lakini pia itabidi tupitie michakato mbalimbali. Kwa hiyo, tumetenga pesa hizi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii inawekwa katika hali ya kupitika kutoka Nata hadi Mugumu isiwe inaendelea kukwamisha watu lakini pia tunaendelea na majadiliano na wahusika.

Barabara hii katika urefu wake haijapata kibali cha Shirika letu la Udhibiti wa Mazingira *(NEMC)* kwamba kuna hali ya athari ya mazingira ambayo itajitokeza katika kipindi cha ujenzi na wakati wa kutumika barabara hiyo. Kwa hivyo, watalaam wa *NEMC* hawajaipa kibali, wameainisha maeneo yale na maeneo haya tunayafanyia kazi ili tuone kama tunaweza tukafikia mahali ambapo tunaweza tukawashawishi *NEMC* lakini pia na wahisani ambao pia jicho lao lipo hapo kama darubini kuangalia kwamba tunafanya kitu gani ili kile ambacho tutakifanya nje ya kile wanachodhani kuwa ni sawa basi pengine na wao watuadhibu kwa namna moja ama nyingine.

Sasa si wahisani peke yao sisi pia tuna watalaam kwa maana ya watalaam wa *NEMC* na kama *NEMC* haijatoa kibali cha ujenzi wa barabara hii Serikali bado ni lazima iendelee kuangalia maeneo yale yote ambayo tunadhani kwamba yanahitaji kufanyiwa

kazi kabla ya kibali hicho kuweza kupatikana. Pesa zilizotengwa ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika na mara ukamilifu wa usanifu utakapokamilika na tukimaliza na sakata hili la mazingira basi tutaanza kazi ya ujenzi wa barabara hiyo ambayo kwa muda mrefu tumeahidi kujenga barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya dada yangu Mheshimiwa Zaynab Vulu, naomba kwanza naye nimpe pongezi nyingi sana kwa ufuatiliaji wa miundombinu ya barabara katika mkoa wake wa Pwani lakini hata katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mheshimiwa Vulu amekuwa anafuatilia sana Wizarani Bungeni na kila mahali kuhusu barabara hizi nampa pongezi sana kwa kazi nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba tangu mwaka juzi tumebuni mradi wa kuongeza mtandao wa barabara katika Jiji la Dar es Salaam tumebuni miradi kumi ya barabara za Dar es Salaam tulizomudu kuanza mwaka huu wa fedha 2009/2010 ni miradi mitatu ambayo ndiyo imeanza kujengwa nayo ni *Ubungo Bus Terminal* mpaka *Kigogo round about,* na *Kigogo round about* kupitia Bonde la Msimbazi kwenda kuungana na Twiga, lakini pia ile ambayo inatoka *Jet corner* katika barabara ya Nyerere mpaka *Davis Corner* miradi hiyo tumeshaanza. Lakini tuna miradi kumi tumeitengea pesa katika Bajeti hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wakiipitisha basi miradi hiyo itaendelea kujengwa. Kubwa zaidi ambalo pia Serikali imefanya ni kuandaa *master plan* ya mtandao wa barabara ya Jiji la Dar es Salaam ili kuweza kujua ni namna gani ambavyo tunaweza tukahakikisha kwamba msongamano huu tunaumaliza katika Jiji la Dar es Salaam kama siyo kupunguza kwa kiasi kikubwa.  Kwa hivyo, angalau tunasema kwamba tuna upeo wa nini tunahitajika kufanya ili tuweze kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vulu pia amezungumzia pia kwa nini Serikali isishirikishe sekta binafsi, nasema kwamba Serikali iko tayari kufanya kazi hiyo na tayari imeshaanza kufanya ushawishi kwa kuwapata watu au makampuni ya kushirikana na sisi, tumezunguza na mashirika kutoka nchi ya Malaysia lakini pia tumezungumza na mashirika mbalimbali ya sekta mbalimbali kutoka nchi ya Korea. Pamoja na hamu yetu kubwa bado hatujapata *response* ile ambayo pengine tungependa. Tujue tu kwamba *PPP* wanawekeza, wanataka wapate pesa zao zirudi na wana-*assess volume* ya magari yetu. Sisi tunaona mengi Dar es Salaam lakini kwa viwango vya *South Korea* au kwa viwango vya Malaysia siyo magari mengi. Kuna vigezo ambavyo vinawafanya wenzetu nao hawaji kwa haraka kama vile ambavyo tumependa kuwashirikisha.

Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya amezungumzia tena msongamano huo nadhani kama nilivyotoa kwa Mhehsimiwa Vulu, naomba kwa hoja ambayo Mheshimiwa Manyanya ametoa. Mheshimiwa Zungu ni kweli tumetenga shilingi milioni moja katika Bajeti ya mwaka ujao wa fedha lakini kazi ya ukarabati tayari imeshaanza na tunaifanya ndani ya mwaka huu wa fedha 2009/2010 mapungufu ambayo yatajitokeza, tutayabeba kadri tunavyokwenda huko mbele. Nakushukuru sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimwia Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilipenda kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa kufungua barabara za Mkoa wa Tabora. Wananchi wa Mkoa wa Tabora tumechoka kuvuta subira,

tunahitaji kufunguliwa katika masuala ya biashara. Tunaomba Serikali ituambie kwamba lini itatekeleza, lini barabara ya Nzega - Tabora itakamilika ndani ya mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Nadhani inanifanya sasa nimwite Mbunge wa Nzega Mheshimiwa Lucas Selelii na Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga ili tuokoe muda nadhani moja ya mambo watakayoyazungumza yatakuwa ni hayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mhonga na Mheshimiwa Owenya mvute subira kidogo.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kweli Bajeti hii ndiyo ya mwisho na hapa ningehitaji ufafanuzi wako, ninahitaji majibu sahihi na ya kweli. Toka mwaka 2006 kama utakumbuka sisi Mkoa wa Tabora tumekuwa tukisema sana juu ya kuufungua Mkoa wa Tabora kwa barabara zetu, lakini muda wote Serikali imekuwa inakuja na majibu ya ufinyu wa Bajeti, majibu ya usanifu, majibu ya jambo hili linafanyiwa kazi na vitu vinavyofanana na hivyo. Juzi Serikali ilikuja ikatangaza juu ya kuweka wakandarasi kwenye barabara zetu za Mkoa wa Tabora ili angalau mkoa wetu wa Tabora uweze kufunguka kwa maana ya Tabora – Manyoni - Itigi, Tabora - Kigoma na Urambo, kitu cha kushangaza mpaka sasa hivi tenda hizo zimefunguliwa lakini hakuna chochote kinachoendelea juu ya lini barabara hizi zitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alipokuwa anajibu hapa alisema tu kwa urahisi kwamba mwezi wa saba, majibu hayo tumekuwa tunayapata kila Bajeti ya Wizara hii inapokuwa inasomwa. Sasa inapofika inatosha, inatosha! Nilizungumza kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nikisisitiza kwamba sisi ni waungwana hatuna matatizo, aseme ni lini na mimi ningechukua tu mshahara wake hapa hapa kwamba ni lini barabara hizi za Mkoa wa Tabora zinawekwa saini tena ziwekewe hapa hapa Dodoma tuone ili watu wote waweze kujua, kama zile barabara zingine zilivyowekwa mikataba hapa hapa Dodoma bila pesa, bila kutangazwa, bila *design* bila nini. Kwa Tabora mnasema pesa hakuna, mchakato unaendelea. Mimi nataka tu aseme ni lini? Vinginevyo tutatumia Kifungu cha 103, mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo ni lini barabara kutoka Tabora kwenda Ipole - Mpanda, ni lini barabara kutoka Tabora - Ipole - Mbeya na zenyewe zitajengwa kwa kiwango cha lami vinginevyo hapa hapaeleweki.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niongeze hapo ambapo wenzangu wamesema. Tumefika mahali pagumu sana. Bajeti ya mwaka jana barabara ya Tabora – Itigi - Manyoni na Nzega Tabora zilitengewa pesa, ile ya Itigi - Manyoni mpaka Tabora ilikwishakuwa imepita kabisa kwenye mchakato kwa maana ya tenda zilikwishaitishwa lakini mpaka hivi leo tunaingia mwaka mwingine hakuna mkataba uliosainiwa. Kutokana na *presidency* hiyo, ya kwamba mwaka jana tulidanganywa, nina sababu gani ya kuamini kwamba mwaka huu tunaambiwa ukweli na kwa hili kwa kumvua Waziri mwenye dhamana juu ya jambo hili, niko tayari kumwomba Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni atupe kauli ambayo mimi kusema kweli ndiyo naweza kuichukua vinginevyo bado suingi mkono Bajeti hii.

**MWENYEKITI:** Waziri labda tusikie kwanza hapa maana yake tusiingie kwenye mengine tena tutahamia wapi Loliondo au? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba nitoe ufafanuzi wa maswali ya Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo, nikianza na Mheshimiwa Magdalena Sakaya kuhusu kufungua barabara za Tabora lakini ameuliza ni lini Nzega na Tabora itakamilika ndani ya mwaka huu. Nzega Tabora kilomita 116 lini itakamilika ndani ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kwanza Serikali ya Awamu ya Nne imejipanga kwa nia thabiti katika ile mikoa yote minne ambayo ilikuwa haijafunguliwa kwa maana ya kuunganishwa na mikoa mingine ya Tanzania, kazi kubwa ifanywe ili Mikoa hii iweze kutengenezewa miundombinu ya barabara ambayo inaunganisha Mikoa hiyo na Mikoa mingine ya Tanzania. Ikumbukwe tuna miaka 49 ya Uhuru na tumepokezana vijiti tangu Awamu ya Kwanza mpaka sasa Awamu ya Nne, Waheshimiwa mbalimbali walikuwa katika dhamana hii. Kwa uwezo wa Serikali tumeenda awamu hadi awamu mpaka hapa ambapo tumefikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka nia thabiti kufanya hivyo na kazi hiyo imeshaanza na kwa Mkoa wa Tabora tumesema kwamba ni lazima tufanye kazi ya kuufungua Mkoa huu, kwanza kwa kwenda Magharibi kwa maana ya Tabora kuelekea Kigoma na Mashariki kwa kuelekea Itigi Kaskazini kwa kuelekea Nzega na pia kutoka Tabora kwenda Singida. Mipango imefanywa na kazi hii ni mchakato kwa hiyo, umeanza muda mrefu, upembuzi umefanywa na usanifu umefanywa na hivi sasa tupo katika hali ya kuanza kujiandaa kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wowote una hatua nyingi na ujenzi maana yake umeshaanza kwa sababu kama hujafanya upembuzi huwezi kujenga, kama hujafanya usanifu huwezi kujenga, kama hujatangaza zabuni huwezi kujenga na taratibu zote hizi zinachukua fedha na zinachukua watalaam, kwa maana Serikali hii imetumia watalaam na pesa nyingi kwa ajili ya kuandaa ujenzi wa barabara za Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lini Tabora – Nzega, zabuni zake zimeshatangazwa na zimetangazwa zabuni mbili, moja ya kuanzia Nzega kuelekea Puge na ya pili kuanzia Tabora kwenda Puge kwa maana barabara hii moja lakini inakuwa na wakandarasi wawili ambao wanatoka pande hizi mbili. Sasa kwa vile zabuni zimetoka na wazabuni wamerudisha maana kuna mchakato wa kutathimini zile zabuni na baada ya mchakato wa kuzitathimini hizi zabuni kuna utaratibu mwingine unaoitwa majadiliano na mkandarasi. Sasa hatua imefikiwa kwa sababu unamuona huyu labda anafaa na kama tulivyosema kwamba thamani ya ujenzi wa barabara hizi zimepanda mno, Serikali inapata matatizo mno kuweza kuamua kuwachukua au kuwakataa wakandarasi kwa sababu thamani zinakuwa juu kuliko vile ambavyo Serikali ingekuwa na uwezo au ingetegemea. Daraja la Kolo kwa mfano zabuni ameleta thamani mara mbili ya ile tathimini ya mhandisi na thamani ambayo tunadhani kwamba hii ndiyo ingeweza kufaa. Kwa hiyo, sasa hivi iko katika hatua ya kufanya majadiliano na huyu mkandarasi. Kwa

hiyo, tunatarajia kwamba mara kazi hiyo ikifanywa vizuri na wakala wa barabara baada ya kazi yote kumalizika tathimini na majadiliano na mkandarasi ambaye watamteua na kukubaliana kwa yale ambayo wamekubaliana basi hiyo kazi itaanza. Tunaamini kwamba kazi hii awamu ya nne imewekea nia thabiti na imeanza kuitekeleza na inatekelezwa kwa nguvu zote kwa ari mpya, nguvu na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucas Selelii amezungumzia hilo hilo la Tabora - Nzega kwamba itajengwa lini nadhani hili nimelitolea majibu kwamba ujenzi utaanza ndani ya mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, fedha zake ndio zimo humu ndani ya Bajeti.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Kanuni ya 68, kwa hatua tuliyofikia majibu anayotoa Mheshimiwa Waziri kwa heshima na taadhima hayajaniridhisha. Sasa nataka kwenda Kanuni yetu ya Bunge, kifungu cha 103 ambacho kinamruhusu Mbunge kuondoa shilingi katika Fungu la Bajeti inayozungumzia. Naomba mwongozo wako kama sasa naweza kufanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Msubiri basi amalize kujibu, kuna barabara tatu zimeulizwa nyingine siyo Nzega peke yake, iko barabara ya kwenda Ipole, iko barabara ya kwenda Itigi na kwa namna ya kushangaza anakwepa kabisa barabara ya kwenda Urambo sasa sijui. Hebu tupate majibu ili tumalize. Mheshimiwa wewe ungelenga tu zabuni hizi zimetiwa sahihi au bado na nani anazuia ni huyu Katibu Mkuu Mhandisi Omar Chambo au ni nani tumjue tu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni hizo zinafanyiwa kazi kwa umakini kama zabuni katika maeneo yote hakuna ajenda ndani ya zabuni hizi, tunajenga kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania na sisi ambao tumepewa dhamana hii na Chama cha Mapinduzi, kusimamia kazi hiyo tunawajibika kusimamia kwa nguvu zetu zote hatutaruhusu mtu yeyote kuweza kuingilia kati kuweza kuzuia kila ambacho ni cha maendeleo kwa Watanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mchakato huu unakwenda vizuri na sitapenda kuwaambia wakala wa barabara wasifanye mashauri na mkandarasi, nataka kuwahakikishia kwamba wakikosea barabara hiyo na wakaweka mkandarasi ambaye mbovu halafu baada ya miezi miwili akaniambia kwamba mkandarasi huyo mbovu mimi siwezi kuyakubali maneno kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wafanye mchakato kikamilifu kuhakikisha kwamba mkandarasi watakayemuweka anaanza kazi na anamaliza kazi kwa wakati wake. Sasa si kwa barabara ya Tabora – Nzega tu, lakini na kwa barabara ya Tabora hadi Urambo mpaka Kaliua. Kwa sasa tunasema barabara ya Tabora – Urambo zabuni imetangazwa na tuko katika mchakato wa kuweza kumpata mkandarasi, tunasema kwamba mkandarasi ambaye hapatikani ni mkandarasi wa viwango na tuna mkandarasi wa kasi kwa barabara hii ya Tabora hadi Urambo. Kwa hiyo, ni *serious note* ni kwamba

hatuna mzaha katika ujenzi wa barabara hizi ambazo tunataka zifungue mikoa hii ambayo tuliita Mikoa ya pembezoni. *(Makofi)*

**KUHUSU TAARIFA**

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri anayatoa kuhusiana na hizi barabara zote mbili ya Tabora – Urambo mpaka Kigoma na ya Nzega Tabora kuna hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwamba mwaka jana zilitengwa fedha ambazo hazijatumika na mwaka huu tunapozungumza hapa kuna fedha nyingine ambayo imetengwa. Je, fedha zile zote zinajumlishwa kwa pamoja kwa mfano kwa Nzega – Tabora inakuwa ni shilingi bilioni 10 sasa badala ya shilingi bilioni 5 na kwa Tabora – Urambo – Kaliua – Uvinza mpaka Kidawe kwenye Bajeti inaonekana ni kuanzia Kigoma na zimetengewa takribani shilingi bilioni 48 za *D fund* hizo za kutoka Tabora kuja Urambo mpaka Kaliua ni kiasi gani maana yake ndio jibu la pamoja la maelezo hayo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yangu ya barabara ya Tabora – Urambo siyaunganishi kipesa na barabara ya Kidawe kwenda Uvinza mpaka Ilunde, ile tumeitafutia fedha yenyewe peke yake na tumekopa fedha kutoka Abudhabi na tutaendeleza ujenzi katika barabara hiyo kwa fedha hizo lakini wakati huo huo tunaitengea fedha na kuitafutia fedha kama mradi peke yake wa ujenzi wa barabara kutoka Tabora kupitia Urambo hadi Kaliua. Kwa hiyo, kwa fedha zetu za Serikali hivi sasa tuna uwezo wa kuanza kazi kama ambavyo tumeitengea fedha katika mradi huu na tunaendelea na majadiliano na wahisani mbalimbali na benki mbalimbali kwa ajili ya kupata fedha ya kujenga jumla ya kilomita 126 kutoka Tabora kuelekea Urambo mpaka hadi Kaliua. Kwa hiyo, hizi fedha ni tofauti na zile fedha za Kidawe – Uvinza mpaka Ilunde. Kwa hiyo, hizo siziunganishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba ujenzi tutaufanya kwa uhakika wake. Sasa tumezungumzia upande wa kuelekea Kigoma na tumezungumzia upande wa kwenda Nzega. Lakini kuna upande wa kuelekea Singida. Kwa maana kwamba tumefanya majadiliano na Serikali ya Iran na tumesainiana mkataba nao wa kifedha kwa ajili ya kupata msaada wa ujenzi wa barabara hiyo. Kwa sababu fedha hizo mchakato wake wa kuziomba hazijafikia mwisho. Tumeamua kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi katika barabara hiyo kwa kipande cha kilomita kama 89 kutoka Tabora kwenda Nyahua na kwa kipande cha kilomita 85 kutoka Manyoni – Itigi hadi Chaya ndani ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu likiwa likipitisha Bajeti hii maana litapitisha ujenzi wa barabara hii. Hata pale *TANROADS* wanaposaini watakuwa wanasaini kwa sababu fedha tayari zimeidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hatuwezi kuanza ujenzi bila Bunge lako Tukufu kuweza kupitisha fedha hizi. Hata pale kusaini mkataba bila fedha kupitishwa pia tumepata cha mtema kuni ambacho nadhani hatutapenda kurudia tena katika hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba nia ni thabiti na wala haina kigugumizi na wala mimi kama Waziri mwenye dhamana ya Miundombinu naheshimu wadhifa ambao nimepewa na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete nitahakikisha nimesimamia kazi hiyo ili kuhakikisha kwamba Ilani ya Uchaguzi imetekelezwa kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lucas Selelii alikuwa na hoja ya barabara ya Tabora kwenda Mpanda kwa maana ile ya Ipole hadi Mpanda. Barabara hii tuko katika usanifu hatujaimaliza.

**MWENYEKITI:** Nikusaidie Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (2) hauturuhusu tena kuendelea lakini nadhani kumaliza hoja hii kama Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kutukutanisha Wabunge wa Tabora tukutane na Waziri wa Miundombinu *this is extremely serious, it is impossible* ku-*go on like this* Mkoa mmoja unatengwa tu *forever* basi haieleweki.

Kwa hiyo, tunataka tuweze kukaa kesho na Waziri wa Miundombinu na huyu Katibu Mkuu Mhandisi Omar Chambo na *TANROADS* wote wanaohusika hebu tupate majibu. Wenzenu hatuwezi kuendelea hivi Mkoa mmoja unakuwa kama unabaguliwa kabisa watu ni shida. Naona wengine mnashangilia tu kwa sababu ninyi mambo yote yamekwisha. Mkoa wa Tabora ndio Mkoa mkubwa kwa eneo kuliko Mikoa yote nchini. Mpaka leo una kilomita kama sita za lami miaka 50 baada ya Uhuru, *we can't accept it*. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara chache sana kusimama kwa ajili ya kusaidia kidogo kutoa ufafanuzi. Lakini nimeona pengine ni vizuri nisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti yetu ya Miundombinu ilikuwa na matatizo mengi sana. Lakini kama tulivyokwishaeleza tulijitahidi angalau tukaweza kupunguza matatizo ambayo yalikuwa yanaikabili Wizara hii. Lakini hata baada ya kumaliza tulijua kwamba bado tatizo litakuwepo lakini tukaamini kwamba Bunge litaweza kusikiliza kilio cha Serikali na kuwaomba Bajeti ipitishwe ili mambo yaweze kuendelea. Sasa nilikuwa nakuomba hapa kama unaona inafaa basi nisimame kidogo kwa niaba ya Serikali ili niweze kutoa *commitment* ambayo nafikiri itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lote la Tanzania eneo ambalo limebaki kwa sehemu kubwa kabisa kwamba halijafunguka ni Mkoa wa Tabora. Nasema afadhali kidogo Kigoma tumeanza kupiga hatua kidogo Rukwa kwa sababu ya *MCC* tumeanza kuondoka kidogo yapo matumaini kwamba ile *western part of the corridor* inaweza pengine ikaanza kuonekana inakwenda mbele. Lakini Tabora pamoja na uzee wake kama mji mkongwe bado ndiyo eneo ambalo ndiyo naona kabisa halijatoka ukilinganisha na maeneo karibu mengine yote hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, safari hii tulikuwa tumedhamiria sana na mimi nilikuwa ni mmojawapo kwa sababu si ukanda lakini natoka maeneo hayo. Kwa hiyo, nilifikiri pengine nitumie nafasi ile kuona namna ya kuweza kusaidia kuhakikisha

barabara hizi za Tabora kwa maana ya kuifungua angalau zionekane zipo ili tusibishane. Tumejitahidi tukaziweka. Tatizo linalobaki ni yale masuala ya kitaalam ili tuweze lini mtaweka mkataba saini, lini litafanyika nini lakini kwamba zipo na kwamba Serikali imedhamiria kufungua eneo hili tuliona ni vizuri hilo tukaji-*commit*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimefanyakazi ya ziada katika kujaribu kuhakikisha kwamba eneo hili linapewa uzito unaotakiwa kama si kwa sababu mwaka huu Bajeti yake imekuwa na mambo mengi na tulijaribu kuyaeleza hapo mwanzoni, Uchaguzi Mkuu tulijaribu kujikita kwenye mishahara kidogo tuongeze lakini tukatambua vile vile mzigo tulionao katika kujaribu kuhakikisha Wabunge mafao yao yanatengewa fedha. Kwa hiyo, nilitaka niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge, kwa kiwango cha *commitment* ambayo imefanywa na Serikali ni dhahiri kabisa na mimi kama mdau vile vile mkubwa katika eneo hili hakuna namna ambavyo Tabora itaendelea tena kuwa ni eneo ambalo linasemwa, linasemwa bila ya hatua ya kwenda mbele kuonekana dhahiri. Nilikuwa nimemwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kwa sababu tunalo eneo ambalo tunalifuatilia la wahisani shilingi bilioni 170 jamani tukipata fedha hii no *matter* ni kiasi gani kwa sababu ile ni *commitment* yao lazima tujitahidi Mkoa wa Tabora tuutoe hapo ulipo angalau na wao waweze kutoka na kwenda mbele. (*Makofi*)

Nimemwambia Mheshimiwa Mkulo, Mheshimiwa Mkulo unafanyakazi ya kumalizia fedha ambazo huwa zinabaki kutoka Wizara mbalimbali. Nimemwambia *please* ukishamaliza hilo zoezi, fedha yoyote itakayopatikana tuirejeshe kwenye miundombinu. Jicho letu la kwanza iwe ni Mkoa wa Tabora kwa sababu kusema kweli ndiyo umebaki na matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, nataka nikubaliane na wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora kwamba *as a government* ni lazima tukubali *something must be done*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kwa hilo ulilolisema kwamba Bajeti iendelee lakini kesho tukutane pengine tuweze kukubaliana kwamba nini hasa kwa Mkoa wa Tabora pengine tunataka kujaribu kufanya katika maeneo yote mawili, mabaki yaliyobaki kidogo hizo jitihada nyingine za Serikali angalau si kutupa *comforts as a matter of right* kama Mkoa ambao umebaki kwa kweli uko nyuma tuna kila sababu ya kusema *we are ready for that* na tunaweza kabisa tukatoka pale na matumaini pengine mazuri zaidi ili na wananchi wa eneo hilo la kati waweze angalau kuonekana wamepiga hatua moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuja mkoani pale utakumbuka nilisema hii mingine mikoa mingine tumekosa nini kwa Mungu lami iliyopo pale kilomita kama sita Rukwa tumekaa miaka nenda miaka rudi ina lami ya kilomita kama nne au tano. Lakini ndio mikoa ambayo tunazalisha chakula tumbaku kwa wingi na vitu vingine kama hivyo. Kwa hiyo, mimi naelewa kabisa hizi *feelings* za Wabunge na hata wewe mwenyewe Spika, kwamba ni *strong* na zina sababu lakini nataka nikuhakikishie katika hili nadhani wote tuko pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Rais mwenyewe naye ameamua kuji-*commit* kwamba lazima ukanda wa Magharibi lazima ufunguke kwa vyovyote vile

itakavyokuwa. Kwa hiyo, naona nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nimeona nitoe mawazo yangu kidogo pengine mkaona *feelings* tulizonazo wengine labda na namna ambavyo tutalitazama suala zima la Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho kabisa sasa wa shughuli hizi. Lakini bado nitumie ile ile Kanuni ya 5 katika mazingira ambayo hayakukaa vizuri naruhusiwa kuzikunja kidogo Kanuni ili tumalize shughuli. Sasa lazima tupitishe haya mafungu kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(2) sasa tutapitisha kwa mafungu *(guillotine). (Makofi)*

**Fungu 98 – Wizara ya Miundombinu**

Kifungu 1001 – *Administration and General* … .. … .. Sh. 2,160,676,100
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … .. … .. Sh. 839,677,770
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division* … … .. … .. Sh. 876,590,700
Kifungu 1004 – *Information, Education, and*
*Comm. Unit* … … .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. .. Sh. 338,130,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit* .. …Sh. 281,094,200
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*… … … .. … .. … … … Sh. 221,238,500
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit* … … … .. … … … … ..Sh. 167,299,100
Kifungu 1008 – *Management Information*
*System Unit*… ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 218,946,500
Kifungu 2002 – *Technical Services Division*… .. … … Sh. 74,611,987,700
Kifungu 2003 – *Transport Division* … … ... ... ... … … … … … … … Sh. 0
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division* … Sh. 214,025,088,200
Kifungu 2006 – *Transport Services Division* … … … Sh. 66,214,414,700
Kifungu 3001 – *Supplies and Services* … ... ... … … … .. … … … …Sh. 0
Kifungu 5002 – *Safety and Environment* … … … … ….Sh. 624,167,600
Kifungu 6002 – *Roads Division* … … … … .. … … …. … ... ... ... ... ...Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 98 – Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu**

Kifungu 1001 – *Administration and General* … .. … Sh. 1,435,213,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division* … … .. … Sh. 4,739,122,000
Kifungu 1002 – *Technical Services Division* … … .. … Sh. 8,224,820,000
Kifungu 2003 – *Transport Division* … … … .. … … … … … ... ... ... Sh. 0
Kifungu 2004 – *Communication* … … … .. … … … … … ... ... ... ...Sh. 0
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*… Sh. 842,333,320,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division* … … .. … Sh. 12,633,351,000

Kifungu 5002 – *Safety and Environment Division* … . Sh. 2,188,090,000
Kifungu 6002 – *Road Division* … … … .. … … … … … ... ... ... ... ... Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Mheshimiwa Waziri kutoa taarifa kazi zilizofanyika kwenye Kamati naomba nimuite Naibu Waziri wa Ulinzi na jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dr. Emmanuel Nchimba atoe taarifa baya limetokea Morogoro.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba niliarifu Bunge kwamba ndege yetu moja ya kivita ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi ambayo ni ndege ya mafunzo ilikuwa kwenye shughuli za kawaida na ilipofika kwenye maeneo ya Manga, kijiji cha Manga katika barabara ya Segera - Korogwe ilipoteza mawasiliano inaashiria kwamba ilipata tatizo la ufundi. Marubani wake walijitahidi kutua salama na kwa taratibu zao unapotaka kutua salama unatafuta eneo lenye barabara.

Katika jitihada ya kutua walifanikiwa kuikamata barabara lakini wakagongana na gari aina ya *Benz Truck* iliyokuwa na watalii. Kutokana na ajali hiyo, marubani wetu, Rubani Mwalimu ambaye ni Meja kwa Cheo na Rubani mwanafunzi ambaye ni Luteni wote wawili wamepoteza maisha yao.

Aidha, abiria waliokuwa kwenye *Benz Truck* ambao ni watalii kutoka Uholanzi hakuna aliyepata majereha wakubwa wameumia kidogo tu na wanaendelea vizuri. Taratibu zimechukuliwa ndege yetu ya kijeshi iliyopata matatizo hayo imepelekwa kwenye kituo chake na miili ya askari wetu imepelekwa Dar es Salaam kwa ajili ya uchunguzi.

Kwa kuwa familia bado hazijataarifiwa kuhusu msiba huo kwa sasa hatutatangaza majina ya marehemu hao nimeona tulitaarifu Bunge kuhusu tukio hilo. Tunaomba Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi. Amina.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namuita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu ili atoe taarifa kuhusu kazi ya Kamati.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nitangulize kwanza kutoa rambirambi kwa Rais Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na wananchi wote wa Tanzania kwa tukio hili la kusikitisha mno. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka

wa fedha 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe rasmi na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa mwaka 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kutangaza kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha rasmi Makaridio ya Matumizi kwa Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa mwaka 2010/2011. Tunawatakia ufanisi katika matumizi hayo ili yaweze kukidhi haja zote za wananchi ambao wanataka maendeleo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wa Bunge umepita kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.25 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano, Tarehe 30 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*